# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

### Kikao cha Nne - Tarehe 1 Februari, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu.

**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatayo ziliwasilishwa Mezani na:

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017.

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. LINA KITOSI - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 37

### Kampeni ya Ukimwi ya Asilimia (90, 90, 90)

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*) ina mikakati mbalimbali ya kupunguza maambukizi mapya ya UKIMWI (VVU).

Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada kuhakikisha inafanikiwa na Kampeni ya Mpango wa asilimia 90, 90, 90 hasa ukizingatia jiji la Dodoma UKIMWI umeongezeka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA IKUPA ALEX)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Hassan Mbunge wa Mtambile kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maafikiano ya malengo ya Tisini Tatu yaliyopitishwa na wadau wa Kanda zote za *UNAIDS*, Serikali ya Tanzania ilianza kuyatekeleza kwa kufanya yafuatayo ili kuhakikisha tunafikia malengo ya 90, 90, 90:-

(i) Kuanzia mwenzi Oktoba, 2016 ilitoa Waraka nchi nzima wa kuridhia utekelezaji wa Mkakati wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)* wa kupima VVU na kutibu bila ya kuzingatia kiwango cha kinga mwilini *(CD4);*

(ii) Imeweka utaatibu wa kuhakikisha watu wote wanaogundulika kuwa na VVU wanaanzishwa dawa za kufubaza VVU *(ARV)* mara moja;

(iii) Kuandaa kampeni mbalimbali kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kujitokeza kupima VVU ili kujua hali zao na hasa mkazo mkubwa umeelekezwa kwa Wanaume ambao utafiti umeonyesha kuwa hawajitokezi sana kupima na kujua hali zao;

(iv) Kufanya mapitio ya Mkakati wa kudhibiti UKIMWI wa Mkoa wa Dodoma (2017) ili kuhuisha mahitaji ya afua za UKIMWI baada ya Serikali kuhamia Dodoma na kuongezeka kwa wawekezaji katika Jiji la Dodoma;

(v) Kurekebisha Mwongozo wa huduma za VVU na UKIMWI wa mwaka 2014 kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukiza au kuambukizwa ili kuboresha mikakati ya kuwapatia huduma za UKIMWI, ikiwemo upimaji wa VVU; na

(vi) Kuanza mchakato wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI (Kuazuia na Kudhibiti) Sura ya 431 ili kushusha umri wa watoto kuruhusiwa kupima VVU kutoka miaka 18 hadi 15 na kuanzisha utaratibu wa wananchi kuruhusiwa kujipima wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa wananchi wote kuendelea kupima afya zao ili watambue hali zao na kuchukua hatua stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Masoud Abdallah swali la nyongeza.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nina maswali mawili ya nyongeza.

Katika majibu ya msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wanaandaa kampeni mbalimbali kwa ajili ya kuamasisha wananchi kujitokeza kupima VVU na

Serikali inasema inautaratibu wa wananchi kujipima wenyewe kwa kutumia mate yaani *HIV self-testing.* Napenda kujuwa mkakati huu wa Serikali wa kuwaruhusu wananchi kujipima wenyewe kwa kutumia mate umefikia hatua gani hadi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, waathirika wakubwa wa VVU ni vijana wa rika balehe kuanzia 15 hadi 24 ambayo baadhi yao wapo katika shule za sekondari na kwenye vyuo, ningependa kujua mkakati wa ziada wa kuwafikia vijana hawa hasa walio shule ya sekondari na kwenye vyuo ili kujuwa hali zao katika mkakati wa kufikia 90, 90, 90?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imeingia imeridhia malengo ya kidunia ya 90, 90, 90 na moja ya mkakati ni kuakikisha kwamba sasa tunapanua wigo wa upimaji na hususani kulenga yale makundi ya wanaume ambayo imekuwa ni changamoto kidogo. Kwa hiyo, Serikali inataka kuja na mkakati wa *self-testing* kama mtu kujipima mwenyewe kwa kutumia sampuli ya kina na hatua ambayo tumefikia sasa hivi mchakato ndani ya Serikali tumeshaazisha na sasa hivi ipo kwenye hatua za mwisho za maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, Mheshimiwa Masoud aliongelea kwamba rika balee umri kati ya miaka 15 mpaka 24. Ni kweli kwa mujibu wa takwimu za hali na viashiria vya UKIMWI vya Mwaka 2017 imeonyesha wazi kwamba maambukizi katika kundi la vijana kati ya miaka 15 mpaka 24 yanazidi kuongezeka ndani ya nchi na hususani

kwa mabinti wa kike. Baada ya sisi kulibaini hilo tumekuja na afua mbalimbali moja ni kuweka msisitizo katika suala la elimu, lakini la pili tunataka tufanye mabadiliko ya sheria kwa sababu ni wazi na dhahiri kabisa kwamba takwimu zinaonyesha mabinti wetu wanaanza kujamiana wakiwa na umri mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunataka tufanye mabadiliko ya sheria kushusha umri wa kuweza kutoa ridhaa ya kupima kwa sababu kwa sasa kwa mujibu wa sheria ya sasa, Sheria inasema mtu atapimwa ni mtu mzima mwenye miaka 18 na atapima kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na mtoa huduma katika sehemu za afya. Kwa hiyo, katika mabadiliko haya ya sheria tunataka sasa kushusha *age of consent* ili sasa hao mabinti ambao wameanza kujiamiana katika umri mkubwa na maambukizi yamekuwa ni makubwa waweze kupata ridhaa ya kuweza kupima. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo maswali yapo mengi niwaombe wenye maswali yao waulize maswali moja kwa moja. Lakini pia Mawaziri na Naibu Mawaziri mnaojibu maswali ya nyongeza mjibu kwa kifupi tafadhali. Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro kusini sasa aulize swali lake.

Na. 38

**Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Vituo vya Afya 100**

**MHE. PROSPER J. MBENA** aliuliza:-

Vigezo vilivyotumika kuchagua Vituo vya Afya 100 kupatiwa shilingi milioni 700 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maabara na upasuaji wa akina mama wanaojifungua kwa maana ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya maabara na upasuaji na shilingi milioni3 00 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa toka *MSD* ni vigezo ambavyo pia vipo katika Vituo vya Afya Duthumi, Tawa, Mvula na Mtamba katika Jimbo la Morogoo Kusini.

Je, ni lini Seikali itawatendea haki wananchi wa Morogoro Kusini kwa kuwatengea fedha ili kukamilisha miundombinu ya upasuaji angalau kituo kimoja Kata ya Duthumi, Tawala Mvuha na Mtamba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mpango wa Kuboresha Vituo vya Afya nchini ambapo hadi sasa Vituo vya Afya 350 vimepatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vilivyotumika kuchagua vituo hivyo vinavyokarabatiwa na kujengwa ni uhitaji mkubwa wa huduma za dharura na upasuaji kwa mama wajawazito, sababu za kijiografia na umbali mrefu ambao wananchi wanatembea kupata huduma za dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilitoa kiasi cha shilingi million 500 kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa Kituo cha Afya cha Duthumi kilichopo katika Jimbo la Morogoro Kusini. Vilevile katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilion1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro inayojengwa katika Makao Makuu ya Halmashauri eneo la Mvuha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Posper Mbena swali la nyongeza.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa msaada huo katika sehemu hizo mbili zilizotajwa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini Serikali itazisaidia Vituo vya Afya vya Mtamba pamoja na Kisaki ambavyo mchakato wake Serikali ulishaanza kushughulikia?

Je, ni lini Serikali itapeleka au itasaidia Hospitali Kuu ya Mkoa wa Morogoro mashine ya *CT-Scan* ili kuokoa maisha ya watu ambao yanapotea bure kwa ajili ya kukosa huduma ya mashine hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Naona hapo swali la mwanzo ni la kwako, la pili naona ni la Wizara ya Afya lakini Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimetaja katika jibu la msingi Wilaya ya Morogoro Vijijini ambayo Mheshimiwa anatoka ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimepata nafasi ya kujengewa Hospitali za Wilaya na tumeanza kupeleka shilingi bilioni 1.5 lakini ili ikamilike tunahitaji tunahitaji jumla ya shilingi bnilioni 7.5. Lakini mwenyewe anakiri kwamba tayari tumeanza kujenga Kituo cha Afya pale Duthumi, najua kabisa kiu ya Mheshimiwa Mbunge kwamba na maeneo mengine Vituo vya Afya vijengwe naomba nimuakikishie kwamba ni azima ya Serikali kwa kadri bajeti inavyoruhusu tumeanza na vituo 350 lakini azma kuhakikisha kwamba katika kata zetu zote kwa kadri bajeti itakavyo kuwa inaruhusu kama ambavyo tumeahidi kwenye ilani ya CCM tunaenda kutekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya *CT-Scan*.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mwongozo wetu wa Wizara ya Afya huduma za *CT-Scan*

zinapatikana kuanzia Hospitali za ngazi ya Rufaa za Kanda. Lakini baada ya kuwa tunafanya mapitio katika hii sera mpya tunajaribu kuangalia huduma sasa hivi katika nchi yetu zimekuwa sana na tumeona kwamba baadhi ya hospitali za mikoa ambazo ziko kimkakati. Lakini vilevile huduma hizi za *CT-Scan* zinahitaji utaalamu wa hali ya juu kuweza kuzitumia ambazo zingine huduma hizi hazipatikani katika Hospitali za Mikoa, Hospitali Wilaya na kushuka chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mkakati wetu sisi kama Serikali nikujaribu ku-*identity* mikoa ile ambayo ni ya kimkakati ikiwa ni pamoja na Morogoro kwa sababu kuna aya inapita pale ili huduma hizi ziweze kupatikana kwa lengo kuhakikisha kwamba tunazuia ajali baadhi ya Mikoa lakini hatutaweza kuzishusha huduma chini ya ngazi ya hospitali ya rufaa Mikoa kwa sasa.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendele na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Dkt. Saada Salum Mkuya, Mbunge wa Welezo aulize swali lake.

Na. 39

**Changamoto za Muungano**

**MHE. SAADA SALUM MKUYA** aliuliza:-

Kumekuwa na changamoto mbalimbali katika Muungano ambazo zinaendelea kutatuliwa mojawapo ikiwa ni ajira za Muungano ziwe asilimia 21 kwa upande wa Zanzibar.

(a) Je, ni kwa kiasi gani makubaliano hayo yametekelezwa hadi sasa?

(b) Je, ni ajira ngapi zimepatikana kwa utaratibu huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira naomba nichukue fursa hii sasa kujibu swali la Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge wa Welezo lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Utaratibu uliokubalika ni kwamba ajira katika taasisi za Muungano zinatakiwa kuwa kwenye uwiano wa asilimia 79 kwa watumishi wa Tanzania Bara na asilimia 21 kwa watumishi wa Zanzibar kwa utumishi wa ngazi ya utaalamu. Katika kutekeleza utaratibu wa muda wa mgao wa nafasi za ajira *(quota)* katika taasisi za Muungano kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipewa kibali cha nafasi tatu, mtumishi mmoja alipangwa Zanzibar ikiwa ni asilimia 33 na watumishi wawili walipangiwa Tanzania Bara sawa na asilimia 67.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilipewa kibali cha nafasi 28 za Maafisa Mambo ya Nje na kati ya nafasi hizo saba zilijazwa na Watumishi kutoka Zanzibar ikiwa ni asilimia 25 na nafasi 21 zilijazwa na watumishi kutoka Tanzania Bara ikiwa ni asilimia 75.

(b) Tangu kufikiwa kwa makubaliano ya uratatibu wa muda wa mgao wa ajira katika Taasisi za Muungano mwaka 2013/2014 na kuanza kwa utekelezaji wa utaratibu huo mpaka sasa jumla ya wazanzibari 8 kati ya 31 wameajiriwa katika taasisi za Muungano ambao ni sawa na asilimia 25 ya waajiriwa hao. Taasisi za Muungano zina mwongozo wa utekelezaji wa makubaliano hayo na zinaendelea kuzingatia utaratibu huo wanaopata fursa ya kuajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo huu ulianza kutekelezwa mwaka 2013/2014 lakini utekelezaji wake umekumbwa na changamoto ikiwa ni kusitishwa kwa ajira Serikalini kuanzia mwaka 2016 hadi 2017 kutokana na kupisha

zoezi la uhakiki wa Watumishi hewa na watumishi wenye vyeti feki. Hivyo, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa taasisi zote za Muungano zilipewa utaratibu huo na zitaajiri watumishi kama ilivyoelekezwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum swali la nyongeza.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante lakini nachuka fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo yametoa mchanganuo mzuri na unaleta matumaini na tunatarajia kwamba hizo changamoto zitatatuka karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo huo haufuatwi katika mashirika ya Muungano, je, Serikali lini itatoa utaratibu huo wa mwongozo katika mashirika ya Muungano kuona na yenyewe yanafuata utaratibu huu katika ajira?

Swali langu la pili ni kwamba utaratibu huu umekuwa ukifuatwa kama ambavyo umeelezea, lakini bado umekumbwa na changamoto, kuna mfumo gani ambao unafuatwa ili kufanya *assessment* kuona kwamba huu utaratibu liowekwa unafuatwa katika taasisi zote za Muungano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Saada Mkuya, lakini pia na mimi nichukue fursa ya kumpongeza kwamba mara nyingi tumekuwa tukishirikiana kwa namna ambavyo tunaweza kutatua changamoto za Muungano, lakini kama nimeeleza kwenye majibu yangu ya swali la msingi kwamba tayari mashirika haya tumeyapa mwongozo na suala kubwa sasa ni ufuatiliaji kwa namna gani wanatekeleza mwongozo ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia suala la pili juu ya *assessment,* Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira tunawajibika moja kwa moja kupata taarifa kutoka kwa wenzetu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa kufuatilia *assessment* huu tumeuweka vizuri na tumeweka bayana, tutakavyo kutana nitamuelekeza vizuri namna ambavyo tumetekeleza. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea Wizara ya Mifugo. Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongezee katika majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo muhimu sana ambalo linatusaidia kuimarisha Muungano wetu. Lazima nikiri kwamba katika maeneo ambayo hatufanyi vizuri ni hili la uwiano wa watumishi katika Taasis za Muungano na Wizara za Muungano, lazima tukiri ukweli huo. Bahati nzuri maamuzi yalishatoka na sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais na kama Serikali katika kuhakiksha kwamba maamuzi hayo yanatekelezwa kwa haraka tumeshirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Rais, Utumishi kuhakikisha kwamba wanafungua Ofisi Zanzibar na kuajiri na kutangaza na kufanya *interviews* kwa Zanzibar vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutampa jedwari la kuonesha kila taasisi ya Muungano iwe Benki Kuu iwe *TCRA* na watu ilionao, Wazanzibari na Wabara ili kuwe na uwazi na tusaidiane katika usukumaji wa jambo hili, hilo la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa rai vilevile kwa vijana wa Zanzibar ambao wanaomba nafasi katika taasisi za Muungano kuandika *address* sahihi, kwa sababu msingi wa taarifa tunazopata ni anuani kwenye maombi. Kwa hiyo, wengine ni Wazanzibar lakini wanaandika anuani za

Bara; kwa hiyo, hatupati taarifa sahihi kuhusu hasa idadi ya Wazanzibar na watu wa Bara katika nafasi hizi. Kwa hiyo, wito wangu ni kwamba ukiandika anuani sahihi inasaidia kupata takwimu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingi Wazanzibar wapo wengi zaidi kuliko inavyoonekana kutokana kwamba walioomba kazi hiyo kutokea Bara na waliandika anwani za Bara.

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo maana yake watu wanatakiwa kuwa wanaandika mimi ni Mzanzibar na kama ni Mzanzibar anayeishi Bara anaajiriwa kama Mzanzibari au kama Mtanzania sasa. Maana kama tukishaanza; kuna haja ya uwiano ndiyo; lakini huo utenganisho wa namna hiyo sina hakika tunaelekea wapi.

Hata hivyo nadhani kwa kuwa umesema utazungumza na Mheshimiwa Saada naamini mtafikia mahala pazuri ambapo hapata tufikisha kule ambako hatutaki kwenda. Kwa sababu kuna wanaoshi bara wanaomba kazi sasa atakosa kazi kwa kuwa tu ni Mzanzibari anayeishi Bara? Nadhani mtalimaliza vizuri ili liende sawa sawa tusije tukafikia mahali ambapo tutawekeana ubaguzi sisi wenyewe.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Zitto Ruyagwa Kabwe, Mbunge wa Kigoma Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 40

**Uvuvi wa Kutumiwa *Purseiner* Ziwa Tanganyika**

**MHE. KABWE R. Z. ZITTO** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali ya Tanzania inazuia wawekezaji wa uvuvi kuvua kwa kutumia *purseiner* katika Ziwa Tanganyika ilhali nchi za Burundi, Zambia na *DRC* zinazopakana na ziwa hilo huruhusu uvuvi huo?

(b) Je, kwa nini Serikali inawaelekeza wawekezaji wa uvuvi katika Ziwa Tanganyika kuhamisha uwekezaji wao na kuupeleka mahali pengine nchini na je, huu sio makakati wa kukwamisha maendeleo ya Mkoa wa Kigoma na watu wake?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Zitto Ruyagwa Kabwe, Mbunge wa Kigoma Mjini lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimwa Naibu Spika, si lengo la Serikali kuzuia uwekezaji wa uvuvi wa kutumia *purseiner* katika Ziwa Tanganyika. Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wake husuani wavuvi wadogo na wazawa wananufaika na rasimali za uvuvi katika kuwaletea maendeleo, inazingatia msingi ya uvunaji endelevu unaoendana na wingi wa rasilimali zilizopo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, tathimini ya wingi wa rasimali za uvuvi katika Ziwa Tanganyika *(stock assessment)* iliyofanya mwaka 1998 ilionesha wingi wa samaki ulikadiriwa kuwa tani 295,000. Serikali inaendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kuweza kujua wingi wa samaki kwa sasa kabla ya kuridhia shughuli za uvuvi mkubwa ili usiathiri wavuvi wadogo wadogo, wananchi wa kawaida na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kuwa Serikali ina mkakata wa kukwamisha maendeleo ya Mkoa wa Kigoma na watu wake, isipokuwa kwa sasa hatuna hakika na wingi wa samaki uliopo katika Ziwa Tanganyika kwani mara ya mwisho tafiti ya tathimini ya wingi wa samaki ilifanyika ya Ziwa Tanganyika ilifanyika mwaka 1998. Iwapo tafiti itaridhia uvuvi huu bila kufanya tathmini ya wingi wa samaki wadogo, wazawa wa Kigoma na mazingira yanawaweza yakaathika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe swali la nyongeza.

**MHE. KABWE R. Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa Serikali itafanya utafiti iweze kutoa kanuni za kuwezesha uvuvi wa kisasa na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi katika Mkoa wa Kigoma kuweza kufanyika? Lini utafiti huo utaweza kufanyika kwa sababu sio wajibu wa wananchi ni wajibu wa Serikali kufanya huo utafiti na miaka 21 imepita bila huo utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sasa hivi kumekuwa na leseni nyingi sana za uvuvi. Mvuvi mmoja yaani kwa chombo kimoja kinahitaji leseni takribani tisa na hivyo kuongeza gharama kubwa sana kwa wavuvi wa Ziwa Tanganyika. Vilevile gharama za kuuza mazao ya uvuvi nje zimeongezeka kutoka senti 0.5 ya dola ya Marekani mpaka dola 1.5 kitu ambacho kinatufanya wavuvi wa Mkoa wa Kigoma kutokushindana vizuri na wenzetu wa Burundi na Congo kwa sababu wao hawana tozo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lini Serikali itahusianisha hizo tozo na kuzishusha ili tueweze kuendeleza *export* tunayoifanya sasa hivi ya mazao yetu kutoka Ziwa Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali linalouliza kuwa ni lini Serikali itafanya utafiti. Kupita taasisi yetu ya *TAFIRI* tumeanza hatua za awali za kufanya utafiti katika maji yetu ya Ziwa Victoria, lakini vile vile tunacho kituo cha *TAFIRI* pale Kigoma. Kwa hivyo hatua za mwanzo za utafiti huu kwa kushirikiana na nchi zinazozunguka Ziwa hili Tanganyika kupitia taasisi inayotuunganisha tutafanya utafiti pia wa kujiridhisha ya *stock assessment* na hatua za kuweza kuwaruhusu wawekezaji wakubwa, wakati na wadogo ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la ni juu ya leseni nyingi zilizopo. Uwepo wa leseni katika tasnia ya uvuvi

ni jambo la matakwa la kisheria lakini vilevile ya kitaalam. Kwa sababu inatusaidia hata kujua idadi ya wavuvi tulionao.

Naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge juu ya tozo tunazozitoza kuonekana kuwa ni nyingi na kubwa na kutufanya tusiwe na ushindaji sahihi na wenzetu. Jambo hili ndani ya mamlaka yetu, tupo tayari kukaa na wadau kuweza kushaurina ili kuweza kufanya tasnia ya uvuvi iweze kuwa na manufaa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimwia Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu makatazo yaliyokuwa yamefanyika Ziwa Tanzanyika yamemefanyika pia Ziwa Victoria hasa kwa kuzuia matumizi ya taa za *solar* kwenye shughuli ya uvuvi wa dagaa. Kwa sababu juzi Mheshimiwa Waziri niliona anatoa tamko kule *Ferry,* ni nini sasa kauli thabiti kwa wavuvi wa Ziwa Victoria ili waendee kutumia taa za *solar* mpaka pale utaratibu utakapo kamili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi katika kufafanua hilo ulieleze sasa kwa jumla maana atasimama na wa ziwa lingine na lingine, ili watu wapate ulewa wa pamoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimwa Mabula kwa swali lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba baada ya kutafakari sana malalamiko ya wavuvi wetu katika maziwa mbalimbali juu ya leseni nyingi, matumizi ya jenereta pamoja na matumizi ya taa za solar; na kwa mamlaka niliyonayo nikaamua kwamba sasa matumizi ya solar na jenereta yaruhusiwe na wananchi wasikamatwe kwa kutokuwa na

leseni hivi sasa wakati tunatatua tatizo hili la kuwa na leseni nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachotaka kuwambia wavuvi wote na Mheshimiwa Mbunge ni kwamba nimeruhusu rasmi matumizi ya taa za *solar* na jenereta mpaka tarehe 1 Julai. Hata hivyo Serikali haikusudii kuzuia wananchi kutumia *solar* isipokuwa ni kuwa-*guide* kwamba ni *solar* zenye *watts* kiasi gani ambazo zitahitajika kutumika, hapo ndio tutatoa hizo *guidelines* tarehe 1 Julai.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 41

**Ranchi za Taifa**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Serikali ilikuwa na nia kuanzisha Ranchi za Taifa katika maeneo mbalimbali.

(a) Je, kuna ranchi ngapi na kati ya hizo ngapi zimebinafsishwa na ngapi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa?

(b) Kwa siku za nyuma Ranchi ya Kongwa na Ranchi ya Ruvu, mifugo ilikuwa inaonekana hata ukipita barabarani hali hiyo sasa haipo, je, kuna tatizo gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Ranchi za Taifa ilianzishwa mwaka 1968 kwa Sheria ya Makampuni *(Cap 212)* kwa lengo la kuendeleza ufugaji wa mifugo bora ya nyama ili kitosheleze mahitaji ya nyama ndani na ziada ya kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NARCO* inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 ikiwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Aidha, *NARCO* inamilikiwa jumla ya ranchi 14 zenye ukubwa wa hekta 544,207 zilizotawanyika sehemu mbalimbali nchini ambazo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa siku za nyuma Ranchi za Ruvu na Kongwa zilikuwa na idadi kubwa ya mifugo ambayo ilionekana hata ukiwa barabarani. Hata hivyo, Kampuni ya Ranchi za Taifa impitia changamoto mbalimbali ikiwemo mwaka 1992 kupendekezwa kubinafsishwa na kuwa nchini ya uangalizi wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashiriki ya Umaa *(PSRC)* kwa miaka 14. Katika kipindi hicho kampuni haikutekeleza shughuli za maendeleo na hivyo kupelekea uchakavu wa miundombinu na mashamba kuvamiwa, vichaka na mifugo kupungua. Aidha, kampuni inafanya jitihada za kuboresha miundombinu na malisho katika ranchi hizi ili kuirejesha hali ya kuwa na mifugo mingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Malembeka swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ninampongeza na ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake zuri ambalo limeleta uelewa na kuonesha nia ya kukufua ranchi zetu. Nilikuwa na maswali mawili ya ziada kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa katika maelezo yake amesema lengo kubwa ilikuwa ni kutoa mifugo bora kwa ajili ya nyama ndani ya nchi na kuuza nje ya nchi, na kwa kuwa Zanzibar inategemea kitoweo cha nyama kutoka Tanzania Bara, je,

Serikali ina mpango gani kupeleka nyama Zanzibar kwa utaratibu maalum?

(ii) Kwa kuwa Ranchi ya Ruvu likuwa inajengwa machinjio kubwa ya kisasa lakini mpaka sasa hvi imesimama na haijulikani itakamalika lini. Serikali ina kauli gani juu ya Ranchi hiyo ya Ruvu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya upelekaji wa kitoweo cha nyama ya ng'ombe Zanzibar hivi sasa wapo Watanzania wengi wanaofanya biashara ya kuchukua nyama ya ng'ombe na kupeleka Zanzibar na ziko kweli changamoto kadha wa kadha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mara changamoto tulizonazo huwa tunazifanyia kazi ya kuhakikisha tunazitatua na hatimaye kuweza kuwasaidia wenzetu kuweza kupata kitoweo cha nyama ng'ombe, mbuzi kwa uhakika na hilo tutaendelea kulifanya kadri litakavyokuwa likiibuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, juu ya machinjio ya Ruvu. Tupo kwenye mkakati mzuri wa kuhakikisha machinjio ya Ruvu inajengwa. Hivi sasa tumeshafanikisha kuona juu ya athari ya mazingira na hatua zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati tulionao ni kutafuta pesa ya kuhakikisha kuwa mradi ule unakamilika na kuwaweza kuwasidia Watanzania kupata nyama ya uhakika, lakini vilevile kuweza ku-*export* nje ya nchi na hata kutengeneza vitu vingine kama vile mazao yanayotokana na ngozi za ng'ombe wetu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 42

## Kuwawezesha Wanaofanya Uvuvi Haramu Kutumia Fursa Zilizopo

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Uvuvi haramu bado unaendelea licha ya adhabu kubwa inayotolewa kwa watu wamaojihusisha nao.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani katika kuwasaidia wananchi wake fursa zilizopo badala ya kutoa adhabu kali zinazowaumiza?

(b) Je, Serikali inavisaidiaje vikundi vya *Beach Mananagement Unit* vinavyojihusisha kuona faida ya kazi wazofanya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mikakati mbalimbali ya kuwasaidia wananchi wake wanaojihusisha na uvuvi ikiwemo:-

(i) Kufata kodi mbalimbali ili kuwapunguzia wavuvi mzigo kama vile Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye injili za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu, nyavu za uvuvi na vifungashio kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2011 na Sheria ya Mamlaka ya Mapato *(VAT Act)* ya mwaka 2014.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tunao mkakati wa kupunguza au kuondoa ushuru na tozo

mbalimbali kama vile ushuru wa usajili kwa vyombo vya uvuvi vilivyo chini ya mita 11 na tozo ya cheti na afya nazo zimeondolea.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwingine ni kuhakikisha wavuvi wanaanzisha vyama vya ushirika ili waweza kunufaika na programu mbalimbali, mfano *wavuvi scheme* iliyopo katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa *(NSSF).*

(iv) Kufanya maboresho ya sheria na kanuni za uvuvi ili ziweze kuendena na mazingira na hali ya sasa ya uvuvi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inafanya yafuatayo ili kuvisaidi vikundi vya vya uvuvi shirikishi wa mazingira ya bahari na maziwa yaani *BMUs.*

(i) Kuvipatia elemu na kuvijenge uwezo wa kusimamia rasilimali za uvuvi kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu.

(ii) Kuziagiza Halmashauri za Wilaya zote nchini kuvipatia vikundi vya *BMUs* uwakala wa kukusanya mapato yatokanayo na uvuvi katika Halmshauri zao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi swali la nyogeza

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wale vijana wanaoishi kando kando wa ziwa waweze kuona umuhimu wa kutunza ziwa lao na kuzuia uvuvi haramu. Ni lini sasa Serikali itaweza kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia kujenga mabwawa kando kando ya ziwa pamoja na *cage* ziwani ili ziweze kuwasaidi hao vijana katika kujipatia kipato ili waweze kuona umuhimu wa kutunza ziwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kila moja amekuwa akishuhudia akina mama wengi wanao nunua samaki wakiwa wamenyanganywa kwenye madishi yao, hata wale waliokaanga samaki wao wanaouza sokoni ambayo hii kusema kweli wao si wavuvi, lakini wanakuja kunyang'anywa samaki wale ambao wameshawanunua. Waziri anatoa kauli gani kuhusiana na unyanyasaji huu ambao unandelea katika baadhi ya maeneo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, mkakati wa Serikali tulionao wa kuhakikisha tunapunguza nguvu ya uvuvi katika maziwa na kuepusha vijana na uvuvi haramu katika kuhamasisha kufanya ufugaji wa samaki; tunaomkakati sana. Hivi sasa ninavyozungumza, tumeshaanza mkakati huo katika Ziwa Victoria ambapo wako watu binafsi walioanza ufugaji wa samaki katika vizimba lakini vilevile na sisi kama Serikali tumejiandaa kuhakikisha tunatengeneza *incubators,* kwa maana ya vikundi vya vijana ambavyo vitakwenda kufanya shughuli ya utengenezaji wa mabwawa lakini vilevile utengenezaji wa *cages* kwa ajili ya ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Manyinyi ahakikishe anawaunganisha vijana wake kama nilivyotangulia kujibu katika swali la awali, wakae katika vikundi vya ushirika, nasi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tuko tayari kwenda kutoa elimu, lakini vilevile utaalam na kuhakikisha tunawasaidia vijana hawa kuwaongoza katika kufikia lengo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni juu ya kauli gani tunatoa kwa ajili ya wale akina mama na wanawake wanaouza samaki katika mabeseni. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa tunalinda rasilimali za uvuvi. Katika lengo hilo, hatuko tayari kuona mwanamama anayefanya biashara ya uuzaji wa samaki katika mabeseni huko masokoni, anaonewa. Kama yuko Afisa wa Serikali anayekwenda

kumsumbua na kumnyanyasa mwanamke anayeuza mafungu yake matatu, manne sokoni ya samaki, hii leo natoa kauli hapa katika Bunge hili Tukufu, jambo hilo ni marufuku. Kwa sababu lengo letu siyo kuangalia hawa samaki wanaowekwa katika mabeseni, lengo letu ni kutazama hasa kiini cha makosa haya yanayotokana na uvunjaji wa Sheria ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niwahakikishie tu akinamama wanaouza samaki nchini kote, wawe huru katika uuzaji wa samaki wao, wahakikishe kuwa wanapata kipato cha familia zao na kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nimeletewa ujumbe hapa. Siyo utaratibu, utusaidie kuzungumza lile katazo lako, wale waliokuwa wamenyang'anywa majenereta na taa zao za *solar* watarejeshewa ama utaratibu utakuwaje? Majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba nimeruhusu matumizi hayo ya *generator*, taa za *solar* na wananchi wote ambao wameshikiwa zana hizo, warudishiwe bila masharti yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nilikuwa nataka kusisitiza katika hili jambo la kwamba suala la ulinzi wa rasilimali zetu hizi ni suala ambalo linahitaji kuungwa mkono na wananchi wote. Rasilimali hizi tulizonazo hapa nchini asilimia 37 ni maji, lakini mazao yetu ya uvuvi mengi yameharibiwa sana na suala la uvuvi haramu. Kwa hiyo, wananchi wote wanawajibika kuziangalia hizi sheria na kuziheshimu. Kwa sababu hata huyo Mama Ntilie anajua samaki wasioruhusiwa. Tukitengeneza mtandao huu wa huyu mama mdogo anaweza kuingia kwenye soko na samaki wasioruhusiwa, tutatengeneza mtandao ambao utawezesha kuwepo kwa soko hili.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nawaomba sana, katika kipindi hiki kigumu cha

kubadilisha watu kuwaondoa kwenye uvuvi haramu, mtuvumilie. Kwa sababu hata huyo mama mjane tunayemhurumia leo, kesho hatapata samaki wa kuuza. Hata mama mjane, mtoto yatima, watoto hawaendi shule; hawataenda shule kabisa kwa sababu samaki hawatakuwepo majini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika kipindi hiki ambacho tunafanya *transformation* hizi kubwa, nakuomba sana na bunge lako Tukufu mtuvumilie kwa nia nje kwa sababu hatua hizi zote tunazochukua ni kwa ajili ya Taifa letu na hatima ya uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto. Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 43

**Kukosekana kwa Mafuta Yanayokinga Ngozi kwa Watu Wenye Ualbino**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

Tatizo la kukosekana kwa mafuta yanayosaidia kukinga ngozi dhidi ya mionzi kwa watu wenye Ulemavu wa ngozi hapa nchini limekuwa kubwa na hivyo kuwa chanzo cha magonjwa ya saratani kwa watu hao na kusababisha vifo. Inakadiriwa kuwa asilimia 70 hadi 75 ya vifo vya watu wenye ulemavu wa ngozi vinatokana na saratani.

Je, ni lini Serikali itatoa huduma hiyo bure kwa watu wenye ulemavu wa ngozi katika maeneo yote nchini kama inavyotoa dawa za kufubaza virusi kwa watu wenye maambukizi ya UKIMWI?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatambua uwepo wa watoto wenye ulemavu wa ngozi kwa maana *albinos (albinism)* nchini na umuhimu wa wao kupata mafuta hayo ili kuwasaidia kukinga ngozi yao dhidi ya mionzi. Kwa kutambua umuhimu wa mafuta hayo, kwa jina la kitaalam tunaita *Sun Protection Factor 30,* Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kuanzia mwaka 2013 iliingiza mafuta hayo kwenye orodha ya Taifa ya dawa muhimu ili ziweze kununuliwa kutunzwa na kusambazwa na Bohari ya Dawa nchini kote.

Aidha, Bohari ya dawa tangu mwaka 2015 imekuwa ikinunua mafuta hayo kadri ya maombi yalivyowasilishwa na vituo vya kutolea huduma ya afya. Baadhi ya taasisi kama vile Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road,* Hospitali ya Mirembe - Dodoma, Hospitali ya Kisarawe na Ilemela zilipata mafuta haya kutoka *MSD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya ualbino ni hali ya kudumu na hivyo kuangukia katika kundi la magonjwa sugu, ambapo Sera ya Afya mwaka ya 2007 inatamka wazi kuwa kundi hili litapata huduma bure, hivyo basi, nitoe rai kwa hospitali na vituo vyote vya kutolea huduma za afya katika mikoa ya Halmashauri kuingiza bajeti ya mafuta hayo katika mipango yao ili iweze kuagiza mafuta hayo kutoka bohari ya dawa.

Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wazalishaji wa ndani ya nchi wa mafuta hayo katika kiwanda kilichopo katika Hospitali ya *KCMC*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri na vilevile nitambue na kupongeza jitihada za Serikali katika kusaidia makundi maalum hasa watu wenye ulemavu. Pamoja na majibu hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, kweli Serikali imeanza utaratibu huo, lakini usambazaji wa mafuta haya hasa kwa maeneo ya vijijini bado ni tatizo. Albino wengi wanaangamia kutokana na saratani. Napenda tu kufahamu jitihada za Serikali katika kuhakikisha kwamba wanafika vijijini ili kuweza kuwanusuru watoto hawa. Nini mpango mkakati wao kuhakikisha kwamba wanawafikia? Hilo ni swali namba moja.

Swali la pili, albino wengi wanaoishi vijijini, tayari wameshaathirika na ugonjwa wa saratani; na hali za maisha kama tunavyofahamu hasa wa vijijini ni duni sana, kupata shilingi 10,000/= ni shida. Nini mpango mkakati wa Serikali kuwasaidia na kunusuru maisha ya watu wenye *albinism* hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, utaratibu ambao Serikali tunatumia sasa hivi katika usambazaji wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba ni utaratibu ambao unaitwa *pool system.* Miaka ya nyuma tulikuwa tunatumia *push system. Push system* maana yake nini? Ni kwamba sisi Serikali tulikuwa tunanunua dawa, vitendanishi na vifaa tiba tunavipeleka katika vituo vya kutolea huduma ya afya pasipo kuzingatia

mahitaji halisi ambayo yako kule. Kwa hiyo, hukuta baadhi ya vifaa, dawa na vitendanishi vinachina kwa sababu uhitaji haukuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ambao tunautumia sasa hivi ni wa *pool system.* Wao kama Vituo vya Afya wanajua mahitaji mbalimbali ya huduma na dawa, vitendanishi na vifaa tiba na wao kuingiza katika mipango yao na kuagiza kutoka *MSD.* Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, dawa hizi na mafuta haya kwa ajili ya kundi hili la walemavu wa ngozi tunavyo ndani ya *MSD,* ni wajibu sasa wa Halmashauri mbalimbali na hospitali za mikoa kuziagiza kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Mheshimiwa Amina amegusia suala la walemavu wa ngozi kwamba wamekuwa wanaathirika na ugonjwa wa kansa. Hili ni kweli, tunakiri. Ni kwa sababu jua hili ambalo ni mionzi yetu ya jua lina *ultraviolet rays* ambazo zinaathiri ngozi za wenzetu hawa ambao wana ulemavu wa ngozi kwa kiasi kikubwa kulinganisha na wengine ambao wasiokuwa walemavu wa ngozi na tunaendelea kutoa elimu kuhakikisha kwamba wenzetu ambao wana ulemavu wa ngozi wanajikinga dhidi ya miale ya jua kwa kuvaa kofia na nguo ambazo zinakinga sehemu kubwa ya miili yao, lakini vilevile kutumia mafuta ambayo yanawakinga dhidi ya hii miale ya jua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, huduma za matibabu ya kansa ni bure ndani ya nchi yetu. Nami nawaomba sana, mtu yoyote ambaye anaona kuna mabadiliko katika ngozi yake, basi aweze kufika katika vituo vya kutolea huduma ya afya aweze kupata huduma kwa haraka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Stella Alex Ikupa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA IKUPA ALEX):** Mheshimiwa Naibu Spika,

naomba kuongezea kidogo kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya pamoja na majibu yake mazuri; ni kwamba naomba tu niendelee kutoa msisitizo kwamba Wakurugenzi katika Halmashauri mbalimbali wajitahidi kwamba wanakuwa na idadi kamili ya haya mahitaji kwa maana ya watu wenye mahitaji, watu wenye ualbino. Kwa sababu wasipokuwa na orodha kamili ya mahitaji, inakuwa ni ngumu upatikanaji wa hizi dawa kutoka *MSD.* Hili limekuwa ni tatizo ambalo katika ziara ambazo nimewahi kuzifanya imeonekana kwamba mahitaji haya hayapatikani kulingana na uhalisia wa watu waliopo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Anna Lupembe.

Na. 44

**Kuwahudumia Watoto Njiti Nchini**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. TASKA R. MBOGO)** aliuliza:-

Tanzania haina wauguzi walisomea kuhudumia watoto njiti.

(a) Je, ni lini sasa Serikali itasomesha wauguzi kwa ajili ya kuhudumia watoto njiti?

(b) Je, kuna hospitali ngapi na vituo vya afya vingapi nchini vyenye chumba atamizi *(incubator)?*

(c) Gharama za kuwatunza watoto njiti ni kubwa na wanakaa hospitali muda mrefu kwa miezi mitatu hadi minne, je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia akina mama wanaojifungua watoto njiti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya kuwahudumia watoto njiti yapo katika Mtaala wa Mafunzo ya Wauguzi na Madaktari na wanafundishwa wakiwa vyuoni. Ili kuboresha ufanisi katika kuwahudumia watoto njiti na upatikanaji wa elimu hii, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na wataalamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, imetengeneza mtaala wa mafunzo haya utakaotumika kuwafundishia wauguzi waliopo makazini kuanzia mwezi Februari, 2019 nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia Mafunzo ya Huduma Muhimu kwa Watoto Wachanga *(Essential Newborn Care),* watoa huduma kwa maana ya Madaktari na Wauguzi 1,453 kutoka vituo vya kutolea huduma 653 katika Mikoa ya Tabora, Simiyu, Shinyanga na Kigoma walio makazini wameshapata mafunzo. Lengo ni kutoa mafunzo haya katika mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma atamizi kwa maana *incubators* hutolewa kwa watoto wote njiti pamoja na walio na uzito pungufu ili kuzuia kupoteza joto ambapo kwa sasa huduma hii inapatikana katika baadhi ya hospitali za Mikoa na Halmashauri tu. Mpaka sasa ni hospitali za mikoa 20 pamoja na Hospitali 24 za Halmashauri ambazo zina vyumba vyenye huduma atamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu wa Serikali ni kuhakikisha huduma za kumhudumia mtoto njiti zinapatikana katika vituo vya kutolea huduma. Serikali inatenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya huduma za afya ya mama na mtoto ikiwa ni pamoja na mtoto njiti. Aidha, elimu kuhusu maandalizi kwa ajili ya kujifungua hutolewa kwa wazazi, mama na mwenza

wake, wakati wa kliniki za ujauzito ikiwa ni pamoja na matunzo ya mama na mtoto kabla na baada ya kujifungua.

Hivyo, Serikali haina kusudio la kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia akina mama wanaojifungua watoto njiti. Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya kuwatunza watoto njiti katika vituo vya kutolea huduma za afya na kutoa elimu ya kulea watoto njiti kwa jamii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hospitali yetu ya Mpanda Manispaa ndiyo ina-*act* kama hospitali ya Mkoa; na ndani ya ku-*act* kwake hatujawahi kupata mafunzo hata siku moja; na Serikali ilitutengea kachumba kadogo sana ambako ndiko kanatunza watoto njiti, lakini hatuna kabisa Muuguzi ambaye anayefanya kazi hiyo; nasi ukiangalia ndani ya Wilaya yetu ya Mpanda, Hospitali ile Wauguzi wako wachache sana, ndiyo maana watoto njiti wanafariki kutokana na huduma inakuwa siyo nzuri; ukizingatia vifaa vyake vile vya kutunzia wale watoto hatuna: Je, ni lini sasa Serikali itatuletea hawa Wakufunzi waje waweze kutufundishia Wauguzi wetu pale katika Hospitali yetu ya Mpanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, katika wodi ya wazazi, ndiko kulitengwa hicho kichumba kidogo, napo kuna vitanda vitatu tu; watu wazima wanakaa mle ndani, hakuna usalama kabisa: Je, ni lini Serikali itatujengea wodi maalum kwa ajili ya watoto njiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**MHE. NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge, nini maana ya watoto njiti? Watoto njiti ni wale watoto ambao wanazaliwa kabla ya mimba kufikisha umri wa miezi tisa au wanazaliwa na uzito pungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto hawa wanakuwa na athari zaidi kwa sababu viungo vyao vinakuwa havijakamilika vizuri, ama havijakomaa vizuri na uwezekano wa wao kupoteza maisha kwa shida za kupumua na kupata magonjwa mbalimbali ni mkubwa sana. Sisi kama Serikali, moja ya mkakati wetu ni kupunguza vifo vya watoto wachanga na tumejikita kuhakikisha katika mwaka huu wa fedha na baada ya Serikali kutukabidhi Hospitali za Rufaa za Mikoa, vipaumbele vyetu sisi kama Wizara, ni kuhakikisha kwamba tunaboresha huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na huduma za magonjwa ya dharura, ujenzi wa *theatre*, uwepo wa *ICU,* lakini tumeweka msisitizo katika huduma ya mama na mtoto, vilevile kuhakikisha kwamba kuna huduma za *ICU* za *Neonatal.* Huo ndiyo mpango mkakati wetu katika ile bajeti ambayo mmetupitishia mwezi Julai, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maswali haya ambayo Mheshimiwa Amina Lupembe ameuliza, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, elimu hii tunaendelea kuitoa kwa awamu na nina uhakika kwamba Mkoa wa Katavi nako tutawafikia. Bahati nzuri nami nimefika katika ile hospitali, nimeliona hilo jengo la mama na mtoto liko katika hali ambayo siyo nzuri sana. Kama nilivyosema katika jibu letu la msingi, tunaendelea kuboresha miundombinu ya vituo vyetu vya kutolea huduma, hususan Hospitali zetu za Rufaa za Mikoa na kuzipatia vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke msisitizo vilevile, pamoja na hii elimu ambayo tuna upatikanaji wa vifaa, kuna utaalam wa gharama nafuu ambao tumeendelea kuwajengea uwezo wataalam wetu wa huduma za afya na jamii kwa ujumla matumizi ya *kangaroo method*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *kangaroo method* maana yake ni nini? Ni yule mtoto njiti au yule *premature baby* mama anatakiwa akae nae atoe joto la ngozi kwa ngozi na imeonekana kwamba utaratibu huu wa *kangaroo method* umekuwa na manufaa makubwa sana katika kuhakikisha uhai wa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ujenzi wa wodi ya watoto kama nilivyosema katika jibu langu la msingi hili tutaendelea kulijenga kwa awamu na hivi ninavyoongea kwamba wataalam wetu wa Wizara wameshapita Hospitali zote ikiwa ni pamoja na hii Hospitali ya Rufaa ya Mpanda kuangalia mahitaji ya nini kinachohitajika pale na taratibu zitakapokamilika tutajenga wodi hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 45

**Kuunganisha Barabara za Mkoa wa Mbeya na Songwe kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Wilaya ya Mbeya, Mkoa wa Mbeya na Wilaya za Ileje na Songwe Mkoa wa Songwe zinaunganishwa kwa barabara za vumbi kuanzia Mbalizi kuelekea Ilembo, Iwinji hadi Ileje na Mbalizi kuelekea Mshewe.

(a) Je, ni lini Serikali itaunganisha barabara hizo kwa lami?

(b) Je, ni lini Serikali italipa fidia wananchi waliopisha upanuzi wa barabara za Mbalizi, Mshewe, Mjele hadi Mkwajuni Songwe?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara alizotaja Mheshimiwa Mbunge ni barabara za Mbalizi - Shigamba - Isongole zenye urefu wa kilometa 96.8 na barabara ya Mbalizi – Chang'ombe – Mkwajuni – Patamela – Makongolosi yenye urefu wa kilometa 117. Barabara hizo ni za Mkoa na zinahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Mbeya na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Serikali kwa sasa ni kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa na nchi jirani kwa barabara za kiwango cha lami, ambapo tayari Makao Makuu ya Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songwe yameunganishwa kwa barabara ya lami ya Mbeya hadi Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hizo, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuijenga kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Mbalizi – Chang'ombe – Mkwajuni – Patamela – Makongolosi kilometa 117, sehemu ya Mbalizi hadi Galula kilometa 56. Aidha, Serikali imekuwa ikizifanyia matengenezo mbalimbali ya barabara hizi za Mbalizi – Shigamba – Isongole kilometa 96.8 na barabara ya Mbalizi – Chang'ombe – Mkwajuni – Patamela – Makongolosi kilometa 117 kila mwaka ili ziweze kupitika na majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wananchi watakaopisha ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Mshewe – Mjele – Galula. Serikali itawalipa fidia kutokana na sheria na taratibu kabla ya kuanza ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nashukuru pia kwa majibu ya Serikali hasa kwa kutambua kuwa hizi ni barabara muhimu za kimkakati na kwa umuhimu huo huo ilikuwa ni ahadi ya kujengwa kwa kiwango cha lami, ambayo ilitolewa na Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete na pia ilikuwa ni ahadi ya Rais wetu wa sasa Mheshimiwa Dkt. John Magufuli kuwa hizi barabara zijengwe kwa lami. Kwa umuhimu huo huo katika Ziara ya Waziri pamoja na Naibu Waziri nao kwa wakati tofauti walitembelea hizi barabara na kuona umuhimu wake na sasa labda ningependa kama ilivyo kwenye swali langu la msingi, ni lini barabara ya Mbalizi – Shigamba – Isongole itajengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa umuhimu huo huo ni lini barabara ya Itewe - Mlima Nyoka - Songwe ambayo ni *by pass* itajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa maswali hayo muhimu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Njeza kwa kufuatilia maendeleo ya Jimbo lake hususan mambo ya miundombinu. Maana yake hii naiona ni *style* ya Mpwapwa hii ni Lubeleje *style*, maana kila ukikutana nae anazungumzia juu ya barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme tu kwamba barabara hii natambua kwamba ni ahadi ya Viongozi, lakini nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Mbeya Vijijini kwamba barabara hii ya Mbalizi – Shigamba – Isongole iko kwenye mpango mkakati wa Wizara kwa ajili ya kuiboresha. Kwa hiyo pindi tukipata bajeti tutafanya usanifu wa barabara hii na kuanza kuijenga katika kiwango cha lami. Vilevile kuhusu barabara hii ya Uyole – Mlima Nyoka

hadi Songwe ambayo ni *by pass* Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba usanifu ulifanyika na kupitia Jiji la Mbeya na anafahamu kwamba eneo hili ni la uzalishaji mkubwa, kuna pareto inazalishwa kwa wingi lakini kuna viazi vinazalishwa kwa wingi, kuna mazao ya mbao, hii ni barabara muhimu pia kuna mahindi yanazalishwa kwa mwaka mzima katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi leo mtaalam mwelekezi anakwenda kufanya mapitio ya barabara hii kwa sababu uko uelekeo sasa wa kupata fedha ya kuijenga barabara hii *by pass* muhimu ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nitaendelea kuku-*update,* kukupa taarifa zaidi tuone namna tunavyokwenda, lakini niseme tu kwa wananchi wa Mbeya Vijijini kwamba tumejipanga vizuri sasa kuanza kuijenga hii *by pass* kwa ajili ya huduma muhimu katika eneo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae kidogo, mliokuwa mmesimama.

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Spika ambaye ataondoka sasa hivi, kwa hiyo nalazimika kumtangaza sasa, na huyu ni Mheshimiwa Yonas Yosef Sanbe ambaye ni Balozi wa Ethiopia nchini Tanzania, yuko leo hapa kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika, karibu sana Mheshimiwa Balozi. Ameambatana na Bwana Tedros Girman Abebe, ambaye ni Afisa wa Ubalozi na pia Bwana Makamba Dahari Makamba, Afisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje. Karibu sana Bungeni na Mheshimiwa Spika, atawaona muda si mrefu kuanzia sasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale sasa aulize swali lake.

Na. 46

**Manufaa ya Msitu wa Nyera – Kipelele – Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Msitu wa Nyera – Kipelele ni miongoni mwa misitu ya asili iliyopo Wilaya ya Liwale. Serikali imekuwa ikiandaa taratibu za uvunaji wa mazao ya msitu huo.

(a) Je, taratibu hizo zitakamilika lini?

(b) Je, Serikali imepata manufaa gani kutokana na uhifadhi wa msitu huo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Msitu wa Nyera – Kipelele ni hifadhi ya msitu ulio chini ya umiliki wa usimamizi wa Serikali Kuu (Wakala wa Misitu wa Huduma Tanzania). Misitu hiyo ipo katika Wilaya ya Liwale, Mkoa wa Lindi, Msitu wa Kipelele ulitengwa kuwa hifadhi ya Serikali Kuu katika Tangazo la Serikali Na. 79 la mwaka 1956 ukiwa na eneo la hekta 98,423. Msitu huo umezungukwa na vijiji tisa, ambavyo ni Kichonda, Nyera, Kimambi, Mtawatawa, Kitogoro, Litou, Legezamwenda, Kipelele na Naujombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kuandaa uvunaji wa mazao ya msitu katika msitu huo zimekamilika mwaka 2018, baada ya kuandaliwa kwa mpango wa usimamizi wa msitu *(Management Plan)* na mpango wa uvunaji *(Harvesting Plan).* Kwa mujibu wa mpango wa usimamizi, kiasi cha hekta 59,053 katika msitu huo zina miti ya kuweza kuvunwa. Aidha, miti ya ujazo 19,970 zimepangwa kuvunwa kuanzia mwaka

2019/2010 kwa kufuata mwongozo wa uvunaji wa mazao ya misitu.

Mheshimiwa Spika, manufaa yanayopatikana kutokana na uhifadhi wa msitu huo ni makazi ya wanyamapori aina tofauti wakiwemo tembo, uboreshaji wa mifumo ya kiikolojia ikiwemo hifadhi ya hewa ya ukaa. Aidha, ni vyanzo vya maji katika Vijiji vya Mtawatawa, Kitogoro, Legeza mwendo, Kipelele na vilevile hifadhi hiyo ni chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kutokana na swali hili. Kwa sababu sasa *Harvesting Plan* imekamilika ina maana sasa Serikali inaenda kuanza kupata mapato kutokana na msitu huo. Hata hivyo, kama ilivyo watu wa baharini au ziwani, uchumi wao mwingi unategemea mali ya bahari na mali ya ziwa. Vilevile sisi tulio kwenye misitu uchumi wetu mkubwa unategemea mazao ya misitu. Sasa kwa nini Serikali mpaka leo hii ile *cess* haijapata kuongezwa kutoka asilimia tano tunayoipata kutokana na uvunaji huu wa misitu, angalau ifike asilimia 10 ili kuweza kuinua kipato cha Halmashauri tunazozunguka?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, *TFS* wamekuwa na tabia ya kutotoa ile *responsibility* kwa vijiji vyetu yaani ile *incentive*. Sio hivyo tu kuna mazao ambayo yamevunwa na wavunaji haramu ambayo yapo kwenye Halmashauri zetu kwa muda mrefu yanaendelea kuharibika. Je, Serikali haioni sasa inaweza kutoa kwenye Halmashauri husika yale mazao ambayo yamevunwa kwa haramu ili yaweze kunufaisha kwenye vijiji vyetu, kwa mfano mazao ya mbao, yanaweza kutusaidia kutengeneza *furniture* au viti, meza na madawati kwa ajili ya shule zetu na hospitali zetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia tano ya *cess* ambayo *TFS* wamekuwa wakitoa kwenye Halmashauri, iko kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 na sisi kama Wizara hatuwezi kuibadilisha na hatuwezi kuikiuka. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge kama anataka ibadilike anaweza kuanzisha mchakato huo, lakini kwa sasa maelekezo yetu ni kutoa asilimia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni kweli kwamba maeneo ya Liwale kuna mbao nyingi ambazo zilikamatwa wakati wa *Operation* Tokomeza, na mbao hizo bado kesi zake ziko Mahakamani. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mara uvunaji huu niliosema utakapoanza, tutawaelekeza *TFS* kuhakikisha kwamba wanatoa misaada kwenye shule zote ambazo ziko jirani na maeneo ya uvunaji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Profesa Norman Adamson Sigalla, Mbunge wa Makete, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Hongoli.

Na. 47

**Kupeleka Wanyamapori Wasio Wakali Hifadhi ya Kitulo**

**MHE. JORAM I. HONGOLI (K.n.y. MHE. PROF. NORMAN A. S. KING)** aliuliza:-

Ili kuboresha utalii katika Hifadhi ya Kitulo, Serikali iliahidi kupeleka wanyama wasio wakali yaani pundamilia 25, lakini mpaka sasa bado wanyama hao hawajapelekwa licha ya Serikali kuahidi kuwa itatekeleza mwezi Mei na Juni mwaka 2018.

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

(b) Je, ni lini Serikali itaongeza aina ya wanyama kama vile paa na swala?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Norman Adamson Sigalla, Mbunge wa Makete, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekwishatekeleza ahadi ya kupeleka Wanyamapori wasio wakali katika hifadhi ya Taifa ya Kitulo mnamo mwezi Oktoba, 2018 ambapo pundamilia 24 walihamishwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na kupelekwa Kitulo. Zaoezi lilifanyika mwezi Oktoba kipindi ambacho hali ya hewa ya Hifadhi ya Taifa ya Kitulo inafanana na hali ya hewa ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuongeza pundamilia wengine 26 kutoka Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kwenda Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, kufikia mwisho wa mwaka 2019/2020. Lengo ni kupandisha idadi ya pundamilia katika Hifadhi ya Kitulo kufikia 50. Pia sambamba na hilo kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2019/2020, Serikali inatarajia kupeleka katika Hifadhi ya Taifa ya Kitulo wanyamapori wengine aina ya swala pala wapatao 50 na kuro wapatao 30.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hongoli, swali la nyongeza.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nianze kuishukuru sana Serikali kwa hatua iliyochukua kuhakikisha kwamba wanapeleka wanyama hawa pundamilia na swala ili kuongeza utalii katika eneo lile la Kitulo. Hata hivyo, nina swali dogo la nyongeza tu kwamba pamoja na hao ambao wanapeleka kwa kuwa wanyama kama twiga huwa wanaweza wakachangamana na wanyama hawa ambao wametajwa pundamilia na swala. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wanyama wengine nje ya hawa swala ama twiga ili waweze kuvutia watalii kwa kuwa watalii wengi wanapenda kuona twiga katika eneo lile?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ambalo pia niulize Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba barabara angalau inayoenda kwenye ile mbuga za wanyama ile barabara ya Chimala – Matamba inakuwa katika hali nzuri muda wote ili kuweza kuvutia utalii katika eneo lile? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla, amefanya juhudi kubwa kuhamasisha Wizara kupeleka wanyama kwenye hii Hifadhi na lengo kubwa ni kujaribu kufungua Hifadhi hii ili iweze kuvutia Watalii. Pia nimpongeze kwa kweli kwa kusimama imara kuhakikisha kwamba hili zoezi linakamilika mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba twiga, swala na pala wanaweza kuishi katika mazingira ambayo yanafanana, lakini kabla ya kupeleka wanyama kwenye Hifadhi ya Kitulo, Taasisi yetu ya *TAWIRI* ilifanya utafiti na kujiridhisha kwamba wanyama hawa wanaweza kuishi katika maeneo hayo na kwamba ikolojia zinafanana. Kwa hiyo ili tuweze kupeleka Twiga nitawaagiza watu wa *TAWIRI* waweze kufanya utafiti na kuona kwamba wanyama hawa wakipelekwa katika Hifadhi ya Kitulo wanaweza kuishi na hawatakuwa na madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali lake la pili, ni kweli kwamba ili watalii waweze kufika maeneo ya utalii na kwenye maeneo ya Hifadhi, taasisi zetu zimekuwa siku zote zikitengeneza miundombinu kuruhusu watalii kuweza kufika maeneo hayo kirahisi. Maeneo ambayo tunayatengeneza ni yale ambayo kimsingi yako chini ya usimamizi wa Wizara yetu. Kwa hiyo nimhakikishie tu kwamba barabara zote ambazo ziko chini ya usimamizi wetu tutazitengeneza kuhakikisha kwamba tunahamasisha utalii katika Hifadhi ya Kitulo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mbunge wa Chwaka, sasa aulize swali lake.

Na. 48

**Hitaji la Gari Kituo cha Polisi Chwaka na Jozani**

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA** aliuliza:-

Kituo cha Polisi Chwaka na Kituo cha Polisi Jozani vina tatizo kubwa la gari la kufanyia doria na ulinzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia upatikanaji wa magari mawili kwa Vituo hivyo katika bajeti ya 2018/2019?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Chwaka na Kituo cha Polisi Jozani vipo katika Mkoa wa Kusini Unguja. Tayari Mkoa wa Kusini Unguja umeshapatiwa magari mawili aina ya *Ashock Leyland – Trooper* na *Sauvana* kwa ajili ya kusaidia utendaji kazi wa Polisi Mkoani humo ikiwemo doria.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi bado linaendelea kupokea magari mapya kupitia mkataba wa magari 777 kutoka Kampuni ya *Ashock Leyland Limited* ya India. Hivyo kutokana na hitajio kubwa la rasilimali ya magari lililopo katika mikoa yote ikiwemo Mkoa wa Kusini Unguja na Jimbo la Chwaka, Jeshi la Polisi litaendelea kugawa magari katika mikoa kwa kadri magari yatakavyopatikana na kwa kuzingatia vipaumbele ambavyo ni kiwango cha uhalifu katika maeneo husika na ukubwa wa maeneo ya doria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria, swali la nyongeza.

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Waziri amejibu vizuri. Katika Mkoa nimepata gari lakini mimi nagombania Jimboni kwangu Chwaka na Jozani nipate gari kwa sababu pana vibaka, ubakaji na wananchi wameongezeka. Kama sijapata hilo gari itakuwa matatizo katika Jimbo langu. *(Makofi)*

Swali la pili, kama sijapata hilo gari hii Baniani peke yake Bungeni sitaweza kurudi kwa mara ya pili. Kwa hiyo, naomba nipatiwe hiyo gari ili niweze kurudi na wananchi wangu wapate huduma. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache Mheshimiwa Waziri, naomba nipate gari katika Jimbo la Chwaka. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Bhagwanji kwa jinsi ambavyo amekuwa mstari wa mbele kabisa kupigania maslahi ya askari wetu kwenye Jimbo lake. Mimi ni shahidi mara kadhaa hapa nimekuwa nikijibu maswali yake na nikiona jitihada zake na hata wananchi wake, nina hakika wanaona jitihada hizo. Kwa hiyo, kwa jitihada hizo sioni kama wananchi wake watakuwa na mashaka naye na kuacha kumrudisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ombi lake, kama ambavyo nimejibu swali la msingi kwamba kwa sasa hivi tumepata magari machache ambayo tumeyagawa katika *level* ya Mikoa na gari mbili za Mkoa Kusini Unguja zimeenda kwenye Ofisi za Wilaya zote mbili. Hata hivyo, kwa kuwa gari nyingine zinakuja na kuzingatia vipaumbele ambavyo nimevieleza basi tunalichukua ombi lake na kulifanyia kazi kwa uzito unaostahili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Harufu Mbaya Kituo cha Polisi Mazizini**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Kuna harufu mbaya inayotoka kwenye chumba cha Mahabusu katika Kituo cha Polisi Mazizini Zanzibar na kuwa kero kwa Askari na wananchi wanaofika kupata huduma kituoni hapo.

Je, ni lini Serikali itakifanyia ukarabati kituo hicho ili kuondoa harufu hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bi. Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa hali ya jengo la Kituo cha Polisi Mazizini hairidhishi. Kwa kutambua hilo, Serikali ikishirikiana na wadau wa usalama inaendelea na ujenzi wa Kituo kipya cha Polisi cha kisasa katika eneo la Chukwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo hili jipya lipo katika hatua za mwisho za umaliziaji na mara ujenzi utakapokuwa umekamilika shughuli za kiusalama za Jeshi la Polisi za Kituo Kikuu cha Wilaya ya Magharibi ‘B’ katika Mkoa wa Mjini Magharibi zitahamishiwa kutoka Kituo cha Mazizini na kwenda Chukwani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali na napongeza juhudi kubwa za Serikali kwa kujenga Kituo kipya huko Chukwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Chukwani ni nyuma kidogo, Mazizini ni barabarani na ni *centre* na karibu na Shehia nyingi kama vile Shakani, Kombeni, Maungani na kadhalika. Sasa kile Kituo cha Wilaya kwa nini hiki cha Mazizini mnataka kukiua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, kwa nini msifanye taratibu kama hivyo mnavyoshirikiana na wadau kufanya kampeni ya kuboresha vyoo na vyumba vya mahabusu kwa nchi zima mkianzia na hapo Mazizini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hatutarajii kukiua Kituo cha Mazizini, kitu ambacho tunafanya ni kuhamisha kuwa Kituo cha Wilaya, kuhamishia Chukwani. Kwa hiyo Kituo cha Mazizini kitaendelea kutumika tu, tutafanya jitahada ya kukikarabati na kwa kuwa kiko barabarani kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, tunaamini kwamba kinahitajika kuendelea kutoa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, kuhusu ukarabati wa vituo vyetu kwa ujumla wake ikiwemo mahabusu, ni jambo ambalo tunakwenda nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wake kuhusu kuwatumia wadau ndiyo tumekuwa tukiufanya kazi, wako wadau ambao wamekuwa wakishirikiana nasi kwa dhamira ya kurekebisha mazingira ya Vituo vyetu vya Polisi ikiwemo mahabusu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Venance Mwamoto.

Na. 50

**Miradi Maalum ya Kuondoa Umaskini Kagera**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO (K.n.y MHE. HALIMA A. BULEMBO)** aliuliza:-

Kagera ni moja ya mikoa mitano maskini zaidi nchini kutokana na utafiti uliofanywa na Bwana Joachim De Weeidt na kuchapishwa kwenye jarida la *Journal of Development Studies* ambao unaonyesha kuwa kuna njia mbili za kuondoa umaskini Kagera ambazo ni kilimo na biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwa na miradi maalum ya kuondoa umaskini kwa watu wa Kagera ambao ndiyo mkoa pekee unaopakana na nchi nyingi zaidi za *EAC* na hivyo kuufanya kuwa Mkoa wa kimkakati kibiashara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote ya kiuchumi na kijamii inayotekelezwa na Serikali pamoja na sekta binafsi katika Mkoa wa Kagera na mikoa mingine nchini ni kwa ajili ya kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya wananchi. Pamoja na ukweli huo, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mkakati wa Serikali wa kutekeleza miradi maalum ya kuondoa umaskini katika Mkoa wa Kagera imeainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021, Mpango Mkakati wa Mpango wa Utekelezaji

wa Mpango wa Maendeleo na Mipango ya Mkoa wa Kagera kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mikakati inayoendelea kutekelezwa na kuratibiwa na Serikali katika Mkoa wa Kagera ni kama ifuatavyo:-

(i) Mkoa wa Kagera umeainisha na kutenga maeneo ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta 58,000 kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kusindika na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo (*Agro Processing Industries*), hususan viwanda vya kusindika nyama, ngozi, maziwa, asali, ndizi, miwa, kahawa, samaki na kadhalika. Aidha, hekta 17,400 kati ya hekta 58,000 zimeshapimwa na zipo tayari kwa uwekezaji.

(ii) Kukuza sekta ya viwanda, hususan viwanda vya kusindika mazao ya maliasili na kilimo. Viwanda vinavyofanya kazi ya kusindika mazao kwa sasa ni *Kagera Fish Company Ltd* na *Supreme Perch Ltd* vinavyosindika minofu ya samaki; *Kagera Sugar Company* Ltd na *Amir Hamza Company Ltd* vinavyosindika miwa na *kahawa*; na Kiwanda cha Maziwa kinachosindika *wine* ya rosella na juisi. Aidha, Kampuni ya Josam imepatiwa eneo lenye ukubwa wa hekta 500 katika Ranchi ya Kikulula na tayari limejengwa bwawa kwa ajili ya kuvuna maji pamoja na kuanza ufugaji wa ng'ombe wa maziwa wapatao mia moja hadi sasa.

(iii) Kuimarisha miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami mfano barabara ya Kyaka - Bugene (Km 59.1); barabara ya Kagoma – Lusahunga (Km 154); barabara ya Ushirombo – Lusahunga (Km 110); barabara ya Bwanga – Kalebezo (Km 67); barabara ya Nyakanazi – Kibondo (Km 50) na ujenzi umefikia asilimia 40; na barabara ya Kyamyorwa – Buzirayombo (Km 120).

(iv) Kuanzisha Kiwanda cha Kuchakata madini ya bati katika Wilaya ya Kyerwa ifikapo Juni 2021. Kampuni ya *Tanzaplus Minerals and African Top Minerals Ltd* zimeonesha nia ya kuwekeza na tayari zimeanza kuleta mashine za uchenjuaji.

(v) Kuendeleza mradi wa Uwekezaji wa Madini ya Nikeli Kabanga, katika Wilaya ya Ngara ifikapo Juni, 2021.

(vi) Kukamilisha Mradi wa *REA Phase III* katika maeneo ambayo hayajapata umeme ifikapo mwaka 2020.

(vii) Kuanzisha na kuendeleza skimu ya umwagiliaji katika eneo la Kitengule, Wilaya ya Karagwe ifikapo mwaka 2021. Ujenzi wa daraja la kuunganisha eneo la mradi na Kiwanda cha Sukari Kagera unaendelea kwa sasa. Wakulima zaidi ya 2,000 wanatarajiwa kunufaika na uwekezaji huo.

(viii) Kukamilisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa MW 80 kutoka Mto Rusumo na Kakono MW 87 katika Mto Kagera ifikapo Juni 2020.

(ix) Kuimarisha usafiri wa majini kwa kukamilisha ujenzi wa meli kubwa itakayotoa huduma ya usafiri na usafirishaji kati ya Bukoba na Mwanza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwamoto, swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kwa kuwa Mkakati wa *East African Community* ni kuhakikisha wanaondoa umaskini si kwa Kagera tu bali na mikoa mingine. Tatizo kubwa la Mkoa wa Kagera pamoja na kuwa na viwanda vingi ni barabara zao kutopitika kwa muda mrefu na kusababisha viwanda vyao visifikiwe kwa wakati na kusafirisha mali nje. Je, Serikali ina mkakati gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kuna baadhi ya mikoa ambayo pia imekuwa ina tatizo ambalo linafanana ikiwepo Mkoa wa Iringa tuna uwanja wa ndege, pamoja na kuwa kuna mazao mengi ambayo yanatoka na

yanafika nchi za Afrika Mashariki lakini Serikali imekuwa ikisuasua katika ujenzi wa uwanja ule.

Ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba ule uwanja wa ndege unamalizika ili tupate na watalii wa kutosha waweze kwenda *Ruaha National Park* kwenye Jimbo la Ismani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambako maswali ya Mheshimiwa Mwamoto yamelenga, naomba kuyajibu maswali yake mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba hapo katikati kulikuwa na changamoto ya barabara, baadhi ya barabara kwa kweli zimekuwa na hali mbaya lakini Serikali imekwishapeleka fedha na kuna tangazo la kutafuta wakandarasi kwa ajili ya kurekebisha barabara za Bukoba na maeneo mengine mbalimbali ya nchi yetu ili ziweze kupitika kupeleka mazao sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, tumekwisha tangaza tenda na kuna mkandarasi ambaye yuko tayari kwenye Uwanja wa Ndege wa Iringa, tunasubiri taratibu za mwisho za kuwalipa ili waweze kufanya ukarabati unaostahili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Suzana Chogisasi Mgonukulima, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 51

**Mradi wa Maji wa Ibofye**

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA** aliuliza:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu Mradi wa Maji kutoka Ibofye kwenda Magulilwa, Kuhota, Lyamgun'we, Ifunda ambao ulipitishiwa bajeti na Bunge?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzana Chogisasi Mgonukulima, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 1982, kupitia ufadhili wa *DANIDA*, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilifanya upembuzi yakinifu wa Mradi wa Maji wa Mtitiriko *(Gravity Scheme)* utakaotumia chanzo cha maji cha Mto Mtitu ili kuweza kuhudumia vijiji 34 vilivyopo katika Kata sita za Magulilwa, Kuhota, Mseke, Ifunda, Mgama na Maboga ambazo zilikuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kabla ya kugawanyika na kuundwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo. Mradi huo ulikadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi milioni 596.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya utekelezaji wa mradi huo kuanza kuligundulika chanzo kingine cha Mto Ibofye katika Kijiji cha Ihimbo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ambacho kingeweza kutumika kwa ufanisi zaidi na kutatua tatizo la maji kwa kata hizo. Hata hivyo, usanifu wa mradi huu haukukamilika na unategemewa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Mradi huu unatarajiwa kuhudumiwa vijiji 17 na kati ya hivyo vijiji 15 vipo katika

Halmashauri ya Wilaya ya Iringa na vijiji viwili katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya maji wakati wakisubiri Mradi wa Ibofye, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa pamoja na wadau wa maendeleo ilichimba visima 53 ambavyo vimewezesha wakazi 8,200 wa kata hizo kupata huduma ya maji. Aidha, ukarabati wa visima katika Kata za Ifunda na Mgama umekamilika na tayari vinatoa huduma kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzana Mgonukulima, swali la nyongeza.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu ya Serikali, nina maswali ya nyongeza mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kutokana na majibu ya Serikali kuwa Halmashauri ya Iringa na wadau wa maendeleo walichimba visima 53, naomba kujua ni visima vingapi vimetatua matatizo ya maji kwa wananchi wa vijiji hivyo nilivyouliza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa maelezo ya Serikali Mradi wa Maji wa Ibofye utatekelezwa mwaka wa fedha 2019/2020. Mradi huu una miaka 37 umeshindwa kutekelezeka. Naomba kujua ni muujiza gani utakaotumika kwa Serikali kutekeleza mradi ndani wa mwaka mmoja? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kuhusu idadi halisi ya visima ambavyo vipo katika vijiji hivyo alivyovitaja. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge baada ya

Bunge saa saba tukutane ili tuweze kumpa kwa maandishi visima halisi katika vijiji anavyohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la Mradi wa Ibofye, hii ni Serikali ya Awamu ya Tano, inapoahidi inatekeleza na hata kama haijatekeleza inakuwa na sababu ya msingi na maalum katika suala zima la utekelezaji. Ssisi ni Wizara ya Maji siyo Wizara ya Ukame, tutahakikisha Mradi huu wa Ibofye tunautekeleza ili wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

**NAIBU SPIKA:** Naona tumepata majibu ya ni muujiza gani, huo ndiyo muujiza wenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho ni la Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Hitaji la Nishati ya Umeme Jimbo la Mikumi**

**MHE. JOSEPH L. HAULE** aliuliza:-

Jimbo la Mikumi linaitwa Jimbo la giza kutokana na kata zake nyingi kutokuwa na umeme, kama Kata ya Ulaya, Zombo, Tindiga, Mhenda, Kilangali, Vidunda na kadhalika:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Jimbo hilo ambalo limebarikiwa kuwa na Mbuga za Wanyama na vivutio kadha wa kadha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mikumi lina vijiji 57, kati ya vijiji hivyo vijiji 16 vina umeme. Katika utekelezaji wa azma ya Serikali ya kufikisha umeme katika vijiji vyote nchini ifikapo mwaka 2021, vijiji 41 ambavyo havijafikiwa na umeme katika Jimbo la Mikumi vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa REA Awamu ya Tatu unaoendelea sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme katika Jimbo la Mikumi kwa sasa inafanyika katika vijiji nane vya Ihombwe, Kwalukwambe, Vidunda, Madizini, Zombolumbo, Malui, Udung'hu na Kigunga. Kazi za kupeleka umeme katika vijiji hivyo vinahusisha ujenzi wa kilomita 26 za njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 na kilometa 32 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4, ufungaji wa transfoma 16 na kuunganishia umeme wateja wa awali 533 na gharama za mradi ni shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa *REA* Awamu ya Tatu, mzunguko wa kwanza katika Jimbo la Mikumi pamoja na Mkoa wa Morogoro kwa ujumla ulianza mwezi Julai, 2018 ambapo Kampuni ya *State Grid Electical and Technical Works Ltd.* inatarajia kukamilisha kazi hizo mwezi Juni, 2019. Vijiji vilivyobaki 33 vitapatiwa umeme katika mzunguko wa pili wa Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu unaotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2020/2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Haule, swali la nyongeza

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Kwanza nioneshe masikitiko yangu makubwa sana kwa Jimbo lenye chanzo kikubwa cha umeme kama Kidatu lakini pia ni Jimbo la Utalii kuwa na vijiji kama 57 lakini ni 16 tu ambavyo vina umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, ni kweli mkandarasi kweli *State Grid* yuko kule *site* na kwa muda mrefu ameonekana kuchimba mashimo na sasa hivi hajaonekana kwa sababu anasema kwamba ana tatizo la

nguzo. Je, ni lini maeneo haya ya Zombo, Ulaya, Muhenda, Tindiga, Vidunda, Uleling'ombe, Kilangali na Mwinsagala wataweza kupata umeme? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali na mbili, kwa kuwa kuna maeneo ambayo kuna nguzo na umeme umepita lakini maeneo hayo hayajapata umeme, mfano maeneo ya Ruaha Darajani, Kikwalaza, Mshimba lakini pia maeneo ya Ruhembe na Tambuka Reli, Kipekenya na maeneo ya Malolo. Je, ni lini serikali itawapatia umeme wananchi wa maeneo hayo kama ilivyofanya kwenye maeneo ya Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Mbunge kwenye swali lake la kwanza la nyongeza amejielekezea katika kazi zinazoendelea katika Jimbo lake kupitia mkandarasi *State.* Amesema mkandarasi alionyesha kuna tatizo la nguzo, naomba nimtaarifu mkandarasi huyo nimewasiliana naye asubuhi hii na kwamba kweli kulikuwa na tatizo la nguzo. Lakini Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu na uongozi wa Mkoa wa Iringa ulifanya kikao kikubwa na ulifikia makubaliano na sasa wakandarasi wote nchi nzima wanapata nguzo na ninavyozungumza takribani nguzo 4000 zimeshaenda katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika eneo la Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kwamba mkandarasi yupo katika Mkoa wa Morogoro na anaendelea na kazi na Mheshimiwa Mbunge amekiri na kwa kweli kwa kuwa nguzo zimeruhusiwa na hivi asubuhi nilivyokuwa nawasiliana naye, mkandarasi ametoa taarifa ya kwamba anaendelea kwenye maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge umeyataja kwenye swali lako la msingi na kwamba pia alikuwa ameagiza mita takribani 3000 na karibu zinafika mwezi wa pili Dar es Salaam. Kwa hiyo, kazi ya uunganishaji katika vijiji hivyo itaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili umejielekeza katika maeneo ambapo kuna miundombinu ya umeme kwa mfano Ruaha Darajani, lakini wananchi hawajaunganishiwa umeme. Nataka nikutaarifu Mheshimiwa Mbunge Serikali yetu ya Awamu ya Tano imekuja na mradi mwingine wa ujazilizi awamu ya pili ambao utaanza Machi, 2019 kwa gharama ya shilingi bilioni 197 na wafadhili wa Norway, Sweden na Serikali ya Ufaransa pamoja na Serikali ya Tanzania na mradi huu unaanza Machi kwa mikoa yote 26.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nitoe wito kwa *TANESCO* na *REA* kubainisha vitongoji zaidi ya 1000 na vijiji ambavyo vimepitiwa na miundombinu ya umeme mkubwa lakini hawajaunganishiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nichukue fursa hii pia kutoa wito kwa wananchi wote ambao miradi imekamilika ya *Densification* Awamu ya Kwanza ya Mradi wa *BTIP* Iringa – Shinyanga na mradi wa Makambako – Songea kulipia shilingi 27,000 na kuunganishwa umeme. Kwa sababu taarifa ambazo tunazo inaonekana wananchi wa maeneo hayo wengi bado hawajalipia na miradi ile inakaribia kukamilika. Kwa hiyo, nitoe wito walipie mapema ili kuepuka gharama wakati miradi itakapokabidhiwa *TANESCO.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa January Makamba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali wakati tunajibu swali la Mheshimiwa Saada Salim Mkuya na katika maelezo yetu ulionesha kuhitaji ufafanuzi wa ziada na ukasema kwamba tutampa maelezo zaidi Mheshimiwa Mkuya. Lakini kwa sababu masuala ya Muungano ni muhimu na yana unyeti tulidhani kwamba majibu hayo pia yawe ya umma na sio ya kwetu tu na Saada Mkuya kwa sababu ya kutoa ufasaha na uhakika kwenye masuala nyeti yanayohusu umoja wa kitaifa. Kwa hiyo niseme mambo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, hakuna mtu yoyote mtanzania atakayepata kazi au kukosa kazi kwenye taasisi ya Muungano kwa sababu anatoka upande mmoja au mwingine, hilo ni la msingi. Hatutaki kuwe na utata kwamba kutakuwa na upendeleo katika kupata kazi kutokana na mtu mahali anatoka, kwa hiyo hilo la msingi. Lakini uamuzi ulifanyika kwamba kuwe na mgawanyo *(quota)* wa taasisi za muungano kwa nafasi za kazi za utaalam kwa sababu za kihistoria kwamba Wazanzibar wamekuwa wachache katika taasisi za Muungano. Kwa hiyo, ukafanyika uamuzi wa makusudi kabisa ili kuwe na uwiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya uamuzi huo lazima zifanyike taratibu za kuhakikisha kwamba malengo hayo yanafikiwa na taratibu hizo ni pamoja na kuanzisha ofisi ya Tume ya Ajira kule Zanzibar, kufanya usaili kule Zanzibar na hata katika matangazo ya ajira hapa chini kuandika kwamba Watanzania wanaotoka Zanzibar wanahimizwa kuomba nafasi hizi na hilo ni jambo la kawaida katika matangazo ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, kupata takwimu ili tujue hasa kwamba kweli tumefikia malengo. Sasa namna ya kupata takwimu, zipo mara mbili, wakati watu wanaomba kazi au baada ya kuwa kazi zimeshatolewa na kufanya *survey.* Sasa hili jambo la kuwaelekeza watu wajaze wanapotoka ili tuweze kujua ni kweli lina ukakasi wake lakini kutokana na umuhimu wa kutaka kujua hilo na sisi tunasema kwamba unapojaza mahali unapotoka haikunyimi nafasi ya kupewa hiyo ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba Wazanzibar pia wapo wengi wanapata fursa katika taasisi hata ambazo sio za Muungano kwa sababu kwenye nafasi za ajira kwenye Wizara na Taasisi zisizo za Muungano Wazanzibar kwa sababu ni Watanzania wana haki ya kupata kazi hizo na wapo wanafanya kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tulitaka tuliweke hilo sahihi na tunaendelea kushirikiana na wenzetu katika

Taasisi za Wizara mbalimbali kuhakikisha kwamba kwanza tunapata kumbukumbu zitakazotuwezesha kupata uhakika kwamba tumefikia lengo ambalo tumejiwekea la kuwa na *quota* ya asilimia 79 kwa asilimia 21. Kwa hiyo, nilitaka niliweke hilo wazi na lisibaki lisiwe la utata wowote kwa sababu ni jambo muhimu na nyeti kwa umoja wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nitaleta kwenu matangazo yaliyotufikia hapa mezani asubuhi hii. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 11 wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kutoka *The Bright Future Foundation* wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Aisha Msantu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni tisa wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni wapiga kura wake kutoka Vwawa Mkoani Mbeya wakiongozwa na Ndugu Nsanjigwa Mwakapalila.

**WABUNGE FULANI:** *(Hapa walizungumza bila kufuata utaratibu).*

**NAIBU SPIKA:** Haya, wageni tisa wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ambaye ni mpiga kura wake anaitwa Nsanjigwa Mwakapalila, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa naye ni Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni Madiwani kutoka Jimboni kwake na mmoja anatoka Kata ya Ruge ambaye ni Mheshimiwa Adrian Kabushoke, yupo pia Diwani Kata ya Nyakakika ambaye ni Mheshimiwa Valency Kasumuni, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye ni Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na hawa ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Stephen Ngatunga na Ndugu Frank Kamugisha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 40 wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje ambao ni walimu wa Shule ya Sekondari Mpwapwa ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Shule Mwalimu Nestory Sanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Susan Kiwanga ambao ni wapiga kura wake kutoka Mkoani Morogoro na hawa ni Ndugu Khafidhi Mtongole na Ndugu Amosi Ntenze, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Joram Hongoli ambaye ni mdogo wake kutoka Mkoani Njombe na huyu ni Ndugu Naiman Hongoli, karibu sana. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Amina Nassor Makilagi ambaye ni mdogo wake kutoka Babati Mkoani Manyara na huyu ni Ndugu Happy Makilagi, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 30 na walimu watano kutoka *Black School of Linguistic and Literature* ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Karibuni sana, Waheshimiwa Wabunge hawa ndio wageni tulionao siku ya leo, tutaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chegeni.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa sambamba na kifungu cha 46.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mifugo na Uvuvi wakati akitoa ufafanuzi mzuri wa shughuli ambazo Wizara yake inazifanya na maamuzi ambayo anayafanya kwa ajili ya kuhusianana mambo ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea *message* na simu nyingi kutoka kwa wananchi walioko huko na wengi walitaka kujua zaidi kuhusu dhamira safi ya Serikali na hasa kutokana na jinsi ambavyo zoezi zima la *operation* ya uvuvi haramu lilivyokuwa linakiuka sheria na taratibu nyingi na kupelekea wananchi wengi ambao waliumizwa kwa kupigwa, wakanyang'anywa mali zao na wengi wameachwa wakiwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba ameanza kuruhusu baadhi ya vitu ambavyo tulivikataa wakati ule kwamba vilikuwa nje ya utaratibu. Sasa wananchi wangependa kusikia kauli ya Serikali hasa kupitia kwa Mheshimiwa Waziri kwamba wale ambao wamepata madhara wakiwemo wananchi wa Jimbo la Busega ambao cha ajabu kabisa kuna binti ambaye alipigwa, akavuliwa nguo na akanyanyaswa. Mheshimiwa Waziri nilimtumia zile picha na hakuchukua hatua mpaka leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unyanyasaji kama huu ambao umekuwa ukitokea imekuwa ni kero kubwa sana na kudhalilisha Watanzania. Sasa nataka kujua hawa wananchi ambao wameonewa, wamenyang'anywa mali zao, zana za uvuvi wametiwa umaskini, ni nini kauli ya Serikali au tamko la Waziri kwamba wananchi hawa watafidiwa namna gani? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(7) inataka mwongozo uzungumzie jambo lililotokea mapema Bungeni moja.

La pili, Mheshimiwa Mbunge hajahitaji mwongozo kutoka kwangu lakini amehitaji kauli ya Serikali kuhusu jambo lake. Kwa hiyo, kwenye jambo hili kwanza kiti hakina mwongozo wowote.

La pili, kuhusu huyo binti ambaye amepata madhara na kwa sababu limesemwa hapa ndani, binti aende polisi, vyombo vya dola vichukue mkondo wake. Kwa sababu haiwezekani binti adhalilishwe, apigwe na aumizwe kesi ielekee Mifugo na Uvuvi. Kama wao ndio waliofanya, wao ndio wachukuliwe hatua lakini binti aelekee polisi kwa sababu watu wa mifugo na uvuvi hilo sio eneo lao na sisi tungependa kufahamu huyo binti hatua gani zimechukuliwa kwa huyo binti ambaye amenyanyaswa, amepigwa na amedhalilishwa kwa kuvuliwa nguo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa sababu limezungumzwa hapa Bungeni tungependa kufahamu hapa ndani na mleta taarifa hizi naamini kwa sababu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi yupo hapa, niagize taarifa Mheshimiwa Chegeni apatiwe Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aje atueleze hapa ndani binti huyo hatua gani zimechukuliwa kwa sababu limezungumzwa hapa Bungeni na Bunge sio chombo kinachoweza kufanya huo uchunguzi, vyombo vikatueleze kama huo udhalilishaji ulikuwepo, binti kapigwa na kadhalilishwa. Tusingependa kusikia kesi kama hizo zikiletwa hapa ndani wakati vyombo vipo halafu kama havifanyi kazi ndio tupewe sisi sasa taarifa ili tuvichukulie hatua na sisi kama Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nadhani huo utakuwa ni mwongozo wa mwisho tuendelee na ratiba iliyopo mbele yetu. Katibu!

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN BRAMBAT – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**HOJA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) NA HOJA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Nanghenjwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa taarifa yangu naomba tuangalie katika taarifa hii kubwa ukurasa wa 73 kuna masahihisho kidogo. Kifungu 3.3.1 kwenye ukurasa wa 73 kimeanzia pale juu; Na kwa kuwa uhakiki huo umethibitisha kutokuwepo kwa tofauti ya shilingi trilioni 1.5 kati ya makusanyo na badala ya mapato inakuwa na fedha zilizotolewa. Naomba isomeke hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani kwa kupata nafasi hii ya kuwasilisha taarifa ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya jumla, utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2018 na kuliomba Bunge lako tukufu liipokee na kuijadili inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2018 *PAC* ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kuhusu ukaguzi wa hesabu za Serikali

Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhtasari wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, kifungu 1.2; Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za jumla ya mafungu ya Serikali Kuu 34 na yale ya mashirika ya umma 38. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu 1.2.1 utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali kipindi kilichopitwa na kupitishwa na Bunge kuwa Maazimio ya Bunge; maazimio sita kati ya maazimio 10 ambayo ni sawa na asilimia 60 yalikuwa yametekelezwa kikamilifu au yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, maazimio manne ambayo ni sawa na asilimia 40 yalikuwa hayajatekelezwa hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia maazimio matatu kati ya hayo manne ambayo hayakutekelezwa:-

(a) Kutokamilika uchunguzi wa ununuzi wa magari 777 yenye thamani ya dola za Marekani 29.6 uliofanywa na Jeshi la Polisi bila uwepo wa mkataba.

(b) Kutokupatiwa ufumbuzi wa kudumu suala la mkanganyiko wa mmiliki wa Benki ya Azania na taasisi ya kifedha ya *Pride Tanzania.*

(c) Kutokamilika kwa uchambuzi na kuchukua hatua husika utekelezaji wa mradi wa *DEGE ECO Village,* Kigamboni ulio chini ya *NSSF* ambao umesimama tangu mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mwaka mzima sasa tangu maazimio haya yapitishwe na Bunge. Bunge linaomba kupata ufafanuzi wa Serikali kuhusu masuala tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, uchambuzi; uchambuzi wa Kamati ulibaini masuala yafuatayo; malipo

ya posho ya resheni ya jumla ya shilingi milioni 888.5 kwa watumishi wasio askari katika Fungu la 28 la Polisi. Katika Fungu 28 - Jeshi la Polisi, taarifa za ukaguzi zimebainisha kuwa kulifanyika malipo ya jumla ya shilingi milioni 888.5 ambayo yalilipwa kama posho ya resheni *(ration)* kwa watumishi ambao si askari kinyume na taratibu za Jeshi la Polisi. Majina ya watumishi hao wanne pamoja na watu walioshirikiana nao yote yako kwenye taarifa kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Kamati katika suala hili ni kuwa pamoja na kugundulika kwa ubadhirifu huo mkubwa wa fedha za umma tangu mwaka 2016 hadi leo hii mwaka 2019 watuhumiwa bado hawajafikishwa mahakamani ili kujibu tuhuma zinazowakabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kifungu 2.12; Kamati ilifanya uchambuzi wa matokeo ya uhakiki wa tofauti ya shilingi trilioni 1.5 kati ya mapato yaliyokusanywa na Serikali ya shilingi trilioni 25.3 na fedha zilizotolewa na Hazina shilingi trilioni 23.7 kama ilivyoripotiwa tarehe 30 Juni, 2017 katika Sura ya Nne ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki huu ulipitia upya fedha zilizoidhinishwa na kutolewa katika Mfuko Mkuu *(Consolidated Fund)* kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018. Aidha, uhakiki ulifanyika ili kuthibitisha endapo fedha zilizotolewa kutoka Mfuko Mkuu zilitoka kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Sheria ya Fedha ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 24 Januari, 2019 Kamati ilifanya mahojiano ya kina na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ili kupata ufafanuzi wa kina wa uhakiki. Aidha, tarehe 25 Januari, Kamati ilifanya mahojiano na Katibu Mkuu - Wizara ya Fedha na Mipango, Maafisa wa Wizara ya Fedha, *TRA* na *BOT* ili kupata ufafanuzi wa maelezo ya ziada kwa hoja zilizokuwa zimejitokeza katika taarifa ya uhakiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hadidu za rejea za uhakiki uliofanyika pamoja na uchambuzi wa Kamati na mahojiano na wadau muhimu, naomba kulifahamisha Bunge lako tukufu matokeo ya uhakiki huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za tofauti ya shilingi trilioni 1.5 katika ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2016/2017; katika kuchunguza sababu ya tofauti ya shilingi trilioni 1.5 inayotokana na kusanyo la shilingi trilioni 25.3 na fedha zilizotolewa na Hazina kiasi cha shilingi trilioni 23.8, *CAG* alifanya uainisho kamili wa tofauti za takwimu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa Hazina uliwasilisha kwa *CAG* marekebisho ya takwimu za hesabu *(accounting adjustments)* ambazo baada ya ukokotozi na usuluhishi wa taarifa ya hesabu za mapato matumizi ya Serikali *(full reconciliation),* suala la tofauti ya shilingi trilioni 1.5 kati ya makusanyo na matumizi ya Serikali halikuwepo kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la fedha za ziada zilizotolewa zaidi ya makusanyo, jumla ya shilingi bilioni 290.13 *(over echequer release),* maelezo ya Hazina yalifafanua kuwa fedha hizo za ziada zilikuwa ni fedha zilizotumwa moja kwa moja kwenye miradi na zilizingatia Sheria ya Benki Kuu. Kamati ilibaini kuwa usuluhisho wa hesabu ulichelewa kufanyika katika masuala kama kutothibitishwa kwa kiasi cha fedha kilichopo benki, mapato ya fedha yaliyokusanywa mwaka wa fedha 2016/2017 ambayo yalihamishwa baada ya Julai, 2017, kuchelewa kurekebisha na kuhamisha hawala za Serikali zilizoiva na kutofautiana kati ya taarifa zilizomo katika ripoti ya utekelezaji wa bajeti ya robo ya mwisho iliyotumika kuandaa ripoti ya ukaguzi wa mwaka ya *CAG* na rasimu ya mwisho ya ripoti ya utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuchunguza mambo yote yanayohusu utoaji wa fedha katika Mfuko Mkuu ili kubaini iwapo kuna mambo ambayo hayakukubaliwa; katika eneo hili *CAG* aliibua masuala kadhaa ambayo Kamati

iliyachambua kwa pamoja na majibu ya Serikali, hoja katika eneo hili zilikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uhakiki mkaguzi alibaini ya kwamba uhamisho wa fedha nje ya fungu kwa kiasi cha shilingi bilioni 697.85 ulichelewa kufanyika kinyume na masharti ya kifungu cha 41(1) cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Kwa mujibu wa majibu ya Hazina ni kuwa walikubaliana na mapungufu hayo na kwamba watazingatia ushauri wa mkaguzi wa kufanya uhamisho wa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kuhusu mtawanyiko wa akaunti na ukosefu wa vielelezo vya bakaa za akaunti zinazounda Mfuko Mkuu wa Serikali; katika uhakiki wa *CAG* alibaini uwepo wa akaunti mbalimbali za Mfuko Mkuu ambazo ni za makusanyo. Hazina walifafanua kwa Kamati kuwa Serikali imeanzisha Akaunti Jumuifu ya Hazina *(TSA)* ambayo itasaidia kuondoa changamoto ya kuwepo kwa akaunti nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine katika hili eneo ni kuhusu kiasi cha shilingi bilioni 189.99 kilichotolewa katika Mfuko Mkuu bila idhini ya *CAG;* Hazina wametoa ufafanuzi kwa Kamati kuwa kati ya kiasi cha shilingi bilioni 189.99 kilichohojiwa na Mkaguzi, shilingi bilioni 171.5 zilikuwa ni marekebisho *(adjustments)* yaliyofanywa na Benki Kuu ndani ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Muamala mwingine wa shilingi bilioni 18.3 ni marekebisho yaliyofanyika ndani ya Mfuko Mkuu na kiasi kilichosalia cha shilingi bilioni 0.25 ni fedha zilizorejeshwa kwenye taasisi za Umma. Miamala hiyo miwili ya mwisho haikuwa imeambatanishwa kwa uhakiki hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uhakiki mkaguzi alionesha kuwa kuna tofauti kati ya kiasi cha shilingi bilioni 656.56 kati ya *Exchequer Issue Warrant* na *Exchequer Release Report.* Jambo hili lilijadiliwa kwa kina na Kamati ambapo sababu kubwa ya dosari hii ilitokana na mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani *(poor internal control systems).*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uhakiki *CAG* alibainisha kuwa kuna *Exchequer Issue Warrant* za kiasi cha shilingi bilioni 12.79 ambazo haziko kwenye *Exchequer Release Report* ambako kwa mujibu wa Wizara ya Fedha na Mipango fedha hizi zilifutwa na kurejeshwa Mfuko Mkuu. Hata hivyo, Mkaguzi hakuwa amepata sababu ya kujitosheleza kuwa ni kwa nini fedha hizi zilifutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kiasi kilichofutwa, kiasi cha shilingi bilioni 3.45 hazikuwa na nyaraka za kuthibitisha kufutwa. Menejimenti ya Wizara ya Fedha ilitoa ufafanuzi kuwa kati ya *Exchequer Release* za shilingi bilioni 3.45 zilizokuwa zimesalia, *Exchequer Release Warrant* za shilingi bilioni 1.135 zilikuwa zimerejeshwa hadi kufikia tarehe 25 Januari, 2019 na kubaki shilingi bilioni 2.315

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha hoja hii, ni muhimu Wizara ya Fedha na Mipango ikaangalia kwa makini suala la watumishi wa Wizara na uwezo wao wa kufanya kazi. Maboresho ya mifumo ya udhibiti wa ndani hayatafanikiwa iwapo suala la watumishi wenye uwezo halitapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha na Mipango imebeba dhamana kubwa na taswira ya nchi kuhusu utunzaji sahihi wa fedha za umma na matumizi yake. Hivyo, haitakiwi Wizara hii inyooshewe kidole kwa masuala yanayohusu uzingatiaji wa sheria na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji usiokuwa na tija uliofanywa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* Katika manunuzi ya ardhi; Taarifa ya Ukaguzi Maalum uliofanyika katika *NSSF* imebainisha udhaifu mkubwa katika suala la uwekezaji kwenye masuala ya ardhi katika miradi saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Apollo Dar es Salaam; mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 23 Septemba, 2014 kati ya *NSSF* na *Apollo Hospital Enterprises,* hadi sasa mradi huo umetumia shilingi bilioni 4.19

kutoka *NSSF.* Hata hivyo *CAG* alipotembelea mradi huo mapema mwezi Februari, 2018 alikuta mradi umetelekezwa na wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ubalozi na Biashara, Nairobi, Kenya; katika mradi huu Wizara ya Mambo ya Nje inamiliki sehemu ya ardhi Jijini Nairobi ambapo waliingia makubaliano na *NSSF* kujenga jengo la ubalozi na biashara. Katika mradi huu *NSSF* walitakiwa kutoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 77.4 na Wizara ingechangia ardhi kuwa sehemu ya mtaji wake *(land for equity).* Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 854.2 zimeshatolewa na *NSSF* katika utekelezaji wa mradi huo. Hadi Kamati inakamilisha taarifa hii hakuna shughuli zozote zinazoendelea katika mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kuzalisha Umeme Mkuranga; Taarifa ya ukaguzi ilibainisha kuwa *NSSF, TANESCO* na *TPDC* waliingia makubaliano ya kuanzisha mradi wa uzalishaji umeme huko Mkuranga, Mkoa wa Pwani. Gharama za mradi zilikadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 490, *NSSF* walinunua ekari 100 na kuchimba visima 100 vya maji katika eneo hilo; *NSSF* wametumia shilingi bilioni tatu katika mradi huo. Hata hivyo, ardhi iliyonunuliwa haijawahi kupimwa wala haina mipaka, pia hapakufanyika upembuzi yakinifu kuonesha faida za kiuchumi *(economic viabilities)* za mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba katika eneo la Kiseke na Bugarika Mkoani Mwanza; mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2008 yaani miaka 11 iliyopita ambapo *NSSF* walikubaliana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kununua viwanja 357 katika eneo la Bugarika na viwanja 299 katika eneo la Kiseke kwa gharama ya shilingi bilioni 1.89. Jumla ya shilingi bilioni 1.51 ambazo ni sawa na asilimia 80 ya gharama za mradi zimekwishalipwa. Ukaguzi umebaini kuwa *NSSF* hawajapewa viwanja vyote vya kwa mujibu wa mkataba. Aidha, baadhi ya wanavijiji wa eneo hilo hawakulipwa fidia, hivyo, wameamua kuvamia eneo hilo na kusababisha hasara kwa *NSSF.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba katika *Plot* Na. 249 Njiro, Arusha; mnamo tarehe 4 Novemba, 2010, *NSSF* waliingia mkataba wa manunizi ya ardhi wa shilingi milioni 440 ili kujenga nyumba za kisasa 34 kwa gharama ya shilingi bilioni 14.7 kwa makubaliano kwamba asilimia 30 ya thamani ya ardhi italipwa wakati wa mchakato wa awali wa ununuzi wa ardhi na asilimia 70 iliyobaki italipwa baada ya kutolewa hati ya viwanja husika. Malipo ya awali ya shilingi milioni 132 yalifanyika mwezi Novemba, 2010 na malipo ya mwisho ya shilingi milioni 308 yalifanyika tarehe 22 Machi, 2011 yaani baada ya miezi kama minne tu hivi, kinyume na makubaliano. Wakaguzi walipotembelea eneo hilo mwezi Januari, 2018 walikuta eneo lote limevamiwa na wanakijiji. Pamoja na dosari hizo, wakaguzi hawakuweza kupata nyaraka za uhamisho wa ardhi hiyo kutoka kwa muuzaji kwenda *NSSF.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *Mwandiga Transport Terminal; NSSF* walipanga kutekeleza Mradi wa Kituo cha Kimataifa cha Usafiri katika eneo la Mwandiga, Kigoma lenye ukubwa wa ekari 28 kwa gharama za shilingi bilioni 33.3. Jumla ya ekari 28 za ardhi zimepatikana kwa gharama ya shilingi bilioni 1.85. Hivyo, ekari moja ya ardhi Kigoma ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi milioni 66. Hadi tunawasilisha taarifa hii hapa Bungeni hakuna shughuli yoyote inayoendelea katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manunuzi ya Ardhi Katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi bilioni 15.8; *NSSF* walitumia jumla ya shilingi bilioni 15.8 kununua ardhi *plots* tano katika Mikoa wa Dar es Salaam na Pwani kwa gharama ya shilingi bilioni 15.8. Taarifa ya ukaguzi imebaini kuwa ardhi yote ilinunuliwa bila kufanyiwa upembuzi wa kina na wala hapakuwa na idhini ya bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati kwa miradi hiyo saba unaonesha kuwa jumla ya shilingi bilioni 27.1 ambazo ni mali za wanachama wa *NSSF* zipo hatarini kupotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutorejeshwa kwa mikopo ya matrekta ya SUMA JKT yenye thamani ya shilingi bilioni 40; hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017, SUMA JKT ilikuwa inadai madeni ya matrekta iliyokopesha yenye thamani ya shilingi bilioni 40 kwa watu mbalimbali ikiwepo..., sikilizeni, ikiwepo viongozi wa Serikali wa zamani na waliopo madarakani hadi sasa. Kamati iliwasilisha kwa Mheshimiwa Spika orodha ya wadaiwa hao ili kurahisisha mchakato wa kulipwa madeni hayo, hadi sasa madeni hayo hayajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya mikataba ya mikopo ya Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* na hali halisi ya mauzo ya nyumba kibiashara; Kamati ilimuomba *CAG* kufanya mapitio ya mikataba ya mikopo mitatu iliyokuwa imechukuliwa na *TBA* ili kubaini iwapo ina masharti hasi ndani yake na iwapo *TBA* kwa niaba ya Serikali wanapata faida stahiki kwa kuchukua mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkopo wa kwanza *TBA* ilichukua kiasi cha shilingi bilioni 25 kutoka Benki ya *CRDB* kwa malengo ya ujenzi wa nyumba 851 za bei nafuu Jijini Dar es Salaam ili ziuzwe kwa wafanyakazi wa Serikali. Kufuatia uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma, wafanyakazi waliokuwa tayari wamelipa fedha zao za kununua nyumba hizo *(down payment)* wameomba kurudishiwa fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkopo mwingine wenye changamoto ni wa shilingi bilioni 6.9 uliochukuliwa katika Benki ya *TIB* ili kuendeleza jengo la biashara lililopo Kitalu Na. 4900 Kilimani, Dodoma na Vitalu Na. 30, 31 na 33 vilivyopo Golindoi, Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spikam, Kamati imebaini masharti hasi katika mkopo huu hasa sharti kuwa *TIB* inaitoza *TBA* asilimia mbili ya kiasi cha mkopo ambacho kitakuwa *committed* lakini hakijachukuliwa. Hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017, *TBA* wametozwa jumla ya kiasi cha shilingi milioni 44.1 kama riba, kiasi ambacho kitaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Taarifa ya *CAG* kuhusu ukaguzi maalum wa ubia kati ya uendeshaji wa Mradi wa *TANCOAL* kati ya Shirika la Maendeleo *(NDC)* na Shirika la *Intra Energy Limited (IETL); NDC* waliingia ubia na Kampuni ya *Pacific Corporation East Africa Limited (PCEA)* ya Australia tarehe 3 Aprili, 2008, katika umiliki wa asilimia 30 yaani Tanzania inapata 30% na *PCEA* 70% kwenye Kampuni ya *TANCOAL Energy Limited* kwa malengo ya kuendeleza uchimbaji wa makaa ya mawe, uzalishaji na usambazaji wa umeme katika mradi wa Mhukuru na Ngaka Kusini mwa Tanzania.

Mheshimimiwa Naibu Spika, pamoja na ukaguzi maalum kukamilika tangu mwezi Machi, 2018 hadi sasa Bodi ya *NDC* ilikuwa haijapeleka kwa *CAG* majibu ya hoja za ukaguzi, jambo ambalo linaonesha kutokuwajibika ipasavyo kwa bodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi maalum, Kamati inaomba kuliarifu Bunge lako tukufu masuala yafuatayo kuhusu ubia huo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, gharama kubwa za ukodishaji magari na mitambo mgodini; *TANCOAL* ilipaswa kuwekeza kiasi cha dola za Marekani milioni 20.49 kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na kiasi cha dola za Marekani milioni 1.41 kwa ajili ya ununuzi wa magari. Hata hivyo, ukaguzi maalum umebaini kuwa kati ya mwaka 2012 hadi 2016, Kampuni imetumia dola za Marekani milioni 42.7 kwa ajili ya kukodisha mitambo na magari, badala ya kuwekeza kwenye maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutojengwa kwa barabara ya kwenda mgodini hivyo kuongeza gharama za uzalishaji; eneo la pili ni kutojengwa kwa barabara inayoelekea mgodini kwa kiasi cha dola za Marekani milioni 14.49. Kutokana na hilo, ukaguzi umebaini kuwa kati ya mwaka 2012 hadi Julai 2016, jumla ya dola za Marekani milioni 2.843 zimetumika kwa ajili ya kukodi magari kutoka mgodini hadi sehemu ya mauzo, umbali wa kilometa 40. Hivyo

kuongeza gharama za uendeshaji na kuondoa fursa ya kampuni kupata faida ambayo ndiyo chanzo cha Serikali kupata gawio.

(c) Udanganyifu katika alama za utafutaji madini *(exploration)* shilingi milioni 880.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa za fedha za *TANCOAL* kwa miaka sita kati ya mwaka 2011 hadi 2016 ilibaini kuwa gharama za utafutaji madini za shilingi bilioni 6.5 zinajumuisha kiasi cha shilingi milioni 880.7 isivyostahili.

(d) Matumizi ya shilingi milioni 940.3 na dola za Marekeni milioni 3.2 kwa shughuli zisizo za kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi maalumu ulibaini kuwa kati ya mwaka 2014/2016 *TANCOAL* walitumia jumla ya shilingi milioni 940.3 kwa shughuli zisizohusiana na uchimbaji wa madini kinyume na mkataba wa ubia. Hali kadhalika jumla ya dola za Marekani milioni 3.3 zililipwa kama gharama za shughuli za madini kwa *TANCOAL* nchini Malawi, yaani pesa zilipelekwa Malawi huko.

(e) Udanganyifu wa mchango wa kampuni kwa ajili ya jamii *(Cooperate Social Responsibility)* wa kiasi cha shilingi milioni 917.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya taarifa za fedha za *TANCOAL* kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2014 yalionesha kuwa *TANCOAL* imechangia jumla shilingi milioni 993 katika shughuli za maendeleo ya jamii, katika maeneo ya Ngaka na Songea kama sehemu ya wajibu wake kwa jamii, *SSRA* wakati ilichangia kiasi cha shilingi milioni 75 tu sawa na wastani wa shilingi milioni 15 kwa mwaka. *(Makofi)*

(f) Dosari katika umiliki wa hisa kati ya *IETL* na *NDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ubia huu rasilimali husika ya makaa ya mawe haikuzingatiwa kuwa sehemu ya mchango wa kampuni ya *NDC* kwenye ubia huo. Hivyo

kulisababisha *PCA* kuwa na hisa asilimia 70 licha ya kuchangia fedha ndogo, mtaji wa kiasi cha shilingi milioni 1.7. Aibu! *(Makofi)*

(g) Malipo yasiyo sahihi kwa hii *IETL* kama malipo ya Menejimenti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2013 hadi 2017 jumla ya shilingi bilioni 1.4 zililipwa kama ada ya Menejimenti kwenda kwa kampuni ya *Intra Energy Corporation* ya Austalia. Matumizi hayo yalioneshwa kama mkopo unaopaswa kulipwa na *TANCOAL* kinyume na mkataba wa ubia. Mkataba huo wa ubia unaendelea kuandikisha hasara kila mwaka na hakuna uhakika wa kuendelea na biashara kwa siku zijazo *(going concern).*

Kifungu 2.1.7, mikopo ya muda mrefu isiyorejeshwa katika Benki ya Maendeleo ya *TIB (Non Performing Loans)* ya jumla ya shilingi bilioni 251.89.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa *TIB* nayo pia inakabiliwa na madeni ya wadaiwa sugu ambayo ni mikopo chechefu yenye kufikia shilingi bilioni 251.8. Ni muda muafaka sasa kwa wadaiwa hawa sugu kutakiwa kurejesha makopo yao na kunusuru Benki ya *TIB* isije kufilisika au kuweka chini ya usimamizi na *BoT.*

Kifungu 2.1.8, mradi wa ubia katika ya Jeshi la Polisi na mwekezaji katika eneo la Oysterbay Dar es Salaam. Kama inavyofahamika Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania alishatoa malekezo ya kusitishwa kwa mikataba ya Jeshi la Polisi na uwekezaji katika maeneo ya ardhi ya Jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeamua kuleta suala hili Bungeni kwa kuwa limechukua muda mrefu kukamilika. Ni muhimu mchakato wa kuachana na mkataba huu ukafanyika mapema kwa mujibu wa Sheria.

Kifungu 2.1.9, kutokamilika kwa hatua za kinidhamu kwa Afisa wa Jeshi la Polisi aliyeidhinisha malipo ya shilingi 798.78 kwa mtoa huduma bila huduma kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi wa Fungu 28 - Jeshi la Polisi, kwa mwaka wa fedha mwaka 2016/2017 ilibainika kuwa Afisa wa Jeshi la Polisi aitwaye SP Emmanuel Mkilia aliidhinisha malipo ya jumla ya shilingi milioni 798.78 kwa mtoa huduma *(vendor)* bila huduma kutolewa. Tangu mwezi Machi, 2018 hadi sasa Mtumishi huyu hajachukuliwa hatua. *(Makofi)*

Kifungu 2.1.1.0, limbikizo la madeni ambalo *TPDC* inaidai *TANESCO,* Songasi na PAT. Uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi *TPDC* kwa mwaka 2016/2017 ulikuwa, *TPDC* inadai deni kubwa kwa Taasisi tatu linalofikia shilingi bilioni 358.6. Taaisis hizo ni *TANESCO,* Kampuni ya Songas na Kampuni ya *Pan African* ya Tanzania wakati huo huo *TANESCO* inadai Taasisi mbalimbali za Serikali jumla ya shilingi bilioni 86.8. Ni muhimu kukawepo na mkakati mahususi wa kulipa deni hilo mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya pili ilikwishagongwa. Kwa hiyo, sasa tukubaliane, nikupe dakika tatu umalizie unachotaka kusema, lakini kwa sababu Wabunge wanavyo vitabu vya taarifa yako, naamini wataweza kupitia na baadaye utapewa fursa ya kumaliza hoja yako. Dakika tatu.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mapendekezo. Menejimenti ya Mfuko Mkuu iboreshe mifumo ya utunzaji kumbukumbu, Wizara ya Fedha na Mipango itoe taarifa za fedha za Mfuko Mkuu ndani ya mwaka husika; Hazina ianze kuandaa taarifa ya kila fedha ya mwezi na kuipeleka kwa *CAG*, Wizara ihakikishe ina wataalam wa kutosha wenye sifa zinazotakiwa katika utunzaji wa kumbukumbu na Ofisi ya Taifa ya ukaguzi waendelee kufanya na Hazina kwa muda unaotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji usiofaa, Serikali ifanye uchunguzi wa wahusika wote katika mchakato wa ununuzi wa ardhi katika majengo ambao haukuwa na tija; mashirika hayo ya *NSSF,* Serikali na Bodi za mifuko mipya ya Hifadhi ya Jamii iliyoundwa zihakikishe masuala ya uwekezaji yanafanyika kwa kuzingatia sheria na miongozo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi maalum wa ubia *NDC* na *IETL*, Serikali ianze mapema iwezekanavyo angalau ndani ya kipindi cha miezi mitatu kufanya mapitio ya mkataba wa ubia kati ya *NBC* na *IETL*. Wakati majadiliano yakiendelea, ripoti ya ukaguzi maalum, Serikali ichukue hatua kuhakikisha mbia anarejesha fedha zote zilizokwishalipwa kinyume na Sheria, Serikali ndani ya miezi mitatu wafanye mapitio ya mikataba ya ubia ya kuandaa masharti mapya yenye tija ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madeni ambayo SUMA JKT yanadaiwa, Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini taratibu zilizotumika katika utoaji wa mikopo ya matrekta kwa watu na Taasisi mbalimbali. Serikali ichukue hatua stahiki kwa mujibu wa mikataba ya ukopeshaji matrekta kurejesha fedha za Serikali ambazo hazikukusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo chechefu, Benki ya *TIB* itoe *notice* ndani ya mwezi mmoja kwa wadaiwa wote kutaka kwanza kulipa madeni yao. Kuhusu kuchelewa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingiza taarifa yako kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, halafu Waheshimiwa Wabunge wataendelea kusoma taarifa kwenye vitabu.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Spika kwa kutusaidia katika Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishasema ripoti yangu yote iingie kwenye *Hansard*. Ahsateni sana.

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja!

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Nimeshatoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHALFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa hoja imeungwa mkono.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) KWA MWAKA 2017 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)*

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu shughuli zilizotekelezwa

kwa mwaka 2018 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2018, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilipokea na kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo yanayotolewa katika taarifa hii yanatokana na Hesabu zilizokaguliwa kama zilivyowasilishwa katika taarifa hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Umma katika Wizara za Serikali yaliyoainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa mapendekezo na Ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa majukumu hayo unatokana na taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

## 1.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017/2018, zililenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara na Mashirika ya Umma kama yalivyobainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2017. Aidha, Shughuli hizo zilikusudia kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) mwezi Januari, 2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2017 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi wa jumla ya Taasisi 122 za Serikali Kuu ikijumuisha Wizara na Idara zinazojitegemea 62, Wakala 37, Mifuko maalum 18, Sekretarieti za Mikoa 26, Taasisi nyingine 42, Vyama vya Siasa 19, Bodi za Mabonde ya Maji 13 na Balozi 34.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mashirika ya Umma, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikaguwa na kutoa taarifa ya jumla ya Mashirika ya Umma 150 kati ya 200 yaliyotakiwa kukaguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za jumla ya Mafungu ya Serikali Kuu 34 na yale ya Mashirika ya Umma 38. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya Miradi ya Maendeleo ikiwamo ya barabara, umeme, ukarabati wa shule na vyuo na uwekezaji katika Miradi ya ujenzi wa nyumba za kibiashara.

### 1.3.1 Utaratibu wa Kamati kushughulikia Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Ni muhimu Bunge lako Tukufu likafahamishwa utaratibu wa jumla wa kushughulikia Ripoti

za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kuwa zimewasilishwa hapa Bungeni kwa mujibu wa Katiba. Kamati imeamua kufafanua utaratibu huu hasa kutokana na mkanganyiko uliojitokeza hivi karibuni ambapo Bunge lilionekana kama linachelewesha kujadili Ripoti ya CAG inayohusu Hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2016/ 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 92 ya kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009[1], utaratibu wa Kamati za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma umefafanuliwa kwa kina. Kanuni hiyo inafafanua kuwa Kamati hizo za Bunge zitajadili na kuchambua taarifa binafsi (*Individual audit reports)* za taarifa za fedha za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa baada ya taarifa jumuifu za CAG kuwa zimewasilishwa Bungeni. Nukuu ya Kanuni hiyo ni kama ifuatavyo: -

**"...The Public Accounts Committee, Local Authorities Accounts Committee and Parastatal Organization Accounts Committee, shall discuss the individual reports of the Controller and Auditor General on the financial statements of the Central Government, Local Government Authorities and public and other bodies respectively, after the general report has been tabled in the National Assembly..."** Mwisho wa Kunukuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hiyo, PAC ilijadili taarifa za fedha mahsusi za ukaguzi za mafungu binafsi *(Individual financial statement)* ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma na kubaini hoja kadhaa za ukaguzi ambapo maoni, ushauri na mapendekezo yalitolewa ili kurekebisha dosari zilizobainika. Hivyo ni muhimu utaratibu huo wa kushughulikia ripoti za CAG ukafahamika ili kuepusha mkanganyiko unaoweza kujitokeza kuhusu namna Bunge linavyoshughulikia ripoti za CAG.

---

[1] Gazeti la Serikali Na. 47 lililochapishwa tarehe 06/03/2009


### 1.3.2 Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali kipindi kilichopita

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliyowasilishwa Bungeni mwezi Januari, 2018 jumla ya mapendekezo kumi ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaliridhiwa na kuwa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kipindi kilichopita, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za Maafisa Masuuli mbalimbali sambamba na uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya shughuli hiyo kwa ujumla yamebainisha kuwa maazimio 6 kati ya maazimio 10 ambayo ni sawa asilimia 60 yalikuwa yametekelezwa kikamilifu au yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, maazimio 4 ambayo ni sawa na asilimia 40 yalikuwa hayajatekelezwa kikamilifu hadi sasa. Hali ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge imefafanuliwa katika chati ifuatayo:-

**Chati Na. 1: Hali ya Utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya PAC kipindi kilichopita**



**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyofafanuliwa katika chati Namba 1 hapo juu, na kwa lengo la kulipa Bunge lako mwendelezo wa majadiliano *(Coherent discussion)* naomba kuyataja maazimio ambayo hadi sasa hayajatekelezwa kikamilifu kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

a) Kutokamilika uchunguzi wa ununuzi wa magari 777 yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 29.6** uliofanywa na Jeshi la Polisi bila ya uwepo wa mkataba;

b) Kuchelewa kurejeshwa kwa fedha ambazo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inakusanya kwa niaba ya Taasisi mbalimbali za Serikali. Suala hili limeendelea kujitokeza kwa ucheleweshaji wa urejeshaji wa fedha hizo kwa Taasisi kama TPA na Wizara ya Maliasili na Utalii;

c) Kutopatiwa ufumbuzi wa kudumu suala la mkanganyiko wa umiliki wa Benki ya Azania na Taasisi ya kifedha ya Pride Tanzania ambazo umiliki wake una dosari kubwa;

d) Kutokamilika kwa uchunguzi na kuchukua hatua kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Dege Eco Village, Kigamboni ulio chini ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) ambao umesimama kwa muda mrefu na umetumia fedha nyingi za umma hadi sasa; na

e) Urejeshaji wa madeni yote ambayo Serikali ilikuwa inadaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Japo suala hili limeshughulikiwa kwa kiasi fulani, lakini halijakamilika kutokana na kuchelewa kukamilika kwa uhakiki wa madeni hayo baada ya kuunganisha Mifuko.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge linaomba kupata ufafanuzi wa Serikali kuhusu masuala tajwa hapo juu ili kuendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

### 2.1 Maelezo ya Jumla kuhusu Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Ili kubainisha maeneo yenye matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma na kwa kuzingatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Kaguzi mahususi za Mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma, vigezo vya msingi vilitumika kuainisha maeneo hayo ikiwa ni pamoja na: -

a) Thamani ya pesa iliyotumika katika matumizi yaliyoripotiwa na kukaguliwa *(Value for money criteria);*

b) Madhumuni ya Bajeti na matumizi yaliyofanyika na iwapo vigezo vya msingi katika matumizi ya fedha za umma vilizingatiwa;

c) Kiasi cha matumizi ikilinganishwa na mahitaji halisi;

d) Matokeo ya Taarifa za Kaguzi Maalum zilizofanyika hivi karibuni;

e) Umakini katika matumizi yaliyoripotiwa na kukaguliwa;

f) Kujirudia mara kwa mara kwa hoja husika ya ukaguzi *(Frequency of reoccurrence)*;

g) Uzingatiaji wa Mamlaka halali za kuidhinisha matumizi ya fedha;

h) Uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma; na

i) Kuwepo kwa Kumbukumbu na nyaraka zinazopaswa kutunzwa kwa ushahidi wa matumizi kama zilivyohitajiwa na CAG.

## 2.2 Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma ulibainisha mambo yafuatayo: -

### 2.2.1 Malipo ya Posho ya Resheni *(Ration Allowance)* ya Jumla ya Shilingi Milioni 888.5 kwa Watumishi wasio Askari katika Fungu 28 (Polisi)

**Mheshimiwa Spika,** Katika Fungu 28, Jeshi la Polisi, taarifa za ukaguzi zimebainisha kuwa kulifanyika malipo ya Jumla ya **shilingi milioni 888.5** ambayo yalilipwa kama posho ya resheni *(Ration allowance)* kwa Watumishi ambao sio Askari kinyume na taratibu za Jeshi la Polisi.

**Mheshimiwa Spika,** Afisa Masuuli wa Fungu 28 aliifahamisha Kamati kuwa hatua za kinidhamu zimechukuliwa kwa kuwasimamisha kazi watumishi wanne wanaotuhumiwa kufanya malipo hayo. Watumishi hao ni hawa wafuatao:-

1. Bw. Frank Charles Msaki – aliyekuwa Mhasibu Mkuu Fungu 28;
2. Bi. Ida Denis Moyo – aliyekuwa Mkuu wa Kitengo cha Mishahara;
3. Bw. Damiani Aloyce Bupamba – aliyekuwa Mhasibu Kitengo cha Mishahara; na
4. Inspekta Mwita Mirambo – aliyekuwa Mhasibu Kitengo cha Mishahara

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Afisa Masuuli alifafanua kuwa, watu wengine watatu wasio watumishi wa Serikali walioshirikiana na watumishi hao wamekamatwa na kupewa dhamana wakati taratibu za kukamilisha upelelezi zikiendelea. Watu hao ni hawa wafuatao:-

1. Bw. Ibrahim Ahmed Mlilima;
2. Bw. Nassor Ahmed Mlilima; na
3. Bw. Lodrick Oswald Massawe.

**Mheshimiwa Spika,** Jalada la shauri hili lilifikishwa kwa mara ya kwanza kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai (DPP) tarehe 9 Septemba, 2016[2] na kisha kurudishwa tena kwa DPP tarehe 29 Juni, 2018[3] kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati katika suala hili ni kuwa, pamoja na kugundulika kwa ubadhirifu huo mkubwa wa fedha za umma tangu mwaka 2016 hadi leo hii mwaka 2019, watuhumiwa bado hawajafikishwa Mahakamani ili kujibu tuhuma zinazowakabili. Uchunguzi wa jambo hili umechukua muda mrefu kukamilika hivyo kuwepo kwa uwezekano wa fedha za umma kupotea bila hatua stahiki kuchukuliwa kwa wahusika.

### 2.2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusuUhakiki wa Mfuko Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa matokeo ya uhakiki wa tofauti ya **shilingi trilioni 1.5** kati ya mapato yaliyokusanywa na Serikali ya **shilingi trilioni 25.3** na fedha zilizotolewa na hazina **shilingi trilioni 23.7** kama ilivyoripotiwa tarehe 30 Juni, 2017 katika sura ya IV ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

**Mheshimiwa Spika,** Uhakiki huu ulipitia upya fedha zilizoidhinishwa na kutolewa katika Mfuko Mkuu *(Consolidated Fund)* kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018. Aidha, uhakiki huu ulifanyika ili kuthibitisha endapo fedha zilizotolewa kutoka Mfuko Mkuu zilitoka kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano[4] na Sheria ya Fedha ya mwaka 2004.

---

[2] Rejea barua Kumb. Na. CID/HQ/C.2/2/VOL.III/41.

[3] Rejea barua Kumb. Na. NPSC/C.180/3/DAR/3118/26.

[4] Rejea Ibara ya 136 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kutekeleza jukumu la uchambuzi wa taarifa hiyo kwa ufanisi, Mnamo tarehe 24 Januari, 2019, Kamati ilifanya mahojiano ya kina na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ili kupata ufafanuzi wa kina wa taarifa ya uhakiki. Aidha, tarehe 25 Januari, 2019 Kamati ilifanya mahojiano na Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Maafisa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ili kupata ufafanuzi na maelezo ya ziada kwa hoja zilizokuwa zimejitokeza katika taarifa ya uhakiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kazi kubwa iliyofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kutekeleza jukumu hili muhimu la kisheria ambalo kwa maoni ya Kamati limefungua ukurasa mpya *(Eye opener)* wa kuhakikisha Hazina ya Taifa inaendelea kuwa salama. Aidha, Kamati inatambua ushirikiano wa uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kutoa ushirikiano kwa wakaguzi ili kukamilisha kazi hii muhimu ya kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia hadidu za rejea za uhakiki uliofanyika pamoja na uchambuzi wa Kamati na mahojiano na wadau muhimu naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya uhakiki huo kama ifuatavyo: -

### 2.2.2.1 Sababu za tofauti ya Shilingi trilioni 1.5 katika Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuchunguza sababu ya tofauti ya **shilingi trilioni 1.5** inayotokana na kusanyo la **shilingi trilioni 25.3** na fedha zilizotolewa na Hazina kiasi cha **shilingi trilioni 23.8,** kama ilivyoripotiwa na CAG katika ripoti ya Hesabu za Serikali Kuu iliyoishia tarehe 30 Juni, 2017[5], CAG alifanya uwianisho kamili wa tofauti za takwimu hizo mbili.

---

[5]Rejea Ukurasa wa 34 wa Taarifa Jumuifu ya Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni 30, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Uongozi wa Hazina uliwasilisha kwa CAG marekebisho ya takwimu za hesabu *(Accounting adjustments)* [6] ambazo baada ya ukokotozi na usuluhishi wa taarifa za hesabu za mapato na matumizi ya Serikali *(Full reconciliation)*[7] suala la tofauti ya shilingi **trilioni 1.5** kati ya makusanyo na matumizi ya Serikali halikuwepo kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati CAG akihitimisha hoja yake katika ukurasa wa 41 wa Taarifa ya ukaguzi, amenukuliwa akifafanua kuhusu sababu ya tofauti hiyo ya **shilingi trilioni 1.5** iliyokuwa imejitokeza hapo awali kama ifuatavyo: -

Nanukuu **"... The difference of TZS 1.515.18 resulted from factors such as differences in information reviewed and adjustments passed by management..."** Mwisho wa Kunukuu

**Mheshimiwa Spika,** Kwa suala la fedha za ziada zilizotolewa zaidi ya makusanyo, jumla ya **shilingi bilioni 290.13** *(Over Echequer Release)*, maelezo ya Hazina yalifafanua kuwa fedha hizo za ziada (**Shilingi bilioni 290.13**) zilikuwa ni fedha zilizotumwa moja kwa moja kwenye miradi. Aidha, Hazina walifafanua kuwa utolewaji huo wa fedha zaidi ya mapato ni kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 kinachoruhusu Benki Kuu kuipatia Serikali wigo wa kutumia fedha zaidi ya mapato yaliyopatikana. Kwa mwaka 2016/2017 wigo uliokuwa umetolewa na Benki Kuu ulikuwa **shilingi bilioni 1,706.46**. Hivyo, utolewaji huo wa fedha za ziada ulikuwa ndani ya wigo wa kisheria.

---

[6] "Accounting Adjustments" Ni marekebisho ya muamala wa kibiashara ambayo hayakuwa yameingizwa kwenye taarifa ya awali ya hesabu kwa tarehe husika. Miamala hiyo hurekodiwa baadaye ikiwa ni pamoja na mapokezi ya fedha na hati za madai au malipo.

[7] " Account Reconciliation" Ni mchakato wa kufanya ulinganifu wa miamala iliyorekodiwa kwa utaratibu wa ndani ya taasisi na taarifa ya Kibenki ya mwezi kutoka chanzo cha nje kama Benki au taasisi ya kifedha ili kujiridhisha kuwa taarifa za ndani ya taasisi zinawiana na zile za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa mkanganyiko wa awali uliokuwa umejitokeza ulitokana na kutofanyika marekebisho *(Adjustments)* kwa wakati ya taarifa zinazohusiana na Mfuko Mkuu ambazo ni muhimu katika kusuluhisha hesabu. Mathalani, uhakiki ulibaini kuwa baadhi ya taarifa muhimu hazikuwa zimeunganishwa wakati wa kutoa salio la Mfuko Mkuu hivyo kuleta utofauti wa takwimu.

**Mheshimiwa Spika,** Usuluhishi wa hesabu ulichelewa kufanyika katika masuala kama kutothibitishwa kwa kiasi cha fedha kilichopo benki; mapato ya fedha yaliyokusanywa mwaka wa fedha 2016/2017 ambayo yalihamishwa baada ya julai, 2017; kuchelewa kurekebisha na kuhamisha hawala za Serikali zilizoiva na kutofautiana kati ya taarifa zilizomo katika ripoti ya utekelezaji wa bajeti ya robo ya mwisho iliyotumika kuandaa ripoti ya ukaguzi wa mwaka ya CAG na rasimu ya mwisho ya ripoti ya utekelezaji wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Ukokotozi wa mtiririko wa mapato na matumizi kutoka katika Mfuko Mkuu umefafanuliwa kwa kina katika jedwali Na. 2.1 hapa chini.

**Jedwali 2.1: Ukokotozi wa Mapato na matumizi ya Mfuko Mkuu kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 *(Computation of Receipts and Releases)***

| Aina | Kiasi (Shilingi Bilioni) | Chanzo |
|---|---|---|
| Mapato ya kodi yaliyokusanywa na TRA | 13,086.94 | Kiasi halisi kilichohamishwa kwenda kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali *(As per Bank Statement and Cash Book)* |
| Mapato mengineyo *(Other receipts)* | 1,517.33 | Kiasi halisi kilichohamishwa kwenda kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (Ushuru wa mafuta kwa REA, barabara, maji, na mfuko wa reli) |
| MAPATO YASIO YA KODI | | |
| Maduhuli *(Retention)* | 608.83 | Kiasi halisi kilichohamishwa kwenda kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali *(As per Bank Statement and Cash Book)* |
| 14 Series | 687.22 | |
| Stand Alone | 0.31 | |
| Mikopo ya Nje | 3,047.43 | Deni la Taifa |
| Mikopo ya Ndani | 5,915.90 | |
| **Jumla ya mapato kabla ya marekebisho** | **24,863.96** | |

| | | |
|---|---|---|
| Mkopo na misaada ambayo hapo awali haikuwa imejumuishwa kwenye ripoti ya CAG | 1,092.50 | Fedha za maendeleo – fedha za nje |
| **Jumla ya mapato baada ya marekebisho** | **25,956.46** | |
| Marejesho kwenda TRA | 70.94 | Taarifa za hesabu za TRA |
| Fedha kutoka vyanzo vya nje ambazo bado zilikuwa kwenye akaunti za mirad | | |
| Fedha ambazo hazikutumika zilizowekwa kwenye akaunti maalum ya amana | 8.71 | Taarifa maalum ya miradi |
| Fedha maalum zilizotolewa mwezi Julai | 93.53 | REA, mfuko wa barabara, mfuko wa maji na reli |
| **Jumla ya marekebisho** | **173.18** | |
| **Jumla ya mapato baada ya marekebisho** | **25,783.28** | |
| Exchequer issue releases | | |
| **Jumla ya fedha iliyotolewa** | **23,792.30** | |
| Rollover adjustment (TB and TB) | 697.85 | Nyaraka za uhamisho |
| Fedha za moja kwa moja kwenye miradi | 1,583.80 | |
| **Jumla ya matumizi** | **26,073.95** | |
| **Fedha iliyotolewa ya ziada** | **(290.67)** | |

**Chanzo:** ***Uchambuzi wa Kamati kutoka kwenye Taarifa ya Uhakiki ya CAG na majibu ya Hazina, Januari, 2019***

**Mheshimiwa Spika,** Kama ufafanuzi uliopo katika Jedwali 2.1 hapo juu unavyobainisha, baada ya marekebisho ya hesabu kufanyika na uhakiki kukamilika, jumla ya **shilingi bilioni 290.67** zilikuwa zimetolewa na Hazina zaidi ya mapato kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, baada ya kuzingatia ufafanuzi na marekebisho yaliyofanyika tofauti ya **shilingi trilioni 1.5** kati ya mapato na matumizi haikuwepo tena katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

#### 2.2.2.2 Utolewaji na uidhinishwaji wa fedha kutoka Mfuko Mkuu kwa miaka ya fedha 2016/2017 na 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Katika eneo hili uhakiki uliofanyika ulithibitisha kwamba malipo ya miaka ya fedha 2016/2017 na 2017/2018 yalifanywa na kuidhinishwa kutoka kwa Mfuko Mkuu kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa suala hili lilifanyika kwa kuzingatia Katiba na Sheria zilizopo, Kamati haikuwa na hoja ya ziada katika eneo hili zaidi ya kusisitiza kuwa utaratibu huu uendelee kwa manufaa ya Taifa.

#### 2.2.2.3 Ulinganifu wa mwenendo wa sasa na wa Miaka iliyopita wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kutoa idhini ya mikopo

**Mheshimiwa Spika,** Uhakiki uliofanyika katika eneo hili umebaini kuwa tangu mwaka 2011/2012 hadi mwaka 2016/2017 CAG alitoa idhini mbili za utoaji wa fedha kutoka Mfuko Mkuu kwa mwaka. Moja kwa idhini ya Rais kabla ya Bunge kupitisha Sheria ya ugawaji na ruzuku na nyingine ya mikopo kwa kiasi kilichosalia kilichopangwa baada ya kupitishwa kwa Sheria ya ugawaji.

**Mheshimiwa Spika,** CAG alifanya hitimisho kuwa, utekelezaji wa awali na wa sasa unafanana, isipokuwa katika matumizi ya awali, baadhi ya kasma hazikupangiwa bajeti kwa mujibu wa Sheria ya matumizi, kwa hiyo matumizi yake hayakuidhinishwa na Bunge. Kwa kuanzia mwaka 2006/2007 na kuendelea kasma zote zimejumuishwa katika Sheria ya matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo CAG hakubaini jambo lolote linalokinzana na kipengele hiki. Kwa msingi huo, Kamati pia haikuwa na hoja ya ziada katika eneo hili.

### 2.2.2.4 Kuchunguza mambo yote yanayohusu utoaji wa fedha katika Mfuko Mkuu ili kubainiiwapo kuna mambo ambayo hayakukubaliwa

**Mheshimiwa Spika,** Katika eneo hili CAG aliibua masuala kadhaa ambayo Kamati iliyachambua kwa pamoja na majibu ya Serikali. Hoja katika eneo hili zilikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Wakati wa uhakiki, Mkaguzi alibaini ya kwamba uhamisho wa fedha nje ya fungu kwa kiasi cha **shilingi bilioni 697.85** ulichelewa kufanyika kinyume na masharti ya Kifungu 41 (1) cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015. Kwa mujibu wa majibu ya Hazina ni kuwa walikubaliana na mapungufu hayo na kwamba watazingatia ushauri wa Mkaguzi wa kufanya uhamisho wa fedha kwa wakati. Aidha, ili kupata uthibitisho wa hoja hiyo, Kamati ilimuelekeza Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwasilisha jedwali la ufafanuzi wa malipo ya dhamana zilizoiva kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Jedwali lifuatalo namba 2.2 linaonesha malipo ya dhamana za Serikali zilizoiva *(Redemption profile)* kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

| Period | Treasury Bonds - Tsh | Treasury Bills - Tsh | Total Redemption - Tsh |
|---|---|---|---|
| July -2016 | 20,734,700,000.00 | 207,192,829,448.00 | 227,927,529,448.00 |
| August - 2016 | 108,070,000,000.00 | 443,609,870,098.00 | 551,679,870,098.00 |
| September -2016 | - | 335,373,597,144.00 | 335,373,597,144.00 |
| October - 2016 | 50,360,000,000.00 | 201,803,350,553.00 | 252,163,350,553.00 |
| November - 2016 | 66,588,200,000.00 | 297,769,098,172.00 | 364,357,298,172.00 |
| December - 2016 | 7,153,900,000.00 | 331,381,939,687.20 | 338,535,839,687.20 |
| January - 2017 | 103,447,500,000.00 | 486,041,659,746.00 | 589,489,159,746.00 |
| February - 2017 | 5,883,000,000.00 | 443,193,860,697.24 | 449,076,860,697.24 |
| March - 2017 | 117,539,300,000.00 | 431,601,072,293.00 | 549,140,372,293.00 |
| Aprili - 2017 | 11,504,900,000.00 | 293,922,894,322.00 | 305,427,794,322.00 |
| May - 2017 | 104,669,500,000.00 | 192,131,213,222.00 | 296,800,713,222.00 |
| June - 2017 | - | 355,697,991,483.25 | 355,697,991,483.00 |
| | **595,951,000,000.00** | **4,019,719,376,865.69** | **4,615,670,376,865.69** |
| | | | |
| | **BAJETI HALISI** | | **3,777,112,000,000.00** |
| | Uhamisho ndani ya Fungu *(Reallocation within)* | | **140,710,255,561.50** |
| | Uhamisho nje ya Fungu *(Reallocation inbetween)* | | **697,848,121,304.19** |

**Table. 2.2: Domestic Debt Principal Redemption Paid 2016/2017**
**Chanzo: *Wizara ya Fedha na Mipango, Januari, 2019***

Kama jedwali 2.2 linavyofafanua hapo juu, mtiririko wa malipo ya dhamana za Serikali zilizoiva na kulipwa kwa mwaka 2016/ 2017 umefafanuliwa. Hata hivyo hoja ya CAG inasisitiza Hazina kuhakikisha inafanya uhamisho wa fedha nje ya mafungu kwa wakati kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015. Aidha, Hazina lazima ihakikishe kuwa uhamisho huo unajumuishwa katika taarifa ya uhamisho wa fedha *(Statement of reallocation between votes in the year 2016/ 2017)*.

(b) Kulikuwa na hoja kuhusu mtawanyiko wa akaunti na ukosefu wa vielelezo vya bakaa za akaunti zinazounda Mfuko Mkuu wa Serikali. Katika uhakiki wa CAG, alibaini uwepo wa akaunti mbalimbali za "17 series" ambazo ni za Mfuko Mkuu zikijumuishwa na nyingine za " 13 na 14 series" ambazo ni za makusanyo. Hazina walifafanua kwa Kamati kuwa, Serikali imeanzisha Akaunti Jumuifu ya Hazina (TSA)[8] ambayo itasaidia kuondoa changamoto ya kuwepo kwa akaunti nyingi. Hivyo, maoni ya ukaguzi katika eneo hili ni kwamba endapo mfumo wa TSA utatekelezwa kwa ufanisi, changamoto zilizoibuliwa na CAG zitakuwa zimepatiwa ufumbuzi.

(c) Hoja nyingine katika eneo hili ilihusu kiasi cha **shilingi bilioni 189.99** kilichotolewa katika Mfuko Mkuu bila idhini ya CAG[9]. Hazina wametoa ufafanuzi kwa Kamati kuwa kati ya kiasi cha **shilingi bilioni 189.99** kilichohojiwa na Mkaguzi, **shilingi bilioni 171.5** zilikuwa ni marekebisho *(Adjustments)* yaliyofanywa na Benki Kuu ndani ya Mfuko Mkuu wa Serikali. Muamala mwingine wa **shilingi bilioni 18.3** ni marekebisho yaliyofanyika ndani ya Mfuko Mkuu na kiasi kilichosalia cha **shilingi bilioni 0.25** ni fedha zilizorejeshwa kwenye taasisi za umma. Miamala hiyo miwili ya mwisho haikuwa imeambatishwa kwa uhakiki hapo awali, hivyo CAG hakuwa amejiridhisha na utolewaji wa fedha hizo.

[8] Treasury Single Account (TSA).
[9] Rejea Kifungu cha 16(2)(c) cha Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001 ambacho kinamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali kuomba Kibali kwa CAG pale anapotoa fedha iliyoingia Mfuko Mkuu wa Serikali kimakosa kwa ajili ya kufanya malipo "Repayments".

Katika kujadili hoja hii ndani ya Kamati, kulitokea mjadala kuhusu tafsiri sahihi ya Sheria kwa suala la marekebisho ya ndani yanayofanyika katika Mfuko Mkuu. Uongozi wa Hazina ulikuwa na maoni kuwa kwa kuwa marekebisho yaliyofanywa na Benki Kuu ndani ya Mfuko Mkuu ni ya ndani hivyo hayakuwa yanahitaji kibali cha CAG. Baada ya mjadala CAG alitoa maoni yake ambapo pia alikiri jambo hilo ni vema likaangaliwa kwa mapana zaidi ili kupata tafsiri sahihi ya kisheria ya iwapo marekebisho ya ndani yanahitaji idhini yake au vinginevyo.

(d) Wakati wa uhakiki, Mkaguzi alionesha kuwa kuna tofauti kati ya kiasi cha **shilingi bilioni 656.56** kati ya *Exchequer Issue Warrant* na *Exchequer Release Report*. Jambo hili lilijadiliwa kwa kina na Kamati ambapo sababu kubwa ya dosari hii ilitokana na mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani *(Internal control systems)*. Aidha, CAG alikuwa na maoni kuwa, endapo Hazina itashindwa kuimarisha mifumo yake ya udhibiti, jambo hili linaweza kusababisha utolewaji wa Exchequer *Release Report* ambayo sio sahihi.

Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa kila tofauti iliyojitokeza katika *Exchequer Release Report* na kubaini kuwa nyingi zilitokana na dosari kadhaa za kimfumo.

Katika majibu yaliyotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali, amekiri mbele ya Kamati kuwa kuimarisha udhibiti wa mifumo ya ndani ni suala la kipaumbele katika Wizara ya Fedha na Mipango. Katika kutekeleza hilo Hazina kwa sasa wanaimarisha mifumo ya *Treasury Single Account*, *Centralised Budget Management System*, *Government Electronic Resource Allocation*, *Government Electronic Fund Transfers*, *Government Salaries Payment System*, *Governemt Payment Gateway* na *Governement Audit Recommendations Implementation Tracking System*. Aidha, CAG ataendelea kuhakiki utekelezaji wa suala hili katika kaguzi zijazo.

(e) Wakati wa uhakiki, CAG alibainisha kuwa kuna *Exchequer issues warrants* za kiasi cha **shilingi bilioni 12.79** ambazo hazipo kwenye *Exchequer Release Report* ambapo kwa mujibu wa

Wizara ya Fedha na Mipango fedha hizi zilifutwa na kurejeshwa Mfuko Mkuu. Hata hivyo, Mkaguzi hakuwa amepata sababu za kujitosheleza kuwa ni kwa nini fedha hizi zilifutwa. Aidha, kati ya kiasi kilichofutwa kiasi cha **shilingi bilioni 3.45** hazikuwa na nyaraka za kuthibitishwa kufutwa.

Menejimenti ya Wizara ya fedha ilitoa ufafanuzi kuwa kati ya *Exchequer release* za **shilingi bilioni 3.45** zilizokuwa zimesalia *Exchequer Release Warrant* za **shilingi bilioni 1.135** zilikuwa zimerejeshwa hadi kufikia tarehe 25 januari, 2019 na kubaki **shilingi bilioni 2.315**. Katika eneo hili, ni muhimu Hazina ikawajibika kuzitaka mamlaka za Serikali ambazo hazijaresha kiasi kilichosalia kufanya hivyo ili kuweka kumbukumbu sahihi za taarifa katika Mfuko Mkuu.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhitimisha suala la tofauti ya **shilingi trilioni 1.5** kati ya mapato ya Serikali na makusanyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 naomba kuweka kumbukumbu sahihi katika Bunge lako Tukufu, ***kuwa tofauti hiyo haikuwepo baada ya marekebisho ya hesabu kufanyika***.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii inafanya shughuli zake kwa weledi, tena kwa kutumia taarifa za kina na za uhakika. Kwa sababu hiyo, katika suala hili hakuna mahali ambapo Kamati ilibaini kuwa fedha yeyote katika Mfuko Mkuu ilikuwa imepotea. Hii inathibitishwa na maelezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama yanavyonukuliwa hapa akijibu swali la Mjumbe wa Kamati. Kurahisisha ufuatiliaji naomba kumrejea mjumbe aliyeuliza swali ambaye aliuliza:

Namnukuu: **".. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nilitaka kujua tu, CAG atueleze, kwamba hizi shilingi trilioni 1.5 ambazo hazionekani je zimeibiwa au laa?.."** Mwisho wa kunukuu**.**

**Mheshimiwa Spika,** Swali hilo lilijibiwa kwanza na Ndugu Benja Majura ambaye ni Msaidizi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Kurahisisha tena nafanya rejea maelezo yake kama ifuatavyo:

Namnukuu:...**" Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha 1.5 trilioni haijaibiwa..."**[10] Mwisho wa Kunukuu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kujibu swali hilo hilo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Prof. Mussa Juma Assad, alijibu kama ifuatavyo:

Namnukuu: **"... Mheshimiwa Mwenyekiti nafikiri swali naweza kulijibu. Kama ukisoma *report* yetu vizuri hatuzungumzii kabisa masuala ya wizi pale, tunazungumzia tofauti kati ya makusanyo na matumizi. *And then* msomaji mzuri ataona kwamba kuna *numbers* ambazo *hazireconcile*. Kwa hiyo kitu tulichokuwa tunashughulika nacho hapa, je tofauti hii imeletwa na nini? Tutapata maelezo ya kutosha kuhusu tofauti hii; na ukisoma *report* yetu utaona ile *table* inaonesha kwamba tunapata *reconciliation*, kwa hiyo hilo linajibu hilo swali..."** Mwisho wa Kunukuu.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuhitimisha hoja hii baada ya uhakiki, Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango iimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani. Aidha, ni muhimu pia ikaangalia kwa makini suala la watumishi wa Wizara na uwezo wao wa kufanya kazi kwa weledi zaidi. Maboresho ya mifumo ya udhibiti wa ndani hayatafanikiwa iwapo suala la watumishi wenye uwezo halitapewa kipaumbele.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango imebeba dhamana kubwa na taswira ya Nchi kuhusu utunzaji sahihi wa fedha za umma na matumizi yake. Hivyo haitakiwi Wizara hii inyooshewe kidole kwa masuala yanayohusu uzingatiaji wa Sheria na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ushahidi madhubuti.

---

[10] Rejea majadiliano katika taarifa rasmi za Bunge (Hansard) ya tarehe 24 Januari, 2019 Ukurasa wa 35.

### 2.2.3 Uwekezaji usiokuwa na tija Uliofanywa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) Katika Manunuzi ya Ardhi

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya ukaguzi maalum uliofanyika katika Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) imebainisha udhaifu mkubwa katika suala la uwekezaji. Ukaguzi huu maalum wa miradi ya NSSF ulilenga zaidi miradi iliyohusu ununuzi wa ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. NSSF walitekeleza miradi kadhaa ya uwekezaji ambayo kwa kiasi kikubwa haijaleta ufanisi hivyo kuashiria matumizi yasiofaa ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa miradi hiyo kama ilivyowasilishwa katika taarifa ya ukaguzi maalum wa NSSF kwa mwaka 2016/2017 na kubaini dosari ambazo zinaweza kuisababishia Serikali hasara. Miradi hiyo na ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo: -

**a) Mradi wa ujenzi wa hospitali ya Apollo, Dar es salaam**

Mkataba wa mradi huu ulisainiwa tarehe 23 Septemba, 2014 kati ya NSSF na *Apollo Hospital Enterprises Limited, Singapore*. Makubaliano ya mradi huu yalikuwa Apollo watoe vifaa na kuendesha hospitali hiyo kwa miaka kumi na tano kwa gharama ambayo ingekubaliwa na kugawanywa asilimia 50 kwa 50 kwa wabia wa mradi huo.

Hadi sasa mradi huo umetumia **shilingi bilioni 4.19**. Hata hivyo, CAG alipotembelea mradi huo mapema mwezi Februari, 2018 alikuta mradi umetelekezwa na Mkandarasi kutokana na eneo hilo kutofikika kwa urahisi sababu ya ujenzi wa mradi wa mabasi yaendayo haraka (DART) katika eneo hilo hivyo kutoruhusu magari ya watu binafsi kupita. Hadi sasa hakuna shughuli inayoendelea hivyo kuthibitisha uwekezaji usio na tija na matumizi yasiofaa ya fedha za umma.

**b) Mradi wa ujenzi wa jengo la Ubalozi na biashara Nairobi, Kenya**

Katika mradi huu, Wizara ya Mambo ya Nje inamiliki sehemu ya ardhi jijini Nairobi ambapo waliingia makubaliano na NSSF

kujenga jengo la Ubalozi na biashara. Katika mradi huu NSSF walitakiwa kutoa fedha kiasi cha [11]**shilingi bilioni 77.4** na Wizara ingechangia ardhi kama sehemu ya mtaji wake *(Land for equity)*.

Hadi sasa jumla ya **shilingi milioni 854.2** zimekwishatolewa na NSSF katika utekelezaji wa mradi huo. Hadi Kamati inakamilisha taarifa hii, hakuna shughuli zozote zinazoendelea katika mradi huo pamoja na fedha zilizokwishatumika.

### c) Mradi wa kuzalisha umeme Mkuranga *(Mkuranga power generation)*

Taarifa ya ukaguzi inabainisha kuwa, NSSF, TANESCO na TPDC waliingia makubaliano ya kuanzisha mradi wa kuzalisha umeme katika eneo la Mkuranga, Mkoa wa Pwani. Gharama za mradi huo zilikadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 490**. NSSF walinunua ardhi yenye ukubwa wa ekari 100 kwa ajili ya mradi na kuchimba visima 11 vya maji katika eneo hilo. Hadi sasa, NSSF wametumia **shilingi bilioni 3** katika mradi huo. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa ardhi iliyonunuliwa haijwahi kupimwa wala haina mipaka jambo ambalo litasababisha migogoro kwa siku zijazo. Pamoja na dosari hiyo, hapakuwepo na upembuzi yakinifu wowote kuonyesha faida za kiuchumi *(Economic viability)* za mradi huo na namna fedha za uwekezaji zitakavyorejeshwa.

### d) Mradi wa ujenzi wa nyumba katika eneo la Kiseke na Bugarika Mkoani Mwanza

Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo mwaka 2008 (miaka 11 iliyopita) ambapo NSSF walikubaliana na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kununua viwanja 357 katika eneo la Bugarika na viwanja 299 katika eneo la Kiseke kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.89**.

Hadi kufikia sasa jumla ya **shilingi bilioni 1.51** ambazo ni sawa na asilimia 80 ya gharama za mradi imekwishalipwa. Hata

---
[11] Takribani fedha za Kenya shilingi bilioni 1.05.

hivyo, ukaguzi umebaini kuwa NSSF hawajapewa viwanja vyote kwa mujibu wa mkataba hivyo kuwepo uwezekano wa kupotea kwa fedha za umma. Pamoja na dosari hiyo, Uongozi wa Kata ya Buhongwa uliwafahamisha wakaguzi kuwa baadhi ya wanavijiji wa eneo hilo hawakulipwa fidia hivyo wameamua kuvamia eneo hilo na kusababisha hasara kwa NSSF.

### e) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba katika Ploti Na. 249 Njiro Arusha

Mnamo tarehe 04 Novemba, 2010, NSSF waliingia mkataba wa manunuzi ya ardhi kwa **shilingi milioni 440** ili kujenga nyumba za kisasa 34 kwa gharama ya **shilingi bilioni 14.7**. Makubaliano ya mkataba yalifafanua kuwa, asilimia 30 ya thamani ya ardhi italipwa wakati wa mchakato wa awali wa ununuzi wa ardhi, na asilimia 70 iliyobaki italipwa baada ya kutolewa hati ya viwanja husika.

Malipo ya awali ya **shilingi milioni 132** yalifanyika mwezi Novemba, 2010 na malipo ya mwisho ya **shilingi milioni 308** yalifanyika tarehe 22 Machi, 2011. Wakaguzi walipotembelea eneo hilo mwezi Januari, 2018 walikuta eneo lote limevamiwa na wanakijiji na kujenga majengo kama nyumba za ibada na shughuli nyingine za kibinadamu.

Pamoja na dosari hizo, wakaguzi hawakuweza kupata nyaraka za uhamisho wa ardhi hiyo kutoka kwa muuzaji kwenda NSSF. Hivyo basi, hakuna uwezekano wa fedha za umma zilizotumika kununua ardhi hiyo kurejeshwa tena kwa sasa.

### f) Mradi wa Mwandiga Transport Terminal

NSSF walipanga kutekeleza mradi wa Kituo cha kimataifa cha usafiri katika eneo la Mwandiga, Kigoma lenye ukubwa wa ekari 28 kwa gharama za **shilingi bilioni 33.3**. Hadi kufikia sasa jumla ya ekari 28 za ardhi zimepatikana kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.85**. Hii ina maana kuwa ekari moja ya ardhi ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi milioni 66 Hata hivyo, hadi tunawasilisha taarifa hii hapa Bungeni, hakuna shughuli

yeyote inayoendelea katika eneo hilo pamoja na kuwa matumizi ya **shilingi bilioni 1.85** yamekwishafanyika.

**g) Manunuzi ya ardhi katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi bilioni 15.8**

NSSF walitumia jumla ya **shilingi bilioni 15.8** kununua ardhi ploti 5 katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa gharama za **shilingi bilioni 15.8**. Taarifa ya ukaguzi imebaini kuwa ardhi yote ilinunuliwa bila kufanyika kwa upembuzi wa kina wa miradi iliyotakiwa kutekelezwa na Shirika.

Kamati imebaini kuwa ardhi hiyo pia ilinunuliwa bila ya kuwepo kwa Kamati ya uwekezaji ya Shirika *(Management Investment Committee, MIC)* na haikupata idhini ya Bodi. Haikuwa hivyo tu, bali imebainika pia, ardhi hiyo haikuwa imepimwa na kufanyiwa tathmini ili kujiridhisha na thamani yake halisi ukilinganisha na bei iliyonunuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kama uchambuzi wa Kamati unavyotanabaisha hapo juu, NSSF walifanya uwekezaji ambao umelitia hasara Shirika kwa kiasi kikubwa. Miradi mingi ilikuwa inabuniwa bila kufanyika upembuzi yakinifu hivyo kuliingizia Shirika hasara.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati kwa miradi hiyo saba unaonyesha kuwa jumla ya **shilingi bilioni 27.1** ambazo ni mali za Wanachama wa NSSF zipo hatarini kupotea kwa sababu ya maamuzi ya uwekezaji usiokuwa na tija.

### 2.2.4 Kutorejeshwa kwa Mikopo ya Matrekta ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 40

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA – JKT) lilikuwa linadai madeni ya matrekta lililokopesha kwa watu mbalimbali yenye thamani ya **shilingi bilioni 40.**

**Mheshimiwa Spika,** Mikopo hii ya matrekta ilitolewa kati ya mwaka 2011 hadi 2016 kama inavyofafanuliwa katika Jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Namba 2.3: Mchanganuo wa Mikopo ya Matrekta ilitolewa na SUMA – JKT kati ya Mwaka 2011 hadi 2016**

| Maelezo | Idadi ya trekta | Mwaka wa mauzo | Kiasi "Shilingi" |
|---|---|---|---|
| Mauzo ya trekta na vifaa vyake | 1,846 | 2011 | 36,293,029,000 |
| | 268 | 2013 | 1,690,084,000 |
| | 108 | 2015 | 1,663,664,000 |
| | 80 | 2016 | 401,160,000 |
| **JUMLA** | **2,302** | | **40,047,937,000** |

***Chanzo:*** ***Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Uk. 153***

**Mheshimiwa Spika,** Kama inavyoonekana katika jedwali 2.3 hapo juu, deni ambalo SUMA JKT inadai katika mradi wa matrekta ni takribani kiasi cha **shilingi bilioni 40.0** likiwa limepungua kutoka **shilingi bilioni 49.22**[12] kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa baadhi ya wadaiwa sugu wa matrekta ya SUMA JKT ni Viongozi wa Serikali wa zamani na waliopo madarakani hadi sasa. Kamati iliwasilisha orodha ya wadaiwa hao kwako ili kurahisisha mchakato wa kulipwa kwa madeni hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kama jitihada za dhati hazitafanyika, kuna viashiria kuwa madeni hayo hayatalipwa na hivyo kuiweka SUMA – JKT katika hali ngumu ya kifedha na kiuendeshaji.

### 2.2.5 Mapitio ya Mikataba ya Mikopo ya Wakala wa majengo Tanzania (TBA) na hali halisi ya mauzo ya Nyumba za kibiashara

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 26 Oktoba, 2018, Kamati ya PAC ilikutana na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ili kujadili taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za TBA kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2017. Uchambuzi wa Kamati

[12] Rejea Taarifa ya PAC iliyowasilishwa Bungeni Mwezi Januari, 2018.

ulibaini viashiria vya masharti hasi katika mikopo iliyokuwa inachukuliwa na TBA kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kibiashara sehemu mbalimbali hapa Nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uchambuzi huo, Kamati ilimuomba CAG kufanya mapitio ya mikataba ya mikopo mitatu iliyokuwa imechukuliwa na TBA ili kubaini iwapo ina masharti hasi ndani yake na iwapo TBA kwa niaba ya Serikali wanapata faida stahiki kwa kuchukua mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya CAG kukamilisha mapitio ya mikataba ya mikopo hiyo aliwasilisha taarifa yake kwa Ofisi ya Katibu wa Bunge tarehe 18 Disemba, 2018[13]. Katika mapitio ya mikopo hiyo mitatu, mikopo miwili imebainika kuwa na dosari katika masharti na utekelezaji wake hali inayoweza kusababisha upotevu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mkopo wa kwanza TBA ilichukua kiasi cha **shilingi bilioni 25** kutoka Benki ya CRDB kwa malengo ya ujenzi wa nyumba 851 za bei nafuu jijini Dar es Salaam. Nyumba hizo zilikuwa ziuzwe kwa wafanyakazi wa Serikali. Hata hivyo, kumebainika changamoto ya uuzaji wa nyumba husika. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kufuatia uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma, wafanyakazi waliokuwa tayari wamelipa fedha za awali za kununua nyumba *(Down payment)* hizo wameomba kurudishiwa fedha zao. Hali hii itasababisha TBA kushindwa kulipa mkopo husika kama hawatafanya mabadiliko ya msingi ya utaratibu wa uuzaji wa nyumba hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Mkopo mwingine wenye changamoto ni wa **shilingi bilioni 6.9** uliochukuliwa kutoka Benki ya TIB. Mapitio ya mkopo huu yamebaini kuwa lengo la mkopo lilikuwa kuendeleza jengo la biashara lililopo kitalu Na. 4,900 Kilimani Dodoma na vitalu Na. 30,31 na 33 vilivyopo Golindoi (Simeon) Arusha.

---

[13] Rejea barua ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwenda kwa Katibu wa Bunge ya tarehe 18 Disemba, 2018 yenye Kumb. Na. AE.27/249/01/68.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini masharti hasi katika mkopo huu hasa katika sharti kuwa TIB inaitoza TBA asilimia 2 ya kiasi cha mkopo ambacho kitakuwa "committed" lakini hakijachukuliwa. Kufuatia sharti hilo hasi hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017, TBA imetozwa jumla ya kiasi cha **shilingi milioni 44.1** kama riba, kiasi ambacho kitaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na uwepo wa masharti hayo hasi.

### 2.2.6 Uchambuzi wa Taarifa ya CAG Kuhusu Ukaguzi Maalum wa Ubia katika uendeshaji wa Mradi wa TANCOAL kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na Shirika la Intra Energy Limited (IETL)

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi maalum huu ulifanyika kufuatia ombi la Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji[14]. Ukaguzi huu ulifanyika kwa kuzingatia Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 na Kanuni Na. 78 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika,** NDC waliingia ubia na Kampuni ya Pacific Corporation East Africa Limited (PCEA) ya Australia, tarehe 03 Aprili, 2008 katika umiliki wa asilimia 30 (Tanzania) kwa 70 (PCEA) kwenye Kampuni ya TANCOAL Energy Limited (TEL), kwa malengo ya kuendeleza uchimbaji wa makaa ya mawe, uzalishaji na usambazaji wa umeme katika mradi wa Mhukuru, Ngaka, Kusini mwa Tanzania. Hata hivyo, mnamo tarehe 28 Aprili, 2011 PCEA ilibadili jina na kuwa Intra Energy Corporation (IEC) Australia. Kampuni ya IEC ndiyo inamiliki hisa za Kampuni ya Intra Energy Tanzania Limited (IETL) kwa asilimia 100. Kampuni ya IETL ndiyo inasimamia shughuli za uendeshaji wa Kampuni ya TANCOAL Energy Limited (TEL).

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi huu ulilenga kubaini iwapo TANCOAL Energy Limited (Kampuni msimamizi wa ubia) ilitekeleza majukumu ya uendeshaji wa ubia huo kulingana

---

[14] Rejea barua ya Katibu Mkuu, Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya tarehe 01 Machi, 2017 kwenda kwa CAG yenye Kumb. Na. 2/CAB.211/263/01/4.

na matakwa ya mkataba. Kamati ilikutana na CAG tarehe 28 Januari, 2019 ili kuchambua na kujadili taarifa ya ukaguzi huo maalum. Aidha, kwa siku hiyo hiyo, Kamati ilikuwa imepanga kukutana na Bodi ya NDC ili kupata majibu ya hoja za ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na ukaguzi maalum kukamilika tangu mwezi Machi, 2018, hadi sasa Bodi ya NDC ilikuwa haijapeleka kwa CAG majibu ya hoja za ukaguzi, jambo ambalo linaonyesha kutowajibika ipasavyo kwa Bodi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi maalum, Kamati inaomba kuliarifu Bunge lako Tukufu masuala yafuatayo kuhusu ubia huo: -

**a) Gharama kubwa za Ukodishaji Magari na Mitambo Mgodini**
**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya uwekezaji wa mradi *(Bankable Feasibility Study)* ilibainisha kuwa mbia mwendeshaji, TANCOAL anapaswa kuwekeza kiasi cha **Dola za Marekani milioni 20.49** kwa ajili ya ununuzi wa mitambo na kiasi cha **Dola za Marekani milioni 1.41** kwa ajili ya ununuzi wa magari.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, ukaguzi maalum umebaini kuwa kati ya mwaka 2012 hadi 2016, Kampuni imetumia **Dola za Marekani milioni 42.7** kwa ajili ya kukodisha mitambo na magari, gharama ambazo ni mara mbili zaidi ya kiasi kilichotakiwa kuwekezwa kwenye ununuzi wa mitambo na magari. Jambo hili linaongeza gharama za uendeshaji na kuitia Serikali hasara.

**b) Kutojengwa kwa Barabara ya Kwenda Mgodini hivyo Kuongeza gharama za Uzalishaji**
**Mheshimiwa Spika,** Eneo la pili ambalo ukaguzi maalum umebaini kuwa linaikosesha mapato stahiki Serikali katika ubia huu ni kutojengwa kwa barabara inayoelekea mgodini kwa kiasi cha **Dola za Marekani milioni 14.49**[15]. Kutokana na kutojengwa kwa barabara hiyo, ukaguzi umebaini kuwa kati

[15] Rejea Kipengele Na. 3.3.1 na Jedwali Na. 12 vya Taarifa ya Utafiti ya Uwekezaji wa Mradi *(Bankable Feasibility Study).*

ya mwaka 2012 hadi Julai 2016, jumla ya **Dola za Marekani milioni 2.843** zimetumika kwa ajili ya kukodi magari kutoka mgodini hadi sehemu ya mauzo ya, umbali wa kilometa 40.

**Mheshimiwa Spika,** Kutojengwa kwa barabara hiyo, kumeongeza gharama za uendeshaji na kuondoa fursa ya Kampuni kupata faida ambayo ndio chanzo cha Serikali kupata gawio.

**c) Udanganyifu Katika Gharama za Utafutaji Madini *(Exploration)* shilingi milioni 880.7**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa taarifa za fedha za TANCOAL kwa miaka sita kati ya mwaka 2011 hadi 2016 ulibaini kuwa gharama za utafutaji madini za **shilingi bilioni 6.5** zinajumuisha kiasi cha **shilingi milioni 880.7** isivyostahili. Gharama hizo ziliainishwa katika taarifa za fedha za mwaka 2013 hadi 2016 isivyostahili kwani utafiti wa madini ulikuwa umekamilika tangu mwaka 2012.

**Mheshimiwa Spika,** Kuingizwa kwa gharama hizo katika taarifa za fedha za TANCOAL kuliathiri upatikanaji wa faida na kuonyesha hasara ambapo Serikali haikuweza kupokea gawio wala kukusanya kodi stahiki.

**d) Matumizi ya Shilingi Milioni 940.3 na Dola za Marekani Milioni 3.2 Kwa Shughuli zisizo za Kampuni**

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi maalum ulibaini kuwa kati ya mwaka 2014 hadi 2016, TANCOAL walitumia jumla ya **shilingi milioni 940.3** kwa shughuli zisizohusiana na uchimbaji wa madini kinyume na mkataba wa ubia. Hali kadhalika, jumla ya **Dola za Marekani milioni 3.3** zililipwa kama gharama za shughuli za madini kwa TANZCOAL nchini Malawi[16].

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi hayo tajwa ni kinyume na mkataba, na yamesababisha TANCOAL kutoripoti faida,

[16] TANZACOAL ni Kampuni Tanzu ya Intra Energy

hivyo kushindwa kutoa gawio kwa mbia, pia kutolipa kodi stahiki kwa Serikali.

**e) Udanganyifu kwa Mchango wa Kampuni kwa Jamii (CSR) wa Kiasi cha Shilingi Milioni 917.6**

**Mheshimiwa Spika,** Mapitio ya taarifa za fedha za TANCOAL kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2014 yalionyesha kuwa TANCOAL imechangia jumla ya **shilingi milioni 993** katika shughuli za maendeleo ya jamii katika maeneo ya Ngaka na Songea kama sehemu ya wajibu wake kwa jamii (CSR).

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa ni kiasi cha **shilingi milioni 75** tu (sawa na wastani wa **shilingi milioni 15** kwa mwaka) ndicho kilichotolewa na Kampuni ya TANCOAL kwa ajili hiyo, badala ya wastani wa **shilingi milioni 198** kwa mwaka. Pamoja na uwepo wa ushahidi wa nyaraka za malipo, Ndugu Boniface Saimon (Meneja wa Usalama, Afya na Mazingira) wa TANCOAL alikiri kutumika kwa kiasi cha **shilingi milioni 75** pekee. Hivyo Kampuni ya TANCOAL ilitumia kiasi cha **shilingi milioni 917.6** kwa matumizi mengineyo kwa udanganyifu kuwa inasaidia jamii ya jirani na Mgodi.

**f) Dosari Katika Umiliki wa Hisa Kati ya IETL na NDC**

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 3.2.1 cha Makubaliano ya Ubia kati ya IETL na NDC kilibainisha kuwa wabia watachangia mtaji kwa kuchangia mradi kwa uwiano wa asilimia 50 kwa 50. Aidha, Kifungu 3.2.1 kinaainisha kuwa katika hatua ya upembuzi yakinifu, PCEA na NDC watakuwa na uwiano wa hisa 70:30 ambapo PCEA na NDC wanapaswa kutoa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo rasilimali husika ya makaa ya mawe haikuzingatiwa kuwa sehemu ya mchango wa Kampuni ya NDC kwenye ubia huo. Kutozingatia thamani ya rasilimali za makaa ya mawe kama mchango wa NDC kulisababisha PCEA kuwa na hisa asilimia 70 licha ya kuchangia fedha ndogo ya mtaji wa kiasi cha **shilingi milioni 1.7** ambacho pia kwa maoni ya Kamati kiasi hicho kilikuwa

ndani ya uwezo wa NDC hivyo kukosekana mantiki ya ubia huo.

**g) Malipo Yasiyo Sahihi kwa IETL kama Malipo ya Menejimenti**

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya mwaka 2013 hadi 2017, jumla ya **shilingi bilioni 1.4** zililipwa kama Ada ya Menejimenti kwenda kwa Kampuni ya Intra Energy Corporation ya Australia. Matumizi hayo yalionyeshwa kama mkopo unaopaswa kulipwa na TANCOAL.

**Mheshimiwa Spika,** Mapitio ya maamuzi ya Bodi ya TANCOAL ya tarehe 15 Novemba, 2012 yalibaini kuwa Bodi iliamua kusiwepo na makubaliano ya huduma za usimamizi *(Management service)* na badala yake Kampuni ya IEC ilipwe gharama halisi zinazoingiwa *(Reimbursable)*. Ni kwa msingi huo, gharama za **shilingi bilioni 1.4** zililipwa kimakosa na lazima zirejeshwe TANCOAL.

**Mheshimiwa Spika,** Kama uchambuzi wa Kamati ulivyobainisha hapo juu, mkataba huo wa ubia unaendelea kuandikisha hasara kila mwaka na hakuna uhakika wa kuendelea na biashara kwa siku zijazo *(Going concern)*. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna changamoto kubwa katika mikataba yote ya ubia baina ya NDC na wabia wenza. Mikataba mingi haikufanyiwa upembuzi yakinifu wa kutosha na ina vipengele ambavyo vinasababisha hasara kwa Serikali. Lengo mahsusi la kuanzishwa NDC halitafikiwa endapo juhudi madhubuti hazitafanyika kuliunda upya Shirika hili na kupitia mikataba yake yote.

**2.2.7 Mikopo ya muda mrefu isiyorejeshwa katika Benki ya Maendeleo ya TIB *(Non Performing loans)* ya Jumla ya Shilingi bilioni 251.89**

**Mheshimiwa Spika,** Hivi karibuni, Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imekuwa ikitekeleza wajibu wake wa kuzifunga, kuweka chini ya ufilisi na kuziunganisha baadhi ya Benki hapa Nchini ambazo uendeshaji wake umekuwa na changamoto hasa kuwa na mtaji wa chini kinyume na Sheria. Miongoni mwa

Benki za Serikali zilizounganishwa ni Benki ya Twiga (Twiga Bancorp na Benki ya Wanawake, TWB) ambazo zimeunganishwa na Benki ya Posta kwa kuwa na mtaji mdogo.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Benki ya Maendeleo ya TIB nayo pia inakabiliwa na madeni ya wadaiwa sugu wasiorejesha mikopo ya Benki kwa wakati. Katika Benki ya TIB kumekuwa na ongezeko la mikopo chechefu *(Non performing loans)* hadi kufikia asilimia 33 wakati asilimia elekezi kwa mujibu wa BOT ni asilimia 5. Hii ni pamoja na ukweli kuwa hali ya mikopo chechefu katika soko kwa sasa ni wastani wa asilimia 23.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2018 mikopo chechefu ambayo Benki ya TIB ilikuwa inadai inafikia jumla ya **shilingi bilioni 251.89.** Aidha, mikopo hii ilikuwa na dhamana za thamani ya **shilingi bilioni 550.83**. Mikopo hiyo chechefu imegawanyika katika makundi makuu matatu. Mchanganuo wa mikopo hiyo ni kama unavyofafanuliwa hapa chini katika jedwali 2.4:-

**Jedwali 2.4: Mchanganuo wa Makundi makuu matatu ya mikopo chechefu katika Benki ya TIB**

| Na. | Aina ya Mkopo | Jumla ya Mkopo kwa tarehe 31 Disemba, 2018 | Thamani ya Dhamana |
|---|---|---|---|
| 1. | Mikopo isiyo safi *(Substandard loans)* | 35,357,471,478.76 | 38,399,235,356 |
| 2. | Mikopo yenye mashaka *(Doubtful loans)* | 41,144,034,644.56 | 83,624,215,503 |
| 3. | Mikopo inayohesabika hasara *(Loss loans)* | 175,395,687,890.27 | 428,808,719,974.00 |
| **4.** | **JUMLA** | **251,897,194,013.59** | **550,832,170,833.00** |

**Chanzo:** ***Taarifa ya Ukaguzi ya Mikopo Chechefu ya TIB hadi Kufikia tarehe 30 Septemba, 2018***

**Mheshimiwa Spika,** Kama jedwali 2.4 hapo juu linavyofafanua, ni dhahiri kuwa kundi la mikopo inayohesabika kama hasara *(Loss loans)* linachukua karibia asilimia 69.72 ya mikopo yote chechefu **(shilingi bilioni 175.35)**. Hizi ni fedha za umma ambazo iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa zinaweza kupotea na kuisababishia Serikali hasara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa wadaiwa sugu katika kundi hilo na kubaini kuwa mikopo mingi ilichukuliwa na watu binafsi na makampuni kwa malengo ya ujenzi wa maghala ya kuhifadhia na kuchambulia pamba, ujenzi wa hoteli, ununuzi wa matrekta, ujenzi wa viwanda vya maji na kilimo cha mazao mbalimbali. Suala la muhimu la ufuatiliaji ni kutaka kujua iwapo kweli wadaiwa hao walitekeleza malengo ya mikopo husika au ilikuwa ni dirisha la kukopa fedha kwa malengo yasiokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Hapo siku za nyuma kulikuwa na hisia kuwa watu wanaweza kukopa fedha kwenye Benki za umma bila kurejesha mikopo hiyo kwa wakati kwa kuwa hapakuwa na utaratibu madhubuti wa kukamata dhamana zao ili kufidia mikopo hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Ni muda mwafaka sasa kwa wadaiwa hawa sugu kutakiwa kurejesha mikopo yao na kunusuru Benki ya TIB isije kufilisika au kuwekwa chini ya usimamizi na BOT. Kampuni na watu binafsi wanaodaiwa wanajulikana na dhamana zao zinajulikana hivyo ni vema zoezi la kurejesha mikopo likafanyika haraka iwezekanavyo kwa kuzingatia Sheria za Nchi na mikataba husika.

### 2.2.8 Mradi wa Ubia kati ya Jeshi la Polisi na Mwekezaji katika Eneo la Osterbay, Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa uwekezaji wa Osterbay unatekelezwa chini ya dhana ya ubia *(Private Public Partnership)*. Mradi huu ni kati ya Jeshi la Polisi Tanzania na mwekezaji M/S Mara World Company ambao ulipangwa kugharimu jumla ya **Dola za Marekani milioni 700**.

**Mheshimiwa Spika,** Awamu ya kwanza ya mradi huu ilikamilika kwa asilimia 100 mwezi Oktoba, 2018. Hata hivyo, kama inavyofahamika Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikwishatoa maelekezo ya kusitishwa kwa mikataba ya Jeshi la Polisi na wawekezaji hasa katika maeneo ya ardhi ya Jeshi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilimtaka Afisa Masuuli wa Fungu 28 Jeshi la Polisi kutoa ufafanuzi wa hatua zilizokwishafikiwa ili kuachana na mkataba huu ili kuendelea kulinda ardhi muhimu ya Jeshi. Afisa Masuuli aliifahamisha Kamati kuwa kuna timu maalum imeundwa ikishirikisha wataalam kutoka katika Taasisi mbalimbali za Serikali ili kushughulikia suala hilo. Timu hiyo imepewa jukumu la kufanya tathmini ya mradi na kutakiwa kutoa mapendekezo na ushauri wa kitaalamu kwa kuzingatia ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeamua kulileta suala hili Bungeni kwa kuwa limechukua muda kukamilika. Ni muhimu mchakato wa kuachana na mkataba huo ukafanyika mapema kwa mujibu wa Sheria. Aidha, ni muhimu Serikali ikahakikisha mikataba mibovu na isiyo na maslahi mapana kwa Taifa haiingiwi tena na Jeshi la Polisi hapa nchini.

### 2.2.9 Kutokamilika kwa hatua za kinidhamu kwa Afisa wa Jeshi la Polisi aliyeidhinisha Malipo ya Shilingi Milioni 798.78 kwa Mtoa Huduma bila Huduma Kutolewa

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi ya Fungu 28 Jeshi la Polisi, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ilibainika kuwa Ofisa wa Jeshi la Polisi aitwaye SP Emmanuel Mkilia, aliidhinisha malipo ya jumla ya **shilingi milioni 798.78** kwa mtoa huduma *(vendor)* bila huduma kutolewa.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisa huyo akiwa Meneja wa mradi wa mfumo wa OMIS alipewa jukumu la kuhakikisha mzabuni wa mfumo huo analeta vifaa vya mradi kwa wakati. Hata hivyo, yeye alithibitisha kuwa vifaa husika vimeletwa na kutoa idhini ya malipo kwa mzabuni wakati kifaa hata kimoja kilikuwa hakijaletwa.

**Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyingine, Ofisa huyo alitoa maelezo ya uwongo kwa Mwajiri wake kwa madai kuwa mzabuni ametekeleza mradi kwa asilimia 90 wakati mzabuni alikuwa hajatekeleza jukumu lolote. Hivyo kwa uzembe huo ameisababishia Serikali hasara ya zaidi ya **shilingi milioni 798.78** bila ya kupata mfumo uliokuwa umekusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo ya Afisa Masuuli wa Fungu 28 katika suala hili ni kuwa, Mtuhumiwa alifunguliwa mashtaka ya kijeshi na kukutwa na hatia. Mashtaka ya Afisa huyo yamewasilishwa kwa Mamlaka yake ya nidhamu mnamo tarehe 10 Machi, 2018[17].

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya Kamati katika suala hili ni kuwa tangu mwezi Machi, 2018 hadi sasa, sio Kamati wala CAG aliyefahamishwa mwenendo wa shauri hilo. Kuchelewa kuchukua hatua kwa ubadhirifu wa wazi wa fedha za umma kama huu kunakwaza juhudi za Serikali na Bunge katika kuzuia matumizi mabaya ya fedha za umma.

### 2.2.10 Limbikizo la Madeni ambayo TPDC inaidai TANESCO, Songas na PAET

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 umebaini kuwa TPDC inadai deni kubwa kwa taasisi tatu linalofikia **shilingi bilioni 358.6**. Taasisi hizo ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Kampuni ya Songas na Kampuni ya Pan Africa Energy Tanzania (PAET). Hadi kufikia Juni 30, 2017 mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyofafanuliwa katika jedwali 2.5 lifuatalo:-

[17] Rejea barua Kumb. Na. PHQ/PF/1556/32.

**Jedwali 2.5: Mchanganuo wa deni ambalo TPDC inadai kwa Taasisi mbalimbali hadi kufikia Juni 30, 2017**

| Na. | Taasisi | Deni Inalodaiwa Kiasi (Shilingi Bilioni) |
|---|---|---|
| 1. | TANESCO | 227.4 |
| 2. | PAET | 70.7 |
| 3. | SONGAS | 60.5 |
| **4.** | **JUMLA** | **358.6** |

**Chanzo:** ***Barua ya Ukaguzi ya TPDC kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Uk. 8***

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuchunguza deni hili lililooneshwa katika jedwali 2.5, ilibainika kuwa kuna Uhusiano mkubwa kwa wadaiwa wote watatu. Maelezo ya TPDC ni kuwa TANESCO imekuwa ikilipa fedha kidogo ukilinganisha na makubaliano ya mauzo ya gesi. Aidha, TANESCO pia imekuwa ikishindwa kulipa madeni yake kwa PAET na SONGAS ambao wanaiuzia umeme hali inayosababisha Kampuni hizo mbili kushindwa kuilipa TPDC kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Madeni ambayo TANESCO inadaiwa na SONGAS na PAET hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2018 yanafikia jumla ya [18]**shilingi bilioni 400**. Ni kwa msingi huo, Kamati ilibaini kuwa jambo hili ni muhimu likapatiwa ufumbuzi mapema ili kuboresha uendeshaji wa TPDC na TANESCO. Hii inatokana na ukweli kwamba, TANESCO pia inadai madeni makubwa kutoka kwa taasisi za Serikali na watu binafsi. Hivyo kwa TANESCO kushindwa kukusanya madeni yake, kunaondoa uwezo wa Shirika hilo kulipa deni la TPDC kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa madeni ambayo TANESCO inadai umebaini kuwa hadi kufikia Desemba, 2018 taasisi za Serikali zilikuwa zinadaiwa jumla ya **shilingi bilioni 86.812.** Hivyo, ni dhahiri bila ya deni hili kulipwa itakuwa vigumu kwa

[18] Rejea ukurasa wa 8 wa barua ya ukaguzi ya TPDC kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

TANESCO kulipa deni la TPDC linaloendelea Kuongezeka. Ni muhimu kukawepo na mkakati mahsusi wa kulipa deni hili mapema iwezekanavyo.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Hesabu kwa mwaka wa fedha uanoishia tarehe 30 Juni, 2017, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati yanazingatia azma ya Bunge kuwa chombo mahsusi cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Msingi wa maoni hayo ni nia ya kuepusha matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kama kanuni za Bunge zinavyofafanua. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa kumeendelea kuwepo na maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara na Mashirika ya Umma hasa katika maeneo ya usimamizi wa mikataba na uwekezaji. Maeneo haya mawili yanahitaji usimamizi wa karibu wa Serikali na Bunge. Pamoja na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, ni muhimu ushauri na mapendekezo ya Kamati, CAG, BOT, SSRA na PPRA yakazingatiwa na Serikali ili kuondoa mianya ya upotevu wa fedha za umma katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ni muhimu Serikali ikafanyia kazi kwa wakati hoja za ukaguzi zinazokuwa zimeibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Jambo hili liende sambamba na uchukuaji wa hatua za kisheria na kinidhamu kwa wahusika wanaokuwa wametajwa kushiriki kwa namna moja

au nyingine katika ubadhirifu wa fedha za umma. Kwa kufanya hivyo, taasisi zetu za kiuwajibikaji zitaongeza kasi na ufanisi katika utendaji wake hivyo kuleta matokeo chanya katika usimamizi wa fedha za umma.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati yamejengwa kwa kuzingatia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika, matokeo yenye kuambatana na hoja husika, uwezekano wa hoja kujirudia na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kushughulikia hoja husika [19]*(Risk levels)*.

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati ni yale yanayolenga hoja zenye athari ya juu *(High risk issues)* na hivyo kuhitaji utekelezaji wa haraka ili kuondoa matumizi yasiofaa ya fedha za umma katika Taasisi za Serikali.

#### 3.3.1 Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya CAG kuhusu Uhakiki wa Mfuko Mkuu

**KWA KUWA,** CAG amekamilisha uhakiki wa Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha unaoshia Juni 30, 2017 na kutoa taarifa yake kwa Bunge;

**NA KWA KUWA,** Uhakiki huo umethibitisha kutokuwepo kwa tofauti ya **shilingi trilioni 1.5** kati ya makusanyo na mapato ya Serikali katika Mfuko Mkuu kwa mwaka wa fedha 2016/ 2017. Aidha, uhakiki huo umebainisha changamoto kadhaa katika mfumo wa usimamizi na udhibiti wa Mfuko Mkuu zinazotakiwa kufanyiwa kazi ili kuimarisha uendeshaji wa Mfuko huo;

**KWA HIYO BASI,** Ili kuimarisha usimamizi, udhibiti, usahihi wa kumbukumbu na uendeshaji wa Mfuko Mkuu, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Menejimenti ya Mfuko Mkuu, iboreshe mifumo ya utunzaji kumbukumbu. Nyaraka zote za Mfuko Mkuu

[19] Grouping of different risks according to their estimated cost of likely impact, likelihood of occurrence and countermeasures required

zihifadhiwe katika namna itakayorahisisha rejea. Aidha, vitabu vya hesabu na leja za mfuko Mkuu zihifadhiwe na kutunzwa ili kurekodi miamala yote na kuwezesha kuwianishwa na miamala ya Benki;

b) Wizara ya Fedha na Mipango itoe taarifa za Fedha za Mfuko Mkuu ndani ya mwaka husika bila kuchelewa na CAG apate fursa ya kutoa maoni yake mapema iwezekavyo;

c) Hazina ianze kuandaa taarifa ya kila fedha ya mwezi na kuipeleka kwa CAG ikionesha kwa kina fedha iliyopokelewa na kuhamishwa kutoka Mfuko Mkuu kuanzia siku ya kwanza ya kwanza ya mwaka wa fedha hadi siku ya mwisho ya mwezi husika;

d) Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe inagawa fedha katika vifungu kwa kulingana na Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 na ugawaji huo ujumuishe taarifa ya mgawanyo wa vifungu kila mwaka. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe usuluhishi unafanyika katika Mfuko Mkuu; na

e) Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Hazina waendelee kushirikiana kwa karibu katika kusimamia uendeshaji wa Mfuko Mkuu. Katika kaguzi zijazo mawanda ya ukaguzi yaongezwe ili kuhakikisha madhumuni ya uwepo wa Akaunti moja ya Hazina yanafikiwa.

### 3.3.2 Uwekezaji usiokuwa na tija Uliofanywa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) katika masuala ya Ununuzi wa Ardhi

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imebainisha dosari kubwa katika mchakato wa wa ununuzi wa ardhi sehemu mbalimbali uliofanywa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa madhumuni ya uwekezaji;

**NA KWA KUWA,** Manunuzi hayo yana viasharia vya matumizi mabaya ya fedha za umma na ukiukwaji wa Sheria za

Manunuzi na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na hivyo kutokuwa na tija kwa Serikali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ifanye uchunguzi wa wahusika wote katika mchakato wa ununuzi wa ardhi husika kwa malengo ya uwekezaji ambao haukuwa na tija na kisha kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi; na

b) Serikali na Bodi za Mifuko mipya ya Hifadhi ya Jamii iliyoundwa zihakikishe masuala ya uwekezaji yanafanyika kwa kuzingatia Sheria na miongozo ya Mamlaka husika kama SSRA na BOT ili kuepuka uwekezaji usiokuwa na tija kwa Taifa na kwa Wanachama wa Mifuko husika.

### 3.3.3 Kuhusu Ukaguzi Maalum wa Ubia kati ya NDC na IETL

**KWA KUWA,** Taarifa ya Ukaguzi Maalum wa Ubia kati ya NDC na IETL kuhusu uendeshaji wa TANCOAL umebaini dosari kubwa ikiwa ni pamoja na mapungufu ya Kimkataba, udanganyifu wa matumizi ya Kampuni, hasara endelevu za Kampuni na mgongano mkubwa wa kimaslahi;

**NA KWA KUWA,** Dosari hizo zimesababisha Serikali kutopata faida stahiki kama gawio na kodi mbalimbali wakati rasilimali ya makaa ya mawe ikiendelea kuchimbwa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali ianze mapema iwezekanavyo angalau ndani ya kipindi cha miezi mitatu (Februari – Mei, 2019) kufanya mapitio ya mkataba wa ubia kati ya NDC na IETL ili kubainisha masharti hasi katika mkataba huo na kuchukua hatua stahiki;

b) Wakati majadiliano yakiendelea kuhusu mkataba huo, na kwa kuzingatia ubadhirifu wa fedha uliokwisha bainishwa katika ripoti ya ukaguzi maalum, Serikali ichukue hatua kuhakikisha mbia anarejesha fedha zote zilizokwishalipwa kinyume na mkataba;

c) Serikali ndani ya miezi sita ijayo (Februari – Agosti, 2019) wafanye mapitio ya mikataba ya ubia ili kuandaa masharti mapya yenye tija kwa Taifa;

d) Serikali ifanye tathmini ili kubaini iwapo muundo wa sasa wa NDC unakidhi malengo ya uanzishwaji wake ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa sifa za Wajumbe wa Bodi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika hilo; na

e) Serikali iangalie mianya ya kisheria iliyopo ili kubaini mbinu zinazotumiwa na Makampuni haya ya kimataifa kubadili majina na umiliki kama PCEA walivyofanya. Mbinu hii hutumika kukwepa kodi na kufanya uhamisho wa bei *(Transfer pricing)* ili kuongeza gharama za uendeshaji na kutotoa gawio stahiki kwa Serikali.

### 3.3.4 Madeni ambayo SUMA JKT inadai kwa watu na Taasisi mbalimbali

**KWA KUWA,** Kumekuwa na malimbikizo makubwa ya deni lisilokusanywa na SUMA JKT kutoka kwa watu na Taasisi mbalimbali hususan deni linalotokana na mradi wa matrekta;

**NA KWA KUWA,** Kutokukusanywa kwa deni hilo kumeenda kinyume na mikataba na hivyo kuisababishia Serikali hasara kubwa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini taratibu zilizotumika katika utoaji wa Mikopo ya matrekta kwa watu na Taasisi mbalimbali;

b) Serikali ichukue hatua stahiki kwa mujibu wa mikataba ya ukopeshaji matrekta kurejesha fedha za Serikali ambazo hazijakusanywa; na

c) Serikali ichukue hatua stahiki za kurekebisha dosari za utoaji wa mikopo ya matrekta na kuchukua hatua kwa watu watakaothibitika walikiuka taratibu katika utoaji wa Mikopo husika.

### 3.3.5 Mikopo Chechefu *(Non Performing Loans, NPL)* katika Benki ya TIB

**KWA KUWA,** Kamati imethibitisha uwepo wa deni la mikopo chechefu katika Benki ya TIB lenye kufikia jumla ya **shilingi bilioni 251.89**;

**NA KWA KUWA,** Mikopo hiyo inaathiri utendaji wa Benki na kuiweka katika hali mbaya katika utendaji na uzingatiaji wa Sheria;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia yafuatayo: -

a) Benki ya TIB itoe notisi ndani ya mwezi mmoja kwa wadaiwa wote kuwataka kuanza kulipa madeni yao kwa mujibu wa mikataba;

b) Serikali kwa kushirikiana na TIB waanze kuchukua hatua stahiki kwa wadaiwa wote sugu ikiwa ni pamoja na kuanza kupiga mnada, dhamana za wadaiwa hao kwani wanafahamika na dhamana zao zinajulikana; na

c) Ili kuondoa dhana kuwa mikopo inayochukuliwa kutoka Benki za umma haipaswi kurejeshwa, Serikali kwa kushirikiana na TIB na vyombo vingine vya Dola wafanye uchunguzi wa wakopaji wote na wale watakaothibitika kufanya udanganyifu iangaliwe uwezekano wa kutumia Sheria ya Uhujumu Uchumi[20] kuwashitaki Mahakamani.

### 3.3.6 Kuchelewa Kuchukua Hatua kwa Ubadhirifu wa Fedha Katika Fungu 28 Jeshi la Polisi

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati umebainisha uwepo wa ubadhirifu wa fedha katika matukio mawili katika Fungu – 28 Jeshi la Polisi, ambapo moja linahusu malipo ya posho ya Resheni kwa watu wasiohusika na la pili malipo yaliyofanywa kwa mtoa huduma bila kutoa huduma stahiki;

---

[20] Rejea Kifungu cha 2 cha Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 pamoja na aya ya 5 Jedwali la kwanza la Sheria hiyo.

**NA KWA KUWA,** Ubadhirifu huo umeisababishia Serikali hasara ya takribani **shilingi bilioni 1.6**;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iwachukulie hatua za kisheria wahusika wote waliotajwa katika ubadhirifu huo ndani ya kipindi cha miezi miwili (Hadi kufikia Machi 30, 2019) na kutoa taarifa kwa Bunge kuhusu utekelezaji wa azimio hili.

### 3.3.7 Mikopo yenye Masharti Hasi iliyochukuliwa na TBA

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG ya mapitio ya mikataba ya mikopo iliyochukuliwa na TBA katika Taasisi mbalimbali za kifedha hapa nchini imebainisha dosari kadhaa katika masharti ya mikopo hiyo ikiwamo tozo ya riba ya asilimia 15 kwa mkopo uliochukuliwa kutoka Benki ya TIB wakati TBA hawajachukua fedha taslim hadi sasa;

**NA KWA KUWA,** Masharti hayo yanaibebesha TBA mzigo wa deni usiokuwa na manufaa kwa Taifa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba TBA wasitishe mara moja mkopo huo wenye masharti hasi kwa kuzingatia matakwa ya kisheria. Aidha, kutokana na Serikali kuhamia Dodoma, TBA wafanye mapitio ya mpango mkakati wa Wakala ili kuendana na Sera ya Serikali kuhamia Dodoma na kuepuka uwekezaji ambao unaweza kuleta hasara kama vile nyumba kutopata Wateja kwa muda mrefu kwa baadhi ya maeneo.

### 3.3.8 Mkataba wa Ubia kati ya Jeshi la Polisi na Mwekezaji Eneo la Osterbay Dar es Salaam

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG ulibaini kuwa kuna dosari kubwa katika mkataba wa ubia kati ya Jeshi la Polisi na mwekezaji wa eneo la Osterbay. Aidha, Mheshimiwa Rais alikwishalekeza kuvunjwa kwa mikataba ya namna hiyo ambayo haina maslahi mapana kwa Taifa;

**NA KWA KUWA,** Hadi sasa, mkataba huo haujapatiwa ufumbuzi hivyo kuwa na athari katika shughuli za kawaida za Serikali;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Timu ya wataalamu iliyoundwa na Serikali ikamilishe mapitio na majadiliano na mwekezaji husika ndani ya mwaka huu wa fedha ili kuhitimisha mkataba huo kwa kuzingatia Sheria za nchi na kwa maslahi mapana ya Taifa.

**3.3.9 Madeni ya TANESCO kwa TPDC, SONGAS na PAET**

**KWA KUWA,** Deni ambalo TANESCO inadaiwa na TPDC, PAET, na SONGAS limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa TANESCO kuzishughulikia kwa sasa ikiwa ni pamoja na mzigo mkubwa wa madeni ya taasisi za Serikali yasiyolipwa kwa wakati;

**NA KWA KUWA,** Deni hilo linaathiri shughuli za uendeshaji za TPDC na TANESCO kwa pamoja;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR) ifanye uchambuzi wa kina wa madeni ya TPDC na TANESCO ambayo yote ni Mashirika ya Umma chini ya Ofisi yake na kuangalia namna bora ya kushughulikia madeni hayo ili kuleta ufanisi katika utendaji wa TPDC na TANESCO; na

b) Serikali izitake Wizara, Idara, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma kutekeleza agizo la kulipa madeni yao ya umeme kwa wakati au wasitishiwe huduma hiyo muhimu.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 HITIMISHO**

**4.0 Shukurani**

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Natoa Shukurani kwa Idara ya

Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati, kupitia kwa Mkurugenzi Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Maseke na Ndugu Wilfred Magova.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Profesa Mussa Assad, Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen) Ndugu Francis Mwakapalila na Msajili wa Hazina (TR) Ndugu Athuman Mbutuka. Aidha naishukuru Kurugenzi ya Usimamizi wa mali za Serikali (DGAM) kwa kuendelea kuisadia Kamati katika utekelezaji wa shughuli zake kwa weledi na ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati imeeleza kwa kina mapungufu mbalimbali yaliyojitokeza katika Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 na kutoa mapendekezo ya namna ya kuondoa mapungufu hayo kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini ambao umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti pale Kamati ilipohitaji msaada wako. Aidha, namshukuru Naibu Spika Dr. Tulia Ackson pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia kuongoza Bunge letu kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa uadilifu na weledi mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuthamini michango ya Wajumbe hao, Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb - **Mwenyekiti**

2. Mhe. Aeshi Khalfan Hilary, Mb **- M/Mkiti**
3. Mhe. Felister Aloyce Bura, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Shukuru Kawambwa, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Jamal Kassim Ali, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Hussein Abraham Makungu, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Musa Bakari Mbarouk, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb
11. Mhe. Hassan Elias Masala, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Ignas Aloyce Malocha, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Ali Salim Khamisi, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Omar Mohamed Kigua, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija Nassir Ali, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Maida Hamad Abdallah, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Josephine Tabitha Chagula, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Abdallah Haji Ali, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Abdallah Haji Ali, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Allan Joseph Kiula, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb - Mjumbe
24. Mhe. Rhoda Edward Kunchela, Mb - Mjumbe
25. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb - Mjumbe
26. Mhe. Joyce Bita Sokombi, Mb - Mjumbe
27. Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb - Mjumbe
28. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb - Mjumbe

## 4.1 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**HESABU ZA SERIKALI (PAC)**
31 Januari, 2018

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Vedasto Ngombale. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI YA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kanuni ya 117 kanuni ndogo ya (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii imekasimishwa na Bunge lako Tukufu jukumu kubwa la kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma katika Serikali za Mitaa. Ili kutekeleza jukumu hilo la msingi, Kamati ilifanya kazi kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Kifungu cha 15 (a) hadi (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu hicho kinaweka katika Kamati hii mawanda ya utekelezaji wa shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa hii ya Kamati imegawanyika katika sura kuu nne (4) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sura ya kwanza inahusu utangulizi pamoja na maelezo ya jumla ya majukumu ya utekelezaji wa shughuli za Kamati; sura ya pili inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017; sura ya tatu inaelezea Taarifa ya

matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati hii pamoja na mapendekezo yake kutokana na uchambuzi huo; na sura ya nne inahitimisha kazi hii ya Kamati kwa kutoa mtizamo kuhusu hoja ya uchambuzi uliofanyiwa kazi kwa njia ya mapendekezo na maoni yaliyofikiwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha mwaka 2018, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017. Taarifa hii ya Kamati ni matokeo ya hesabu zilizojadiliwa na kuwasilishwa na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Bunge lako Tukufu katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii imepewa jukumu kubwa la kusimamia matumizi ya fedha za Umma za Serikali za Mitaa ambayo yamechukua zaidi ya asilimia 20 ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Eneo hili ndilo linalogusa maisha ya kila siku ya Watanzania ambamo matamanio yao makubwa ni kuona Serikali yao inaboresha na kuendeleza utoaji wa huduma bora za kijamii. Kwa kuzingatia hayo, kwa mujibu wa Kifungu cha 15 (a), (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, inaelekeza majukumu ya Kamati kama ilivyooneshwa katika Taarifa ya Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanasiasa mmoja nguli akiwa Waziri wa fedha nchini Uingereza *(Chancellor of the Excheqer), Ndugu George Osborne* aliwahi kusema, *"if we don't get a grip on government spending, there will be no growth."* Kwa tafsiri isiyo rasmi ni sawa na kusema, tusiposimamia matumizi ya Serikali, hakutakuwa na ukuaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki ya mwanasiasa huyo, ni muhimu kwa Kamati hii kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili kusaidia nchi yetu kuendelea kupiga hatua zaidi kupitia Serikali za Mitaa ambazo ndizo

Mamlaka zinazoshughulikia moja kwa moja ustawi wa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya tathmini ya mapendekezo yake saba na kubaini maeneo ambayo hayajafanyiwa kazi kikamilifu kama ifuatavyo:-

(a) Manunuzi yasiyozingatia sheria;

(b) Udhaifu katika usimamizi wa matumizi yasiyozingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha;

(c) Usimamizi usioridhisha wa mikataba na miradi ya maendeleo;

(d) Kasi isiyoridhisha ya upelekaji wa asilimia 20 vijijini; na

(e) Kutothibitishwa kwa Wakuu wa Idara na Vitengo kwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha utendaji wa Halmashauri, Kamati inaendelea kutoa wito kwa Halmashauri kutekeleza mapendekezo yake kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari, 2018, hadi kufikia Januari, 2019 Kamati ilitekeleza majukumu mbalimbali. Kama ilivyoelezwa awali, Kamati imeweza kukutana na Halmashauri zipatazo 58 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilifanya ziara ya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Umma katika baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Halmashauri mbalimbali nchini. Miongoni mwa maeneo yaliyotembelewa ni Manispaa ya Morogoro Halmashauri zilizopo katika Mkoa wa Tabora, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega na Halmashauri ya Igunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilipata fursa ya mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe kuhusu uelewa wa

maoni ya ukaguzi wa Hesabu na namna ya kuhoji Maafisa Masuuli. Kwa ufadhili wa program ya *PFRMP* iliyo chini ya Ofisi ya *CAG*. Kwa kupitia mradi wa *LSP II,* Kamati ilipata fursa ya kupata semina mbili za mafunzo ya utekelezaji wa Bajeti na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Umma. Vilevile Kamati ilipata fursa ya kupata Semina kutoka Taasisi ya Wajibu yenye madhumuni kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ni matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkuu wa Hesabu za Serikali. Maelezo ya jumla kuhusu uchambuzi; Kamati imebaini ongezeko la hati zinazoridhisha hali ambayo inaonesha kuendelea kuboreshwa kwa Kamati zetu nchini. Idadi ya hati zinazoridhisha imeongezeka kutoka 132 katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi kufikia hati 166 katika mwaka wa fedha 2016/2017. Kadhalika hati zenye shaka zimepungua kutoka hati 32 katika mwaka wa fedha 2015/2016 hadi kufikia hati 16 katika mwaka wa fedha 2016/2017 .

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasikitishwa na mwenendo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji ambayo imeendelea kupata hati isiyoridhisha kwa miaka mitatu mfululizo licha ya hatua mbalimbali kuchukuliwa na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma *(RAS)*. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kuwasimamisha kazi wafanyakazi, lakini bado uwezo wa Halmashauri hiyo kusimamia fedha za Umma umeendelea kuwa mbaya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mamlaka za Serikali za Mitaa za Wilaya ya Longido, Rombo, Korogwe na Ukerewe ambazo zimeendelea kupata hati zenye mashaka kwa miaka mitatu mfululizo. Kujirudia kwa hati hizo kumetoka na Halmashauri hizo kutoboresha taarifa zao kwa kuzingatia vigezo vya kuandaa taarifa za fedha katika Sekta za Umma Kimataifa *(IPSAS)* kama inavyoainishwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017: Udhaifu katika mfumo wa uthibiti wa ndani, Kamati imebaini changamoto nyingi katika utendaji

wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Ikumbuke kuwa lengo la udhibiti wa ndani wa mapato na matumizi ni kwenye Halmashauri zetu. Hata hivyo kitengo hiki cha ukaguzi wa ndani kimekosa ufanisi kutokana na uhaba mkubwa wa rasilimali watu, fedha na vitendea kazi muhimu kama vile *computer,* kamera, gari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Halmashauri 58 zilizohojiwa na Kamati, Halmashauri 23 ambazo ni sawa na asilimia 40 zilibainika kuwa na upungufu mkubwa katika Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Hata hivyo, Halmashauri 35 zilizosalia bado hazikuwa na utendaji unaorisha katika kitengo hiki. Licha ya jitihada kubwa ambazo Ofisi ya Rais *TAMISEMI* imekuwa ikizifanya kwa kuendesha mafunzo mbalimbali ya mifumo mipya ya udhibiti wa mapato na malipo kama vile *EPICOR, LAWSON, PLANREP* na *LGRCIS*, baadhi ya Halmashauri hazijaweza kutumia mifumo hiyo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini udhaifu mwingine wa kutotekeleza Agizo Na. 12 la *Memorandum* ya Fedha ya Serikali za Mitaa la 2009 ambalo linataka Kamati ya Ukaguzi ikutane angalau mara moja katika kila robo mwaka. Vilevile Kamati imebaini kutozingatiwa kwa mwongozo wa usimamizi wa fedha za Umma uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu uendeshaji wa Kamati za Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele hicho kinaeleza Mwenyekiti achaguliwe kutoka nje ya Halmashauri na awe mtu mwenye uelewa wa masuala ya Uhasibu na Ukaguzi. Hata hivyo, bado Halmashauri nyingi zimeendelea kuteua Wenyeviti wake kutoka miongoni mwa Watumishi wa ndani kitendo kinachoathiri kwa kiasi kikubwa dhana iliyokusudiwa ya uwazi, uwajibikaji katika Ukaguzi wa Ndani na usimamizi wa fedha za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini upungufu katika uanzishaji wa Sera ya Kusimamia Vihatarishi *(Risk Management Policy)*. Halmashauri zote zilielekezwa kuanzisha Sera hii ya Udhibiti wa Viashiria Hatarishi na kuteua Mratibu

katika eneo hilo. Lengo ni kuzisaidia Menejimenti za Halmashauri nchini kutambua viashiria hatarishi punde vinapojitokeza. Katika Taarifa ya Ukaguzi, jumla ya Halmasahuri 71 zimebainika kutoweka *register* ya viashiria hatarishi *(Risk Management Register)* na hakuna hatua zilizochukuliwa kukabiliana na viashiria hivyo. Vilevile Menejimenti katika Serikali za Mitaa haina uelewa juu ya umuhimu wa Sera hiyo Vihatarishi na Udhibiti wa Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutotekelezwa kikamilifu kwa maagizo ya Kamati na kutojibiwa kwa Hoja za ukaguzi; kuendelea kwa mwenendo huu kila mwaka kunatoa taswira mbaya kwa menejimenti za Halmashauri kuwa zimekosa umakini ama zimekuwa zikipuuzia kwa makusudi hoja ya ukaguzi na maagizo ya Kamati. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali juu ya umuhimu wa kuliangalia suala hili kwa ukaribu ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu katika uendeshwaji wa Mfuko wa Wanawake na Vijana; Kamati imebaini kuwepo kwa deni kubwa la Mfuko wa Wanawake na Vijana katika Halmashauri nyingi nchini ambapo deni hilo limeonekana likiendelea kuongezeka kadri ya siku zinavyozidi kwenda. Hali hii inaonesha kwa miaka ijayo deni hilo halitaweza kulipika tena na Halmashauri nyingi zitashindwa kutekeleza majukumu yake kutoka mapato ya ndani. Kwa mujibu wa Taarifa ya Ukaguzi wa *CAG* kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hali ya deni ni kama inavyooneka katika Jedwali namba nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imebaini kuwa mfumo wa uratibu na usimamizi wa utoaji na ukusanyaji wa mikopo haujawa mzuri katika halmashauri zetu nchini na hivyo, kusababisha fedha hizo kukosa usimamizi. Kamati imebainika pia kuwa Vikundi vingi vimekuwa vikisuasua kurejesha madeni yake. Hali hii imeathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya ukuaji wa Mfuko kwani baada ya fedha hizo kuwa za mzunguko *(revolving funds)* fedha hizo zimekuwa hazirejeshwi kwa wakati au kutorejeshwa kabisa. Katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2013/2014 hadi

mwaka 2016/2017 zaidi ya shilingi bilioni 13.9 zilizotakiwa kurejeshwa na vikundi 253 hadi sasa hazijarejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hizo Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuleta Muswada Bungeni kutunga Sheria ya kusimamia Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kupitia Sheria ya fedha ya mwaka 2018. Aidha, kupitia sheria ya sasa Kamati inapenda kupongeza Bunge lako Tukufu kwa kuongeza kipengele cha watu wenye ulemavu, hivyo, kuanzia sasa itasababisha kundi hilo kutambuliwa na kushirikishwa katika shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa usimamizi wa rasilimali watu katika Serikali za Mitaa; Taarifa ya Ukaguzi katika baadhi ya halmashauri inaonesha bado kuna changamoto ya upungufu mkubwa wa watumishi katika Serikali za mitaa. Kwa kuzingatia taarifa ya idadi sahihi ya watumishi na ujuzi stahiki wa wafanyakazi wa kada mbalimbali imeonesha kuwa, katika mwaka wa fedha 2014/2015 upungufu ulikuwa asilimia 22 kwa mamlaka 117 zilizokaguliwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 upungufu ulikuwa asilimia 30 kwa mamlaka 126 zilizokaguliwa na kwa mwaka wa fedha 2016/2017 upungufu uliongezeka hadi kufikia asilimia 32 kama inavyojionesha kwenye jedwali. Hali hii, imeathiri halmashauri kwenye sekta ya elimu, afya, kilimo kwani watumishi wachache waliopo wanalazimika kubeba majukumu ya ziada kukidhi matarajio ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuendelea kucheleweshwa kwa mchakato wa kuwathibitisha Wakuu wa Idara na vitengo wanaokaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miezi sita licha ya jitihada za Serikali kutatua changamoto hii. Kamati haioni sababu ya kuendelea kuwepo kwa tatizo hili katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Aidha, kuna baadhi ya Wakurugenzi katika Halmashauri ambao wamekuwa wakichelewesha mchakato huu kwa sababu ya kutofuata taratibu za uthibitishaji. Kupitia taarifa ya ukaguzi ya mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati imebaini Halmashauri tatu za

Mji wa Ifakara, Halmashauri ya Mbeya na Halmashauri ya Kigoma kuwa na idadi kubwa ya watumishi wanaokaimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; taarifa ya ukaguzi inaonesha ipo miradi 38 ambayo haijatekelezwa kabisa na Mamlaka za Serikali za Mitaa licha ya miradi hiyo kuwa imetengewa fedha. Kati ya miradi hiyo ipo miradi 13 ambayo imeshindwa kutekelezwa kutokana na kiasi cha shilingi bilioni 1.05 kutotolewa na Hazina. Pamoja na miradi hiyo, ipo miradi 25 ambayo haikutekelezwa kabisa licha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 kupokea kiasi cha shilingi bilioni 7.79 kwa ajili ya miradi hiyo. Aidha, Taarifa hiyo imebainisha changamoto ya miradi kukamilika lakini haitumiki. Imeelezwa kwamba ipo miradi yenye thamani ya shilingi milioni 782.4 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 13 ambayo imekamilika lakini haitumiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mradi wa *Public Finance Manangement Reform Program (PFMRP)* unaoratibiwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi *(NAOT),* Kamati hii ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* iliweza kutembelea na kukagua mradi wa barabara za Tubuyu, Nanenane na Maelewano katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ambayo ilikuwa imekaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa kiwango cha lami nzito kwa urefu wa kilomita 4.6 kupitia mkopo wa Benki ya Dunia *(World Bank)* wenye thamani ya shilingi bilioni 12.6. Hadi Kamati inapotembelea mradi huu ulikuwa umekamilika kwa asilimia 99 na kiasi cha shilingi 9.91 milioni kilikuwa kimeshalipwa sawa na asilimia 79. Kamati ilielezwa kuwa, kiasi cha shilingi bilioni 2.4 kipo kwenye hatua za mwisho kulipwa huku kiasi cha shilingi milioni 633 kikibakizwa kwa ajili ya kipindi cha matazamio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini faida ambazo zimetokana na kukamilika kwa mradi huo kama ilivyoonyeshwa katika taarifa ya Kamati hii pamoja na

changamoto ambazo zilihitajika kutatuliwa kabla ya mradi kukabidhiwa kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haikuridhika na gharama kubwa za mradi huu ambapo shilingi bilioni 12.6 zilitumika kujenga barabara yenye urefu wa kilomita 4.6 tu. Kwa uzoefu wa kawaida kiasi hicho cha fedha kingeweza kutumika kujenga barabara yenye zaidi ya urefu wa kilomita 10. Kamati inasubiri taarifa ya ukaguzi maalum *(comprehensive specific autity)* katika miradi yote inayotekelezwa na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto katika usimamizi wa mali; mambo muhimu yaliyobainika katika ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kipindi cha kuanzia 2012 - 2017; Kamati katika kuijadili taarifa ya ukaguzi wa Halmasahuri ya Wilaya ya Kaliua ilibaini uwepo wa mambo ya kutilia shaka katika matumizi ya fedha za umma. Hali hiyo ilisababisha Kamati hii kutoa maombi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum kwa Halmashauri hiyo. Ukaguzi huu maalum umeisaidia Kamati kubaini ubadhirifu mkubwa wa fedha unaokadiriwa shilingi bilioni 3.5 za miradi ya maendeleo uliosababishwa na matumizi mabaya ya madaraka katika ngazi ya mkoa na halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kumuwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali kurahisisha hiyo, Kamati iliainisha hadidu za rejea nne ambazo zimeoneshwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi huu maalum umeisaidia Kamati kubaini mambo muhimu ambayo yamefanyika bila nidhamu ya usimamizi wa fedha za umma yaani *financial in discipline* na ukiukwaji wa taratibu na kanuni zinazosimamia masuala ya fedha. Katika matokeo ya Ukaguzi huu Kamati imebaini kuwa kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, kuingiliwa kwa Bodi ya Zabuni, kuingiliwa kwa Kamati ya Tathimini na Kitengo cha

Menejimenti ya Ununuzi. Ukaguzi huo umebaini jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kimetumika vibaya na kina sura ya kijinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati kama tulivyoelezwa awali, uchambuzi wa Kamati kuhusu Ukaguzi huu maalum umebaini kwamba ni Watumishi wawili tu wa Kitengo cha Manunuzi kati ya watumishi 66 wa halmashauri walibainika kuhusika na ubadhirifu huu ndio wamechukuliwa hatua. Ukaguzi Maalum umebaini kwamba, mojawapo ya chanzo kikubwa cha ubadhirifu huu ni matumizi mabaya ya madaraka ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa wakati huo, Bi. Fatma Mwassa katika miradi iliyotekelezwa na Kampuni ya *Saram Company limited* kwa kuelekeza Mkurugenzi, Wenyeviti wa Kamati za Tathimini, Bodi ya Zabuni na Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi kutoa zabuni kwa Kampuni hiyo ya *Saram Company Limited* ambayo Mkurugenzi wake ni mtu mwenye mahusiano ya ndani na Mkuu wa Mkoa wa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu, mapendekezo ya Kamati; naomba sasa nitoe mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha kwa mfumo wa udhibiti wa ndani:-

KWA KUWA imebainika kwamba kuna udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani wa mapato na matumizi katika Halmashauri kutokana na utendaji usioridhisha wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani *(Internal Audit Unit)*, Kamati ya Ukaguzi *(Audit Committee)* na kutokuwepo kwa Sera ya Kudhibiti Viashiria Hatarishi *(Risk Management Policy);*

NA KWA KUWA udhaifu huo umeathiri kwa kiasi kikubwa nidhamu katika Halmashauri na kusababisha kuongezeka kwa matumizi mabaya ya fedha za umma;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge liazimie kuwa:-

(a) Serikali ihakikishe kuwa katika kila Halmashauri Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinapewa rasilimali watu, fedha za kutosha na vitendea kazi muhimu kama vile kompyuta, kamera na magari;

(b) Ofisi ya Rais, TAMISEMI ihakikishe kuwa Kamati ya Ukaguzi itakuwa inakutana katika kila robo ya mwaka na kutoa taarifa ya mrejesho wa vikao hivyo. Aidha, ihakikishe pia kila halmashauri inaanzisha mfumo wa kudhibiti viashiria hatarishi ili kuondokana na uwezekano wa kupata hasara; na

(c) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali *yaani Internal Auditor General* pamoja na Ofisi ya Rais, TAMISEMI waweke utaratibu wa ufuatiliaji wa utendaji kazi wa Vitengo vya Ukaguzi wa ndani katika Halmashauri nchini. Vilevile Kitengo cha Ukaguzi cha ufuatiliaji cha Mamlaka za Serikali za Mitaa kilichopo katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kiwezeshwe kwa kupewa rasilimali watu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutekelezwa kikamilifu maagizo ya Kamati na kujibiwa kwa hoja za ukaguzi:-

KWA KUWA halmashauri nyingi zimebainika kutotekeleza kikamilifu mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo ya Kamati;

NA KWA KUWA kuendelea kutotekelezwa kwa mapendekezo hayo kunajenga taswira mbaya ya kazi iliyofanywa na Kamati hii pamoja na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

(a) Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ichukue hatua za kisheria na za kinidhamu kwa Menejimenti za Halmashauri ambazo zimekuwa zikishindwa kutekeleza mapendekezo haya na kwa wakati; na

(b) Ofisi ya Rais, TAMISEMI ihakikishe kuwa mtumishi yeyote atakayebainika kuhusika na matumizi mabaya ya fedha za umma asihamishwe kituo cha kazi mpaka shauri la mtumishi huyo litakapoisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuboresha uendeshwaji wa Mfuko wa Wanawake na Vijana:-

KWA KUWA imebainika kwamba Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kulilipa deni la zamani la Mfuko wa Wanawake na Vijana na kwamba bado hakuna mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa madeni hayo toka kwenye vikundi;

NA KWA KUWA Hali hii ikiendelea inaweza ikakwamisha nia njema ya Serikali ya kuwawezesha vikundi ;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

(a) Serikali iharakishe mchakato wa utungaji wa kanuni za Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ili kuweka mfumo rasmi wa usimamizi wa mfuko huo; na

(b) Serikali izifutie Halmashauri madeni ya nyuma ya Mfuko wa Wanawake na Vijana kwani fedha ambazo hazikuchangiwa kwenye Mfuko huo zilitumika katika uendelezaji wa halmashauri na utekelezaji wa shughuli nyingi za mendeleo. Aidha, fedha ambazo zilikuwa zimekopeshwa katika vikundi ziendelee kukusanywa kama ilivyo katika utaratibu wa awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kukamilisha usimamizi wa rasilimali watu katika Serikali za Mitaa:-

KWA KUWA Kumebainikika kuwepo kwa upungufu mkubwa wa watumishi katika Halmashauri nchini na kwamba utaratibu wa upekuzi na uthibitishaji wa Wakuu wa Idara na Vitengo huchukua muda mrefu hali inayosababisha

Watumishi hao kukaimu kwa muda mrefu zaidi ya miezi sita tofauti na Sheria za utumishi wa umma zinavyoelekeza;

NA KWA KUWA upungufu huo umeendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa hali ya utendaji katika Halmashauri nchini;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

(a) Serikali iongeze jitihada za kuajiri watumishi wa halmashauri hususani katika Kitengo cha Kilimo, Afya na Elimu ili kuboresha hali ya ubora wa huduma zitolewazo kwa jamii; na

(b) Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ziangalie njia bora ya kuharakisha mchakato wa kuwathibisha watumishi ili kuongeza morali zaidi katika utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha usimamizi wa utekelezaji wa Miradi ya maendeleo:-

KWA KUWA Imeendelea kuonekana kuwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni mdogo sana ukilinganisha na matarajio ya Serikali na Wananchi ya upatikanaji wa huduma bora;

NA KWA KUWA Hali hii imeendelea kukwamisha utoaji wa huduma kwa wananchi sambamba na jitihada za kimaendeleo;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

(a) Serikali iboreshe eneo la usimamizi katika halmashauri pamoja na kuzijengea uwezo Halmashauri zote kwa kuajiri wataalam kwenye sekta mbalimbali;

(b) Uwekwe mfumo mzuri wa kusimamia taratibu za utoaji zabuni kwa Wakandarasi ili kuondoa mazingira ya vitendo vya rushwa; na

(c) Mfumo wa malipo baada ya kazi yaani *certificate award* uangaliwe upya na ikiwezekana uboreshwe ili kuwaondolea Wakandarasi ukiritimba mwingi kipindi wanachodai haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuimarisha usimamizi wa mali:-

KWA KUWA imebainika kwamba Halmashauri nyingi zimeendelea kukaa na mali chakavu kwa muda mrefu ilihali upo utaratibu wa ufutaji wa mali hizo na kwamba Serikali za Mitaa zinatakiwa kulipa bima mali zake husasan magari, wakati Serikali Kuu hailazimiki kufanya hivyo;

NA KWA KUWA kuendelea kuwa na mali chakavu kunaiongezea halmashauri gharama ya uendeshaji na utunzaji wa mali hizo na gharama isiyo ya lazima kuzingatia uwezekano *(probability)* ya magari yote kupata ajali kwa wakati mmoja;

KWA HIYO BASI Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie:-

(a) Ofisi ya Rais, TAMISEMI ihakikishe kuwa Halmashauri zinafuta mali chakavu na kuondokana kabisa na tabia ya kurundika mali chakavu; na

(b) Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ifanye utaratibu wa kurahisisha ufuatiliaji wa mali hizo ikiwezekana madaraka hayo yakasimishwe kwa Mhakikimali wa Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mambo muhimu yaliyobainika katika Ukaguzi wa Halmashauri ya Kaliua; kwa...

**NAIBU SPIKA:** Kengele, Mheshimiwa Ngombale kengele ya pili imeshagonga dakika mbili umalizie.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE-MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yangu nachukua fursa hii pia kumshukuru…

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa zote ziingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuyajadili mapendekezo ya Kamati hii na yapitishwe ili yaweze kuwa sehemu ya Maazimio ya Bunge kuhusu usimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa Hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. KHALIFAN H. AESHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono ahsante sana.

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC) KUHUSU USIMAMIZI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA KATIKA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)*

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba

kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoisha tarehe 30 Juni, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii imekasimishwa na Bunge lako Tukufu jukumu kubwa la kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za mitaa. Ili kutekeleza jukumu hilo la msingi Kamati ilifanya kazi kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Kifungu cha 15 (a)-(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu hicho kinaiwekea Kamati hii mawanda ya utekelezaji wa shughuli zake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Taarifa hii ya Kamati imegawanyika katika sura kuu nne (4) kama ifuatavyo:-

(i) **Sura ya kwanza** inahusu utangulizi pamoja na maelezo ya jumla ya majukumu na utekelezaji wa shughuli za Kamati ;

(ii) **Sura ya pili** inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017;

(iii) **Sehemu ya tatu** inaelezea Taarifa ya matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati hii pamoja na mapendekezo yake kutokana na uchambuzi huo;na

(iv) **Sehemu ya nne** inahitimisha kazi hii ya Kamati kwa kutoa mtizamo wa kuhusu hoja na uchambuzi uliofanyika kwa njia ya mapendekezo na maoni yalioafikiwa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi cha mwaka 2018, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017. Taarifa

hii ya Kamati ni matokeo ya hesabu zilizokaguliwa na kuwasilishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Bunge lako Tukufu kwa kipindi hicho.

## 1.2 Majukumu ya Kamati:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii imepewa jukumu kubwa la kusimamia matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa, ambayo yamechukua zaidi ya **asilimia 20** ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Eneo hili ndilo linalogusa maisha ya kila siku ya Watanzania ambao matamanio yao makubwa ni kuona Serikali yao inaboresha na kuendeleza utoaji wa huduma bora za kijamii. Kwa kuzingatia hayo kwa mujibu wa Kifungu cha 15 (a)-(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati hii ina majukumu yafuatayo:-

(i) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo yaliyokwisha tolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

(iii) Kutoa Mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya CAG iliyoshughulikiwa na Kamati ilihusu kaguzi za Halmashauri mia moja na themanini na tano (185). Kwa mujibu wa kanuni ya 92 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009, Kamati inayo wajibu wa kujadili na kuchambua taarifa binafsi (Individual reports) ya Halmashauri zilizokaguliwa baada ya CAG kuwasilisha taarifa yake ya ukaguzi wa Jumla wa Halmashauri Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia kanuni hiyo, Kamati ilitumia vigezo mbalimbali, kuteua Halmashauri hamsini na nane (58) ambazo imejadili na kuchambua Hesabu zake

katika kipindi cha Kamati cha kuanzia Julai, 2018 na Januari, 2019. Kamati ilifanya hivi kwa kuwa si rahisi kuweza kukutana na Halmashauri zote kwa muda wa kazi wa Kamati uliopo. Hatua hii imeiwezesha Kamati kupata picha ya jumla ambayo inatolewa maoni na mapendekezo katika taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** katika kushughulikia kaguzi za halmashauri ambazo ziliteuliwa na Kamati kama ilivyoelzwa hapo juu, Kamati ilitumia utaratibu ufuatao katika vikao vyake;

(i) Kamati mara kwa mara imekuwa ikitumia fursa iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (18) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kujigawa katika Kamati ndogo ili kuweza kushughulikia Halmashauri nyingi kwa wakati mmoja. Hatua hii imeisaidia Kamati kuweza kukutana na halmashauri nyingi Zaidi katika muda rasmi wa vikao vya Kamati;

(ii) Kamati imekuwa ikipata maelezo ya ufafanuzi wa kina kutoka kwa CAG (Briefing) kuhusu hoja za ukaguzi zilizoelekezwa kwa Halmashauri husika kabla ya kukutana na Halmashauri hiyo.

(iii) Baada ya kikao cha Briefing na CAG, Kamati hufanya Mahojiano na Menejimenti za Halmashauri kwa lengo la kupata majibu yao kuhusu hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Halmashauri husika.

(iv) Kwa kuzingatia hoja mbalimbali za CAG, Kamati hufanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri ili kufuatilia na kujiridhisha namna fedha za umma zilivyotumika. Utaratibu huu huiwezesha Kamati kupima kama fedha husika zimetumika kwa tija inayotegemewa.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu huu umeiwezesha Kamati kuongeza ufanisi wa Kazi zake katika kuhakikisha kuwa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inafanyiwa kazi kikamilifu. Ufanisi wa Kamati hii ni muhimu katika kuhakikisha

kuwa Bunge linaendelea kuisimamia na kuishauri Serikali kuhusu matumizi mazuri ya fedha za Umma katika Halmashauri zetu za Serikali za Mitaa. Mwanasiasa mmoja nguli akiwa Waziri wa fedha wa Nchi ya Uingereza ***(Chancellor of the Exceqer) Ndg. George Osborne*** aliwahi kusema ***"if we don't get grip on government spending, there will be no growth"***

> kwa tafsiri isiyo rasmi ni sawa na kusema kwamba, "***tusipo simamia matumizi ya Serikali, hakutakuwa na ukuaji."***

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mantiki ya maneno ya mwanasiasa huyo, ni muhimu kwa Kamati hii kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo ili kuisadia nchi yetu kuendelea kupiga hatua zaidi kupitia Serikali za Mitaa, ambazo ndizo Mamlaka zinazoshughulikia moja kwa moja ustawi wa Watanzania wote.

## 1.3 Muhtasari wa Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya Kamati kwa mwaka 2016/2017 yalilenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kama yalivyobainishwa katika Taarifa ya ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2017.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwa muhtasari matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo:-

### 1.3.1 Maeneo yenye Matumizi yasiyofaa ya Fedha za Umma

**Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyobainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17 ni kama ifuatavyo;

a) Mapungufu yanayohusu fedha zinazotolewa na Serikali Kuu pamoja na zinazokusanywa kutokana na vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida;

b) Udhaifu katika Mifumo ya Udhibiti wa ndani;

c) Manunuzi yaliyofanyika bila kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011;

d) Usimamizi mbovu katika mikataba ya mawakala wa kukusanya mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kulikosababisha mapato ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.53** kukusanywa na Wakala bila kuyawasilisha kwa mamlaka husika;

e) Kutowasilisha kwa Ukaguzi vitabu 379 vya kukusanyia mapato pamoja na kupewa wito wa kuviwasilisha kwa muda muafaka;

f) Jumla ya kesi zipatazo 1,111 zenye madai ya **Shilingi Biloni 186** zinatokana na kusitishwa kwa mikataba kwa Wazabuni, kesi za Watumishi na kesi zinazotokana na migogoro ya ardhi pamoja na gharama nyinginezo. Endapo Mamlaka hizo zitashindwa katika kesi hizo zitalazimika kulipa fedha hizo hivyo kuathiri utoaji huduma;

g) Kutokutekeleza Maagizo ya Kamati ya kipindi cha nyuma na kutokujibu kikamilifu hoja za ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati;

h) Kuchelewa kukamilisha miradi ya maendeleo kwa wakati, hivyo baadhi ya miradi kutekelezwa chini ya kiwango;

i) Kuna kasoro katika urekebishaji wa Ikama katika baadhi ya Halmashauri na Mikoa kuhusu mgawanyo sahihi wa Rasilimali Watu katika Sekta za Elimu, Kilimo na Afya;

j) Kutokufanyika tathimini ya kina kuhusu madeni ya nyuma ya Mfuko wa Wanawake na Vijana kuona kama madeni hayo yanalipika au la na namna bora ya kushughulikia suala hili ambalo tayari limetungiwa sheria lakini mpaka sasa kanuni hazijatungwa;

k) Kuna ucheleweshaji wa mchakato wa kupitisha sheria ndogo kwa baadhi ya Halmashauri, hivyo Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kukusanya mapato kisheria;

l) Kuna Changamoto katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu urasimu mkubwa katika ufutaji wa mali chakavu kwenye Hesabu na uteketezaji wa madawa yaliyokwisha muda wake; na

m) Kukaimu nafasi za wakuu wa idara na vitengo kwa muda mrefu bila kuthibitishwa.

### 1.3.2 Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa katika taarifa yake kwa mwaka wa fedha 2015/16.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliwasilisha taarifa Bungeni iliyohusu usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/16. Taarifa hiyo ilikuwa na mapendekezo saba (7) yaliyopitishwa kama maazimio ya Bunge na hivyo kuhitaji utekelezaji. Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa maazimio hayo na mpaka tunaandika taarifa hii, muhtasari wa hali ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge ni kama inavyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 1**.

**Jedwari Na. 1:** Muhtasari wa mapendekezo ya Kamati yaliyokubaliwa na Bunge kuwa Maazimio kwa mwaka wa fedha 2015/16 na utekelezaji wa Serikali.

| Na | Muhtasari wa mapendekezo ya Kamati | Muhtasari wa utekelezaji wa Serikali |
|---|---|---|
| 1 | Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011. Kwamba Serikali iweke utaratibu wa kutoa Taarifa za tathmini ya Manunuzi za PPRA *(Public Procurement Regulatory Authority)* inayohusu Serikali za Mitaa sambamba na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. | Serikali imechukua hatua za kinidhamu kwa Watumishi waliobainika kutofuata matakwa ya sheria hiyo katika Halmashauri mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya Mikataba yote ya miradi kabla ya kusainiwa. |
| 2 | Usimamizi wa matumizi usiozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha za Umma; Kwamba Serikali iimarishe ufuatiliaji wa mfumo wa kudhibiti malipo, kuimarisha kitengo cha Ukaguzi wa ndani na kuwachukulia hatua watumishi wote wanaohusika na upotevu wa nyaraka mbalimbali. | a) Serikali imeimarisha sehemu ya ufuatiliaji wa mara kwa mara kupitia kitengo cha Ukaguzi na Ufuatiliaji Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (IFTU) na tathmini katika Ofisi ya Rais TAMISEMI.<br><br>b) Hatua za kinidhamu zilichukuliwa kwa Watumishi wahusika pamoja na utenguzi wa uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmashauri ya Jiji Mwanza, Halmashauri za Manispaa Kinondoni, Kigoma, Halmashauri za Wilaya za Mpanda, Gairo, Nzega, Kondoa na Halmashauri ya Mji Tunduma. Hatua zimeendelea kuchukuliwa kwa Halmashauri ambazo zimekuwa zikikiuka taratibu za manunuzi zikiwemo Halmashauri za Wilaya za Nkasi, Butiama, Tunduru, Kilosa, Mbeya na Mji wa Mbinga. |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Usimamizi usio na tija wa utekelezaji wa mikataba na miradi ya maendeleo, kwamba Serikali itoe maelezo ya kina na sababu za kushindwa kukamilika kwa miradi mbalimbali ya Maendeleo hususani Miradi ya maji katika baadhi ya Halmashauri na kufuatilia changamoto za Mradi wa soko la Mwanjelwa kwa kupitia upya ukokotoaji wa deni la Benki ya CRDB la zaidi ya Shilingi Bilioni 63. | a) Serikali imetoa maelezo kuwa sababu zinazokwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni pamoja na kuteuliwa kwa wakandarasi wasio na sifa, upungufu wa wataalamu wa kusimamia utekelezaji wa miradi, kupokelewa kwa huduma zilizo chini ya kiwango na kupitia kwa Makatibu Tawala wa Mikoa kwa barua kumb.na AD/303/509/01 ya tarehe 23/11/2017 inasisitiza kuhakikisha kuwa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na marekebisho yake ya Mwaka 2016 zinazingatiwa.<br>b) Benki ya CRDB imeingia mkataba na Prolaty Consultant Ltd anasimamia uendeshaji ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato ya soko hilo. Hata hivyo, bado zipo changamoto za kimkataba kati ya CRDB na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuhusu ukokotoaji wa riba ya mkopo (Capitalisation of Interest) ambayo inafanya deni kuwa kubwa, kwa ujumla kunafanyika mazungunzo na Benki ili kupitia upya mkataba na kuondoa kipengele hicho. |
| 4 | Udhaifu katika kusimamia mapato kutoka vyanzo ya ndani na Serikali itoe maelezo ya mpango uliopo katika kuhakikisha kuwa tathimini ya vyanzo vya mapato kwa Halmashauri zote inafanyika na kutoa muda maalum wa kusimika na kutumia mfumo wa kieletroniki. | a) Serikali imesimika na kuanza kutumia mfumo wa kukusanya mapato kwa njia ya kieletroniki-LGRCIS katika Halmashuri zote.<br>b) Serikali imeanzisha na kusisitiza matumizi ya vifaa vya kukusanyia mapato *Point of Sales (POS)* badala ya kutoa stakabadhi zinazoandikwa kwa mkono.<br>c) Halmashauri zimeelekezwa kufanya tathimini ya vyanzo vya mapato ikiwa pamoja na kufanya mapitio ya sheria ndogo. |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Kutotekeleza maagizo ya Kamati na kutojibu Hoja za Ukaguzi kwa wakati. Kamati ilibainisha kuwa Halmashauri zimekuwa zikitekeleza maagizo ya Kamati na hoja za Ukaguzi kwa kuchelewa na kwa kiwango cha chini, hali iliyosababisha Halmashauri nyingi kubaki na maagizo mengi yasiyotekelezwa na hoja nyingi za ukaguzi zisizojibiwa. | Muundo wa ofisi ya Rais-TAMISEMI umefanyiwa marekebisho kwa kuanzisha kitengo cha Ukaguzi na Ufuatiliaji ambacho majukumu yake makubwa ni pamoja na kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).<br>Hivyo, Ofisi ya Rais TAMISEMI imetoa agizo kwa Makatibu Tawala kusimamia utekelezaji wa agizo hili kwa kushirikisha kitengo cha ukaguzi na ufuatiliaji ambacho kinasimamia utekelezaji wa Taarifa ya CAG. |
| 6 | Kutotenga mchango wa asilimia kumi (10%) ya Mapato kutoka vyanzo vya ndani kwa Mfuko wa Wanawake na vijana na asilimia ishirini (20%) ya ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na vijiji. | Serikali inakiri umuhimu wa michango ya asilimia 10 kwa vikundi vya Wanawake na Vijana na utoaji wa asilimia 20 kwenda katika Ofisi za serikali za vijiji na mitaa. Hata hivyo, kumekuwepo na changamoto kwa Halmashauri nyingi kushindwa kuchangia kwa sababu za uwezo mdogo wa kukusanya mapato ya ndani na baadhi ya vikundi vinavyokopeshwa kutorejesha fedha za mkopo kwa wakati au kutorejesha kabisa. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 uchangiaji katika Halmashauri nyingi umeongezeka kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa sasa Serikali imetunga sheria ya Mfuko huu kwa Wanawake, Vijana na Walemavu nchini. |
| 7 | Watumishi kukaimu nafasi za Wakuu wa Idara na Vitengo zaidi ya Miezi sita (6) bila kudhibitishwa. | Kimuundo, Halmashauri zote 185 zinahitaji kuwa na Wakuu wa Idara na Vitengo 3,505 ambapo Wakuu wa Idara 2,398 na Wakuu wa Vitengo 1,107. Idadi ya wakuu wa idara na vitengo waliopo kwenye upekuzi imeongezeka kutoka 802 hadi 927 na ufuatiliaji unaedelea kufuatia hatua za upekuzi kwa Watumishi wanaokaimu. |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Majibu wa Ofisi ya Rais TAMISEMI ya mwezi Aprili, 2018 kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya tathmini ya mapendekezo yake saba na kubaini kuwa jitihada kubwa zimefanywa na Serikali katika kuimarisha mfumo wa kukusanya mapato wa LGRCIS na matumizi ya vifaa vya kukusanyia mapato *(POS)* sambamba na urasimishaji na kupitisha Sheria ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Walemavu. Hata hivyo, yapo maeneo ambayo Kamati haijaridhishwa na utekelzaji wake. Kwa maoni ya Kamati, maeneo hayo hayajafanyiwa kazi kikamilifu kama ifuatavyo:-

a) **Manunuzi yasiyozingatia sheria**

Kamati haijapata taarifa rasmi ya tathmini ya manunuzi inayohusu Serikali za Mitaa na Mpango mkakati wa kuzingatia sheria katika Halmashauri nchini hususan eneo la manunuzi ya umma.

b) **Udhaifu katika usimamizi wa matumizi usiozingatia sheria, Kanuni na taratibu za fedha**

Serikali iimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani na kitengo cha ukaguzi wa ndani kwa kuchukua hatua za kukiwezesha kwa raslimali watu na vifaa ili kitekeleze majukumu yake.

c) **Usimamizi usioridhisha wa Mikataba na Miradi ya Maendeleo** Bado kuna maelezo yasiyojitosheleza katika utekelezaji wa mikataba na miradi mbalimbali ya maendeleo isiyokamilika kwa muda mrefu au kutumika kinyume na ilivyokusudiwa. Kwa mfano uwekezaji wa ubia katika Halmashauri ya Ilala na Tanzania Remix Centre Limited (TRSL); mazungumzo na benki ya CRDB Katika kupunguza gharama za mkopo wa ujenzi wa soko la Mwanjelwa (H/Jiji Mbeya); na kutokamilika kwa miradi ya maji na umwagiliaji kwa sababu za fedha kutotolewa au idhini ya ongezeko la gharama za miradi ya maji na umwagiliaji Inala Irrigation Scheme katika (H/M Tabora), Changalikwa na Mlembule (H/W Korogwe) na Masoko (H/W Rungwe)

d) **Kasi isiyoridhisha ya upelekaji wa asilimia 20 vijijini**

Hakuna maelezo yakutosheleza kuhusu utekelezaji madhubuti wa kurejesha asilimia 20 ya fedha kwa vijiji na serikali za mitaa.

e) **Kutothibitishwa kwa wakuu wa Idara na Vitengo kwa wakati**

Bado kuna kasi ndogo ya kuwathibitisha Wakuu wa Idara na Vitengo katika nafasi kwani suala hilo liko kisheria.

Ili kuboresha utendaji wa Halmashauri, Kamati inaendelea kutoa wito kwa Halmashauri kutekeleza mapendekezo yake kwa ukamilifu na kwa wakati.

## 1.4 Utekelezaji wa shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari 2018, hadi kufikia Januari, 2019 Kamati ilitekeleza majukumu mbalimbali. Kama ilivyoelezwa awali, Kamati imeweza kukutana na Halmashauri zipatazo hamsini na nane (58) katika kipindi hicho. Katika mikutano na hamashauri hizo, Kamati ilipata fursa ya kuchambua kwa kina taarifa za ukaguzi wa halmashauri hizo na kufanya mahojiano na watendaji wake wakuu. Mikutano hii ilikuwa ni fursa nzuri kwa Kamati kutoa ushauri na maelekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha usisimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifanya ziara za ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika baadhi ya miradi inayotekelezwa na halmashauri mbalimbali nchini. Miongoni mwa maeneo yaliyotembelewa ni Manispaa ya Morogoro ambapo Kamati ilikaguwa mradi wa barabara ya Tubuyu, Nanenane na Maelewano. Katika ziara hii mkoani Morogoro Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto katika ubora wa taa za barabarani na upungufu wa vivuko katika maeneo yenye watu wengi. Kamati ilitoa ushauri mbalimbali uliolenga kutatua changamoto zilizobainika. Kamati ilipata fursa nyingine ya kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri zilizo katika Mkoa wa Tabora (H/M-Tabora, H/W za Nzega na Igunga).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipata fursa ya mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe kuhusu uelewa wa maoni ya ukaguzi wa Hesabu na namna ya kuhoji maafisa masuuli. Mafunzo hayo yalifanyika mjini Singida kuanzia tarehe 19 hadi

24 machi, 2018 kwa ufadhili wa program ya *PFRMP* iliyotekelezwa kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Aidha, kupitia mradi wa LSP II, Kamati ilipata fursa ya kupata semina mbili za mafunzo ya utekelezaji wa Bajeti na ufuatiliaji matumizi ya fedha za umma. Vilevile Kamati ilipata fursa ya kupata Semina kutoka Taasisi ya Wajibu yenye maudhui kama hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kufanyika kwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe mara kwa mara ni jambo la muhimu sana kwani inasaidia kuongeza tija, ufanisi, uwajibikaji na utawala bora katika usimamizi wa matumizi wa fedha za umma.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI *(CAG)*

### 2.1 Maelezo ya Jumla kuhusu Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kutambua jitihada zilizofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi *(NAOT)* kwani katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri zote 185 nchini zilikaguliwa na kupatiwa Hati ya Ukaguzi *(Audit Opinion)* kulingana na matokeo ya Ukaguzi uliofanyika. Hatua hii inaonyesha ongezeko kubwa katika jitihada za usimamizi wa matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa nchini. Ongezeko hili ni sawa na **asilimia 7.6** ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita 2015/2016 ambapo Halmashauri 171 tu ziliweza kukaguliwa. Aidha, ongezeko hili ni zaidi ya **asilimia 11.4** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2014/2015 ambapo Halmashauri 164 tu ndizo zilikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.


Aidha, Mwenendo wa hati za Ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha miaka minne mfululizo 2013/14 hadi 2016/17 unaonesha kuwepo kwa ongezeko la Hati zinazoridhisha na kupungua kwa Hati zenye shaka, zisizoridhisha na mbaya katika kipindi hicho kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 2**

**Jedwari Na. 2**: Mwenendo wa hati za Ukaguzi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha miaka minne mfululizo (2013/14 hadi 2016/17).

| Mwaka | Hati Zinazoridhisha | Hati Zenye Shaka | Hati Zisizoridhisha | Hati Mbaya |
|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 166 | 16 | 3 | 0 |
| 2015/2016 | 138 | 32 | 1 | 0 |
| 2014/2015 | 47 | 113 | 3 | 1 |
| 2013/2014 | 150 | 13 | 0 | 0 |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/17*

**Mheshimiwa Spika,** ufafanuzi zaidi wa ulinganisho kati ya mwenendo wa idadi za Hati zinazoridhisha na Hati zenye shaka kuanzia mwaka 2013/14 hadi mwaka 2016/17 unaonekana katika **Chati namba 1**.




za Ukaguzi
4) kuanzia

**Chanzo:***Jedwali namba 2*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini ongezeko la Hati zinazoridhisha, hali ambayo inaonyesha kuendelea kuboreshwa kwa utendaji na uwajibikaji katika Halmashauri zetu nchini. Idadi ya Hati zinazoridhisha imeongezeka kutoka 132 katika mwaka 2015/16 hadi kufikia hati 166 katika mwaka wa fedha 2016/17. Kadhalika, hati zenye shaka zimepungua kutoka hati 32 katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi kufikia hati 16 katika mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio yaliyoelezwa hapo juu Kamati inasikitishwa na mwenendo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji ambayo imeendelea kupata hati isiyoridhisha kwa miaka mitatu (3) mfululizo licha ya hatua mbalimbali kuchukuliwa na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma (RAS). Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kuwasimisha kazi na kuwahamisha wafanyakazi, lakini bado uwezo wa Halmasahuri hiyo kusimamia fedha za umma umeendelea kuwa mbaya zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Zaidi ya hapo kuna Mamlaka za Serikali za mitaa za Wilaya ya Longido, Rombo, Korogwe na Ukerewe ambazo zimeendelea kupata hati zenye mashaka kwa miaka mitatu mfululizo. Kujirudia kwa hati hizo kumetokana na Halmashauri hizo kutoboresha taarifa zao kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo:-

(i) Vigezo vya kuandaa taarifa za fedha katika Sekta ya Umma;

(ii) Usimamizi wa mali za Umma usiozingatia Sheria na Kanuni;

(iii) Malipo yasiyostahili kutoka kwenye akaunti ya Amana kwa mfano H/W Korogwe iliweza kutoa kiasi cha shilingi **milioni 569.1** kwenye akaunti hiyo na kutumia kama fedha za matumizi ya kawaida (OC);na

(iv) Upotevu wa vitabu vya kukusanyia mapato kwa mfano H/W Longido (vitabu 22) na H/W Mbinga (vitabu 4).

## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi huu umezingatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambao umebainisha maeneo mbalimbali yenye matatizo sugu ambayo Kamati hii imeweza kuyatolea ufafanuzi na mtazamo jumuifu ili kulisaidia Bunge lako kujenga mtazamo wa jumla kuhusu hali na mwenendo wa matumizi ya fedha za Umma kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa muhtasari ufuatao:

### 2.2.1 Udhaifu katika mfumo wa Udhibiti wa ndani

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuendelea kuwepo kwa mapungufu katika usimamizi wa mfumo wa ndani wa udhibiti wa mapato na matumizi. Mapungufu hayo yamekuwa yakichangiwa na Utendaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani *(Internal Audit Unit),* Kamati ya Ukaguzi *(Audit Committee)* na kutokuwepo kwa Sera ya kudhibiti viashiria hatarishi *(Risk Management Policy & Fraud Manangement Policy)*. Mapungufu haya yamekuwa yakisababisha Halmashauri nyingi nchini kukosa mfumo madhubuti wa usimamizi wa mapato na matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini changamoto nyingi katika utendaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani. Ikumbukwe kuwa lengo la kuanzishwa kwa kitengo hiki lilikuwa ni kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani wa mapato na matumizi kwenye Halmashauri zetu. Hata hivyo, Kitengo hiki cha Ukaguzi wa ndani kimekosa ufanisi kutokana na uhaba mkubwa wa rasilimali watu, fedha na vitendea kazi muhimu kama vile Kompyuta, kamera, gari n.k

**Mheshimiwa Spika,** kati ya Halmashauri 58 zilizohojiwa na Kamati Halmashauri 23 ambazo ni sawa na **asilimia 40** zilibainika kuwa na mapungufu makubwa katika Kitengo cha Ukaguzi wa ndani. Hata hivyo, Halmashauri 35 zilizosalia bado

hazikuwa na utendaji unaoridhisha katika Kitengo hiki. Licha ya jitihada kubwa ambazo Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) imekuwa ikizifanya kwa kuendesha mafunzo mbalimbali ya mifumo mipya ya udhibiti wa mapato na malipo kama vile EPICOR, LAWSON, PLANREP na LGRCIS, baadhi ya Halmashauri hazijaweza kutumia mifumo hiyo kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini udhaifu mwingine wa kutotekelezwa kwa Agizo Na. 12 la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya 2009 ambalo linaitaka Kamati ya Ukaguzi ikutane walau mara moja katika kila robo mwaka. Vilevile Kamati imebaini kutozingatiwa kwa muongozo wa usimamizi wa fedha za Umma uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango kuhusu uendeshaji wa Kamati za Ukaguzi. Kipengele hicho kinaelekeza Mwenyekiti achaguliwe kutoka nje ya Halmashauri na awe na uelewa wa masuala ya Uhasibu na Ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri nyingi zimeendelea kuteua Wenyeviti wake kutoka miongoni mwa Watumishi wa ndani kitendo kinacho athiri kwa kiasi kikubwa dhana kusudiwa ya uwazi na uwajibikaji katika Ukaguzi wa ndani na usimamizi wa fedha za umma. Vilevile Wenyeviti wa Kamati hizo wameshindwa kufanya kazi kwa ufanisi na kushindwa kuzisaidia Menejimenti za Halmashauri katika utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini mapungufu katika uanzishaji Sera ya kusimamia vihatarishi *(risk management policy)*. Halmashauri zote zilielekezwa kuanzisha sera hii ya udhibiti wa viashiria hatarishi na kuteua Mratibu katika eneo hilo. Lengo ni kuzisaidia Menejimenti za Halmashauri nchini kutambua viashiria hatarishi punde vinapojitokeza. Katika Taarifa ya Ukaguzi, jumla ya Halmasahuri 71 zilibainika kutoweka rejista ya viashiria hatarishi *(risk management register)* na hakuna hatua zilizochukuliwa kukabiliana na vihatarishi hivyo. Vilevile menejimenti katika Serikali za Mitaa hazina uelewa juu ya umuhimu wa sera hiyo ya vihatarishi na udhibiti wa ndani.

### 2.2.2 Kutotekelezwa kikamilifu kwa maagizo ya Kamati na kutojibiwa kwa Hoja za ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuendelea kusuasua katika kujibu Hoja za Ukaguzi na kutekelezwa kwa maagizo yaliyotolewa na Kamati. Taarifa ya ukaguzi imeonesha hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2015/2016 mapendekezo 14 yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hayakuwa yametekelezwa kikamilifu. Katika mapendekezo hayo, mapendekzo tisa (9) sawa na **asilimia 64** yalikuwa yakiendelea kutekelezwa na mapendekezo matano (5) sawa na **asilimia 36** yalikuwa hayajashughulikiwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Hali hiyo imeendelea kuonekana pia kwa upande wa maagizo yanayotolewa na Kamati kwa kuzingatia Taarifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Bado hali ya utekelezaji wa mapendekezo siyo ya kuridhisha sana kwani kati ya mapendekezo 748 yaliyotolewa na Kamati kwa halmashauri zilizohojiwa, mapendekezo 233 sawa na **asilimia 31** yalitekelezwa, mapendekezo 256 sawa na **asilimia 34** yapo katika hatua za utekelezaji na mapendekezo 259 sawa na **asilimia 35** hayajatekelezwa kabisa.

**Jedwari Na. 3:** Muhtasari wa majibu ya Hoja za Ukaguzi na utekelezaji wa maagizo ya Kamati kwa miaka mitatu (3) mfululizo (2013/14 hadi 2015/16)

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Jumla ya Mapendekezo | Yaliyoteke-lezwa | Yanayote-kelezwa | Yasiyoteke-lezwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 115 | 784 | 233 | 256 | 259 |
| Asilimia ya utekelezaji | - | 100 | 29.7 | 32.6 | 33 |
| 2014/2015 | 142 | 1094 | 433 | 231 | 430 |
| Asilimia ya utekelezaji | - | 100 | 39.6 | 21 | 39.3 |
| 2013/2014 | 118 | 900 | 408 | 201 | 291 |
| Asilimia ya utekelezaji | - | 100 | 45.3 | 22 | 32 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/17*

**Mheshimiwa Spika,** Kuendelea kwa mwenendo huu kila mwaka kunatoa taswira mbaya kwa Menejimenti za Halmashauri kuwa zimekosa umakini ama zimekuwa zikipuuza kwa makusudi hoja za Ukaguzi na maagizo ya Kamati. Hali hiyo imeendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa hali ya utendaji katika Halmashauri kwani hoja za ukaguzi na maoni ya Kamati hii zimekuwa zikilenga zaidi kuzisaidia Halmashauri zetu kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya matumizi mazuri ya fedha za Umma. Kamati inaendelea kuisisitizia Serikali juu ya umuhimu wa kuliangalia suala hili kwa ukaribu, ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma.

### 2.2.3 Udhaifu katika uendeshwaji wa Mfuko wa Wanawake na Vijana

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa deni kubwa la Mfuko wa Wanawake na Vijana katika Halmashauri nyingi nchini ambapo deni hilo limeonekana likiendelea kuongezeka kadiri ya siku zinavyozidi kwenda. Hali hii inaonyesha kwa miaka ijayo deni hilo halitaweza kulipika tena na Halmashauri nyingi zitashindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na mapato ya ndani. Kwa mujibu wa Taarifa ya Ukaguzi wa CAG kwa mwaka wa fedha 2016/17 hali ya deni ni kama inavyooneka katika **Jedwali Na. 4**


**Jedwari Na. 4:** Muhtasari wa Deni la Halmashauri katika Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa kipindi cha miaka minne (4) (2013/2014 hadi 2016/2017)

| Mwaka wa fedha | Idadi ya Halmashauri | Kiasi cha Deni (TZS) |
|---|---|---|
| 2016/2017 | 143 | 53,222,719,138 |
| 2015/2016 | 151 | 28,521,878,199 |
| 2014/2015 | 112 | 17,690,754,651 |
| 2013/2014 | 104 | 38,741,094,214 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/17*

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa hali ya ongezeko la deni la Mfuko wa Wanawake na Vijana katika Halmashauri nchini kwa kipindi cha miaka minne (4) kuanzia mwaka 2013/14 hadi kufikia mwaka 2016/17 inaonekana katika **Chati Na. 2**

**Chati Na. 2** Kielelezo cha ukuaji wa deni la Mfuko wa Wanawake na Vijana kwa kipindi cha miaka minne (4), (2013/14 hadi 2016/17)




***Chanzo:*** *Jedwali namba 4*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini kuwa mfumo wa uratibu na usimamizi wa utoaji na ukusanyaji wa mikopo haujawa mzuri katika Halmashauri zetu nchini na hivyo, kusababisha fedha hizo kukosa usimamizi. Kamati imebainika pia kuwa Vikundi vingi vimekuwa vikisuasua kurejesha madeni yake. Hali hii imeathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya ukuaji wa mfuko kwani badala ya fedha hizo kuwa za mzunguko yaani ***"revolving funds"*** fedha hizo zimekuwa hazirejeshwi kwa wakati au kutorejeshwa kabisa. Katika kipindi cha miaka minne (4) kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2016/17 zaidi ya shilingi bilioni 13.9 zilizotakiwa kurejeshwa na vikundi 253 hadi sasa hazijarejeshwa.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na changamoto hizo Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuleta muswada na Bunge

kutunga Sheria ya kusimamia Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kupitia Sheria ya fedha ya mwaka 2018 *(finance Act, 2018)*. Lengo la sheria hii ni kuviwezesha vikundi mbalimbali vya Wanawake na vijana kushiriki katika uzalishaji. Aidha, kupitia sheria ya sasa Kamati inapenda kulipongeza Bunge lako Tukufu kwa kuongeza kipengele cha watu wenye ulemavu, kwa kuwa nguvu kazi hii imekuwa ikisahaulika mara nyingi katika mipango mbalimbali. Hivyo, kuanzia sasa itapelekea kundi hilo kutambulika na kupewa kipaumbele sawa katika ushiriki wa shughuli za uzalishaji.

### 2.2.4 Mapungufu ya usimamizi wa rasilimali watu katika Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Ukaguzi bado imeonesha kuwa kuna changamoto ya upungufu mkubwa wa watumishi katika Serikali za mitaa. Hii imetokana na Ukaguzi uliofanywa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa baadhi ya halmashauri katika kipindi cha miaka mitatu (3) mfululizo. Ukaguzi huo ulizingatia Taarifa ya idadi sahihi ya Watumishi na ujuzi stahiki wa wafanyakazi wa kada mbalimbali. Taarifa imeonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 upungufu ulikuwa **asilimia 22** kwa mamlaka 117 zilizokaguliwa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 upungufu ulikuwa **asilimia 30** kwa mamlaka 126 zilizokaguliwa na kwa mwaka wa fedha 2016/2017 upungufu uliongezeka hadi **asilimia 32** kama inavyojieleza katika **Jedwali Na. 5:** la Taarifa hii.

**Jedwari Na.5:** Muhtasari wa mwenendo wa idadi ya upungufu wa watumishi kwa miaka mitatu (3) kuanzia mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2016/17

| Mwaka | Mamlaka Zilizohakikiwa | Mahitaji | Upungufu | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 161 | 477,829 | 155,013 | 32 |
| 2015/2016 | 126 | 349,974 | 106,426 | 30 |
| 2014/2015 | 117 | 324,577 | 71,803 | 22 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi ya CAG kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/17*

Hali hii, imeathiri Halmashauri nyingi kwani Watumishi wachache waliopo wanalazimika kubeba majukumu ya ziada ili kukidhi matarajio ya wananchi, hivyo, kusababisha huduma zinazotolewa kutokuwa na ubora wakuridhisha, hususani kwenye sekta ya Afya, Elimu na Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeendelea kukutana na changamoto ya Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miezi sita. Hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuchelewa kwa upekuzi *(vetting)* wa watumishi kupitia mamlaka mbalimbali ndani ya Serikali. Itakumbukwa kwamba jambo hili limeongelewa sana na Kamati hii katika Bunge lako Tukufu. Licha ya jitihada za Serikali kutatua changamoto hii, Kamati haioni sababu ya kuendelea kuwepo na tatizo hili katika Mamlaka za Serikali za mitaa. Aidha, kwa mujibu wa miongozo na kanuni za utumishi wa Umma [Agizo D 24(3) la Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009] Zimeelekeza wazi kuwa mtumishi yeyote hatatakiwa kukaimu nafasi ya ukuu wa idara au vitengo kwa zaidi ya miezi sita (6).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kiasi kikubwa kanuni hii imekuwa haizangatiwi kwani katika Halmashauri nyingi suala la Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu kwa muda mrefu limekuwa ni la kawaida. Pia, kuna baadhi ya Wakurugenzi katika Halmashauri ambao wamekuwa wakichelewesha mchakato huu kwasababu ya kutofuata taratibu za uthibitishaji. Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imebainisha Halmashauri 10 ambazo zilikuwa na Maofisa 67 wanaofanya kazi kwa kukaimu. Katika mahojiano na Kamati ilithibitika kuwepo kwa tatizo hili katika Halmashauri kadhaa zilizofika mbele ya Kamati. Mfano wa Halmashauri hizo ni H/Mji Ifakara (Watumishi 8), H/W Mbeya (Watumishi 7) na H/W Kigoma (watumishi 6).

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa Halmashauri mpya na zile zilizo pembezoni *(peripheral)* zimekuwa wahanga wa hali hii licha ya mabadiliko mbalimbali ya Serikali. Watumishi hawa wamejikuta mara nyingi kwenye mazingira ya kukosa hamasa ya kufanya kazi

na kushindwa kuwajibika ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuwa na wasiwasi wa kufanya baadhi ya maamuzi. Vilevile wapo baadhi ya watumishi ambao wametumia mwanya huo kufanya kazi kwa maslahi yao binafsi. Hivyo, shughuli nyingi hasa zile ambazo zinahitaji maamuzi zimekuwa zikiathiriwa kutokana na kuwa na idadi kubwa ya Wakuu wa Idara na Vitengo wanaokaimu. Hali hii ikiendelea inaweza kuathiri sana Uongozi katika Halmashauri zetu na kukwamisha utoaji wa huduma za maendeleo kwa Taifa.

### 2.2.5 Utekelezaji wa Miradi ya maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwa Serikali za Mitaa zimeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini. Miradi hiyo imekuwa ikitekelezwa kwa kutumia makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani, fedha kutoka Serikali kuu, michango ya jamii pamoja na misaada kutoka kwa wahisani na wadau wa maendeleo. Ukaguzi huu umebainisha na kuchanganua changamoto na mapungufu mbalimbali ambayo yamekuwa yakiathiri utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo katika Halmashauri zetu.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya ukaguzi inaonyesha ipo miradi 38 ambayo haijatekelezwa kabisa na Mamlaka za Serikali za Mitaa licha ya miradi hiyo kuwa imetengewa fedha. Kati ya Miradi hiyo ipo miradi 13 ambayo imeshindwa kutekelezwa kutokana na kiasi cha **shilingi bilioni 1.05** kutotolewa na Hazina. Pamoja na Miradi hiyo, ipo Miradi 25 ambayo haikutekelezwa kabisa licha ya Mamlaka za serikali za Mitaa 19 kupokea kiasi cha **shilingi bilioni 7.79** kwa ajili ya miradi hiyo. Aidha, Taarifa hiyo imebainisha changamoto ya Miradi kukamilika lakini haitumiki. Imeelezwa kwamba ipo miradi yenye thamani ya **shilingi milioni 782.4** katika mamlaka za serikali za mitaa 13 ambayo imekamilika lakini haitumiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Tatizo la utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni changamoto inayojitokeza katika sura kuu mbili. Changamoto ya kwanza inahusu upatikanaji duni wa fedha za Serikali ambapo ama fedha zilizotengwa hazipelekwi kabisa, au kiasi kidogo tu cha fedha kinapelekwa

na wakati mwingine fedha zinapelekwa kwa kuchelewa sana, hivyo kuathiri miradi. Changamoto ya pili ni kwamba Halmashauri nyingi zina udhaifu katika maeneo ya manunuzi, utoaji wa zabuni na usimamizi wa mikataba *(procurement and contract management)* udhaifu ambao umeisababishia Serikali hasara na upotevu mkubwa wa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia mradi wa *Public Finance Manangement Reform Program (PFMRP),* unaoratibiwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Kamati hii ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) iliwezeshwa kutembelea na kukagua Mradi wa barabara za Tubuyu, Nanenane na Maelewano katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ambayo ilikuwa imekaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu katika Mwaka wa Fedha 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilipanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami nzito *(asphalt concrete)* wenye urefu wa kilomita 4.6 katika barabara za Tubuyu, Nanenane na Maelewano. Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa fedha za mkopo wa Benki ya Dunia *(World Bank)*, kwa thamani ya shilingi bilioni 11.9 kwa mujibu wa makisio ya awali. Lakini, kutokana na kuongezeka kwa siku 150 gharama za mradi ziliongezeka kwa shilingi milioni 649.7 na kufanya gharama mpya ya mradi huo kufikia shilingi bilioni 12.6

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri iliingia mkataba na mkandarasi *M/S Group Six JV Lukoko Company LTD* wenye kumbukumbu namba *LGA/079/2015 – 2016/HQ/W/04* Tarehe 15 Machi, 2017 kwa matarajio kwamba mradi huo kufikia Tarehe 15 Machi, 2018 ungekamilika. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huo ulikuwa umekamilika kwa asilimia 99 na kiasi cha shilingi bilioni 9.91 kilikuwa kimeshalipwa sawa na asilimia 79. Kamati ilielezwa kuwa kiasi cha shilingi bilioni 2.4 kipo kwenye hatua za mwisho kulipwa *(certificate No.9)* huku kiasi cha shilingi milioni 631.5 kikibakizwa kwa ajili ya kipindi cha matazamio (*rentention period).*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini faida ambazo zimetokana na kukamilika kwa mradi huo. Miongoni mwa faida hizo ni kuwa umeboresha mazingira ya makazi kwa wakazi wa mitaa ya Changarawe, Nane nane na Tubuyu. Aidha, umechangia kurahisisha hali ya usafiri katika Manispaa ya Morogoro na kuongeza hadhi ya Mji huo pamoja na kuchochea ukuaji wa biashara mbalimbali kando kando ya barabara hizo. Mbali na mafanikio hayo Kamati imebaini changamoto za kukosekana kwa baadhi ya vivuko vya barabara, kuchelewa kukamilika kwa mifereji ya maji machafu na barabara ya watembea kwa miguu *(pedestrian walk ways)* , kukosekana kwa baadhi ya alama za barabarani na kuwekwa kwa matuta ambayo kiutaalamu hayatakiwi kuwepo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhika na gharama kubwa za Mradi ambapo shilingi bilioni 12.6 zilitumika kujenga barabara yenye **urefu wa kilomita 4.6 tu**. Kwa uzoefu wa kawaida kiasi hicho cha fedha kingeweza kutumika kujenga barabara yenye urefu wa zaidi ya kilomita 10. Baada ya Wajumbe kuomba ushauri kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) walielezwa kuwa mradi huu unafanyiwa ukaguzi mwingine maalum *"comprehensive specific audit"* katika miradi yote inayotekelezwa chini ya mradi huu *Urban Local Government Strengthening Program (ULGSP)* ili kuhakiki upya gharama na ubora wa mradi huo. Hivyo, Wajumbe walikubaliana kusubiri Taarifa hiyo ya uchunguzi ili Kamati iweze kuishauri Serikali vizuri juu ya hatua zaidi zinazopaswa kuchukuliwa.

### 2.2.6 Changamoto katika usimamizi wa mali

**Mheshimiwa Spika**, Agizo la 45(1) la Memoranda ya fedha za Serikali za Mitaa la mwaka 2009 linataka mali zote ambazo hazihitajiki tena, hazitengenezeki au zilizochakaa zitambuliwe na zifutwe kwa idhini ya Baraza la madiwani. Katika mahojiano Kamati iliweza kugundua kati ya Halmashauri 58 ambazo zilihojiwa Halmashauri 19 ziliripotiwa kuwa na tatizo katika usimamizi wa mali chakavu. Hii ilitokana na baadhi ya Halmashauri hizo kutofuata taratibu za ufutaji wa mali hizo na nyingine zilitoa sababu ya kukosa fedha za

kukamilisha mchakato huo. Kutokana na hali hiyo Kamati inaona Serikali itaendelea kupata hasara kubwa kwani kuendelea kuwepo kwa mali chakavu katika Halmashauri hizo kwa muda mrefu kunapelekea mali hizo kushuka thamani zaidi na kushindwa kuuzika tena.

**Mheshimiwa Spika,** Lipo tatizo lingine la magari ya Halmashauri kukosa bima, kwani kwa mujibu wa Agizo la 95 (1) la memoranda ya fedha ya Serikali za Mitaa, 2009 ambalo linawataka maafisa usafiri kuhakikisha kuwa magari yote yanawekewa bima dhidi ya majanga yasiyotarajiwa na kuhakikisha malipo ya bima yanafanyika kwa wakati uliotakiwa. Kwa kiasi kikubwa katika baadhi ya Halmashauri utaratibu huo umekuwa haufuatwi, hivyo kupelekea matumizi ya magari pamoja na vyombo vingine vya usafiri kutumika bila kuvikatia bima kwa muda mrefu. Zipo Halmashuari tano ambazo zilikutwa na Idadi kubwa ya magari ambayo hayajakatiwa bima kwa muda mrefu. Halmahsauri hizo ni pamoja na H/W Kwimba (Magari 25), H/W Ileje (Magari16), H/Mji Iringa (Magari16), H/Momba (Magari15) na H/W ya Shinyanga (Magari13)

### 2.2.7 Mambo muhimu yaliyobainika katika Ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kipindi cha kuanzia 2012/13 hadi 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kuijadili Taarifa ya Ukaguzi wa Halmasahuri ya Wilaya ya Kaliua ilibaini uwepo wa mambo yakutilia shaka katika matumizi ya fedha za umma. Hali hiyo ilisababisha Kamati hii kutoa maombi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi maalum kwa Halmashauri hiyo. Ukaguzi huu maalum umeisaidia Kamati kubaini ubadhirifu mkubwa wa fedha unaokadiriwa **shilingi bilioni 3.5** za miradi ya maendeleo uliosababishwa na matumizi mabaya ya madaraka katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kumwezesha mdhibiti na Mkguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali kurahisisha ukaguzi huo. Kamati iliainisha hadidu za rejea nne (4) kama ifuatavyo:-

(i) Kupitia taratibu zote zilizotumika katika kumpata Mkandarasi *Saram Co. Ltd* katika zabuni za ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi na Kituo cha Afya kwa thamani ya **shilingi bilioni 1.2**;

(ii) Kukagua fedha zilizopangwa kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo kama zilitumika kama ilivyokusudiwa;

(iii) Kukagua mifumo ya udhibiti wa ndani *(internal control systems)* na Sera ya vihashiria hatarishi *(risk management policy)* kama zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria ;na

(iv) Kukagua maeneo mengine ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo ataona yanaviashiria vya ubadhirifu *(extension of scope).*

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi huu maalum umeisaidia Kamati kubaini mambo mengi ambayo yamefanyika bila nidhamu ya usimamizi wa fedha za umma ***(financial in discpline)*** na ukiukwaji wa taratibu na kanuni zinazosimamia masuala ya fedha. Katika matokeo ya Ukaguzi huu Kamati imebaini kuwa kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria ya manunuzi ya umma, kuingiliwa kwa bodi ya zabuni, kuingiliwa kwa kamati ya tathimini na kitengo cha menejimenti ya ununuzi. Ukaguzi huo umebaini jumla ya kiasi cha **shilingi bilioni 3.5** kimetumika vibaya na kina sura ya kijinai kama ifuatavyo:-

(i) Malipo ya awali ya shilingi milioni 121.7 yaliyofanyika kwa kutumia nyaraka za dhamana toka Benki ya Equity. Nyaraka hizo zilighushiwa na mkandarasi.

(ii) Malipo ya awali ya shilingi milioni 51.6 hayakurejeshwa na Mkandarasi na hivyo kusababisha hasara kwa Halmashauri.

(iii) Fedha kiasi cha shilingi milioni 11.3 alizolipwa mkandarasi ni zaidi ya thamani ya kazi zilizofanyika kwa mujibu wa mchanganuo wa gharama za kazi zilizotekelezwa.

(iv) Malipo yaliyofanyika kwa mkandarasi bila kuonyesha vipimo vya kazi na mchanganuo wa kazi zilizofanyika kiasi cha shilingi milioni 197

(v) Malipo ya shilingi milioni 27.6 kwa mkandarasi kwa kazi ambazo hazikufanyika katika mradi wa ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD)*

(vi) Malipo ya shilingi 44.7 milioni kufanyika mara mbili kwa mkandarasi kwa kazi zilizofanyika katika mradi wa ujenzi wa nyumba za watumishi.

(vii) Udanganyifu wa shilingi milioni 178 katika ununuzi na hati za malipo na kutozingatia masharti ya sheria za ununuzi.

(viii) Malipo Mkandarasi kwa kazi za mfuko wa barabara kwa kazi ambazo hazikufanyika kiasi cha shilingi milioni 31.6.

(ix) Malipo yalipo shilingi milioni 393.6 yaliyofanyika katika akaunti ya Amana ambayo hati zake hazijawasilishwa kwa ukaguzi.

(x) Matumizi ya kiasi cha shilingi milioni 78.5 yenye mashaka kwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa maabara

(xi) Usimamizi dhaifu katika ukusanyaji wa ushuru wa tumbaku uliopelekea kutokukusanya mapato ya zaidi ya shilingi bilioni 1.35

(xii) Malipo mbalimbali yenye viashiria vya ubadhirifu na kughushi nyaraka yenye kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 1.02

**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyoelezwa awali uchambuzi wa Kamati kuhusu Ukaguzi huu maalum umebaini kwamba ni Watumishi wawili (2) tu wa kitengo cha manunuzi kati ya Watumishi 66 wa halmashauri waliobainika kuhusika na ubadhirifu huu ndio wamechukuliwa hatua. Ukaguzi maalum umebainisha kwamba moja wapo ya chanzo kikubwa cha ubadhirifu huu ni matumizi mabaya ya madaraka yaliyotumiwa na Mkuu wa Mkoa (wa wakati huo) Bi. Fatma

Mwasa katika miradi iliyotekelezwa na Kampuni ya Saram Co. Ltd kwa kuwelekeza Mkurugenzi, Wenyeviti wa Kamati za Tathimini, Bodi ya Zabuni na Mkuu wa Kitengo cha ununuzi kutoa zabuni kwa Kampuni hiyo ya Saram Co. Ltd ambayo Mkurugenzi wake ni mtu mwenye mahusiano ya ndani na Mkuu wa Mkoa wa wakati hu.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijikita zaidi katika maeneo saba (7) ambayo yameonekana kuwa na matatizo sugu katika matumizi ya fedha za umma. Katika maelezo ya awali, msingi wa kazi ulitoakana na Taarifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 ukifuatiwa na mahojiano kati ya Kamati na Halmashauri 58. Kufuatia uchambuzi uliofanywa na Kamati hii kwa niaba ya Bunge lako Tukufu naomba niwasilishe maoni na mapendekezo saba (7) kwa niaba ya Kamati ili Bunge lako Tukufu liyajadili na hatimaye kuyaafiki ili yaweze kuwa sehemu ya Maazimio ya Bunge. Lengo ni kusimamia na kuhakikisha kunakuwa na nidhamu ya Matumizi ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa.

### 3.2 Maoni (Opinion)

**Mheshimiwa Spika**, Sambamba na lengo la Bunge kama chombo kikuu cha uwakilishi, Kamati imetunza mtazamo wa kuhakikisha kwamba matumizi ya fedha za umma yanaendelea kuwanufaisha wananchi wote. Kamati imeendelea kusimamia sheria za matumizi bora ya fedha za umma na kuishauri Serikali kila mara inapokosea, lengo likiwa ni kuboresha huduma za jamii kupitia Serikali za Mitaa ambako ndiko wananchi wote walipo.

### 3.3 Mapendekezo (Recommendations);

**Mheshimiwa Spika,** Naomba sasa nitoe mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo

### 3.3.1 Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa ndani

**Kwa kuwa** Imebainika kwamba kuna udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani wa mapato na matumizi katika Halmashauri kutokana na utendaji usioridhisha wa Kitengo cha Ukaguzi wa ndani *(Internal Audit Unit)*, Kamati ya Ukaguzi *(Audit Committee)* na kutokuwepo kwa Sera ya kudhibiti viashiria hatarishi *(Risk Management Policy)* ;

**Na kwa kuwa** Udhaifu huo umeathiri kwa kiasi kikubwa nidhamu katika Halmashauri na kusababisha kuongezeka kwa matumizi mabaya ya fedha za umma;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge liazimie kuwa:-

a) Serikali ihakikishe kuwa katika kila Halmashauri Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kinapewa rasilimali watu, fedha za kutosha na vitendea kazi muhimu kama vile kompyuta, kamera, magari n.k;

b) Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) ihakikishe kuwa Kamati ya Ukaguzi inakutana katika kila robo ya mwaka na kutoa Taarifa ya mrejesho wa Vikao hivyo. Aidha, ihakikishe pia kila Halmashauri inaanzisha mfumo wa kudhibiti viashiria hatarishi ili kuondokana na uwezekano wa kupata hasara;na

c) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali *(Internal Auditor General)* pamoja na Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) waweke utaratibu wa ufuatiliaji wa utendaji kazi wa Vitengo vya Ukaguzi wa ndani katika Halmashauri nchini. Vilevile Kitengo cha ukaguzi na ufuatiliaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kilichopo katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kiwezeshwe kwa kupewa rasilimali watu na vitendea kazi muhimu.

### 3.3.2 Kutekelezwa kikamilifu maagizo ya Kamati na kujibiwa kwa hoja za ukaguzi

**Kwa kuwa** Halmashauri nyingi zimebainika kutotekeleza kikamilifu mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo ya Kamati;

**Na kwa kuwa** kuendelea kutotekelezwa kwa mapendekezo hayo kunajenga taswira mbaya kwa kazi inayofanywa na Kamati hii pamoja na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

a) Serikali kupitia Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) ichukue hatua za kisheria na za kinidhamu kwa Menenjiementi za Halmashauri ambazo zimekuwa zikishindwa kutekeleza mapendekezo haya kwa wakati;na

b) Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) ihakikishe kuwa Mtumishi yeyote atakaye bainika kuhusika na matumizi mabaya ya fedha za umma asihamishwe kituo cha kazi mpaka shauri la Mtumishi huyo litakapoisha.

### 3.3.3 Kuboresha uendeshwaji wa Mfuko wa Wanawake na Vijana

**Kwa kuwa** Imebainika kwamba Halmashauri nyingi hazina uwezo wa kulilipa deni la zamani la Mfuko wa Wanawake na Vijana na kwamba bado hakuna mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa madeni hayo toka kwenye Vikundi;

**Na kwa kuwa** Hali hii ikiendelea inaweza ikakwamisha nia njema ya Serikali ya kuviwezesha vikundi hivi;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

a) Serikali iharakishe mchakato wa utungaji wa kanuni za Mfuko wa Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu ili kuweka mfumo rasmi wa usimamizi wa Mfuko huo; na

b) Serikali izifutie Halmashauri madeni ya nyuma ya Mfuko wa Wanawake na Vijana kwani fedha ambazo hazikuchangiwa kwenye Mfuko huo zilitumika katika uendelezaji wa Halmashauri na utekelezaji wa shughuli

nyingine za mendeleo. Aidha, fedha ambazo zilikuwa zimeshakopeshwa katika vikundi ziendelee kukusanywa kama ilivyo katika utaratibu wa awali.

### 3.3.4 Kuimarisha usimamizi wa Rasilimali Watu katika Serikali za Mitaa

**Kwa kuwa** Kumebainikika kuwepo na upungufu mkubwa wa Watumishi katika Halmashauri nchini na kwamba taratibu za upekuzi na uthibitishwaji wa Wakuu wa Idara na Vitengo huchukua muda mrefu, hali inayopelekea Watumishi hao kukaimu kwa muda mrefu zaidi ya miezi sita tofauti na Sheria za Utumishi wa Umma zinavyoelekeza;

**Na kwa kuwa** Upungufu huo umeendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa hali ya utendaji katika Halmashauri nchini;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa;

(a) Serikali iongeze jitihada za kuajiri watumishi wa Halmashauri hususani katika sekta za kilimo, afya na elimu ili kuboresha hali ya ubora wa huduma zitolewazo kwa jamii; na

(b) Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ziangalie njia bora ya kuharakisha mchakato wa kuwathibisha Watumishi ili kuwaongezea morali zaidi katika utendaji.

### 3.3.5 Kuboresha usimamizi na utekelezaji wa Miradi ya maendeleo

**Kwa kuwa** Imeendelea kuonekana kuwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni mdogo sana ukilinganishwa na matarajio ya Serikali na Wananchi ya upatikanaji wa huduma bora;

**Na kwa kuwa** Hali hii imeendelea kukwamisha utoaji wa huduma kwa wananchi sambamba na jitihada za kimaendeleo;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

a) Serikali iboreshe eneo la usimamizi katika Halmashauri pamoja na kuzijengea uwezo Halmashauri zote kwa kuajiri wataalam kwenye sekta mbalimbali;

b) Uwekwe mfumo mzuri wa kusimamia taratibu za utoaji zabuni kwa wakandarasi ili kuondoa mazingira ya vitendo vya rushwa; na

c) Mfumo wa malipo baada ya kazi yaani *"certificate award"* uangaliwe upya na ikiwezekana uboreshwe ili kuwaondolea Wakandarasi ukiritimba mwingi kipindi wanapodai haki zao.

### 3.3.6 Kuimarisha usimamizi wa mali

**Kwa kuwa** Imebainika kwamba Halmashauri nyingi zimeendelea kukaa na mali chakavu kwa muda mrefu ilihali upo utaratibu wa ufutaji *(disposal)* wa mali hizo na kwamba Serikali za Mitaa zinatakiwa kulipia bima mali zake husasan Magari, wakati Serikali kuu hailazimiki kufanya hivyo;

**Na kwa kuwa** kuendelea kuwa na mali chakavu kunaiongezea hamashauri gharama za uendeshaji na utunzaji wa mali hizo, na kwamba ulipaji wa bima kwa magari ya halmashauri kunaziongezea gharama isiyo ya lazima kuzingatia uwezekano *(probability)* ya magari yote kupata ajali kwa wakati mmoja

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa;

a) Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) ihakikishe kuwa Halmashauri zinafuta mali chakavu na kuondokana kabisa na tabia ya kurundika mali chakavu;

b) Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ifanye utaratibu wa kurahisiha ufutaji wa mali hizo ikiwezekana madaraka hayo yakasimishwe kwa Mhakiki Mali wa Mkoa; na

c) Serikali ianzishe mchakato wa kuzifutia bima ya magari na vyombo vingine vya usafiri Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kufanya hivi kutazipunguzia halmashauri gharama za uendeshaji lakini pia kuleta usawa kwani magari ya Serikali kuu hayalipiwi bima.

### 3.3.7 Mambo muhimu yaliyobainika katika Ukaguzi maalum

**Kwa kuwa** Imebainika kuna ubadhirifu wa fedha za miradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kilichofanyika katika kipindi 2012/13 hadi 2016/17;

**Na kwa kuwa** Hadi sasa Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) imepokea Taarifa hiyo lakini hatua stahiki hazijachukuliwa dhidi ya wahusika wote walioshiriki katika ubadhirifu huo;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie kuwa:-

a) Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) ichukue hatua stahiki dhidi ya wahusika wote walioshiriki katika ubadhirifu huo mara moja, kwani suala hili lina sura ya kijinai;

b) Watumishi wanaohusika moja kwa moja na ubadhirifu huu warejeshwe kwenye Kituo hicho ili waweze kujibu tuhuma hizo za jinai;

c) Taarifa hii ya ukaguzi maalum ikabidhiwe vyombo vya dola kwa ajili ya kuendelea na taratibu za kisheria

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya kamati naomba kuchukua fursa hii kukupongeza wewe kwa uongozi wako uliouonyesha katika kipindi chote hiki cha Bunge la 11 mpaka kufikia sasa.

Umeweza kuwa karibu nasi na kutupatia ushirikiano mkubwa hasa pale Kamati inapohitaji muongozo wako katika kufanikisha shughuli mbali mbali za Kamati na kuhakikisha nchi yetu siku zote inakuwa na nidhamu kubwa katika usimamizi wa fedha za umma. Aidha, nitoe shukrani zetu kwa Naibu Spika na Viongozi waandamizi wote wa Bunge kwani wamekuwa wakikusaidia vyema katika kuliendesha gurudumu hili na hadi leo matunda ya umoja wenu tunayaona na tunazidi kuyafurahia.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Ndg. Steven Kagaigai Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wa hali na mali anaozidi kutupa na kuhakikisha kuwa hatukwami. Napenda pia kumshukuru Ndg. Athuman Hussein Mkurugenzi wa Kamati za Bunge na Ndg. Michael Chikokoto Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge. Wamekuwa nasi bega kwa bega katika kipindi chote hiki wakihakikisha kwamba shughuli zetu zinafanikiwa. Naomba pia kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kuhakikisha Kamati hii inapata muongozo makini na wakina katika Mahojiano yake na Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kutambua mchango wa Mhe. Suleiman Jafo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwani amekuwa nasi karibu katika wakati wote wa utekelezaji wa shughuli zetu na aliposhindwa kuja yeye alihakikisha manaibu wake hawakosi kwenye Kamati hii pale wanapohitajika. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa Mhe. Josephat Sinkamba Kandege ambaye tumekuwa naye kwa kipindi chote hiki cha shughuli za Kamati. Naomba pia, kumpongeza Mhe. Mwl. Mwita Mwikabe Waitara ambaye ameteuliwa hivi karibuni kama Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, (TAMISEMI). Napenda pia kumpongeza Mhandisi Joseph Nyamuhanga kwa Kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu katika Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) pamoja na watumishi wote katika Ofisi yake, hasa Watumishi kutoka kitengo cha usimamizi na ufuatiliji wa Fedha katika serikali za mitaa kwa ushirikiano wao waliotupa katika kipindi chote hiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati yangu, nachukua fursa hii pia kumshukuru Mhe. Abdallah Dadi Chikota ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii kwa ushirikiano mkubwa anaonipa wakati wote wa utekelezaji wa shughuli za Kamati. Aidha, napenda kuwapongeza Makatibu wa Kamati hii Ndg. Dismas Muyanja na Ndg. Victor Mhagama wakisaidiwa na Ndg. Waziri Kizingiti kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinaratibiwa vizuri na kwa mafanikio makubwa ikiwemo na Taarifa hii ya leo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba sasa nitoe heshima ya pekee kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii ambao wamekuwa ndio msingi wa utekelezaji wa Kazi zote za Kamati hii. Naomba kuwatambua kwa kuwataja na majina yao pia yaweze kuingia kwenye Hansard kwa ajili ya kumbukumbu za Taifa hili. Na sasa nita wasoma kama ifuatavyo:
1.Mhe. Vedasto Edgar Ngombale,(Mb) - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Abdallah Dadi Chikota,(Mb) – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Seif Ungando Ally, (Mb)
4. Mhe. Tauhida Cassian Gallos, (Mb)
5. Mhe. Rose Kamili Sukum, (Mb)
6. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, (Mb)
7. Mhe. Mary Pius Chatanda, (Mb)
8. Mhe. Faida Mohammed Bakar, (Mb)
9. Mhe. Tunza Issa Malapo, (Mb)
10. Mhe. Ezekiel Magolyo Maige, (Mb)
11. Mhe. Selemani Jumanne Zeddy, (Mb)
12. Mhe. Juma Kombo Hamad, (Mb)
13. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, (Mb)
14. Mhe. Anastazia James Wambura, (Mb)
15. Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, (Mb)
16. Mhe. Mangungu Ali Issa, (Mb)
17. Mhe. Martin Mtonda Msuha, (Mb)
18. Mhe. Edward Franz Mwalongo, (Mb)
19. Mhe. Alex Raphael Gashaza, (Mb)
20. Mhe. Zainab Mussa Bakar, (Mb)
21. Mhe. Prof. Norman Adamson Sigalla King, (Mb)
22. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, (Mb)
23. Mhe. Azza Hamad Hillal, (Mb)

24. Mhe.Dkt Godwin Oloyce Mollel (Mb)
25. Mhe. Ahmed Ally Salum, (Mb)
26. Mhe. Eng Christopher Kajoro Chiza (Mb)

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuyajadili mapendekezo ya Kamati hii na kuyapitisha ili yaweze kuwa sehemu ya Maazimio ya Bunge kuhusu usimamizi wa matumizi ya fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa Hoja.

Vedasto Edgar Ngombale, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**
1 Februari, 2019

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na utaratibu wetu ninayo majina hapa ya wachangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Boniventura Desdery Kiswaga atafuatiwa na Mheshimiwa Allan Kiula.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee kwa Kanuni hizo ukisema Kuhusu Utaratibu maana yake unamzungumzia aliyekuwa anazungumza hapa mbele ndiyo utaratibu wako unamhusu yeye?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, inahusiana na Kanuni ya kinachoendelea, Kanuni ya 117(15) ambayo inaenelezea Kamati za Kudumu za Bunge kuwasilisha taarifa Bungeni. Sasa wametoka kuwasilisha taarifa Wenyeviti wawili, Mwenyekiti wa *LAAC* na Mwenyekiti wa *PAC.* Kwenye taarifa ya Mwenyekiti wa *PAC* inazungumzia ukaguzi maalum

uliofanywa na *CAG* wa shilingi 1.5 tilioni. Sasa katika taarifa za ukaguzi huwa tuna taarifa za Serikali Kuu ambayo *PAC* anawasilisha na taarifa za Serikali za Mitaa ambayo *LAAC* anawasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunatambua kwamba kutokana na hii taarifa kubwa *CAG* alifanya Ukaguzi Maalum wa shilingi trilioni 1.5 ambao uko kwenye ripoti, lakini Wabunge...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa. Anatumia Kanuni gani huyu mbona hatuambii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga naomba ukae, Mheshimiwa Halima malizia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili taarifa ya *CAG* hii hapa ya Serikali Kuu ambayo ndani yake kuna hoja ya shilingi trilioni 1.5 ambayo ambayo *CAG* amefanya Ukaguzi Maalum wa Mfuko Mkuu wa Hazina. Sasa Bunge lako Tukufu mbali ya kuwa na taarifa hii inatakiwa iwe na taarifa ile ya Ukaguzi Maalum ili wakati wa majadiliano iweze kuangalia taarifa kubwa ilisema nini, taarifa ya Ukaguzi Maalum ilisema nini, taarifa ya Kamati ya *PAC* imesema nini ili tuweze kujadiliana kwa ufanisi. Sasa tunavyozungumza sasa tunajadiliana kwa kadri ambavyo Kamati ya *PAC* imetaka na siyo taarifa ya Mkaguzi imesema nini. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Na *LAAC*.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ndiyo na *LAAC* vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Kanuni hii, naomba Kiti chako kiagize kwa sababu taarifa za *CAG* siyo siri, ni taarifa za umma na Bunge tunajadili taarifa za mwaka, naomba Kiti chako kiagize ili mjadala uweze kuwa na bora, tija na wenye ukweli. Ili tuweze kutoa mapendekezo yenye tija na ukweli kwa Taifa hili Taarifa hiyo Maalum isambazwe kwa Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kujadiliana na kuazimia ipasavyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Halima Mdee amesimama akizungumzia utaratibu ambao kimsingi kanuni zinazohusu utaratibu zinataka kanuni fulani iwe inavunjwa na yule anayezungumza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Halima ametupeleka kwenye Kanuni ya 117(15) akieleza kuhusu Kamati kuleta taarifa kwa Mheshimiwa Spika halafu baadaye kuleta Bungeni ili Bunge liweze kujadili taarifa za Kamati. Wakati akielezea hoja yake anaeleza kwamba Kamati ya *PAC* pamoja na mambo mengine imeleta taarifa inayoonesha kwamba wao walikuwa na taarifa za ziada kwa maana ya kwamba ulifanyika Ukaguzi Maalum kwa ajili ya shilingi trilioni 1.5. Katika maelezo yake amekitaka Kiti kitoe agizo kuhusu kuletwa kwa taarifa hiyo. Mheshimiwa Halima pamoja na maelezo yake yote mpaka sasa hajasema ni kanuni gani iliyovunjwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo, kama ambavyo taarifa ile kubwa wote tunayo, hata hiyo taarifa nyingine maana yake inapaswa kupatikana kwa utaratibu huo huo. Si sehemu ya wakati huu wa mjadala ambao taarifa imeshaletwa na Kamati kuagiza taarifa fulani ije. Kwa sababu utaratibu wa namna tunavyofanya kazi ni kwamba Kamati inapewa mamlaka ya kufanya kazi kwa naiaba yetu sote, tumegawana majukumu kwa mujibu wa kanuni zetu. Maana yake ni kwamba sisi wengine wote ambao tulikuwa na kazi kwenye Kamati zetu wengine tumeshaleta, wengine hatujaleta tutaendelea kujadili hizi taarifa za Kamati kila mtu alivyopangiwa majukumu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya *PAC* hizi taarifa lazima wao wanazo ndiyo maana wametuandikia humu na Bunge hili tunawatarajia kwamba wao watatoa hayo maelezo ambayo sisi tunawaamini kwamba wao wamefanya kazi kule kwenye Kamati. Kwa hivyo, sasa hivi tutaendelea na ratiba yetu iliyo mbele, mtu anayetaka taarifa ya ziada wajumbe tuko nao humu ndani na wanajulikana, kama anaitaka hiyo taarifa anaweza kuipata hivyo. Kwa hiyo,

kwa sasa tutaendelea na michango kwa sababu hakuna kanuni yoyote iliyovunjwa. *(Makofi)*

Tunaanza na Mheshimiwa Kiswaga, atafuatiwa na Mheshimiwa Kiula na Mheshimiwa Juma Kombo Hamad ajiandae.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niipongeze Kamati hii ya *PAC* ikiongozwa na Mama Kaboyoka kwa kadri ambavyo ilijikita kuchambua Taarifa Maalum za Ukaguzi. Maana kitabu hiki chote kina Taarifa Maalum za Ukaguzi. Kwa hiyo, naipongeza sana Kamati hii kwa sababu imefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke wazi jambo hili kwamba watu wengi walihitaji kuingia kwenye Bunge, zaidi ya watu 5,000 tuliokuwa tunagombea nao kwenye Majimbo, lakini Mwenyezi Mungu aliweka kibali cha Waheshimiwa Wabunge 393 tu kuingia ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, sisi ni wateule yale ambayo tunapaswa kuyafanya kwa niaba ya wananchi lazima tuzingatie haki na ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie hapo hapo ambapo wengi wanataka kujua na wananchi wanataka kujua kwamba kwa nini trilioni 1.5 ilileta kizaa zaa kwa Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali. Wengi hapa wanapotosha ukweli na umma unapotoshwa lakini kwa sababu sisi Kamati ya *PAC* ni Kamati makini na ina maadili ilisubiri ripoti halisi ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ameipitia akaileta kwetu. Kamati hii siyo ya *twitter* au *instagram* kwa hiyo tunataka tueleze kwa umma yale yaliyoonekana kwa *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki wa *CAG* na bahati nzuri wanaopotosha tulikuwa nao ndani wakati Mheshimiwa Maida anauliza kwa *CAG* kwamba hebu tupe ufafanuzi wa

shilingi trilioni 1.5 wapotoshaji tulikuwa nao ndani. Kwa mujibu wa *Hansard* Mkaguzi alisema hakuna hata shilingi iliyoliwa baada ya kufanya uhakiki, kwa hiyo, haya mambo ni ya upotoshaji. Ni vizuri tukajikita kueleza umma dosari na yale ambayo tunaweza kuishauri Serikali ili iweze kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, uhakika ni kwamba shilingi trilioni moja haijaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najiuliza sana, hivi nyakati hizi kwa Mheshimiwa Magufuli unaweza ukala shilingi trilioni moja kweli? Nilikuwa nashangaa, hivi hawamjui vizuri Mheshimiwa John, inaweza ikawa hawamjui Mheshimiwa John, lakini nataka kuwahakikishia kwamba sasa mali za Watanzania, miradi ya Watanzania inadhibitiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi ya haki ilikuwa imeharibika na maandiko Matakatifu yanasema, misingi ya haki ikiharibika mwenye haki afanyeje? Kwa hiyo, yaweza kuwa wapotoshaji zamani walikuwa wenye haki lakini misingi ilipoharibika na wao waliharibika. Nataka kukuhakikishia kwamba misingi ya haki sasa inapangwa vizuri, inajegwa vizuri na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa John Pombe Magufuli kwa hiyo mambo yatakwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye kifungu cha 3.1 ambacho kinahusu *NSSF.* Tumethibitishiwa na Ukaguzi Maalum, Kamati imepitia kwa kina tumeuona ubadhirifu mkubwa ulikuwa ukifanywa na *NSSF* kwa kununua viwanja ambavyo havina tija vingine hata tu kuhamisha umiliki kutoka kwa yule aliyenunuliwa haijafanyika na viwanja vingine vimevamiwa. Kamati yetu imependekeza vizuri sana na mimi nataka kuongezea uzito tu na haya yote yalifanywa na wanaopotosha wengine walikuwa viongozi kwenye Kamati hizo leo wanakuja wanageuka. Naomba sasa nipendekeze mambo ili Serikali ya Awamu ya Tano iweze kuchukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* kama Serikali haitaunda Kamati Maalum ya kuchunguza na kuchukua

hatua stahiki tutatia hasara mashirika haya ambayo tumeyaunganisha kwa sasa. Kwa hiyo, tuombe Serikali...

**TAARIFA**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga taarifa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayechangia, wakati huu ubadhirifu mkubwa wa *NSSF* unafanyika Mwenyekiti wa *PAC* alikuwa Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe. Maeneo mengine viwanja vilivyonunuliwa kwa bei kubwa ni Mwandiga ambapo ni nyumbani kwa Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe. Kampuni zilizokuwa zinafanya kazi katika ubadhirifu huo moja ni kampuni ya kiongozi wa *ACT* Wazalendo mpaka sasa hivi, Katibu wa Mkoa wa Mara. Kwa hiyo, hiyo Kamati itakayoundwa imchunguze na Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe kwenye ufisadi huu anahusika 100%. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, unaipokea taarifa hii.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hii. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mmoja akae tafadhali, Mheshimiwa Heche naomba ukae. Mheshimiwa Ester Bulaya, endelea.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba wakati ubadhirifu huu unafanyika Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mama

Gaudentia Kabaka alikuwa Waziri anayeshughulikia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Ndiyo miongoni mwa watu walioleta Muswada na tukamfurusha hapa Bungeni, Muswada wa kunyonga wafanyakazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei taarifa hiyo....

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa. *(Kicheko)*

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Kwa sababau aliyekuwa anaongea alikuwa mwingine.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba uovu na uozo uliofanywa na taasisi hii siyo wa kuvumiliwa. Kwa sababu inaonesha wazi kwamba kilikuwa ni kama kichaka cha upigaji...

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima iundwe Kamati itakayoweza kushughulikia watu hawa. Hawa watu wakipatikana wakusanywe wote wapelekwe huko kizuizini ili kuleta heshima ya nchi. Watanzania wanategemea Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii inapoendesha shughuli zake ilete faida ili *impact* ile iweze kuwasaidia wanachama wake lakini ilionekana kwamba ni kama kikundi ambacho kinaunda, miradi yote haijafanyiwa upembuzi yakinifu, miradi yote imebuniwa na watu wachache sana. Kwa hiyo, niombe sana jambo hili kwa kweli Serikali isilifumbie macho kwa sababu *CAG* ametuletea na sisi Kamati tumetoa mapendekezo yetu hapa. Tunaomba

iundwe Kamati kwa haraka sana ili kuipa nguvu Kamati kwa yale ambayo imeyapendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo Shirika letu la Maendeleo (*NDC)* liliingia uwekezaji na Kampuni ya *IETL* na kuunda kampuni ya *TANCOAL*. Ukaguzi huu Maalum umebaini mapungufu mengi sana hasa ya kimkataba. Mikataba ambayo iliingiwa ni mibovu na haiwezi kuisaidia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, unaingia mkataba ardhi na madini uliyonayo hayakuingizwa kwenye mtaji. Kwa hiyo, ardhi na madini hayo yamekwenda bure, *share* yetu ni fedha taslimu bila kuanzia kwanza ardhi tuliyonayo, hii ni mikataba mibovu sana. Kama ambavyo tumeeleza kwenye taarifa yetu ya Kamati lazima tuhakikishe kwamba ndani ya miezi sita tuna *review* ili mkataba mmoja baada ya mkataba mwingine irekebishwe ili kuleta faida kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imekiukwa mikataba mingi sana. Kwa mfano, Kamati tumebaini kuna fedha nyingi zilikuwa zikilipwa bila kufuata mkataba jambo ambalo kwa kweli limeisababishia hasara Serikali. Kampuni hii haijawahi hata siku kuipa faida Serikali kwa kulipa gawio, kwa hiyo, kila siku inapata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *NDC* kama wabia tumegundua kwenye Menejimenti kuna udhaifu mkubwa sana, kwa hiyo, Menejimenti ni ya upande ule mwingine na Bodi ya Wakurugenzi ipo inaangalia bila kuyaangalia haya makandokando ambayo yanaitia hasara Serikali. Kwa hiyo, pamoja na mambo hayo tuangalie kama kuna mapungufu kwenye Shirika letu la Maendeleo kwa maana ya Menejimenti ibadilishwe na wachukuliwe hatua za kutosha. Kwa sababu huwezi kuwa na Shirika la Maendeleo ambalo haliangalii mbele. Tunaingia uwekezaji ambao hauleti faida kwa nchi, haiwezekani. Kwa kweli hatuwezi kukubaliana na kuendelea na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana yale ambayo Kamati imeyabaini, yale ambayo tumeyapendekeza kwa Serikali, Serikali ichukue hatua mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Allan Kiula atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Hamad Kombo na Mheshimiwa Ali Salim khamis ajiandae.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Kamati yetu. Mimi natoka Kamati ya *PAC,* kwa hiyo, hiyo hotuba ni ya wana-*PAC* wote. Nilivyoona makofi mengi yanatoka upande wa Upinzani nikawa najiuliza maswali mengi sana lakini kumbe hoja hii ilitakiwa isijadiliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuweka kwenye *record* ni kwamba watu wanaotaka ile *verification report* iletwe, maana ule haukuwa Ukaguzi Maalum ilikuwa ni *verification,* hili jambo nalo lifahamike. Mheshimiwa Halima Mdee alikuwepo, Mheshimiwa Ester Bulaya alikuwepo na Mheshimiwa Zitto Kabwe tulikuwa naye. Hata dakika ya mwisho Mheshimiwa Zitto Kabwe alivyokuwa anatoka alituachia maswali ya kuuliza kwa ziada kwa maana tulijua ni Mbunge mwenzetu na tuliuliza yale maswali kupata ufafanuzi kwa sababu kila mtu alitaka ajue ufafanuzi wa shilingi 1.5 trilioni imekwenda wapi.

Nataka kuonesha tu kwamba kama alivyosema mwenzangu kwamba wapotoshaji wako humu humu badala ya kuchukua taarifa wanakuja ili waweze kupotosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo tunaliomba Bunge liweze kuzingatia Maazimio manne yale ambayo hayajatekelezwa kwenye ripoti iliyopita yaweze kufanyiwa kazi. Vilevile, tunaomba Maazimio ya Kamati..

**T A A R I F A**

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Allan Kiula kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa anayeendelea sasa hivi kwamba kwenye hicho kikao anachokisema hata mimi nilikuwepo. Maelezo aliyoyatoa *CAG* alisema hivi, kama Bunge kweli lina nia ya kuisaidia Serikali basi iamue kufanya *scrutiny* na kuona namna vifungu hivyo vilivyotumika ndipo Bunge liseme kama kuna wizi uliotokea au la. *CAG* hana mamlaka ya kusema kama ni wizi au siyo wizi isipokuwa sisi Wabunge tukifanya *Special Audit* tunaweza tukavijua hivyo. Pia tunaomba hiyo ripoti iingizwe humu tuweze kuiona na alisema inatakiwa ifanyike *forensic investigation. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe, naona unatoa taarifa na maombi humo ndani sasa mpokea taarifa ni yule kule sijui kama yeye ndiyo unamuomba hiyo taarifa uliyoomba. Mheshimiwa Kiula unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwambe zima Bwana Mwambe!

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa siipokei. Namheshimu sana Mheshimiwa Mwambe, lakini nafikiri kwamba anatulisha matango mwitu hapa. Hapa subiri tutoe taarifa na ambazo nyingine tumezinukuu ziko humu, tumefanya *quotation,* maana yake Kamati haiwezi kuleta *quotation* za uongo, *quotation* zilizoko humu ni *quotation* sahihi na kama unafikiri unaweza kunitoa kwenye reli huwezi. Ni mti mkavu usiochimbwa dawa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea na uchangiaji wetu kuhusu trilioni 1.5 *CAG* kwenye *verification report* yake ameonesha hesabu zake zime-*balance,* hesabu zake

zimewiana mapato na matumizi. Tumeona kwamba, zilipatikana trilioni 26 ukiangalia kwenye ukurasa wa 24 na matumizi kulikuwa na *over release* ya shilingi bilioni 290 na *over release* aliyoieleza inasababu yake, *BOT* walitoa kibali cha *over release* ya *1.2 trillion* Serikali ikatumia bilioni 290 tu. Kwa maana nyingine kungekuwa na jambo ambalo si sahihi wangeweza kutumia pesa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, Serikali imeonesha *transparency* ya hali ya juu kuruhusu Mfuko Mkuu wa Serikali kuweza kukaguliwa na *CAG* na kueleza mambo yote yaliyoko mle ni jambo kubwa sana. Si hivyo tu, watu wote tunafahamu kwamba ukaguzi unapofanyika wanaangalia *checks and balance* na wanatoa hoja kwa hiyo, hoja ni kitu cha kawaida na baada ya ripoti hii kutolewa Machi ndipo ilipokwenda kufanyika *verification report. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walikuwepo na ndio maana nasema wapotoshaji walikuwepo, maelezo yaliyotolewa na *CAG...*

**MBUNGE FULANI:** Wapeeee!

**MHE. ALLAN J. KIULA:**...na mtu anayehojiwa alisema kwamba wakati ripoti inatolewa ziko *transaction* ambazo zilikuwa hazijawa *recorded.* Moja ya *transaction* ni pesa ambazo zinakwenda *direct to project,* unapopeleka pesa *direct to project* wakati gani una-*recognize?* Na watu wengine, wafadhili wetu *(development partner),* wanapeleka vifaa na nini kwenye *project* moja kwa moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiula kuna Taarifa nyingine. Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Nilikuwa nataka tu kumpa Taarifa mchangiaji kwamba, katika taarifa hii ambayo

tunaijadili ambayo imewasilishwa na Mwenyekiti wa *PAC,* ukurasa wa 18 kuna nukuu pale ya *CAG* kuhusu hiyo tofauti ya trilioni 1.5 na inasema; "*the difference of 1.5 trillion resulted from factors such as differences in information reviewed and adjustment passed by management.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini taarifa hii inaendelea, ukurasa wa 25 tena Taarifa ya *PAC* inamalizia kwamba tofauti ya trilioni 1.5 kati ya mapato na matumizi haikuwepo tena katika Mfuko wa Serikali baada ya ukaguzi na ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba kumpa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiula unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hiyo na kwa taarifa za ziada ndio maana niliamua niende kipengele kwa kipengele. Kwa sababu watu wamesoma humu uhasibu, wamesoma kodi, sasa tunataka tuoneshane hapa tumekwenda hatua kwa hatua na twende sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndio maana tumezungumza suala la pesa ambazo zilikuwa zimekuwa *over spent* na pesa nyingine za Zanzibar zilikusanywa Zanzibar na zilibaki Zanzibar, kwa hiyo, ile *verification report* ilikwenda kufanya usuluhishi wa takwimu zote hizo kwa undani wake na *CAG* mwenyewe akakiri na kwenye *Hansard* inaonesha na kitabu hiki kinafanya nini, kinaonesha kwamba usuluhisho ulifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yapo mambo yalijitokeza na mambo hayo yaliyojitokeza ambayo Kamati ilihoji na tukapata kinachoendelea kule Hazina, tunaipongeza Hazina kwa ku-*adapt* hii *Integrated Financial Management System* inafanyika. Lakini pili, pia kuna *single treasury account.* Hayo mambo yote yalitakiwa yafanyiwe

kazi na yakifanyiwa kazi kwa wenzetu wanaojua kuangalia haya mambo utaona kwamba zile hesabu zitakwenda sawa, sasa na taarifa, *system* zitaongea pamoja na taarifa zitaweza kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la kwamba kwa nini kulikuwa na hoja, *data* zimekwenda kuwa *marched* hizo *data.* Kwa hiyo, suala la *1.5 trillion* ni suala ambalo limekuwa *closed,* limeshahitimishwa na *CAG* alisema suala hilo limehitimishwa, alisema suala hilo limekwisha hitimishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo iko hoja ya *TIB Development,* kuna madeni kule kama tulivyoeleza kwenye taarifa yetu. Tunaomba Serikali suala hilo ilifuatilie na ilifuatilie kwa sababu madeni hayo ukiangalia huku ndani takwimu kwenye ukurasa wa 61 na 62, naomba kunukuu kwa kusoma inasema; "Katika jedwali 24 hapo juu inavyofafanua ni dhahiri kuwa kundi la mikopo inayohesabika kama hasara *(loss loans)* inachukua karibu asilimia 69. Kwa hiyo, *TIB* pia ina-*operate* chini ya *required capital.* Hasa hilo ni jambo muhimu sana ambalo Bunge tuazimie kwa sababu kwenye maazimio yetu yapo na Serikali iweze kulifuatilia kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tulilizungumza na tumelipitia tena ni suala la mikopo ya matrekta. Tunaamini kabisa kwamba haijafanyika juhudi kubwa ya kuweza kukusanya madeni hayo kwa sababu, tunaamini madeni hayo yanakusanyika na kama wenzetu wakichukua hatua za makusudi kuweza kufuatilia tunaweza ku-*recover* hizo pesa ambazo ni pesa za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na mchango wangu ndio huo na suala la *1.5 trilion* ni *chapter closed.* Nashukuru sana, asanteni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Kombo Hamad.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi, nichukue fursa ya kuwapongeza Wenyeviti wote wawili wa Kamati ya *LAAC* na *PAC* kwa kuwasilisha ripoti kwa ufasaha na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nirudi kwa kaka yangu pale Mheshimiwa Allan Kiula kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa maelezo juu ya fedha ulizodai kwamba zilipelekwa Zanzibar na Serikali ilijibu kwamba, hakuna fedha waliyopokea kwa, ile fedha ambayo ilitajwa na *CAG.* Hii fedha... *(Makofi)*

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Taarifa.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:**... hii fedha hakuna, *otherwise* utupatie *document* ambazo zinathibitisha kwamba fedha ile ili...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Kombo kuna Taarifa. Mheshimiwa Kiula.

**T A A R IF A**

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tusilishane maneno, sikusema kwamba, kuna pesa zimekwenda Zanzibar, nimesema pesa zilizokusanywa Zanzibar zilibaki Zanzibar na kwenye Taarifa ya *CAG, verification report* ipo. Sasa muangalie sana kauli zenu, msilishe watu matango mwitu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Waongo madalali hao, madalalii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Kombo unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuache unafiki na uwongo. Hii fedha Waziri wa Fedha alikuja hapa akatuambia kwamba fedha hii ilikwenda Zanzibar na, baada ya kushindwa kuthibitisha ndio mara nyingine akaja tena hapa akatuambia kwamba, fedha hii imekusanywa Zanzibar.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, tusilishane uongo kwa jambo ambalo halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hoja...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kombo naomba ukae kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, twende sawasawa, kwanza tusikilize kwa sababu tunajibizana kwa michango na kwa taarifa iliyoko hapa mbele, tuwe tunasikilizana vizuri ili tusikatishane pale ambapo hakuna sababu. Tusikilizane vizuri, mtu anayechangia kwanza umsikilize vizuri ili unapojibu usizungumze kile ambacho hajasema tunafikia hapo.

Nafikiri hilo limeeleweka, tusikilizane vizuri ili tuweze kwenda sawasawa, tusikilizane kwa makini. Kama unataka kumjibu mwenzio msikilize kwa makini. Mheshimiwa Juma Kombo.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, kuna falsafa ya uongo ambapo muongo anatakiwa awe na kumbukumbu, ili asisahau kile ambacho kwamba anakizusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hoja na nianze na ku-*declare* ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC.* Na nianze na upungufu ambao tuliuona wakati wa kukagua hizi Halmashauri kwamba pungufu moja ambalo tumeliona ni suala la upungufu wa watendaji katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika changamoto kubwa ambayo tunaenda nayo kama Tanzania ni suala la ajira, lakini kila halmashauri ambayo ilikuwa inakuja mbele ya kamati basi unakuta kama kuna kila kitengo kina upungufu wa watumishi au wafanyakazi. Niombe kwa Serikali na TAMISEMI kwamba, suala hili ni vyema walishughulikie kwa sababu, Watanzania wengi hawana ajira na kama hawana ajira kila Halmashauri inayokuja pengine ina upungufu wa asilimia zaidi ya 50 ya watendaji katika Halmashauri, hiki ni kitendo cha aibu kwa Tanzania kwamba, vijana wako wamemaliza chuo, wamemaliza kusoma, lakini nafasi za ajira Tanzania kwenye Halmashauri zetu zipo, lakini kila siku wanapiga kelele ajira hakuna, ajira hakuna, lakini nafasi za vijana kuwaajiri zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali kupitia TAMISEMI ambao ndio *responsible* kwa Halmashauri zetu walitizame hili kwa kina na kwa sababu vijana wapo ambao hawana ajira, hawana kazi, basi wawaajiri ili waende wakatumikie wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo naomba niizungumze ni suala la udhibiti wa mfumo wa wa fedha, Kitengo cha Udhibiti wa Fedha za Ndani. Na hapa pia, kuna changamoto hiyo hiyo kwamba, katika kila Halmashauri, takribani Halmashauri 50 ambazo sisi tumejaribu kuzihoji, basi unakuta kitengo kinahitaji watu wanne, lakini ama kuna mtu mmoja, ama kuna wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni udhaifu mkubwa ambao unajitokeza, lakini pia, kitengo hiki hakina *facility* yoyote. Kina upungufu wa watendaji, kina upungufu wa fedha, kina upungufu wa vifaa kama vile gari, kamera na vitu vingine. Kwa kweli ni jambo ambalo na ukizingatia Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ni kitengo muhimu na ndio jicho la halmashauri, ndio jicho la Mkurugenzi wa Halmashauri. Sasa kama hawezeshi na bahati mbaya sana ya Halmashauri nyingi utakuta mkurugenzi anamfanya kama yule Mkaguzi wa Ndani kama ni adui, kwa maana ya kwamba hataki kumpa taarifa za kina, kwa hiyo, hawezi kumuwezesha

kwenye kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo na kwenye vitabu vya fedha wakati mwingine anamwekea vikwazo mbalimbali na kwa sababu yuko chini yake inakuwa Mkaguzi wa Ndani hana nguvu za kuweza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikaanza kufikiria kwamba wale watu Wahasibu, Wakaguzi wa Ndani kama ikiwezekana na inayowezekana basi wawe nje ya mfumo wa uajiri wa Halmashauri ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi, waweze kuwakabili Wakurugenzi na kuwahoji juu ya masuala ya matumizi ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kutokutekelezwa kwa maagizo ya Kamati. Utakuta kila Halmashauri kama imepewa maagizo kumi, basi ikija imetekeleza maagizo mawili na hii ni aibu sana kwamba Kamati ya Bunge ambayo ipo kwa niaba ya Bunge imetoa maagizo kwenye Halmashauri, maagizo kumi, lakini Halmashauri inakuja mara nyingine au mwaka mwingine imetekeleza maagizo mawili au matatu. Kwa kweli hii ni dharau kubwa na Halmashauri lazima TAMISEMI isimamie vizuri suala hili, Ofisi ya *CAG* isimamie vizuri suala hili, lakini na Bunge litoe maagizo makali na maazimio makali juu ya suala hili la utekelezwaji wa maagizo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ni Bunge, kwa sababu, Kamati ya Bunge ipo kwa niaba ya Bunge haipo kwa niaba kwamba labda ni Mheshimiwa Vedasto au ni Mheshimiwa Mama Kaboyoka, hapana, ni Bunge. Kwa hiyo, maagizo yanayotolewa pale yanatolewa na Bunge. Sasa halmashauri kwenda kukaa kitako wakajishughulisha nyingine bila kutekeleza maagizo yale hii kwa kweli si jambo jema na ni jambo la aibu ambalo mwisho wa siku linakuwa halileti ufanisi mzuri kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba kulizungumza... eeh! Vipi sasa? Hata tano bado!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala la Mfuko wa Wanawake, suala hili lina changamoto nyingi, juzi hapa/ mwaka jana tumepitisha sheria na uko mfumo wa 4:4:2 kwamba asilimia 4 iende kwa waawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu kwa kweli, ilikuwa ni jambo zuri na jambo jema. Lakini halmashauri zote ambazo tumezikagua zimebakia na madeni makubwa katika kipindi hiki kabla ya sheria hii kuipitisha. Ni vyema Serikali itafakari upya kama ikiona kwamba ni jambo la busara basi madeni yale ya nyuma, sio mikopo maana kuna vitu viwili tofauti, kuna mikopo ambayo wamekopa, lakini kuna na madeni ambayo yamebebwa na Halmashauri ambayo kimsingi hayalipwi wala hayatalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie utaratibu mzuri hapa wa kuweka jambo hili, ikiwezekana na ikionekana ni jambo la busara, basi Halmashauri, Taasisi za Serikali zisamehewe madeni yale ya nyuma na sasa tuanze upya na mfumo huu wa 4:4:2 ambao upo kisheria. Na mfumo huu ukisimamiwa vizuri basi tutaweza kuleta ufanisi kwa makundi haya ya akinamama, vijana pamoja na watu wenye ulemavu kuliko kuhangaika sasa na madeni yale ya nyuma ambayo kimsingi hayalipwi na yanatumiwa kama ni muamvuli au ni kichaka cha kujificha kwa hii 4:4:2 ambayo ipo sasa hivi kisheria. Naomba Serikali iliangalie hili vizuri na ikiwezekana walifanyie utaratibu, ili liweze kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende na sakata hili la Halmashauri ya Kaliuwa. Kaliuwa kuna kashfa kubwa na fedheha kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika watumishi 66 ambao walibainika na ripoti ya *CAG* kwamba wamehusika na ubadhirifu wa shilingi bilioni 3.3 ni watumishi wawili tu ambao hadi sasa wamechukuliwa hatua, bahati mbaya sana na hapa nakuwa najiuliza inawezekana wengine wasiridhike, lakini huu ndio ukweli. Nakuwa najiuliza huo utakatifu wa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli uko wapi? Kwa sababu ni lazima tujiulize hata ikiwa kuna watu

litawananihii, lakini huo utakatifu unaozungumzwa humu tena na Wabunge wa Serikali hii uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuishauri Serikali ili iwachukulie hatua watu ambao waepiga fedha za Serikali. Kama shilingi bilioni 3.3 zimepigwa halafu mtumishi/ Mkurugenzi ambaye yuko pale kipindi hiki fedha hizi zinapigwa, alikuwa Mtendaji baadae akawa Mkurugenzi leo ni Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tunakuja hapa tunajisifu kwamba sisi ni watakatifu, Rais anatumbua. Hebu tumuone basi, leo kwa ripoti hii ambayo imemtoa Mkurugenzi huyu kwa Tume ya Uchaguzi ambaye anaitwa Athumani Kihamia, tumuone Rais Dkt. John Pombe Magufuli katoka na kauli na leo kamtumbua. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Kengele imegonga Mheshimiwa, kengele imegonga.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Mmetuchakachua.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane. Mheshimiwa Kangi Lugola mchangiaji ameshamaliza muda wake.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Alikuwa bado anaongea.

*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim Khamis, tutamalizia na Mheshimiwa Stanslaus Mabula. *(Makofi)*

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu siku hii ya leo kuweza kutujalia hapa tukiwa wazima na nikushukuru wewe kunipatia hii fursa kwa ajili ya na mimi kutoa maoni yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti imeeleza wazi na *query* zote ambazo zilitokea ni kwa sababu ya Hazina. Hazina ndio ambao wamesababisha *query* hizi na Mkaguzi ikabidi atoe hoja zake na ninafikiri sote tunakubaliana kwamba na mwisho yametolewa mapendekezo huku kwamba, mfumo wa mahesabu wa Hazina ni shida, kwamba ikiwa leo Halmashauri zinatumia mfumo wa hesabu wa *EPICOR* lakini Hazina inatumia mfumo wa *excel. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli taarifa zimeletwa kutoka Serikalini, lakini bado Mkaguzi aliweka hoja kwa sababu hazikupita katika mfumo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kibaya ni kwamba fedha ambazo zimetoka kwenye Hazina, tuchukue mfano leo Serikali, Serikali ndio inapanga bajeti, wanakaa wanapanga bajeti yao wanakutana na *CAG, CAG* anafanya *approval* akishafanya *approval* inaletwa Bungeni hapa sisi tunapitisha. Sasa ikishapitishwa hapa na Sheria ya Matumizi ikishapitishwa matokeo yake Hazina wanakwenda kubadilisha matumizi ya bajeti ambayo imepitishwa na Bunge pasipo na kumtaarifu *CAG. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna *exchequer* chungu mzima hapa zimeonesha kwamba, kuna fedha zimefanyiwa matumizi ambayo hayakupitishwa na Bunge na wala hakutaarifiwa *CAG,* jambo ambalo lilikuwa rahisi tu. Serikali walikuwa na uwezo wa kwenda kwa *CAG* kutokana na bajeti tunayoipeleka hapa kumetokea dharura hii tufanyie marekebisho hapa tupate *approval* halafu baadaye inaletwa Bungeni kuja kupitishwa pia hili limeshindikana, lakini

Hazina wanafanya halafu baadae ndio Mkaguzi anakuja kuona. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali kuna Taarifa. Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**TAARIFA**

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa na kumkumbusha Mjumbe mwenzangu wa Kamati kwamba Serikali yaani Hazina wanao uwezo wa kufanya *adjustment* kwenye *account* yoyote bila kibali cha *CAG.* Kwa hiyo, Serikali ilipokuja walieleza hilo na *CAG* mwenyewe alikubali kwamba, hiyo inawezekana kufanya mabadiliko yoyote ndani ya *account* ya *BOT.*

**WABUNGE FULANI:** Buuuuu!

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Nampa taarifa Mjumbe wa Kamati au na mkumbusha mjumbe mwenzangu, ninyi nizomeeni na ninyi mlikuwepo wakati anaongelewa hayo, achene uzushi.

**WABUNGE FULANI:** Buuuuu!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali kabla hujaendelea, Waheshimiwa Wabunge kuzomeana pande humu ndani itakuwa hapakaliki, kwa sababu wote tuna fahamu kwamba hizi pande ziko mbili humu ndani, sasa kila upande ukiamua kuzomea hatutaweza kuendesha vikao Bunge. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwakajoka tafadhali, mjifunze kiti kinapoongea unanyamaza unasikiza usiposikiliza ndiyo maana mnarudia makosa hayo hayo kila siku, Mheshimiwa Ali Salim endelea na mchango wako.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi kwanza sina shida na *adjustment, adjustment* ni mambo ya ndani ya utawala, sina shida nayo na wala

sijazungumzia habari ya *adjustment*, mimi nimezungumzia *reallocation.* Kuna *reallocation* mbalimbali ambazo zimefanyika na ndiyo maana CAG ali-*raise query* kwa sababu hazikufata utaratibu kwa mfano... *(Makofi)*

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI :** Mheshimiwa Naibu Spika taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim kuna taarifa kuna taarifa nyingine, mheshimiwa Khadija Nassir.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nipende tu kumpa kumkumbusha Mheshimiwa Ali ambaye ni Mjumbe mwenzangu wa Kamati kwamba *reallocation within the budget* unaweza kufa bila *consultation* ya *CAG,* ahsante nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salum endelea.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unitunzie muda wangu kwa hisani yako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Soika, siipokei kwa sababu siyo utaratibu huo. Kama ikitokea hivyo Serikali inayo mamlaka ya kufanya *reallocation,* hilo halina mjadala, lakini kwa sababu bajeti hii ilishapitishwa Bungeni na Serikali inafanya *reallocation* imtaarifu CAG *approve* hiyo *reallocation* yao. Hilo ndilo tatizo, si kwa sababu...

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tukasikilizana kwa sababu hizi ni taarifa zinazokwenda kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *reallocation within votes, reallocation between votes,* kulingana na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 ni mamlaka ya Waziri wa Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Ali, kwamba kinachotakiwa kurudishwa kwa *CAG* ni kama kungekuwa na *extra budget*, hatujawa na *extra budget* Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo wasiendele kuwapotosha wananchi. Hata hiyo mamlaka ya Waziri wa Fedha na Mipango hatujawahi kutoa ile asilimia iliyotamkwa kwenye sheria Mheshimiwa Waziri wa Fedha hajawai kuitoa yote ili aweze kurudi kwa Bunge au aende kwa CAG, kwa hiyo, walifahamu hilo. *(Makofi).*

**MHE. KABWE. Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto nimesimama kwa hiyo ukae.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wa kikanuni ni huu anayepewa Taarifa ni mchangiaji. Kwa hiyo, mchangiaji ni Mheshimiwa Ali Salim, lazima taarifa ile aliulizwe kikanuni anaikubali au haikubali ili tujuwe inaingia kwenye *Hansard* au hapana? Ninyi mnataka sasa yule akimaliza taarifa uendeleze taarifa tatu hapo, haiwezekani, tufuate utaratibu.

Kwa hiyo, mwache amalize na yule aliyekuwa anampa taarifa likisha isha ilo unaanza lingine, tuwe tunasikilizana usianze kulalia mbele kana kwamba umeshajibiwa, tufuate utaratibu. Mheshimiwa Ali Salim unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei hiyo taarifa kwa sababu kwanza mimi nataka nimfahamishe Mheshimiwa Naibu Waziri. Yeye alileta taarifa hapa Bungeni, na taarifa hii amesema kwamba bilioni 203 zilikuwa *transfered to Zanzibar,* lakini Mheshimiwa Kiula amesema fedha zile zilikusanywa Zanzibar na hazikuondoshwa Zanzibar zilitumika pale pale Zanzibar, sasa hapa dakika kumi zilizopita hapa taarifa zinatofautiana. Ndiyo maana nasema kuna shida ya mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaposema tusikilizane tunasema haya kwa maslahi ya nchi yetu, mimi nimezungumzia kuhusu mfumo...

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim kuna taarifa nyingine.

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim kuna taarifa nyingine, Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwa kumrudisha kwenye taarifa ya CAG na naomba kunukuu; *“A comparison of the allocated funds after the reallocation between votes for financial year 2016/2017 with actual funds released to votes revealed six incidents where amount aggregating nine hundred and seventy six billion were released over and above the allocated funds without appropriate approval.”*

Mheshimiwa Naibu Spika*, I am not saying, CAG is saying. CAG* anamaliza kwa kusema; *"This means the statement of the reallocation differ materially from the approved budget." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Serikali anawezaje kuja ndani ya Bunge akazungumza kinyume na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena kama nilivyomwambia Mheshimiwa Mwande, anayepewa taarifa ni mchangiaji, kwa hiyo usiulize swali kwa sababu hakuna mtu atakujibu hilo swali maana mchangiaji ndiyo unayempa taarifa, Mheshimiwa Ali Salim unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo naipokea na kwa kuongezea tu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto zima *microphone* yako.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** ... baada ya *query* hii ya *CAG* ya shilingi bilioni 976 Hazina ilipeleka *document* za *clear* dola bilioni 1.25 lakini bilioni 975.1 hazijapatiwa majibu mpaka sasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Salim muda wako umekwisha, kengele ya pili imeshagonga. Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na mimi mchana huu nikiamini kwamba kazi tunayoifanya hapa ni kazi ya kuisaidia na kuishauri Serikali na kulisaidia Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe ya Kamati ya *PAC,* pamoja na mambo mengi yaliyozungumzwa lakini pia nasikitika kuamini kwamba na sitaki kuamini kwamba watu wanatamani kusikia mabaya siku zote, lakini wakati

unakumbuka kusikia mabaya lazima tukubaliane na hili wala halina ubishi na mazuri yapo na kazi hizi zinafanywa na binadamu. Kama zinafanywa na binadamu hakuna mwanadamu aliye mkamilifu katika nchi hii au dunia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachotaka kusema *CAG* kwa mara ya kwanza amefanya kazi kubwa sana na ninyi ni mashaidi wakati tunaingia hapa tulilalamika sana suala juu ya kumuwezesha *CAG* kufanya kazi kwenye maeneo makubwa. Kwa mara ya kwanza *CAG* hajakuwa na malalamiko ya kibajeti kwa mwaka wa fedha ulioisha na kazi kubwa sana aliyoifanya. Yeye mwenyewe amedhibitisha, kati ya mashirika 200 aliyotazamia kukagua amekagua mashirika 188, lakini taasisi za Serikali pamoja na taasisi zingine alipanga kukagua taasisi zaidi ya 241 na zote hizo amezikagua kadri alivyoweza na kwa nguvu zake zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukaguzi huu kama nilivyosema haiwezekani watu hawa wote wakawa malaika, lakini makosa ya kibinadamu yanakuwepo. Mimi niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati na Mwenyekiti wa Kamati, mmefanya kazi kubwa na kwa utulivu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nijikite tu kwenye hoja kama tatu hivi; cha kwanza cha kwanza ni *ration* za polisi ni aibu sana na mimi nimuombe kwa sababu Mheshimiwa Kangi yupo hapa ripoti karibu zote tunazozizungumza humu ndani, Mheshimiwa Halima alisema kwamba ripoti moja tu ndiyo ilikuwa ya ukaguzi maalum, tuna ripoti takribani nne ni ukaguzi maalum kwenye taarifa tunayoisoma hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala *ration* za polisi Mheshimiwa Waziri yupo hapa, maana humu tunaweza tunahangaika, kila mmoja amekariri jambo moja, anataka aseme hilo hilo apotoshe afurahi aendelee mbele. Fedha zaidi ya bilioni 888 zimelipwa kwa watu wasiokuwa maaskari wakati askari wetu wanahangaika awapati *ration* kwa wakati Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Jambo hili

limekuwepo muda na hakuna mtu anayechukua hatua hata mmoja. Tukuombe sasa Mheshimiwa Kangi tunataka watu hao wapatikane, wachukuliwe hatua na fedha za umma zilizotakiwa kwenda kwa wahusika zipelekwe, vinginevyo tutabaki hapa tunalaumiana tunapiga kelele alafu atuendi kwenye mambo ya msingi ambayo tunataka yawasaidie Watanzania, ni lazima tuhakikishe mambo haya yanafanyiwa kazi na yanapata ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nigusie kidogo suala la *NSSF*. Inawezekana kabisa watu waliokuwa wanafikiria, walifikiria vizuri, lakini wale waliokuja kutenda wametenda kinyume na mipango iliyokuwa imetengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tumezungumza hapa na sisi tumeangalia upande mmoja tu hapa, tumeangalia upande wa ardhi ambazo zilikuwa zinanunuliwa kwa ajili ya kuhifadhi kwa matumizi ya uwekezaji. Uwekezaji ulikuwa wa aina gani? Mpango wa kuekeza ulikuwa ulikuwa upi? *Feasibility study* ilifanyika kwa kiwango gani? Yote haya hayakuonekana. Hapa tunazungumza ukienda Mwanza, ukienda Arusha, ukienda Dar es Salaam, ukienda sijui Pwani, kila sehemu ni matatizo matupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano fedha iliyonuniliwa ardhi peke yake ni zaidi ya bilioni 27. Shilingi bilioni 27 inaponunua ardhi tafsiri yake ni nini, lazima tuwe na mipango madhubuti ambayo tulielekeza kule. Hizi taasisi sio kwamba hazikuwa na watu au zilikuwa hazisimamiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikupe tu mfano mmoja mdogo ukichukua pale wanasema mfano ukienda Dar es Salaam wanasema wamenunua ardhi Dar es Salaam na Pwani kwa zaidi ya shilingi bilioni 14 *plots* tano, zinatajwa *plots* tano. Inaweza kuwa ya *square* mita 4,400, inaweza kuwa *square* mita 30 ama inaweza kuwa *square* mita 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachosema hapa ni kwamba hatuwezi kuendelea kubaki tunalalamika.

Mimi niishukuru sana Serikali kwa kuamua kuunganisha mifuko hii na kupata mifuko miwili. Sasa ni wajibu wa *BOT* na *SSRA* kuhakikisha mifuko hii haiingii tena kwenye mikataba ya hovyo itakayotupeleka taifa na watumishi wetu kukosa michango yao wanapohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo tutakuwa tumeisaidia Serikali tutakuwa tumelisaidia Taifa, lakini ardhi yote ambayo inaonekana ipo ipo juu ufanyike uhakiki wa kina sasa itambuliwe na Halmashauri zote zinazohusika zihakikishe hati ardhi hizi zinapatikana, vinginevyo tunapiga tu *mark time* tu hapa halafu hatuwezi kuisaidia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Suala lingine ningependa nizungumzie *NDC*. Ni kweli *NDC* ni shirika la maendeleo ambalo limetengenezwa maalum kwa ajili ya kusaidia kwa haraka na kwa kazi uwekezaji kwenye sekta ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa mfumo wa shirika hili lilivyo, kama tutaendelea kuliegemea, nataka nikuahakikishie hakuna hata siku moja linaweza kuwa zao bora kwenye viwanda tunavyovitegemea na haliwezi kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano limezungumzwa hapa *TANCOAL* na *PCEA*. *TANCOAL* tunafahamu ni taasisi au ni kampuni iliyoundwa kutoka Serikalini na hii inayoitwa *PCEA* ni mwekezaji aliyekuja, sasa cha ajabu kabisa uwezi kukifikiria *TANCOAL* imechukua asilimia 30 lakini hawa waliokuja kama wawekezaji wamepewa asilimia 70. Mtaji wa mwekezaji ni shilingi milioni 1.75. Moja ya makubaliano ni lazima atoe dola milioni 20 na dola milioni moja 1.47 zinunue vifaa na kuwekeza kwenye magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka mmoja baadae, mwaka 2012 mwekezaji kaenda kukodi vyombo na magari vyenye dhamani ya dola milioni 42.7. Tafsiri yake ni nini, mwekezaji huyu awezi kulipa kodi ya Serikali hata senti moja, hawezi kulipa mrabaha wa makubaliano ya Serikali, lakini

zaidi ya yote kila mwaka kukicha kukirudi anapata hasara na hata walioingia mkataba Mheshimiwa Kiswaga hapa amesema hivi kweli tuna watu leo wanakaa kwenye ofisi hawezi kufikiria mkataba alioingia asilimia 70 na 30 anazobaki nazo kama Serikali hatujui hata dhamani ya mawe yanayokwenda kuchimba na kwa umri upi?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa wapo, wanaishi, wanakula maisha, hakuna hatua, tumekaa, bodi imeuliza maswali ya kutosha lakini imetumia muda muda mchache sana mpaka leo haijaleta hata jibu moja juu ya hii. Tuombe sana Serikali na Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji upo hapa, hili ndilo eneo sasa tunataka tumsaidie Mheshimiwa Rais anayefanya kazi kubwa ya kulinda rasilimali za taifa hili ya kuhakikisha tunafaidika na rasilimali zetu ya kuahakikisha tunapambana na mambo yote yaliyokuwa ya ovyo, kuisaidia Serikali irudi kwenye wakati unaofaa kwa ajili ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu na mimi nimesema sana, haiwezekani na haitakaiwezekani kila siku tukikaa hatuna suluhu, tunataka tufike sehemu. Leo tunasema Mheshimiwa Kangi kuna magari 777 hayaonekani na ninyi mpo. Tusaidieni haya mambo yashughulikiwe, tuondoe maswali kwa watu, tumwache Mheshimiwa Rais ashungulike na mambo ambayo yanaweza kulisaidia Taifa hili na kuweka maendeleo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumza fedha zote tunazozisema hapa, pale Nyamagana ukija nahitaji Vituo vya Afya vitatu tu ninacho kimoja sasa hivi. Fedha hizi ni nyingi nahitaji barabara za lami kama kilometa 30 hivi. Fedha hizi zingeweza kusogezwa pale zikawasaidia wananchi na maeneo mengine mengi. Ndiyo, ananikumbusha kwa mfano ukiwa unatoka Nyegezi unaenda Majengo barabara ni mbaya kule, ingewezwa kutengenezwa kupitia hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakushukuru sana na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane kidogo. Nitaleta kwenu baadhi ya majina ya wachangiaji wa mchana Mheshimiwa Catherine Ruge, Mheshimiwa Tunza Malapo, Anatropia Theonest, Mheshimiwa Selemani Zed, Mheshimiwa Abdallah Chikota Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Khadija Nassir, halafu wengine tutawataja kadri tutakavyokuwa tukiendelea na wachangiaji mchana.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi mpaka mchana, sasa ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

**HOJA ZA KAMATI**

**HOJA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI *(PAC)* NA HOJA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA *(LAAC)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Catherine Ruge atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Abdallah Chikota na Mheshimiwa Tunza Malapo ajiandae.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na nimi niweze kuchangia. Napenda kujikita kwenye Taarifa ya Kamati ya *PAC* na ningependa kuzungumzia *issue* ya *1.5 trillion*. Kabla sijachangia, napenda kumnukuu aliyekuwa Rais wa 16 wa Marekani, Marehemu Abraham Lincolin ambaye alisema; *"You can fool all people some of the time, but you cannot fool all people all the time." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amelithibitishia Bunge, lakini pia ameuthibitishia umma kwamba kulikuwa na tofauti ya *1.5 trillion* kwenye Mfuko Mkuu wa pesa za Hazina ambazo hazikukaguliwa wakati anafanya ukaguzi wake kwa hesabu zilizoishia Juni, 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati ya *PAC* kwa kumtaka *CAG* aweze kufanya *verification* na kujua tofauti ya *1.5 trillion* na leo kuleta taarifa ya Bunge ambayo tunaijadili sasa.

*Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na verification kufanyika, badala ya hoja ya 1.5 trillion kufungwa, zimeibuka hoja nyingine na sasa hatuzungumzii 1.5 trillion, tunazungumzia 2.4 trillion. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweka *records clear,* siyo kazi ya *CAG* kusema kama kuna wizi. Kazi ya *CAG* ni kufanya ukaguzi na kutambua upungufu uliopo na mamlaka husika inatakiwa i-*take charge*. Kuna hoja mbalimbali ambazo zimeibuliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye hii ripoti ya ukaguzi maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kuna *issue* ya *overdraft* ya shilingi bilioni 290.7, Hazina wanasema hii ilikuwa ni *overdraft* na majibu yao wanasema zilikuwa ni pesa zilizokwenda kwenye miradi ya maendeleo na hazikupita kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, lakini Mkaguzi hakupata vielelezo kuthibitisha hii hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkaguzi alienda mbali zaidi akaamua kuomba *confirmation letter* kutoka *BOT* kuthibitisha hiyo *balance* ya shilingi bilioni 290.67. Kuna *confirmation letter* kutoka *BOT* hii hapa ambayo wame-*confirm* kwamba kulikuwa na *zero balance* wakati Hazina inafunga mahesabu yao Juni, 2017. Pia taarifa za Ukaguzi za Hesabu za *BOT* za Juni, 2017 zinaonyesha *balance* ya *overdraft* ya *Central Government* ilikuwa ni *1.5 trillion*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina *Hansard* hapa ya tarehe 20 Aprili, 2018, ukurasa wa 22 mpaka 25. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango alisimama hapa kutoa maelezo ya Serikali kuhusu tofauti ya *1.5 trillion*. Alisema; *overdraft* ilikuwa shilingi bilioni 79.1. Sasa hapa tuna *figure* nne za kutoka kwenye Serikali moja, tuamini ipi? ya *BOT* ya *1.5, confirmation letter* ya *zero balance*, maelezo ya Naibu Waziri ya shilingi bilioni 79.1 au taarifa za hesabu za *BOT* za *1.5 trillion*? Yaani kwa kifupi hapa naona Serikali ilipoteana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili, ni kuhusu shilingi bilioni 976.96 ambazo zilifanyiwa *reallocation* kwenye *vote* mbalimbali kutoka kwenye mfuko wa Hazina kwenda kwenye *vote 20* na fedha hizi hazikupitishwa na Bunge. Lakini pia *reallocation* hiyo haikupata *approval* ya *BoT*. Hizi pesa zimeenda *vote 20* ambako ni Ofisi ya Rais. Wote tunatambua, *vote 20* haikaguliwi. Kwa hiyo, Serikali imefanya *vote 20* ni kama kichaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, mpaka leo...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Ruge, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

## T A A R I F A

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba mzungumzaji anayeongea kwanza ni Mjumbe wa Kamati...

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa ifuatayo; katika mambo yaliyofanyika kwenye kitabu hiki, yaliyomo kwenye kitabu hiki;

sijui watu wanazungumza mambo gani tofauti na haya yaliyoko humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imesemwa kwamba katika mambo yote, kuna jambo linasema kwamba aidha, Hazina walifafanua kuwa utolewaji huo wa fedha zaidi ya mapato ni kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 kinachoruhusu Benki Kuu kuipatia Serikali wigo wa kutanua fedha zaidi kwa miradi inayoendelea. Sasa shida iko wapi hapa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena. Tuwe na uvumilivu wa kusikilizana. Mheshimiwa Zitto tuwe na uvumilivu wa kusikilizana ndiyo tutaweza kufika. Kwa sababu wengine pengine hamjajua, humu kuna maazimio ambayo Waheshimwia Wabunge tutatakiwa kuazimia leo. Sasa kama tunazomeana hapa, tutaazimia leo vitu vya ajabu humu.

Kwa hiyo, tusaidiane ili tufikie maazimio yatakayokuwa na hadhi yetu sisi Wabunge. Maana tusijekuwa tunabishana hapa, hatujui tunafanya nini sasa hivi. Kuna maazimio humu ambayo tunatakiwa kuazimia.

Mheshimiwa Catherine Ruge, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei, naomba niendelee kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee nilipoishia. Hizi pesa ninazozizungumza zilizoenda *vote 20* hazikupata *approval* ya *CAG* pamoja na *reallocation* iliyotokea. Kinachonisikitisha zaidi, hoja hii haiko kwenye Taarifa ya Kamati, lakini pia, Hazina mpaka leo hawajatoa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kueleza jinsi gani Mheshimiwa Naibu Waziri alilipotosha Bunge lako tukufu aliposimama na kusema kwamba kulikuwa na

*receivable* kwenye pesa ambazo zilikuwa zimekusanywa na Hazina.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaomba tuwe na uvumilivu. Kama ambavyo ninyi mnatoa taarifa, wasikilizeni wenzenu pia wanazo taarifa. Muwe na uvumilivu tafadhali. Mheshimiwa Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba taarifa rasmi ni ya *CAG* iliyotolewa Machi, 2018 na *verification report* na ripoti iliyojadiliwa hapa. Mambo ya Mheshimiwa Naibu Waziri hapa hayapo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Ruge, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei hiyo taarifa na ninaomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, ripoti ya *PAC* ni matokeo ya taarifa ya *CAG* na taarifa ya *CAG* ni *public document*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Ruge, naomba ukae.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**T A A R I F A**

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia kanuni ya 64(1)(a) nisingependa kuisoma, lakini ningependa mzungumzaji anayezungumza hapa...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Isome.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima unasisitiza hapa mwenzio asome, wewe asubuhi nimekusikiliza hapa hukutaja kanuni gani ilikuwa inavunjwa. Kwa hiyo, tuwe wavumilivu tafadhali.

Mheshimiwa endelea na taarifa yako.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji ambaye alikuwa anazungumza sasa hivi amezungumzia kwamba hoja iliyopo siyo shilingi trilioni 1.5 zimekwenda shilingi trilioni mbili. Hizo taarifa amezipata wapi? Kwa sababu kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* haipo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto, naomba ukae. Mheshimiwa Zitto, tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, nimetoka kuwakumbusha sasa hivi, tuna kazi nzito mbele yetu ya kuazimia ili tujue tunataka kuiambia nini Serikali kuhusu hesabu zake za Serikali Kuu na kuhusu hesabu zake za Serikali za Mitaa. Hizi taarifa tunazozijadili hapa tuliwapa kazi Wabunge wenzetu kwa mujibu wa kanuni zetu, waende wakapitie yale aliyokagua *CAG.* Wenyeviti wa Kamati hizi wote wanatoka Kambi ya Upinzani; na Wajumbe wako wa CCM, wako na wa Upinzani. *(Makofi)*

Hapa ndani namna tunavyokwenda hivi, kiti kazi yake ni kusimamia majadiliano yaende, mwishoni Bunge tufikie maamuzi. Hizi taarifa mbili Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena, mwisho wa haya tunayoyazungumza

ni Maazimio ya Bunge wote tukiwa humu ndani. Yatakuwa ni maazimio ya Bunge.

Sasa tukiamua kufanya mizaha hapa na pale na kejeli na nini, kama ndicho tunachotaka kuazimia, pia ni sawa. Mimi kazi yangu ni kuwakumbusha na ndicho ninachokifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tukumbuke tuko hapa leo kwa ajili ya kazi hiyo, kazi ngumu kweli kweli. Sasa naona kama tunataka kuelekea mahali ambapo hakutatufanya tufikie kile ambacho tuna kazi nacho.

Mheshimiwa Halima tafadhali. Nadhani tutakuwa tumeelewana.

Mheshimiwa Catherine Ruge.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 20 Aprili, 2018 Naibu Waziri alisimama mbele ya Bunge lako tukufu na kulihadaa Bunge kwa kusema kulikuwa na *receivable* za shilingi bilioni 687 ambazo zilisababisha tofauti ya *1.5 trillion* na akasema hii ilitokana na Hazina kuanza kutumia mfumo wa *IPSAS Accrual*. Taarifa ya Mkaguzi hii hapa haionyeshi hiyo hoja, haijaongelea kabisa *receivable. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wahasibu na *tax administrators* tulioko humu ndani, tunajua kabisa, hakuna pesa tarajiwa zinazokwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Hakuna *non cash item,* kule zinakwenda *cash* tu. Mapato yote yako *on basis of cash*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni hoja ya hati fungani. Hazina walikuja na vielelezo ambavyo vilikuwa kwenye *excel* na *CAG* amesema hizi taarifa haziaminiki na haziko *credible.* Naomba ni-*quote* taarifa ya *CAG; "The weaknesses continue during the verification of the difference,*

*the document were required as to meet numerous types from various department also it took a long time to locate and extract information most of which was in MS Excel spread sheet in different location*. Kwa hiyo, kwa *statement* hii, hakuna *credibility* ya hii *information.*

**MBUNGE FULANI:** *Different* siyo *diffelent.*

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonishangaza, hivi inakuwaje Hazina inaweza kutumia *excel* kuweka hesabu zake ambayo inaweza ikabadilishwa, ikaongezwa kitu, ikatolewa kitu bila *traces?* Sasa kweli tuko *serious?* Hazina ambako tunaamini inalinda pesa za walipakodi wanyonge, lakini ndiyo tunaona haya matatizo na uongo mkubwa na *weaknesses* za mfumo na udhaifu mkubwa wa Hazina! Tusipofanyia kazi udhaifu wa mfumo wa Hazina, haya matatizo yataendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa...

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Ruge kuna taarifa.

## TAARIFA

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashangazwa kabisa na mzungumzaji anayezungumza, mimi naamini ni *very professional,* ni mbobezi katika hesabu. Ninachotaka nikwambie ni kwamba suala la *CAG* siyo *conclusive* katika taarifa. Haiwezekani Hesabu za Serikali ambazo ni *consolidated* zikatumiwa kwa njia ya *excel*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anajua kabisa kwamba hesabu hizo zinatumia *EPICOR*. Kwa

hiyo, naomba asilidanganye Bunge. Nimesema kwamba taarifa ya *CAG* siyo *conclusive*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Ruge, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei.

**MBUNGE FULANI:** Pokea.

**MBUNGE FULANI:** Usipokee.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hii taarifa na naomba nikwambie, *I am a Certified Public Accountant,* najua ninachokizungumza. Inawezekana hiyo *syllabus* yako uliyosoma ilikuwa ya zamani, mimi *I am very current. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ya hati fungani ambapo hizi hati fungani zilionekana zimeiva na zikawa *rolled over*. Lakini vielelezo hivyo pia vimeletwa kwenye *excel* na ukiangalia hii taarifa, ukijumlisha kwanza hizo hati fungani, haziji-*figure* hiyo ya shilingi bilioni 656, zinakuja shilingi bilioni 853. Angalieni hii taarifa. Kwa hiyo, kuna tofauti ya kitu kilichosemwa na kitu ambacho *CAG* amekizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kujua *figure* ya *bonds* unakwenda kuangalia kwenye taarifa ya *BOT*; na kwenye taarifa ya *BOT* zimeonyeshwa *bonds* zote. Sasa naomba Serikali ikija hapa ituambie, hizo *bonds* zilizo-*mature* 2016/2017 Juni, ni *bonds* gani? Za muda gani? Zilikuwa zina kiasi gani na zililipwa lini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa. Angalia muda kule, msipende kelele. Angalia muda kule, nadhani sasa mmeuona ndiyo mmeridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Selemani Zedi, atafatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota. Mheshimiwa Tunza Malapo ajiandae.

**MBUNGE FULANI:** Yaani umetema cheche mwanangu. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili jioni hii name niweze kuchangia taarifa hii ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* na kwa hiyo mchango wangu kwa kiasi kikubwa utajikita kwenye mapendekezo ya Kamati yangu ya *LAAC* kama ambavyo yalivyo kwenye kitabu cha taarifa ya Kamati tulichokiwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ya *LAAC* imependekeza mambo kadha lakini mojawapo ambalo nitaelezea kwa kwa kifupi kwanini tumependekeza ni kwamba katika kamati ya *LAAC* baada ya kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya Serikali tumependekeza kuhusu Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, kwamba yale malimbikizo ya nyuma ya michango ambayo halmashuri zilipaswa kuchangia kwenye Mfuko huo kabla ya sheria mpya ya kufanya jambo hili kuwa sharia, malimbikizo yale kwa hali ya halisi kwa sababu hayawezi kulipika, tumeomba Serikali ianze mchakato wa kuangalia namna ya kuyafuta yale malimbilikizo ya nyuma kabla ya Sheria ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumependekeza jambo hili baada ya kuangalia kwa kina karibu halmashauri zote zilizokuwa zikija mbele ya Kamati yetu ukiangalia malimbikizo ya fedha ambazo halmashauri hazikuweza kuchangia

kwenye Mifuko hii miaka ya nyuma kabla ya mwaka jana kabla hatujaweka sharia, utakuta halmashauri zina madeni makubwa ambayo kwa hali halisi hayawezi kulipika. Kwa hiyo tukaona kwamba hata kama tukilazimisha halmashauri zilipe malimbikizo hayo ambayo hawakuchangia itakuwa ni kazi bure kwa sababu ni *figure* kubwa ambazo hakuna halmashauri hizi za kawaida zinazoweza kulipa, kwa sababu kutokana na *analysis* imeonekana kwamba halmashauri nyingi haya malimbikizo ni makubwa kulingana na mapato yao ya ndani ya mwaka .

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unakuta halmashuri mapato ya ni bilioni moja, lakini malimbikizo ambayo hawajayapeleka kwenye Mfuko ni zaidi ya bilioni moja, kwa hiyo hakuna namna halmashauri hii inaweza kulipa. Kwa hiyo tumependekeza kwamba yale malimbikizo ya nyuma, jambo la kukusisitiza hapo ni kwamba kabla ya mwaka jana tulipoamua kwamba jambo hili liwe sharia, huko nyuma ambako halmshauri zili-*relax* na kutengeneza malimbikizo mengi Serikali iangalie namna ya haya malimbikizo kuyafuta, tuanze upya kwa sababu nina uhakika Halmashauri zitaweza kulipa *current figure,* lakini huo mzigo wa nyuma tusaidie namna ya kuondoa, kwa hiyo hilo ni pendekezo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tumependekeza baada ya kuangalia taarifa ya Mkaguzi ni kwamba, bado kuna tatizo kubwa la upelekaji wa fedha za maendeleo kwenye halmashauri zetu ambazo zimeidhinishwa kwenye bajeti. Taarifa ya Mkaguzi kwamba bado halmashauri zinakuwa na bajeti za maendeleo ambazo zinaidhinishwa na Bunge lakini mwaka unaisha Hazina haijapeleka fedha za maendeleo kwenye halmashauri na miradi mingi inashindwa kufanyika.

Mheshimiwa naibu Spika, jambo hili limevunja moyo hasa katika maeneo ambayo miradi kwa hatua ya kwanza ilichangiwa na nguvu za wananchi. Leo hii ukipita kwenye majimbo yetu utakuta kuna maboma ya madarasa, nyumba za Walimu, zahanati, vituo vya afya ambavyo wananchi

walichangia kwa fedha zao na ilikuwa kazi ya Serikali kukamilisha na halmashauri nyingi zimekuwa zikipitisha fedha hizi kwenye bajeti ili Hazina itoe ili kwenda kumaliziai kazi hizo ambazo zilianzwa na wananchi, lakini miaka yote fedha zimekuwa haziji pamoja na kwamba zipo kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jambo hili limekuwa likivunja morali ya wananchi kuchangia kwa sababu wamechangia sana lakini maboma yamebaki maboma tu. Kuna maboma mengine yana miaka mitano, sita, saba mpaka 10 hayajaweza kumaliziwa na Serikali. Kwa hiyo tumeiomba Serikali kwamba miradi ya maendeleo ambayo fedha zake zinapitishwa na Bunge, Hazina iweze *serious* kuhakikisha angalau kwa 90% fedha zinakwenda kwa sababu jambo hili limekuwa likifunja moyo wananchi ambao wanachangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo Kamati imeliona na kupendekeza ni kuhusu udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani katika halmashauri nyingi. Taarifa ya Mkaguzi imebaini kwamba kumekuwa na miamala isiyofuata taratibu mingi katika miamala inayofanywa na halmashuri na sisi Kamati tumeona hili jambo linasababishwa na ubovu wa mifumo ya udhibiti wa ndani. Katika dunia ya leo unaweza ukadhibiti kiasi kikubwa miamala ambayo inafanywa kinyume cha taratibu kwa kuwa na mifumo ya kisasa inayozuia.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo kama unakuta halmashauri inahamisha fedha kutoka kwenye akaunti ya amana, fedha ambazo labda zilikuwa kwa ajili ya malipo ya Walimu au mitihani, halmashauri inazihamisha na kuzipeleka kununua mafuta au kufanya jambo ambalo halijakusudiwa. Jambo hili unaweza ukalizuia kama una mfumo wa kisasa wa kudhibiti kwa sababu unatakiwa mfumo ndio ukatae. Ukitaka kuhamisha fedha kutoka kwenye akaunti ya amana kwenda kwenye jambo lingine ambalo halikubaliki inatakiwa mfumo ukukatalie, yaani inatakiwa jambo hili lizuiwe na mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Kamati tumebaini kwamba mifumo na *accounting package* ambazo zinatumika kwenye halmashauri bado kuna haja zikaboreshwa zikawa za kisasa na zikaweza kuzuia *irregularity* mbalimbali ambazo kwa sasa zinafanyika kwa sababu mifumo inaruhusu. Ushauri mkubwa wa Kamati hapa ni kwamba TAMISEMI ijaribu kuja na mifumo ya kisasa ya udhibiti wa ndani wa namna hesabu zinafanyika ili kuzuia *irregularity* na miamala ambayo inakwenda kinyume cha taratibu. Haya mambo kwa dunia ya kileo yanatakiwa kuzuiwa na mifumo. Ukiwa na mfumo wa kisasa, wenyewe ndio unakuzuia. Ni kama vile sasa hivi ukitaka ku-*raise purchase order* ya kununua bidhaa fulani, kama kwenye bajeti hela hiyo haipo kwenye maana yake *purchase order* haitoki, huwezi kui-*process* ikatoka. Kwa hiyo tunataka mifumo ya namna hiyo kwa dunia ya kisasa ili kuweza kuzuia mambo ambayo hayatakiwi yafanyike. Kwa hiyo kuna kila haja ya TAMISEMI kuja na *accounting package* ya kisasa ili kuweza kuzuia mambo mengi ambayo yanaweza yakazuilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tumegundua ukosefu wa ujuzi wa kutumia mifumo kwa watumishi wengi wa halmashauri zetu. Kumekuwa na matatizo ya miamala mingi kushindwa kufanyika, ripoti kushindwa kuchapishwa katika halmashauri zetu kwa sababu mifumo iliyopo ya TAMISEMI watu walipo kwenye halmashauri nyingi wamekuwa hawana ujuzi na utalaam mzuri wa kuitumia. Kwa hiyo mambo mengi yanashindikana na sababu unaambiwa mfumo haufanyi kazi, lakini kumbe ni utaalam. Kwa hiyo tumependekeza kwamba TAMISEMI iwe na progamu za kutoa mafunzo kwa ajili ya watumishi wa halmashauri mbalimbali ili waweze ku-*master* hii mifumo ya kisasa iliyopo ili shughuli nyingi za halmashauri ziweze kufanyika kwa mifumo na taratibu za kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa jumla taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali za Mitaa ambapo sisi kama Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa wajibu wetu ni kuangalia maeneo sugu katika taarifa ya Serikali za Mitaa ukilinganisha na miaka ya nyuma, ukiangalia *trend* utaona

kwamba pamoja na kwamba matatizo bado yapo, lakini kwa kiasi kikubwa kadri tunavyokwenda matatizo katika maeneo yote yanapungua; maeneo ya malipo yasiyo na nyaraka, maeneo ya ukiukwaji wa taratibu za manunuzi na maeneo mengi yenye matatizo, ukingalia *trend* mtiririko ni kwamba kuna *improvement* kubwa na kwamba matatizo hayo yanaenda yakipungua kadri siku zinavyokwenda. Kwa hiyo ni imani ya Kamati kwamba jitihada zinazofanywa na TAMISEMI zikiendelea tunakwenda mahali ambapo kutaleta picha nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono taarifa yangu ya Kamati ya *LAAC* kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Malapo.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kwa kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* mchango wangu utajikita katika taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati yetu ya *LAAC*. Kwanza nianze kuipongeza TAMISEMI kwa hatua ambazo zinachukuliwa kwa sababu ukisoma hikhi kitabu cha taarifa ya *CAG* inaonekana kuna maboresha katika hati zinazopatikana. Hati za kuridhisha kwa *councils* ambazo zilikaguliwa mwaka jana 185, kuna ongezeko la halmashauri ambazo zimepata hati ambayo inaridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu utaona kwamba kwa taarifa ya mwaka 2015/2016 tulikuwa na *councils* 135 kati ya 171 ndio zilipata hati ya kuridhisha, lakini taarifa hii tunayoijadili kuna ongezeko, mwaka huu kuna halmashauri 165 zimepata hati ya kuridhisha kati ya halmashauri 185 ambazo ni sawa na 90%. Kwa hiyo, niwapongeze sana TAMISEMI kwa shughuli za ufuatiliaji ambazo zinafanywa na matokeo yake tunaanza kuyaona sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu halmashauri ambazo zinapata hati za mashaka nazo zinaanza kupungua, ukiacha halmashauri za Kigoma Ujiji ambayo imepata hati mbaya kwa miaka mitatu mfululizo, lakini katika maeneo mengine kuna maboresho ambayo yanaonekana. Kwa hiyo kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani, nimshauri kaka yangu Mheshimiwa Zitto kwamba naye awe anahudhuria vikao vya Kamati ya Fedha ili inapojadiliwa ripoti ya *CAG* na yeye aweke *inputs* zake kwa sababu kupata hati isiyoridhisha kwa miaka mitatu mfululizo ni kitu kisicho cha kawaida na kinahitaji *intervention* za haraka ili Kigoma Ujiji iweze kupata hati safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi sasa nichukue nafasi hii kuishauri TAMISEMI, kama walivyosema wenzangu kwenye taarifa yetu tumesema matatizo yote ambayo yanatokea katika halmashauri zetu sababu kubwa ambayo inasabisha ni mifumo yetu ya ndani kutokuwa imara. Kwa hiyo mifumo wa udhibiti wa ndani inabidi iimarishwe. Tunapozungumzia mifumo ya udhibiti wa ndani tunaangalia Kitengo cha Ukaguzi, Kamati za Ukaguzi za Wilaya, matumizi ya TEHAMA katika ukaguaji au ufungaji wa hesabu, kuwepo kwa sera ya viashiria hatarishi na vilevile kuwa na *fraud assessment.* Kwa hiyo hayo yakizingatiwa, tutapunguza sana ubadhirifu ambao unatokea katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma agizo la 12, *Local Authority Financial Memorandum* kuna agizo kabisa limetolewa pale kwamba, kila halmashauri lazima kuwe na Kitengo cha Ndani. Changamoto iliyopo kwenye Kitengo chetu cha Ukaguzi wa ndani ni kukosekana kwa rasilimali fedha na rasilimali watu. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kama walivyopendekeza kwenye Kamati yetu, TAMISEMI na kwa kushirikiana na Mkaguzi Mkuu ambaye yupo Wizara ya Fedha *Internal Auditor General,* basi waimarishe kitengo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma kulikuwa na jitihada za makusudi TAMISEMI walikuwa wanahangaika na vitendea kazi, lakini na *Interanal Auditor General* ambaye yupo Wizara ya Fedha na Mipango ambaye alikuwa anatoa

mafunzo kwa Wakaguzi wa Ndani. Kwa hiyo tunaiomba Serikali sasa kurejesha yale mafunzo ili Wakaguzi wetu waweze kuwa na ujuzi wa kuweza kufanya kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, ripoti hii inaonesha wazi kwamba kuna uchache, ikama inasema kila halmashauri kuwe na Wakaguzi wasiopungua wane, lakini halmashauri nyingi ambazo zilikuja ndani ya Kamati zina Mkaguzi wa Ndani mmoja au wawili. Kwa hiyo wanashindwa kutekeleza majukumu yao. Kama tulivyopendekeza kwenye ripoti yetu kwamba, Serikali ichukue jitihada za makusudi kuomba kibali cha jumla ili Wakaguzi wa Ndani waweze kuajiriwa na wasambazwe kwenye halmashauri kwa ajili ya kuimarisha Kitengo hiki cha Ukaguzi wa Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Kamati za Ukaguzi, ukisoma agizo la 13 la *Local Authority Financial Memorandum,* zinazitaka halmashauri kuwa na Kamati za Ukaguzi na Mwenyekiti atoke nje ya ile taasisi, lakini hapa kinachoendelea ni tofauti, halmashauri nyingi ambazo zimekuja kwenye mahojiano, Wakuu wa Idara au watendaji wa halmashauri ndio walikuwa Wenyeviti wa hizo Kamati, kinyume na mwongozo ambao umetolewa na Wizara na kinyume na agizo hili hapa. Kwa hiyo naomba TAMISEMI kusimamia kwa karibu ili halmashauri zote zipate Wenyeviti wa Kamati za Ukaguzi ambao wanatoka nje ya taasisi ili kuimarisha kamati kwa ajili ya kuweza kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye udhibiti wa ndani kuna suala la TEHAMA; kumekuwa na mtindo sasa hivi mwezi wa Saba, mwezi wa Nane halmashauri zinasimama kila kitu, ukiuliza wanasema mfumo, Madiwani hawalipwi, vikao haviendelei, hakuna malipo yanayoendelea. Tulipofanya mahojiano na TAMISEMI, walisema hakuna kitu kama hicho, tatizo ni changamoto ya utalaam. Kwa hiyo naiomba Serikali kutoa mafunzo, kama tulivyopendekeza kwenye taarifa yetu, kwa wataalam ili kusiwe na kisingizio kwamba mwezi wa Saba na wa Nane hakuna kinachoendelea halmashauri kwa sababu ya kusingizia hiyo mifumo iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni mafunzo kwa hawa Wakaguzi; inachekesha sana kwamba kuna mifumo mingi ambayo Serikali imeanzisha tuna *EPICOR*, *Lawson* kwa ajili ya mishahara, tuna ile ya kukusanya mapato *(LGRCIS),* lakini Mkaguzi wa Ndani hajapata mafunzo jinsi ya kuingia kwenye mifumo hii. Kwa hiyo, Mkaguzi wa Ndani anapokwenda kukagua anakumbana na changamoto ya matumizi ya mifumo hii. Hivyo, kama tulivyoshauri kwenye Kamati yetu *Internal Auditor General* ambaye ipo Wizara ya Fedha na Mipango na TAMISEMI wahakikishe kwamba Wakaguzi wetu wa Ndani wanapata mafunzo ya kutosha ili waweze ku-*assess* hii mifumo ambayo imeanzishwa kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze TAMISEMi kwa kuanzisha kitengo cha ukaguzi na ufuatiliaji wa fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hiki ni kitengo muhimu sana na kitengo hiki kikiimarishwa kitasaidia sana kupunguza ubadhirifu au utekelezaji wa miradi usioridhisha katika halmashauri zetu. Tulipowahoji maafisa ambao wapo kwenye kitengo hiki kuna changamoto kubwa sana, kitengo kimeanzishwa lakini ni ombaomba, tunaomba Wizara ya Fedha na TAMISEMI ihakikishe kwenye bajeti inatenga fedha za kutosha ili kitengo hiki kiwezi kutekeleza majukumu yake. Ni kitengo kizuri ambacho kikiimarishwa kitazuia ubadhirifu ambao unatokea kwenye halmashauri zetu kabla *CAG* hajaingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kitengo hiki kina watumishi wachache lazima kiongezewe watumishi kitengo hiki ili kiweze kutekeleza majukumu yake na kitengo hiki pia kiwezeshwe kutumia mifumo iliyopo ya TAMISEMI iliyopo sasa hivi ili waweze ku-*assess* ku-*information,* sio lazima wakimbie kwenye halmashauri, wanaweza kuitisha taarifa zilizopo kwenye mifumo na wakajua kwamba kwenye halmashauri X kuna changamoto hii na baadaye wakaenda kufuatilia kule kule kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo hiki kikiimarishwa kitasaidia na kitapunguza wazo ambalo watu wanalo, kuna

watu wana wazo kwamba *Internal Audit* asiwe sehemu ya Mkurugenzi, sasa *Internal Auditor* akiwa nje ya Mkurugenzi inavuruga maana ya kuwepo *Internal Auditor, Internal Auditor* kile kitengo kimeungwa ili liwe jicho la Mkurugenzi au Afisa Masuuli. *Internal Auditor* akitolewa nje ya ofisi huyu atakuwa *External Auditor* mwingine, kwa hiyo tukiimarisha kitengo hiki itasaidia kutoa ishara kwa Mkurugenzi kwamba idara yako X kuna hali mbaya, kwa hiyo chukua hatua haraka. Kwa hiyo, napendekeza kitengo kiimarishwe na sio kuondolewa kwenye Ofisi ya Afisa Masuuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie mchango wangu kuhusu utekelezaji wa miradi kwenye Halmashauri zetu. Kuna changamoto nyingi sana katika kutekeleza miradi kwenye Halmashauri yetu. Changamoto ya kwanza, ni fedha kupelekwa pungufu. Fedha zinatengwa kwenye bajeti lakini hazipelekwi na hivyo mipango ya Halmashauri kushindwa kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba TAMISEMI kila wanapopata fedha wahakikishe kwamba wanapeleka kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa ili waweze kutekeleza miradi kwa wakati. Kuna wakati mwingine tunaambiwa Halmashauri hazina uwezo, kumbe tunapeleka fedha Mei, 30 halafu tunawaambia watekeleze mradi. Mradi huu hauwezi kutekelezeka kwa sababu *procurement process* yenyewe inachukua siku nyingi. Kwa hiyo, mpaka kumaliza mchakato wa manunuzi fedha zile zitakuwa bakaa kwenye mwaka unaofuata. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni gharama za mradi kama ilivyoelezwa kwenye taarifa yetu pale Morogoro Manispaa tuliona mradi wa lami ambao ni wa kilomita 4.6 lakini unagharimu takribani shilingi bilioni 12. Sisi kwa hesabu zetu za haraka fedha zile zingeweza kujenga zaidi ya kilomita 10. Tulipouliza kwenye Halmashauri zingine viwango vinakuwa tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Kitengo cha Usimamizi wa Miradi kwenye Halmashauri kilichopo TAMISEMI

lazima tuweke *standard* za miradi yetu, *standard* za utekelezaji katika mamlaka ya Serikali za Mitaa ili kutotoa mwanya kwa wale ambao wana nia mbaya ya kupiga fedha za Halmashauri wasiweze kufanya hivyo. Tunapokuwa na viwango tofauti na Halmashauri inajiamulia kwamba nitajenga barabara kilomita 1 kwa shilingi bilioni 3, mwingine anajenga kilomita 1 kwa shilingi bilioni 2, hapo lazima upotevu wa fedha utajitokeza. Kwa hiyo, naomba Kitengo cha Usimamizi wa Fedha TAMISEMI, Kitengo kinachosimamia miradi kihakikishe kinatoa *standard* ili miradi yetu tuweze kutekeleza kwa kile kiwango ambacho tumekikusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* naunga mkono taarifa ya Kamati yetu kwa asilimia 100 na nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Tunza Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Khadija Nassir ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimwia Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote, nataka kusema kitu kimoja kieleweke, Halmashauri zote Afisa Masuuli ni Mkurugenzi ambaye anateuliwa na Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, tukiona Halmashauri ya Kigoma Ujiji inapata hati chafu, tatizo sio Zitto tatizo ni Mkurugenzi na watendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia suala la barabara ya Tubuyu – Nanenane na Maelewano ya kilometa 4.6...

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa msemaji anaeendelea kuzungumza kwamba Wabunge wote sisi hapa ni Wajumbe wa Kamati ya Fedha kwenye Halmashauri zetu. Vilevile ni Wajumbe wa Halmashauri zetu kwa maana ya *Full Council* na Halmashauri zinakutana kila mwezi wanapitia mahesabu ya Halmashauri. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Fedha akiwemo Mheshimiwa Zitto na sisi Wabunge wote tukiwa makini, kama kuna upotevu wa fedha utaonekana mapema kabla ya kuchukua muda mrefu hilo kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa taarifa hiyo, hakuna namna ambayo Mjumbe wa Kamati ya Fedha kwenye Halmashauri anaweza akajiondoa inapokuwa na kuna madhara yametokea na yeye yupo. Mheshimiwa Zitto ni mtaalam wa mahesabu, ni mhasibu, msomi mzuri sana. Naomba nitoe taarifa hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, asitafute umaarufu kupitia mimi, kwa hiyo, niache niendelee na hoja zangu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema barabara hii ya kutoka Tubuyu kwenda Nanenane mpaka Maelewano katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kilometa 4.6 imejengwa kwa shilingi bilioni 12.6 maana yake ni kwamba kila kilometa moja imejengwa kwa shilingi bilioni 2.74. Sio *highway* tuelewane, ni barabara ya mtaa. *(Makofi)*

## TAARIFA

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hiyo barabara ambayo anaisemea hata mimi kwa mara ya kwanza nilishtuka, lakini nilipoenda kuiona, *standard* zake waliotoa pesa ndiyo waliotaka tofauti na barabara tunazozifikiria, iko tofauti kabisa, ina *standard* za Ulaya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee, taarifa yake sipokei.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ni ya mtaa na tumeitembelea sehemu nyingi haina hata vituo vya daladala, unajengaje kilometa moja kwa shilingi bilioni 2.74 na ni mkopo kutoka Benki ya Dunia, sisi Watanzania maskini tutakuja kulipa. Kitu chochote unapofanya lazima uangalie *value for money*. Hii barabara ni ya mtaani sio *highway* kwamba labda itapitisha malori, unaenda kujenga barabara ya mtaani ya kwenda nyumbani kwako kwa shilingi bilioni 2.7 halafu ni pesa ya mkopo ambayo tunakuja kulipa mtu anasema kama tuko Ulaya! *That is the shame.* Mimi sikubaliani nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kuhusu Ukaguzi Maalum. Wakati naongelea hii naomba yaeleweke mambo yafuatayo; Mkuu wa Mkoa wa kipindi hicho Bi. Fatma Mwassa alikuwa na uhusiano wa karibu, mtu na mume wake na mkandarasi ambaye alipewa *tender* hizo.

Wakati huo huo, kwa sababu ukaguzi unaozungumziwa hapa ulifanyika kuangalia mambo ya fedha ya mwaka 2012/2013 mpaka 2016/2017; wakati huo huo miongoni mwa Wakurugenzi ambao walihudumu katika Halmashauri hiyo, ni Dkt. Athumani Kihamia ambaye sasa hivi ni Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakati naongea hapa, naomba nieleweke hivi ...

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, kuna kanuni inavunjwa, Mheshimiwa Amina Mollel, kanuni.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 64(1)(a). Kwa kuwa ametajwa Mkurugenzi Athumani Kihamia ambaye kwa hivi sasa ni Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, naomba nitoe tu taarifa kwamba Mkurugenzi Athumani...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Tulieni sasa, Mkurugenzi Athumani...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Tatizo hamnisumbui ninyi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Selasini, naona umekaa sehemu ya *Chief Whip* wa upande huu sio? Wewe si ndiyo *Chief Whip* wa sasa kwa upande huu, umekalia Kiti cha Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa hiyo haya ndiyo majukumu yako sio? Kwa sababu nataka nikuulize jambo kwa hiyo nijibu tu, wewe ndio *Chief Whip?*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Ndiyo.

**NAIBU SPIKA:** Hebu waambie watu wako tafadhali, kwa sababu hii siyo mara ya kwanza Waheshimiwa Wabunge, nilishawahi kumsimamisha Mheshimiwa Mbowe hapa awaambie mtulie ndio mkasikia. Kwa hiyo, mkiambiwa msikilizeni Mbunge mwenzenu, msikilizeni muelewe hoja yake. Kwa nini mnapenda kudakiadakia kila wakati? Msikilizeni

mwenzenu, *Chief Whip* hebu hakikisha watu wako ukishaona wanapiga kelele, mimi nakuruhusu nyanyuka waambie hivi ndiyo wanasikia hawa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika,...

**NAIBU SPIKA:** Hilo ni ombi kwako, kwa hiyo, huhitaji hata kulijibu Mheshimiwa Selasini. Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa bahati nzuri sana kelele za chura hazimshindi ng'ombe kunywa maji.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama kwa Kanuni ya 64(1)(a), wakati taarifa hii inatolewa na niweke tu kumbukumbu sahihi kwamba Mkurugenzi Athumani Kihamia aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kaliua Januari, 2015 na wakati huo anateuliwa tayari mikataba ilikuwa imekwishaingiwa mwaka 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Athumani Kihamia ndiye aliyetoa hizo taarifa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa kwa wakati huo akatuma Tume kwa ajili ya kwenda kufuatilia jambo hili. Kwa hiyo, Mkurugenzi ambaye sasa ni Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi hahusiki na hizi tuhuma. Naomba kuweka utaratibu huu ili ifahamike kwamba Athumani Kihamia aliteuliwa Januari, 2015 na mkataba huu wa hiyo miundombinu uliingiwa mwaka 2014. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Unatumia vibaya hali yako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Amina Mollel amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a) na Kanuni hii inazungumzia mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Fasili hii inasema Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa aliyekuwa anachangia kabla ya Mheshimiwa Amina hajasimama ni Mheshimiwa Tunza Malapo, na kwa maelezo yake ndiyo Mheshimiwa Amina amesimama kwamba anazungumza mambo yasiyoruhusiwa Bungeni na kwamba taarifa aliyokuwa anaizungumza kuhusu Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi ametoa maelezo ama tuseme anataka kuonesha kwamba maelezo ya Mheshimiwa Tunza Malapo si sahihi, kwa maana hiyo ni taarifa ambayo haina ukweli.

Waheshimiwa Wabunge, nataka niwakumbushe jambo moja, Kanuni zetu hizi, namna zilivyoandikwa na sasa tunaelekea mwishoni mwa Bunge hili, tuzielewe vizuri, nawasihi sana. Tusitoe tuhuma ambazo hatuna uwezo wa kuzithibitisha. Nasema hivi kwa sababu, pamoja na kwamba nimeombwa na Mheshimiwa Amina kueleza kama huu ni utaratibu, hili jambo lilishazungumzwa hata kabla hajasimama Mheshimiwa Halima asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa tunayoijadili ambayo Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Mama Kaboyoka na Mheshimiwa Ngombale, mambo yaliyoko humu ndiyo yanayopaswa kutuongoza. Kama taarifa tunazo za nje ya hapo, basi ziletwe hapa Bungeni kwa namna ambayo hazivunji Kanuni. Niwasihi tena tujielekeze kwenye taarifa hizi kwa sababu mwisho wa haya tutatakiwa kufikia Maazimio kama Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tujielekeze kwenye taarifa zetu kwa sababu tuliipa kazi Kamati ya *PAC* na Kamati ya *LAAC*. Mambo ambayo hayapo humu kwenye hizi taarifa hayatufikishi kama Bunge kufikia maamuzi tunayotaka kuyafanya siku ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kuhusu hizi tuhuma zilizotolewa kwa sababu nimeshatoa maelezo kwa kirefu, Mheshimiwa Tunza Malapo na Wabunge wengine tutakaoendelea kuchangia tujielekeze kwenye taarifa zetu za Kamati na tusivunje kanuni. Zaidi ya hapo tutarudi, nimesema kanuni zetu zinajitosheleza, uongo unapelekwa

wapi wote tunafahamu kanuni zinasemaje. Kwa hiyo, tutaenda kwa namna hiyo hii nadhani itakuwa ni mara ya mwisho kutumia muda mrefu namna hii kuelezea jambo hili. Ahsante sana.

Mheshimiwa Tunza Malapo.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi naomba twende taratibu, *Hansard* naomba ichukuliwe, mimi nilichosema, kwanza mimi ni Mjumbe wa *LAAC* mnielewe, nimesema hivi Ukaguzi Maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua umefanyika kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 mpaka 2016/2017. Nikasema miongoni mwa Wakurugenzi waliohudumu kipindi hicho ni pamoja na Mheshimiwa Dkt. Athumani Kihamia, nimesema lipi la uongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niendelee.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza cha kuelewa ni kwamba ulivyotaja kuanzia 2012 mpaka 2017 Wakurugenzi wengine wote hukuwataja ikiwa ni pamoja na aliyekuwepo 2014 aliyeingia mkataba, ni jambo rahisi tu. Kwa hiyo, maana yake ni hivi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuelewane, maana yake ni hivi, kama lengo ilikuwa ni kuonesha Wakurugenzi waliopita basi ungemtaja aliyekuwepo wakati wa mkataba ndiyo hoja iliyopo hapa.

Kwa hiyo, naomba twende vizuri, hiyo ndiyo hoja, usiseme miongoni mwao halafu unamtaja mmoja kwa kuwa yeye anahusika sana. Kwa hiyo, inakuwa kana kwamba yeye ndiyo aliingia huo mkataba wakati wewe unajua wazi hakuingia yeye aliingia mwingine lakini wewe umemchagua yeye. Kwa hiyo Mheshimiwa Tunza Malapo endelea na mchango wako. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi bwana naomba mniache nichangie, mbona hiyo mmeonesha sana *interest*, nimemtaja hapa Mkuu wa Mkoa, nimemtaja hapa mkandarasi, lakini ngoja niache sasa niendelee na hoja yangu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nataka kusema ni kwamba kumekuwa na ubadhirifu mkubwa katika Halmashauri hiyo ya Kaliua wa shilingi bilioni 3.5. Sasa ukiangalia mambo yenyewe, nasoma ukurasa wa 41 kwenye Ripoti ya Kamati ili twende sawa, ukiangalia ile namba (xii) inasema, malipo mbalimbali yenye viashirio vya ubadhirifu na kugushi nyaraka yenye kiasi cha zaidi ya shilingi bilioni 1.2. Mpaka sasa hivi hatujui hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba (xi), usimamizi dhaifu katika ukusanyaji wa ushuru wa tumbaku uliopelekea kutokukusanya mapato zaidi ya shilingi bilioni 1.35. Sasa hapa kwenye ushuru kuna mambo mawili, mimi ni Mjumbe wa Kamati. La kwanza, hawakutoza ushuru kwa maana hawakuchukua tu lakini la pili ilikuwa wametoza ushuru siku wanaenda kulipa ushuru wao, kwenye *exchange rate* wakaenda kwenye *Bureau De Change* ambazo zinabadilisha kwa kiwango kidogo kuliko ya Benki Kuu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Duh.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, ukiangalia namba (viii), malipo kwa mkandarasi kwa fedha za Mfuko wa Barabara kwa kazi ambazo hazikufanyika, hakufanya kazi lakini alilipwa. Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, ukienda namba (i), malipo ya awali ya shilingi milioni 121.7 yalifanyika kwa kutumia nyaraka za dhamana toka Benki ya *Equity*, nyaraka hizo zilighushiwa. Kughushi maana yake ni jinai lakini mpaka sasa hivi bado wanatanua mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ukienda ile namba (iv) malipo yalifanyika kwa mkandarasi bila kuonyesha vipimo vya kazi na mchanganuo wa kazi zilizofanyika kiasi cha shilingi milioni 197, bado wanatanua mtaani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa Tunza Malapo, naambiwa kengele ya pili imegonga.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, shida ni kwamba mnapenda sana kulalamika. Asubuhi mmelalamika nikawaonyesha saa pale.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura dakika kumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Nassir dakika 10, Mheshimiwa Anatropia Theonest ajiandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa neema yake iliyonipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako tukufu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Athuman Kihamia, nachukua nafasi hii kumpongeza Athuman Kihamia aliyekuwa Mkurugenzi wa Kaliua, alipofika Kaliua yeye ndiye aliyetoa taarifa Serikali juu ya ubadhirifu mtu kama huyu anastahili kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashangaa mtu aliyesema juu ya ubadhirifu analaumiwa leo, sasa je, angenyamaza taarifa hizi zingepatikana wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mjumbe wa *PAC* na nitasema kweli yale ambayo tuliyazungumza Kamati ya *PAC*, *Vote 20* haikujadiliwa *PAC* na hatukuwahi kuijadili na mtu anaposimama na kusema kwamba *vote 20* ni kichaka anamkosea yule anayetumia *vote 20.* Huwezi kusema kwamba *vote 20* ni kichaka, wakati *vote 20* haikuwahi kujadiliwa na *PAC* na mimi nakwambia mimi ni Mjumbe...*(Makofi)*

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura kuna taarifa, Mheshimiwa Catherine Ruge.

## T A A R I F A

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa NAibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir, subiri kwanza, Mheshimiwa Catherine Ruge.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru ninayo taarifa hapa ya Ukaguzi Maalum uliofanywa na *CAG* ku-*verify 1.5 trillion* ukurasa wa 20 mpaka ukurasa wa 22, unathibitisha hicho ninachokizungumzia bilioni 997 ambazo zilikuwa *re-allocated* kutoka *votes* mbalimbali na zilienda *vote 20,* kwa hiyo *numbers don't lie. (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wala siwezi kupokea taarifa ya mtu ambaye sio Mjumbe wa Kamati, siwezi kupokea taarifa ya mtu ambaye sio Mjumbe wa Kamati.

**WABUNGE FULANI:** Buuuu!

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika naendelea, Kamati yetu, Kamati ya *PAC,* upande wa pili sijui wamepatwa ugonjwa gani wa kelele!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shilingi trilioni 1.5, tumezungumza sana, vizuri sana Kamati yetu imezungumza vizuri sana na taarifa tumeandika kuanzia ukurasa wa 15 hadi ukurasa wa 31 na tumefafanua kila jambo, kila kipengele hata yule ambaye hajui mahesabu anaweza akasoma na akaelewa kwamba tumeeleza nini kuhusu pesa trilioni 1.5 na naomba nisome ukurasa wa 35 inasema hivi na taarifa hii amesoma Mwenyekiti wa *PAC;* "Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha suala la tofauti ya shilingi trilioni 1.5 kati ya mapato ya Serikali na makusanyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 naomba kuweka kumbukumbu sahihi katika Bunge lako tukufu kuwa tofauti hiyo haikuwepo baada ya marekebisho ya hesabu kufanyika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunajadili taarifa hii tulikuwa Wabunge mchanganyiko chama cha CCM Wajumbe walikuwepo, vyama vya upinzani Wajumbe wake walikuwepo, na waliuliza maswali na walisikia jinsi *CAG* alivyoeleza na walisikia *TRA* walikuwepo, *BOT* walikuwepo, Wizara ya Fedha walikuwepo walisema waziwazi wala hawakuficha jambo lolote, leo mtu anakuja anauliza trilioni 1.5 iko wapi?

**MBUNGE FULANI:** Wazushi hao,

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sema humu, utapata taarifa zote.

**MBUNGE FULANI:** Wazushi hao

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, soma taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliodhani kwamba Tanzania bado itakuwa shamba la bibi, watapata taabu sana.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu yuko makini na anafanya kazi kwa umakini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa John Heche.

**MBUNGE FULANI:** Sikiliza.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa shamba la bibi, ni pamoja na anayezungumza kusoma taarifa ya *PAC* ukurasa wa 13 inasema kwamba shilingi milioni 888 pesa za walipa kodi maskini zimelipwa kama *ration allowance* kwa watu ambao sio maaskari, na wamelipwa kufanya nini kama sio hao watu wanaopiga watu risasi, kwa hiyo, ajue shamba la bibi ni pamoja na kuiba pesa kama hizi, wakati wa Serikali hii. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Naomba uzime *microphone* yako, Mheshimiwa Felister Bura unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei taarifa hiyo, unajua naomba unajua kupe aking'ang'ania kwenye ngozi hata kama anachomwa moto, ile ngozi inachomwa moto hawezi kujua, kwa hiyo,

ameng'ang'ania jambo moja ambalo limefafanuliwa mbele kwenye taarifa hataki kusoma, asome taarifa yetu mpaka ukurasa wa 37 ataona maelezo, sasa aking'ang'ania ukurasa wa 15; atang'ang'ania na sisi tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano, inapiga vita ufisadi na wale watendaji waliodhani kwamba…

**MHE. JAMES O. MILLYA:** Taarifa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** …ukifanya ufisadi, ndio namna ya kufanya kazi...

**MHE. JAMES O. MILLYA:** Taarifa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika hawatafika mbali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura kuna taarifa nyingine, Mheshimiwa James Ole Millya.

**MHE. JAMES O. MILLYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati ya *PAC* ambayo inaongozwa na wenzetu wa upinzani, ukurasa wa 36 mtu anayeitwa Benja Majura ambaye ni Msaidizi wa *CAG* amenukuu pale akisema; Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha *1.5 trillion* hazijaibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo taarifa ililetwa na mtu wa awali kabisa mwaka jana, Mheshimiwa Zitto Kabwe aliyopata *source* yake sijui kwenye *Twitter* au kwenye *Instagram* wenzetu hawa, wakaanza kusema fedha zimeibiwa, zimeibiwa, zimeibiwa ingekuwa leo, *CAG* amesema fedha hizi zimeibiwa, hawa ndugu zangu wangesema dunia nzima, ninaomba, ninaomba, naomba ni-*challenge* uzalendo wa Mheshimiwa Zitto Kabwe, kwa mara ya kwanza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu, kama kweli aje wazi aseme, shilingi trilioni 1.5 hazijaibiwa, naye atoke kwenye *public*

aseme kwamba hizi hazijaibiwa tuone mwenendo wake na uimara kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu,

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura unaipokea taarifa hiyo.

**MBUNGE FULANI:** ... kwa hiyo mimi... masuala ya Zitto.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee, na niseme kwamba...

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. FELISTER A. BURA:...** kwa sasa Serikali ya Awamu ya Tano, haina muda kabisa na wale wabadhirifu wa mali ya umma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura, kuna taarifa. Mheshimiwa Mwambe.

**T A A R I F A**

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Ninataka nimpe taarifa msemaji anayeendelea sasa hivi na yule ambaye ametusalitia...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kangomba, kangomba kaa chini.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:...**kwamba kwenye ukurasa wa 30...

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa utulivu, Waheshimiwa utulivu tafadhali, Mheshimiwa Mwambe.

**MBUNGE FULANI:** Kangomba.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Kwamba kwenye ukurasa wa 37…

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kangomba**.**

**MHE. CECIL D. MWAMBE:…** na kwa taarifa hiyo hiyo, ambayo huyu alikuwa anaisoma na mimi naomba nisome, sehemu ambayo yeye kairuka.

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mwambe, taarifa anapewa yule kule kwa yale anayoyazungumza huwezi kumpa taarifa, yule pale kwa sababu yeye mwenyewe anampa taarifa mzungumzaji, ndio Kanuni zinavyosema Waheshimiwa Wabunge. Wewe mwenyewe ndio umesema, na mimi nimekusikia kwa hiyo Mheshimiwa Felister Bura endelea.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Si nitarudia tena.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Kangomba, kangomba huyo.

**MHE: FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuwa macho na kuwarudisha Waheshimiwa Wabunge kwenye mstari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo Serikali ya Awamu ya Tano, haina mchezo, na wabadhirifu wa mali ya umma, haina mchezo na Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli alipoingia madarakani aliona mambo yaliyofanywa na baadhi ya mashirika ya umma na akawatoa wale, haraka ilivyowezekana. Nitoe mfano, kuna uwekezaji usio tija ambao Serikali iliona na baadhi ya watendaji kwa mfano *NSSF* Wakurugenzi wote, walifukuzwa kazi, kwa miradi isiyokuwa na tija. *(Makofi)*

Sasa niombe Serikali yangu…

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ya Awamu ya Tano, kusimamia miradi yote…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura kuna taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Ninaomba nimpe taarifa msemaji anayeendelea kusema kwamba ukurasa wa 37 wa taarifa hiyo hiyo ya Kamati inanukuu maneno ya yule mtu aliyetajwa hapo nyuma ni kwamba inasema hivi; "Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri swali naweza kulijibu, kama ukisoma ripoti yetu vizuri hatuzungumzii kabisa masuala ya wizi pale, tunazungumzia tofauti kati ya makusanyo na matumizi." Lakini ukisoma pia ukurasa wa 12 kinacholalamikiwa na *CAG* ni kwamba; (g) uzingatiaji wa Mamlaka halali za kuidhinisha matumizi ya fedha; suala la (h), uzingatiaji wa Sheria Kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za Umma, haya ndio mambo tunayotakiwa sisi kama Wabunge kuyasimamia. Kwa hiyo, ninampa taarifa nayo ayachukue ili, tuyafanyie kazi na kuishauri Serikali. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kangomba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura, unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Kangomba.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Cecilia, Cecilia tulia.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei taarifa kwa sababu Mheshimiwa Mbunge hataki kusoma taarifa yote, hataki kusoma kuanzia ukurasa wa 15 hadi ukurasa wa 37, asome apate mantiki yote ya maelezo ya *CAG,* Ofisi ya Hazina, *BOT* na Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa hiyo taarifa yake sipokei.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba nchi yetu, Serikali ya Awamu ya Tano, ambaye anafanya kazi...

**MHE. JAMES O. MILLYA:** Taarifa! Taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Endelea, hiyo hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Millya.

**T A A R I F A**

**MHE. JAMES O. MILLYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa ndugu yangu kwenye ukurasa wa 37 kwamba ripoti ya *PAC* pale mwisho inasema hivi naomba ninukuu; "Kwa hiyo kitu tulichokuwa tunashughulikia nacho hapa, je, tofauti hii, imeletwa na nini? Tutapata maelezo ya kutosha kuhusu tofauti hii na ukiisoma ripoti yetu, utaona ile *table*, inaonesha kwamba tumepata *reconciliation." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu ni *CAG*, kwa hiyo hilo linajibu hilo swali, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Millya kwa kunisaidia na kuwasaidia wengine wasiotaka kusoma, wasome hii taarifa, kwa nini hawataki kuisoma!

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema, tunaiomba Serikali yetu, sasa isimamie miradi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga, kwa Mheshimiwa Felister Bura hiyo itakuwa ni taarifa ya mwisho, Mheshimiwa Haonga.

**T A A R I F A**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, mzungumzaji naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Felister Bura kwamba amesema Rais alichukua hatua kwa wale wabadhirifu, lakini katika kumbukumbu zangu ni kwamba, Dau aliyekuwa Mkurugenzi wa *NSSF* hakuchukuliwa hatua na badala yake amepewa Ubalozi, kwa hiyo hatua hazijachukuliwa, nilitaka nimpe taarifa tu kwamba hajachukua hatua yoyote ile. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa sipokei, kwa sababu wamefukuzwa kazi, Wakurugenzi wote waliokuwa *NSSF* kwa ajili ya ubadhirifu, Wakurugenzi kumi wamefukuzwa kazi. Kwa hiyo, hiyo taarifa siwezi kupokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sasa Serikali yangu, kwamba sasa, tuelekeze muda wetu, tuelekeze nguvu zetu katika kusimamia miradi yenye tija, maeneo yale, ambayo kwa mfano *NSSF* walikuwa wajenge Ofisi kule Nairobi, Wizara ya Mambo ya Nje wapo, kwa hiyo wawasiliane na *NSSF* huu mradi uendelee. Kuna mradi wa kuzalisha umeme Mkuranga, mradi huu uendelee kwa sababu Halmashauri ya Mkuranga ipo, *NSSF* wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna madeni ya SUMA JKT, Taasisi zilikopa watu binafsi walikopa, tuiombe Serikali wale waliokopa hawajaresha madeni, wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui ni kengele ya kwanza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ya pili Mheshimiwa, muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Khadija Nassir atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Omar Kigua ajiandae. *(Vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Umejitahidi hujatoka kwenye reli.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, na mimi kuweza kunipatia nafasi ya kutoa maoni yangu juu ya hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa nipende kuzipongeza Kamati zote mbili kwa kuweza kutuletea taarifa iliyosheheni maoni na mapendekezo ambayo yana maslahi mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu niwakumbushe wenzangu ambao wanajifanya kusahau kwamba hawafahamu msingi wa Kamati hizi mbili kitu gani ambacho wanatakiwa kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa kazi za Kamati ya *PAC...*

**MBUNGE FULANI:** Ooohhh Hadija.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** ...zinatokana na taarifa iliyokaguliwa na CAG. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawaelezea machache tu ili waweze kurudisha kumbukumbu zao na hisia zao karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliweza kubaini mapungufu na madhaifu mbalimbali katika ripoti ya *CAG*,

nitayaelezaa machache. Kamati yetu iliweza kubaini mapungufu katika makusanyo ya mapato yetu ya nchi. Lakini baada ya Kamati ya *PAC* kuishauri Serikali iliweza kuleta mfumo mzuri wa makusanyo wa mapato yetu na sasa hivi tunaweza kuona tija, ya mapato yetu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu iliweza kubaini mapungufu katika mikataba yetu ya madini baada ya Kamati yetu kuishauri Serikali iliweza kuchukua hatua mbalimbali. Kamati yetu iliweza kubaini upungufu wa kiutendaji, kwenye mashirika na taasisi zetu za umma, baada ya Kamati kuishauri Serikali iliweza kuteua Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu, na sasa hivi Mashirika yetu yanaweza kufanya kazi vizuri baada ya kuweza kuweka ile mianya ambayo ilikuwa iko wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu iliweza kuona mapungufu katika ufanisi wa kazi katika Halmashauri zetu. Baada ya Kamati yetu kuishauri Serikali, Serikali imeweza kuzidisha ufanisi, sasa hivi Halmashauri zetu nyingi zimeanza kupata hati safi katika mchakato wetu wa Ukaguzi. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M.GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Endelea wewe, endelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

## T A A R I F A

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa anayeongea kwamba Kamati hiyo anayoitaja inafanya vizuri katika kuamua mambo fulani, iliamuakatika ukurasa wa 13 shilingi milioni 885.5 na baada ya kuamua Rais ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Serikali na ambaye anadhibiti ubadhilifu akachukua hatua kuwasimamisha wale waliokula hela wanne, hawa kwenye karatasi hii hapa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hii. Hiyo ni moja ya kati ya...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Taarifa.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** ...na utekelezaji wa Serikali baada ya kupata maelekezo ya...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara.

**T A A R I F A**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nashukuru sana kwamba nakupa taarifa bibie/Mbunge...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** ... kuna bibie Mheshimiwa...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Hatuna bibie humu bwana!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Taarifa kwamba mimi namshukuru Mheshimiwa Zitto...

**MBUNGE FULANI:** Futa kwanza kauli.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:**...walificha hela yeye akafichua, haramu kuiba, walificha ili muibe yeye akafichua na sasa hivi mmetoa habari yake, hiyo ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachojua mtu kama...

**NAIBU SPIKA:** Taarifa ni moja Mheshimiwa, Mheshimiwa Khadija Nassir unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo siipokei, Mheshimiwa Zitto ni kati ya wahasibu ambao tupo hapa Bungeni, tupo *very competent,* yeye ni mmoja kati ya wengi ambao tupo wazi na macho kuangalia ufanisi wa Kamati na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuendelea. Kamati yetu pia iliweza kubaini madeni ya Serikali kwenye taasisi na mashirika yetu ya umma, lakini baada ya kamati yetu kuweza kushauri Serikali, Serikali imeweza kuanza kulipa madeni hayo na sasa mashirika na taasisi zetu za umma zimeanza kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo sasa naomba niende kwenye uwekezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo. Napenda kuipongeza Serikali yangu na ninapenda kuwashauri Wabunge wenzangu, kwa vile Serikali yetu ni sikivu, inasikia maelekezo ya Kamati na ushauri mmoja mmoja wa Wabunge tuendelee kufanya kazi yetu ya kikanuni kuisimamia na kuishauri Serikali katika mambo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imeanza kwenye uwekezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo. Tumeona Serikali imewekeza kwenye mradi wa *SGR* ambayo inaenda kuipa vijana ajira zaidi ya 3,000. Mradi huu unaenda kutoa uboreshaji wa Wilaya zaidi ya 16 nchini na kutoa uwezeshaji wa vijiji zaidi ya 120 katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali imewekeza katika ununuzi wa ndege, ndege hizi zitarahisisha usafiri wa wananchi na kutatua changamoto katika sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali imeweza kuwekeza katika miradi mikubwa ya umeme ambayo ita-*stabilize* uwezeshaji na uwekezaji katika miradi ya viwanda vya ndani. Mradi huu pia utachangia na kumwezesha Mtanzania mmoja mmoja katika kuweza kujikimu kimaisha. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya mambo mazuri sana...

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ulinde muda wangu.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hayo anayochangia yapo katika ukurasa gani? *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara nimetoka kukukumbusha hapa ukiwa unatoa taarifa usiulize swali kwa sababu hautajibiwa, yule anachangia sasa maswali sijui unamuuliza nani? Mheshimiwa Khadija Nassir. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Taarifa za kibwege hizo.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumezoea kuwaona wanachukua muda mwingi kupotosha,

lakini sasa tumeamka na tupo tayari kuwaeleza wananchi nini Serikali inafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo naomba sasa niende moja kwa moja katika utekelezaji wa miradi mikubwa ambayo Serikali yetu imejikita...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Wewe Tunduma kaa chini bwana.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ulinde muda wangu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka.

**TAARIFA**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza maana yake taarifa anayoitoa sasa hivi hapa anatoa taarifa...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Kanuni.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** ...ya kutekeleza miradi badala ya kujadili taarifa ya *PAC* na *LAAC.* Kwa hiyo, tunaomba ajikite, watu wana uchungu na trilioni 1.5 yeye anazungumzia utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei taarifa yake. Kwanza tu nimueleze kati ya majukumu

ya Kamati ya *PAC* ni kusimamia mashirika changa na kusimamia mashirika ambayo yameanza kazi yake. Kwa hiyo miradi ambayo tunaielezea hapa ni miradi ambayo tumeianzisha sisi na kuisimamia kama Kamati ya *PAC. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niendelee na mchango wangu ambao nitajikita kuelezea...

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mkaongee Zanzibar na wewe.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa ya mwisho hiyo inayomuhusu Mheshimiwa Khadija Nassir, Mheshimiwa Yussuf.

**T A A R I F A**

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mimi nataka nimpe taarifa kwamba kinachogomba nadhani ni hii lugha tu hapa. Sio kwamba sisi tunakataa hiyo miradi ya kununua ndege, *Stiegler*'s na nini na nini, hatukatai. Kinachogomba labda nitoe mfano ambao kila mtu hapa Bungeni ataelewa...

**NAIBU SPIKA:** Mpe taarifa mchangiaji usianze habari za mifano, mpe taarifa ukianza mifano sasa huko ndio wanakoita wenzio kuchangia. Mpe taarifa kama ni hiyo umeshamaliza sema umemaliza taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Ustaadhi kaa chini.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa hii kwamba kinachogomba hapa ni utaratibu

wa namna ya kutumia hizi fedha za Serikali, ndicho kinachogomba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sawa, Mheshimiwa Khadija Nassir unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei taarifa yake na kwa vile walizoea *tantalila* na kwa vile walizoea baada ya kuimba nyimbo zao hatuwajibu walijua kwamba hakuna watu *specific* wa kuweza kuwajibu *tantalila* zao. Naomba niwaambie hivi uwekezaji ambao Serikali imefanya... *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi kwa Mheshimiwa Khadija Nassir nimesema ile ilikuwa ni taarifa ya mwisho, Mheshimiwa Khadija Nassir una dakika mbili malizia muda wako.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuendelea na naomba ulinde muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nielezee fursa ambazo tutazipata...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mbilinyi unasubiri kunyolewa Mbeya 2020.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama mradi wa *SGR* tutaweza kupata nafasi za ajira 2,500 nchini, uchumi wa Wilaya zaidi ya 16 na uchumi wa vijiji zaidi ya 106.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo naomba nitoe ushauri, kwa vile Serikali imejikita katika kuwekeza katika miradi mikubwa naomba wakati wananza kuwekeza katika miradi mikubwa waweze kuanzisha miradi wezeshi ili tuweze kupata muda sahihi ambao tunatakiwa kuutumia katika

uwekezaji. Pia kiasi sahihi ambacho tunaweza kukitumia katika uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama kwenye mradi wa *SGR* tungeweza kuanzisha mradi wa kokoto, mradi wa chuma na miundombinu mizuri kabla ya kuanzisha huo mradi wa *SGR* tungeweza kupata *specific term* ambayo tutaitumia katika mradi wa *SGR* lakini pia tungeweza kubana matumizi katika uanzishaji wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile, mimi ni mwanakamati nimeshatoa maoni mengi sana kwenye Kamati...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako pia umeisha pia Mheshimiwa Khadija, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mbilinyi umesikia?

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija muda wako umekwisha, asante sana. Mheshimiwa Khadija muda wako umekwisha, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anatropia Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Kigua, Mheshimiwa Anastazia Wambura ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nitaanza kwa kum-*quote* anaitwa Authon, aliwahi kusema; *"accuracy is the twin brother of honesty,"* lakini Edward akasema; *"accuracy of the statement is one of the first element of truth"* au unazunguka unasema *in accuracy is the near keen to falsehood,* kwamba

usipokuwa *accurate you are likely to lie,* usipokuwa na taarifa ambazo ziko sahihi, utasema uongo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina-*quote* hotuba ya Kamati ambayo mimi ni Mjumbe wake, tumetoa mapendekezo mazuri, akasema ni; "ni muhimu pia ikaangalia kwa makini suala la watumishi wa Wizara na uwezo wao wa kufanya kazi kwa ueledi zaidi."

Ninarudi kwenye ripoti ya *CAG,* yeye akasema tulikuwa/tumekuwa na *issue* kwa muda mrefu ya kutoonekana kwenye vitabu *1.5 trillion;* alikuja kwenye kamati yetu na ametoa taarifa yake. Nina-*quote* sehemu ndogo anasema; *however these re-worked totals did not fully reconcile as there where an excess of expenditure over revenue amounting to figure of 290.13 billion. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kumbe alienda kukagua *authenticity* ya *1.5 trilion* akakuta kuna kitu kingine, kuna ongezeko la 290 bilioni. Kwa hiyo kwa jibu *simple* na alichoenda kuangalia kwamba wapi *1.5 trillion* akakuta kuna kingine zaidi ya *1.5 trillion,* akakuta kuna ku-*spend* zaidi kwa bilioni 290. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini tumefika hapa, ni kwa nini tumekuwa na hoja za ukaguzi? Ninarudi kwa watumishi wa Hazina ambao tunawategemea na hawafanyi kazi inayostahiki. Mjumbe yeyote wa Kamati akisimama hapa asiongelee suala la utendaji usioridhisha wa Hazina ambao umeleta hizi *auditing queries.* Kama tusipo-*address* hili suala litaendelea kujitokeza*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali najiuliza, ilikuwa ni bahati mbaya kwamba taarifa hazikuwasilishwa kwa wakati kwa ajili ya kukaguliwa na *CAG?* Ilikuwa ni bahati mbaya kwa wafanyakazi ambao wapo *competent,* kwa watu ambao wanajua nini…

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** ...*deadline* ni lini ya kuwasilisha hesabu...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Nataka nimpe taarifa Mhesimiwa Mbunge anayechangia kuwa nampongeza kuwa ameelewa, kumbe si suala la upotevu wa pesa, kumbe suala la ulegelege wa watendaji kwa hiyo awaambie hao, awaelezee, nampongeza sana ndio maana kofia yangu nilimwachia. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, sita-*deal* na watu wanaotafuta umaarufu mdogo mdogo, nakushukuru.

*Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza na quote yangu kuonesha weakness kubwa ambayo ipo Hazina ambayo ndio imepelekea kupotea kwa kiwango kikubwa cha fedha ambacho hata leo Mheshimiwa Catherine ametuweka wazi si tena 1.5 trillion bali ni two plus trillion. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji ambaye anaendelea kuongea kwamba shilingi bilioni 290 ambayo tumeelezewa, tumeelezewa vizuri kwamba Serikali ina mamlaka ya kuongeza matumizi kulingana na Sheria ya *BOT* na mzungumzaji anayeongea sijui ni mwanasheria sijui ni nani ndio maana anaongea ambayo hayafahamu. Naomba sasa nimpe shule kidogo ili aweze kujikita na hoja zake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaweza kutumia zaidi ya kile ambacho kimepangiwa kutokana na mujibu wa sheria ambazo tumezitunga humu ndani na shilingi bilioni 290 hiyo ambayo anaiongelea tulishapewa maelezo yake. Sasa hivi labda anaielezea kutokana na kwamba vyombo vya habari vipo hapa aweze kupata kile ambacho wanakitaka kila siku. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge utulivu kidogo tuelewane.

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, muda wetu unakwenda mbio na wachangiaji bado ninayo orodha hapa mbele. Mheshimiwa Anatropia Theonest ataendelea kuchangia bila taarifa na wachangiaji wanaofuata pia kutakuwa hakuna taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nimesema utendaji wa Hazina, siamini kwamba ni wa bahati mbaya, ninaamini kwamba ni utendaji mbovu wa makusudi unaotupeleka au unaotufikisha hapa tulipo leo. Ninaongea kwa masikitiko kutoka kwenye *executive summary* ya *CAG* anasema wakati wa kutunza kumbukumbu zao katika...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata taratibu)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:...** huyu wa mwisho, naomba nimpe taarifa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi nimeshatisisha taarifa zote sasa hivi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Ulisema huyu wa mwisho, nina taarifa muhimu.

**MBUNGE FULANI:** Huyo mfungwa.

**NAIBU SPIKA:** Hata kwake yeye hawezi kupokea.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Nina taarifa muhimu sana naomba nimpe taarifa...

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** 2020 unang'oka wewe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi huwezi kuongea nimezima *microphone* yako kwa hiyo hautasikika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbilinyi nimezuia taarifa tafadhali, Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MBUNGE FULANI:** Wewe mfungwa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naomba nimpe taarifa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi taarifa tumeshasitisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuelewane kwa sababu nikishairuhusu ya kwake peke yake mtaanza kulalamika muda sio mrefu kwa hivyo hakuna taarifa kama nilivyoamua. Mheshimiwa Anatropia Theonest. Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini tafadhali. Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** ...ana miaka! Ana miaka chini ya 18.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongelea Hazina ya Taifa inayotumia...

**MBUNGE FULANI:** Mbilinyi Mungu akuweke hai...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** ...*spread sheet* katika kutunza taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mfungwa

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge msiwashe *microphone* tafadhali.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana haya mambo yamefanywa *deliberately,*

haya mambo yamefanywa kimkakati na tupo *likely* kuendelea kuona hayo mambo, tutakuwa na *reconciliation* leo, kesho na keshokutwa. Ni Hazina gani haijui lini mwisho wa kuwasilisha taarifa kwa ajili ya ukaguzi wa *CAG?* Kama haitoshi *CAG* pia ameanisha kwamba kumekuwepo na *mismatch* ya *hundreds billions of money* kutoka kwenye *exchequer issue warranty. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kuna *exchequer issue warranty* ya bilioni 656.5 ambazo *exchequer issue warranty* hazi-*match* na *exchequer issue report.* Tuna *exchequer issue warranty* za bilioni 3.45 ambazo zimekuwa *cancelled* na hakuna taarifa kokote kuonyesha zimekuwa *cancelled.* Pia kuna *exchequer issue warranty* ya bilioni 56.07, wameweza *ku-verify only 51.3 billion* ambayo kuna *earning* ya bilioni tano na ikaonyesha kwamba Wizara ili-*cancel* bilioni moja na hapo tunabaki na bilioni 3.29 hazijulikani taarifa zake zipo wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama haitoshi, kuna *exchequer warrant* ambazo ni za shilingi bilioni 234. Kwenye *Exchequer Release Report* hazionekani kokote na wanavyoulizwa, nina-*quote* hapa, anasema: *"The Ministry explained that the fund were released for the previous year transcations which were processed but would not be cleared in The Financial Year 2015/2016." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* akaenda mbali akasema: "*The lack of disclosure records of the prior year transaction in the question indicates that the exchequer report was misstated." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako madudu mengi sana ambayo ukiyatazama sisi kama Wanakamati tunaamini kwamba ni lazima mfumo ufanyiwe *overhaul.* Tusipofanya hivyo, tutakuta fedha nyingi zimeibiwa kuliko ambavyo tunafikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongelea kuiba siyo lazima uzipeleke kwenye mfuko wako. Kama fedha zimekuwa *planned* kufanya kitu A na umefanya na hakuna *detail* au hakuna viambatanisho, kwa Mhasibu au kwa mtu yeyote anaye-*deal* na hesabu, hizo fedha zimepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye suala la matumizi ya Fedha za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF).* Kumekuwepo na ununuzi usioridhisha au uwekezaji usiokuwa na tija wa *billions and billions of money.* Mfano, ardhi iliyonunuliwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, ameeleza mwenzangu kwamba *plots* nne tu. Nimekwenda mbali zaidi, wanasema ni kama ekari 1,000, lakini fedha iliyotumika ni takribani shilingi bilioni 16 *point something.* Haiingii akilini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakaeleza hata eneo lingine liko Kigoma, Mwandiga, ekari moja kwa shilingi milioni 66. Haiingii akilini! Unaona kwamba kama Serikali ipo, kwa sababu mmeongea leo kana kwamba hii Serikali ndiyo kwanza ina mwaka wa tatu; hii Serikali tuliyonayo leo ina takribani miaka 56 *plus* madarakani. Kwa hiyo, haya madudu tunayoyaongelea leo yametokea miaka yote ambayo mmekuwa madarakani na ninyi ambao mnapaswa kuisimamia Serikali mnapaswa kuwa *answerable. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongea kwamba kuna fedha, shilingi milioni 888 wamelipwa watu ambao sio Askari Jeshi, sio Polisi, majina yao yapo yameainishwa na Mheshimiwa Waziri anayaona, Waziri ambaye anajitamba kwamba anafanya kazi. Mmeshindwa nini kuwafikisha kwenye vyombo vya dola, kama siyo kwamba tunalea watu na tunaonea watu ambao tunadhani tunaweza tukawaonea? *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Ni *Campaign Manager* wa Bonnah Kaluwa huyo.

**MBUNGE FULANI:** Wewe!

**MBUNGE FULANI:** Futa kauli huko!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tafadhalini sana. Mheshimiwa Anatropia, dakika moja, muda wako umekwisha, kengele ya pili ilishagonga.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *In a nutshell* nasema, tulichokiona katika Hazina ya Taifa ina-*reflect* nia yetu kama taifa, ina-*reflect* kwamba hayo makosa yaliyofanyika katika kuweka takwimu yamefanywa *deliberately,* kwa lengo la kupoteza au ku-*misdirect* fedha za walipa kodi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omari Kigua, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuzungumza jioni ya leo. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana kama kila mmoja wetu miongoni mwa sisi Wabunge anaweza kusimama tu na kutoa taarifa ambayo inaweza ikawa ina-*distort* nchi hii. Nchi hii ina wafadhili, nchi hii ina walipa kodi; unaposema *1.5 trillion* imepotea, imetumika vibaya, maana yake unawafanya walipa kodi wasiweze kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli usiopingika ni kwamba Kamati za *PAC* na *LAAC* msingi wa kazi zao ni kupitia ripoti ya *CAG. CAG* ndio jicho la Kamati hizi mbili. Niwakumbushe wazungumzaji waliopita hapa kwamba Ripoti ya *CAG* inapopita, inapokuja kwenye Kamati zetu, tunapitia lakini pia tunawashirikisha Makatibu Wakuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *audit query* ni suala la kawaida kabisa. Huwezi ukasema kwamba hoja hazitakuwepo. Tukumbuke kwamba suala la mifumo hii ni ya kawaida kabisa. Wamezungumza hapa ndugu zangu, baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya *PAC,* wanasema kwamba Hazina wanatumia *excel.* Haiingii akilini hata kidogo. Huwezi ukafanya *integration* ya hesabu…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukafanya *integration* ya hesabu...

**MBUNGE FULANI:** Tulia wewe!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukajumuisha hesabu za Serikali za Mitaa, Serikali Kuu na mashirika kwa kutumia *excel.* Hii haiingii akilini hata kidogo. Narudia kusema tena kwamba ripoti ya *CAG* siyo *conclusive.* Maana yake ni kwamba bado kuna *room* ya kukaa na kuweka sawa. Ndiyo maana kwenye taarifa hii kuna sehemu kuna neno "*reconciliation"* na "*adjustment." (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake ni nini? Maana yake hoja ya *CAG* walikaa na watu wa Hazina. Sasa wapo Wajumbe hapa ambao hawakupata fursa ya kumsikiliza *Accountant General* kazungumza nini. Sasa kuna watu hapa wamefundishwa taarifa, ambao nawalaumu sana. Nadhani hili siyo jambo zuri. Mtu kuwa na weledi mkubwa wa mambo ya hesabu, usikubali kuchukua taarifa za mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumziwa suala la shilingi bilioni 290, sheria inasema kwamba *BoT* wanaweza wakatoa 1.2 *expenditure* kwa Serikali kwa hiyo bado Serikali iliweza kutumia kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Zanzibar, mapato yale yanakusanywa na *TRA* Zanzibar, lakini ni lazima yaingie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali lakini yanarudi Zanzibar. Ubaya uko wapi hapo? Sasa tukubaliane jambo moja; hebu tuweke utaratibu wa kutoruhusu kila mtu kuzungumza jinsi mtu anavyoona.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe unazungumza taarifa ya *CAG* ambayo haijawa-*verified,* sisi tumemwona *CAG*

hapa, amesema mwenyewe kwamba hakuna matumizi mabaya wala hakuna wizi. Suala la *CAG* yeye hagundui *theft* na *fraud,* anatoa *opinion.* Hawa wenzetu suala la wizi wamelitoa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mjumbe hapa kasema kwamba siyo *1.5 trillion,* imekwenda mpaka trilioni mbili, atuambie ana ripoti nyingine ya *CAG* nyingine*?* Hilo naomba athibitishe, kwa sababu sisi tume-*rely on* Taarifa ya *CAG,* yeye taarifa ya shilingi trilioni mbili kaipata wapi? Huwezi uka-*distort profession* yako kwa sababu ya mambo ya kisiasa. Umeapa, lazima uwe mkweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Wajumbe badala ya kuipitia taarifa vizuri na kuangalia maoni ya Kamati yetu, tumezungumza mambo mazuri sana. Serikali hii mambo yote ambayo hayako sawa yamezungumzwa kwenye taarifa hii, kwa nini wanang'ang'ania eneo ambalo tayari *CAG* ameshali-*clear? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe ushauri mmoja, kama kuna Mjumbe ambaye bado ana wasiwasi, anaweza bado akamwomba *CAG* na utaratibu unaruhusu, lakini suala la *1.5 trillion* tayari limeshafungwa *page* na halipo tena. Naomba msiwaaminishe Watanzania kuwa kuna wizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa sana, wakati tunaandika ripoti hii tulikuwa pamoja na wenzetu. Walikuwa na nafasi ya kumwuliza *CAG.* Vile vile *PST* kwa maana ya *Paymaster General,* alikuja, kwa nini hawakumwuliza maswali hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuthibitishie jambo moja; watumishi waliopo Wizara ya Fedha pale ni watu ambao ni *very professional.* Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mhasibu Mkuu Msaidizi wa Serikali, wote ni *CPA holders.* Hiyo ni sambamba na watu wa *CAG. (Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuanza kuhoji *competence* yao, nadhani siyo sahihi. Tukubaliane kabisa kwamba suala la kurekebisha mifumo ni sawasawa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua subiri. Mheshimiwa Salome, kanuni inayovunjwa.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 68 na Kanuni inayovunjwa ni Kanuni ya 64(1)(a) inayosema: "Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli;"

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge anayezungumza anasema *CAG* amethibitisha kwamba 1.5 hazijaibiwa. Siyo kazi ya *CAG* kusema pesa zimeibiwa au hazijaibiwa. *CAG* analeta ripoti Bungeni Wabunge ndio tunaojadili na kufanya maamuzi kama pesa zimeibiwa au hazijaibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mzungumzaji anayezungumza anavunja utaratibu. Kamati imeleta taarifa thabiti inayoonesha kwamba Hazina wanatumia *excel,* kama anapingana na maamuzi ya Kamati, aseme, lakini asipotoshe ripoti iliyokuwa *tabled* mbele yako na mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Salome Makamba amesimama akionesha kwamba Kanuni ya 64 inavunjwa na Mheshimiwa Omari Kigua. Ametoa hapo maelezo yake kuhusu taarifa ambayo Mheshimiwa Kigua anachangia; naye anatoa maelezo yake.

Sasa kwa sehemu ya kwanza ya maelezo yake ambayo ni ya jumla, kwamba *CAG* alisema yeye kazi yake

ni ipi; na anachozungumza Mheshimiwa Kigua; hilo halina uhusiano kama Mheshimiwa Kigua anaongea uongo ama ukweli. Kwa hiyo, huwezi kutumia Kanuni hii kwa maelezo ya sehemu ya kwanza aliyoyasema Mheshimiwa Salome Makamba. *(Makofi)*

Pia ameeleza, Waheshimiwa Wabunge, hivi mnakuaje kama watoto? Mnakuwaje kama watoto jamani? Tuko Bungeni hapa, kila siku mnakumbushwa mnarudia jambo hilo hilo. Sisi wote ni watu wazima, tunaitwa Waheshimiwa, tuheshimiane.

Mheshimiwa Salome Makamba pia ameeleza sehemu ya pili ya maelezo yake anasema taarifa iliyotolewa na *CAG* inaonesha kwamba kuna matumizi ya *excel* na Mheshimiwa Omari Kigua yeye anasema ni ngumu kufanya hayo mahesabu ambayo yanatarajiwa kufanywa na Hazina kwa kutumia *excel.* Sasa mimi katika kusikiliza kwangu niseme wazi ningeweza kupata *Hansard* ningejua alichokisema ni kipi. Kwa sababu ukisema huwezi kutumia *excel* kwenye mahesabu kama hayo, ni tofauti na ukisema *CAG* anadanganya kwa kusema watu wametumia *excel.*

Sasa kwa sababu siko na *Hansard* hapa, siwezi kulizungumzia sana hilo, naomba tuendelee. Isipokuwa kwa sababu limeombewa utaratibu jambo hili na ni lazima tufuate hizo taratibu, hatuwezi kuanza kumwuliza Mheshimiwa Kigua umesemaje na yeye huyu kasemaje? Tutakapozipata zile *Hansard* tutakuja kutoa hapa maelezo.

Mheshimiwa Kigua endelea. *(Makofi)*

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pengine labda niendelee kwa kusema maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano kati ya Ofisi ya Bunge na *CAG* ni mazuri sana na Kamati za *LAAC* na *PAC* zimeweza kufanya kazi nzuri sana kwa kupitia Ofisi ya *CAG.* Tukubaliane kwamba hata katika utaratibu wetu wa Kamati

hizi, pia watumishi wa *CAG* wakija pale huwa tunawapa *challenge,* umekagua hili; hili siyo sawa na hili siyo sawa. Huo ndiyo utaratibu wetu wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia suala la kutumia *excel,* nazungumza *professionally* kwamba haiwezekani kutumia *excel* kuweza ku-*consolidate* hesabu za Serikali nzima, haiwezekani. Pia na-*refer* majibu ya *Accountant General* kwamba hilo halijafanyika. Sasa haya ni mambo tu ya kawaida. Hizi zinaitwa hoja za ukaguzi na hoja za ukaguzi zipo kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza eneo hilo, sasa nirudi kwenye suala la mikataba hasi ya *NDC.* Hapa tulijikita zaidi, tuliona ni eneo ambalo haliko vizuri, nadhani katika taarifa yetu ya Kamati hapa tumeelezea vizuri sana. Ushauri wangu kwa Serikali, kupitia kwa *Attorney General* pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda, wapitie waangalie mikataba ya *TANCOAL,* haijakaa vizuri hata kidogo. Kwa sababu tunaiona dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kwamba tunapata mapato, sasa inawezekana vipi kama una mikataba hasi? Maana yake gawio lile haliwezi kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri sana, maeneo yote ambayo tumeainisha yahakikishwe kwamba yanafanyiwa kazi. Naamini kabisa kwamba taarifa hii, kwa sababu tumewashirikisha wenzetu wa upande wa pili, italeta mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista Mhagama.

## MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ambayo inasema: *"Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba "Mwongozo wa Spika" kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa."*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ambayo iko hapa mbele yetu ni ripoti mbili za Kamati. Ripoti hizi mbili za Kamati zimejieleza vizuri na hasa ripoti ya *PAC* ambayo msingi wake ni Taarifa ya Ukaguzi ya *CAG.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waheshimiwa Wabunge wakiendelea kuchangia hapa ndani, kumezuka taarifa tata mpya ambayo haiko kwenye hii ripoti; na kama tukiiacha na tunakaondoka hapa ndani ya Bunge lako bila kupata maelezo fasaha ya jambo hili, ninadhani hatutakuwa tumejitendea haki wenyewe, hatutakuwa tumewatendea haki Watanzania na hatutakuwa tumeitendea haki ripoti ya *PAC. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge hapa wanazungumzia upotevu wa fedha za Kitanzania shilingi trilioni 2.4 ambazo kwenye ripoti hii hazijaonekana na wala kwenye taarifa yoyote ambayo iko kwenye meza yako, na kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1) Mbunge anatakiwa kuzungumza jambo ambali liko ndani ya Bunge na liko kwenye mjadala tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako ili tusije tukatoka hapa leo na taarifa nyingine ambazo siyo taarifa rasmi za taarifa hii ambayo inajadiliwa hapa ndani

na ni taarifa ambazo hatujui zimetolewa wapi; chanzo chake ni nini; na ukweli wake ni upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo katika jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Ameelekeza Mwongozo wake kwenye taarifa ambayo imetolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge wawili kwamba pamoja na ile shilingi trilioni 1.5, sasa zimeongezeka nyingine shilingi bilioni 900, kwa hiyo, inakuwa shilingi trilioni 2.4.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu nimeombwa mwongozo kwamba je, hili jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi hapa Bungeni? Waheshimiwa Wabunge mnaweza kukumbuka hili jambo limekwenda kwa muda mrefu kidogo, hasa hili la shilingi trilioni 1.5 lilitolewa maelezo hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kipindi chetu kilichopita mwaka 2018 likaendelea huko mtaani niite na vyombo vya habari na hapa na pale na sisi wenyewe Wabunge tukichagiza hapa na pale.

*CAG,* kwa taarifa nilizonazo kutoka kwa Kamati, lakini pia kwa hii taarifa iliyo mbele yetu, tatizo ninaloliona ni kwamba Waheshimiwa Wabunge tukishajiambia akili zetu zilikoelekea, basi hata ukelekezwa njia hii inakwenda shimoni, unataka uende mpaka utumbukie kwanza.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, taarifa hii ya *PAC* imeeleza kuhusu trilioni 1.5 kwa wazi kabisa, lakini Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ambazo pengine zinajulikana ama hazijulikani bado wameendelea kutokumsikiliza huyo ambaye ndiye anayetuletea mahesabu ili sisi tufanye kazi. Kwenye Kamati wote waliozungumza hapa ndani kwa taarifa zilizopo walikuwepo huko na kama kungekuwa na maswali ya ziada yangeulizwa huko, lakini kwa kuwa hili ni jumba la kisiasa pamoja na mambo mengine, watu hupenda kufanya siasa hata kwenye vitu ambavyo

Mheshimiwa Mbunge wangu wa Mbeya Mjini anasema *number don't lie*, *CAG* amekwisha kutoa majibu ambayo Mwenyekiti wa Kamati hii ni Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka ambaye huyu ni Mwenyekiti kutoka chama cha upinzani ili aweze kusema kwa uhuru anayoyaona yeye, maana ndiyo aliyekuja kusoma taarifa hapa. *(Makofi)*

Sasa tunavyoendelea kuonesha kana kwamba trilioni 1.5 bado haina majibu mpaka leo, tunayatafuta majibu kutoka wapi? Kama tunasema tunasoma taarifa za Mkaguzi wa Hesabu na Mkaguzi alishakuja akatoa taarifa vizuri, tunataka kumsikiliza nani? Hilo ni moja.

La pili, imeongozeka sasa taarifa nyingine kana kwamba juu ya hii trilioni 1.5 pamoja na majibu ya *CAG* bado kuna shida, sisi Waheshimiwa Wabunge tuna matatizo kwa sababu tunapenda mambo ambayo yamekaa kinamna ya kuandikwa hivi na chombo cha habari, usiposema basi hutaandikwa, kwa hiyo unaona kama umaarufu unashuka kidogo hivi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimeombwa mwongozo, kama jambo hilo je, linaruhusiwa au haliruhusiwi. Mwongozo wangu ni huu jambo hilo haliruhusiwi, huo ndiyo Mwongozo wangu. Kwa sababu wasiwasi ama niseme mawazo ya Mheshimiwa Jenista ni kwamba watu watatoka hapa wakiwa wamejumlisha kama wenzetu ambao wameamua kupotosha jambo hili namna walivyojumlisha, halafu ikaonekana kule nje kwamba ndiyo uhalisia wenyewe. *(Makofi)*

Sasa katika Mwongozo wangu kwa kuwa nimesema jambo hilo haliruhusiwi, jambo hilo kwa kadri lilivyozungumzwa na Mheshimiwa Catherine Ruge, lakini pia na Mheshimiwa Anatropia Theonest linaondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hasunga.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii, kuzipongeza sana Kamati zote mbili kwa kazi nzuri ambayo wamezifanya na kwa ripoti ambazo wamezitoa ambazo zimetoa ufafanuzi na uchambuzi wa kina wa masuala mbalimbali. Inawezekana tukajadili mambo ya msingi na inawezekana wakati mwingine tukaingia kwenye siasa katika mambo ambayo hayastahili siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu tunachokijadili hapa ni mahesabu ya Kamati hizi mbili, mahesabu yaliyokaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Kamati ya *PAC* na Kamati ya *LAAC* na hizi Kamati kwa kawaida ndiyo zinafanya kazi kwa niaba ya Bunge, kwa niaba ya sisi wote hapa, katika kuchambua taarifa mbalimbali zinazohusiana na masuala ya mapato na matumizi ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema tu kidogo kwamba tunapozungumzia suala lolote kuna vitabu vya uhasibu ambavyo ni vya msingi ambavyo ndiyo vinatupa taarifa za kuzichambua. Hivyo vitabu visipoonesha chochote, ukichangia tofauti na hicho utakuwa una jambo lako kichwani. Sasa ukisoma Kanuni za Kimataifa za Utayarishaji wa Mahesabu ya Umma, ambazo ni *IPSAS,* ambayo tunaizungumzia sasa hivi imekuja na utaraibu kwamba tunatumia *Accrual Account System.* Pengine nikilisema hili watu wanaweza wasielewi nifafanue, kuna misingi mitatu unaweza ukatumia *Accrual Account System*, unaweza ukatumia *Cash Accounting System*, unaweza ukatumia *Modified Accrual Account System*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka yote ya nyuma, miaka ya nyuma tulikuwa tunatumia *Cash Accounting System* ambayo tulikuwa tunalinganisha fedha ulizokusanya na matumizi uliyotumia, basi umemaliza. Unaposema *Accrual Accounting System* maana yake, mapato unayoiripoti kwenye vitabu ni mapato ambayo unaweza ukawa umepokea *cash*, unaweza ukawa hujapokea *cash,* lakini tayari huduma imeshatolewa. Unapozungumzia matumizi, tunayoyasema yanaweza yakawa ni matumizi ambayo

tumeshalipa tayari fedha na yanaweza yakawa matumizi ambayo bado hujalipa fedha, lakini tayari unadaiwa unatakiwa ulipe,

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiyajua hayo vizuri, utazichambua hizo taarifa vizuri. Taarifa ya kwanza ambayo tunaichambua ni kitabu cha mali na madeni ambacho kinaitwa *Statement of Financial Position* inaonesha hayo na hili ukielewe hicho uelewe mali zilizopo, uelewe madeni yaliyokuwepo tarehe ile kwa tarehe 30 Juni mwaka 2017, ndiyo maana tunaita *as at 30th June.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu cha pili cha muhimu ni kitabu cha mapato na matumizi ambayo tunaita *Statement of Financial Performance*. Katika hili tunaonesha mapato yote, yale tuliyopokea na ambayo bado hatujapokea lakini tunadai, yote tunaonesha. Ndiyo maana kwenye ripoti ile ya awali mlielekezwa kwamba kuna *receivables*, ambazo maana yake ni mapato ambayo tumeshatoa huduma, lakini bado hatujayapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hayo kwa mantiki hiyo hayo ukiangalia kwenye *exchequer* huwezi kuyaona, sitosikia, kwa sababu ni mapato bado hujapokea, ndivyo hivyo kwenye matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitabu cha tatu na cha msingi kinaonesha mtiririko wa fedha yaani *Cash Flow Statement*; sasa ukiunganisha *Cash Flow Statement* itakavyoonesha *balance* huko ilingane na kile kitabu cha mali na madeni ile *cash and cash equivalent* inayokuwa *reported* pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiendelea kuchambua kuna kitabu cha nne *changes in equity;* kuna kitabu cha tano kinaitwa *Budgetary Performance Report. Budgetary Performance Report* ndiyo inatupa taarifa ya bajeti nzima ya Serikali na matumizi yalivyofanyika katika mwaka huo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unapokuja na hoja kwamba kuna trilioni 1.5 imepotea cha kwanza tunakuuliza unatumia kitabu gani ambacho taarifa hizo zipo? Ndiyo maana ukisoma kwenye vitabu vyote hivyo nilivyovisema ukiongeza *Directors report*, sijui *Accounting Officers report,* hakuna hayo. Mtu pekee ambaye angeweza kutuambia hayo kwamba kuna matatizo ni *CAG.* Kwenye ripoti yake alipoileta hakuonesha kama kuna tatizo, haiwezekani *CAG* ambaye ni Mtaalam ambaye ana wataalam waliobea akaandika eti akaficha trilioni 1.5 haiwezekani, hilo ni ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya pili, kwenye Kamati ndiyo maana hoja hii tunayoijadili, ni hoja ambayo imetoka kwenye uchambuzi wa mitaani ambao haupo kwenye misingi ya vitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtu anayeelewa ukichukua huu ukurasa wachambua hata hili ripoti ya Kamati inayoongoza na wenyewe wenzetu, ripoti hii kuanzia pale ukurasa wa 21, 22 23 mpaka 24 wameonesha maana ya *reconciliation* kuanzia mwanzo mpaka mwisho, mmesoma hizi mmezielewa? Inawezekana tunajadili kwa sababu hatujapata tafsiri hizi za *figures.* Naomba tuwe na muda wa kutosha wa kuchambua kilichoandikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafurahia sana ninapoona kwamba *CAG* hajaonesha, Kamati yenyewe ya kwao haijaonesha, ambayo ndiyo msingi wa majadiliano ya humu Bungeni. Kwa hiyo na maazimio yao waliyoyasema wameonesha waliuliza, je fedha zilipotea? Wakasema hazijapotea, sasa tunapoteza wa nini? Kwa hiyo, hilo naomba, liwe vizuri, lieleweke vizuri na tusitake kupotoshana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kusema, vitabu vinafungwa tarehe 30 Juni. Baada ya vitabu kufungwa kuna miezi mitatu, miezi mitatu ile maana

yake nini? Maana yake kama kuna matumizi mengine yako yuko kama kuna *adjustment,* mnatakiwa mzifanye, ndiyo maana mnapewa miezi mitatu. Kwa mfano, inawezekana ikawa watu walichukua *imprest, imprest* hatuzitambui kama matumizi mpaka pale zinapokuwa zimekuwa *retired*; sasa zile zote zitakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ukija mwezi wa Tisa ukifunga na ukifunga mwezi wa Tisa unapopeleka kwa *CAG* vile vinaitwa *draft financial stastement*, *draft* maana yake nini, maana yake unapompelekea *Auditor* akienda akakagua kama kuna maeneo yakurekebisha atakwambia karekebishe hiki, usiporekebisha nitakupa *qualified opinion*, ukirekebisha hakuna hoja; akikwambia fanya hiki, ukafanya, hoja imekwisha, ndiyo maana ya *audit.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kuna haja ya Bunge lako Tukufu kupewa muda wa kutosha na kupatiwa semina ya kutosha ya namna ya kuchambua hivi vitabu, kwa sababu tukiipata hiyo, nadhani hata matatizo ya tofauti zetu hizi yatakuwa yamekwisha. Hata hivyo, nataka kusema tunafanya kazi nzuri, lakini tunahitaji kuwa na uchambuzi wa kisayansi na wa kina ili tuchangie vizuri tuisaidie Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana na nawapongeza wote. Ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa. Mheshimiwa Selemani Jafo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza binafsi napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe kwa kutuongoza. Pia nishukuru Kamati zote kwa kazi kubwa waliyofanya na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni michache sana, kubwa zaidi kwanza naomba nishukuru kwa mchango wa Kamati ya Bunge ya *LAAC* kwa kazi kubwa tunayoendelea kuifanya kwa pamoja. Nikiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, niishukuru sana Kamati hii toka tulipoanza kufanya kazi pamoja, mimi mwenyewe binafsi nashuhudia mapinduzi makubwa sana katika usimamizi hasa wa rasilimali fedha, kwa upande wangu naishukuru sana Kamati. Kwa kweli kwa upande sisi hata utapoona leo hii kuna mabadiliko makubwa sana ya jinsi gani rasilimali fedha na upatikanaji wa hati safi mpaka zimefikia asilimia 90, hili si jambo haba ni Kamati imefanya na Serikali tumetekeleza katika baadhi ya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue mapendekezo ya Kamati yalivyotoka kwa ajili ya kwenda kuyafanyia kazi kwa sababu lengo kubwa ni kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Serikali katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, kwa sababu wamechangia mambo mbalimbali na naamini lengo lao ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa rasilimali fedha. Ndiyo maana tunaona hata ripoti ya *CAG* inavyotoka na hata Kamati inavyotushauri tumeamua kuchukua hatua mbalimbali katika vipindi tofauti, takribani toka ripoti zilivyotolewa tumechukua hatua kwa watumishi takribani 343. Hili siyo jambo dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikwambie hakuna jambo kubwa katika maisha kama kuchukua hatua kwa watu ambao wamefanya makosa na tunajua kwamba watu hawa wana familia zao, lakini kama viongozi lazima tufanye maamuzi na hili niseme tumechukua hatua mbalimbali; kuna watu wengine wamefukuzwa kazi kabisa, kuna watu wengine wamepewa onyo na kuna wengine wamepelekwa Mahakamani hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka hata ripoti ya *CAG* ilivyotoka siku ile ile unakumbuka, kwamba maelekezo yalitoka na karibu Wakurugenzi watatu siku ile ile walipoteza kazi, tukiangalia Halmashauri ya Ujiji, Halmashauri ya Kigoma

na hali kadhalika Halmashauri ya Pangani. Hata hivyo, sisi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatekeleza maelekezo ya Kamati, kama Kamati ilivyosema kwamba pale tumeanzisha Kitengo ambacho kinaitwa *Follow up and Investigation Unit,* kitengo ambacho kimetusaidia kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakumbuka hata juzi juzi kulikuwa na tukio kule Ulanga ambapo unaona kwamba ni maamuzi na mwelekeo sahihi ya kitengo hiki. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba, tunaboresha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa na mwisho wa siku tuhakikishe kwamba zile rasilimali fedha zinaenda kusimamiwa vizuri katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikuhakikishe kwamba Ofisi yangu itaendelea kutekeleza maelekezo ya Kamati kwa kadri iwezekanavyo, lengo kubwa ni kwamba rasilimali fedha zielekezwe katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ziende zikajibu matatizo ya wananchi. Katika kipindi hiki cha karibuni tumeweza kuchukua maamuzi mbalimbali, kwa mfano, ukiangalia kule Nyang'wale, Nkasi na Tunduru na maeneo mengine mbalimbali. Haya yote tumeyafanya tukiwa na lengo kwamba, basi zile hoja mbalimbali zinazotolewa ziweze kufanyiwa kazi kwa ajili ya mustakabali na Serikali yetu iweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ilijitokeza katika suala zima la Mfuko wa Vijana hasa upande wa kanuni na ni kweli tulitunga sheria hapa. Bahati nzuri sheria yetu iko *very straight forward*, kwamba sheria yetu inatekelezeka moja kwa moja. Hata hivyo, ofisi yangu mchakato wa kanuni sasa hivi uko hatua za mwisho, wadau mbalimbali wameshashiriki, tuko katika *stage* ya mwisho kabisa ambayo nina imani na kupitia ofisi yangu pale tunatarajia huenda mwishoni mwa mwezi huu mchakato huu utakuwa umekamilika. Kwa hiyo jambo hili litakuwa tayari utekelezaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru sana hasa niwashukuru wenzetu wa Wizara ya Fedha. Zamani kwa vipindi tofauti tumeona tatizo la upelekekaji wa fedha lilikuwa

kubwa sana, lakini hivi sasa nadhani kutokana na maelekezo yanayotolewa na Kamati ya *LAAC,* leo hii ninavyozungumza zaidi ya kati ya shilingi *1.3 trillion* ambayo ni *development budget* iliyopaswa kwenda katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa zaidi ya shilingi bilioni 640 zimeshafika, ni wastani wa asilimia 48.8, mpaka hivi sasa ndani ya kipindi hiki mpaka mwezi Desemba. Naona *trend* hii mpaka tukapofika mwezi wa Sita hali itakuwa ni shwari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika jambo hili Waheshimiwa Wabunge naomba niwaambie katika suala zima la utekelezaji wa ripoti ya *CAG*, lakini halikadhalika maelekezo ya Kamati, jambo hili sasa nina imani linaenda vizuri zaidi. Maana yake leo hii ukizungumza zaidi ya shilingi bilioni 640, ambayo katika kipindi cha nyuma inawezekana hiyo ndiyo fedha ya mwaka nzima, leo hii Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wanashuhudia katika Wilaya zetu jinsi gani zaidi ya shilingi bilioni 105 zinaenda kujenga hospitali 67, haijawahi kutokea ndani ya muda mfupi zaidi ya shilingi bilioni 105 inatoka. Pia zaidi ya shilingi bilioni 23 inaenda kuhakikisha tunajenga majengo ya halmashauri katika halmashauri zetu, lengo kubwa Watendaji wapate ofisi rafiki, hii haijawahi kutokea. Zaidi ya shilingi bilioni 1.4 watu ambao wako kandokando ya ziwa na bahari, ambao ilionekana kwamba tatizo kubwa lilikuwa ni boti, fedha hizo zote zimeshatoka kwa asilimia 100. Hii ni fahari kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali kwa upande wake hasa katika upelekaji wa fedha na nikiangalia *trend* hivi sasa mabadiliko yamekuwa makubwa sana. Hata hivyo, juzi juzi tumepeleka zaidi ya bilioni 54 kwa ajili ya Sekta ya Elimu, tukiboresha miundombinu ya elimu, hii ni kazi kubwa sana ambayo nina imani jambo hili zamani halikuwepo. Kwa hiyo tukiri wazi kwamba ,Serikali imendelea kutekeleza maelekezo ya *CAG*, halikadhalika maelekezo ya Kamati yetu ya Bunge ambayo inatushauri vyema katika kipindi chote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine kuhusu ripoti ya ukaguzi maalum uliofanyika kule Kaliua.

Naomba niwaambie kwamba, ofisi yangu iliamua hivyo kwa sababu ukiangalia idadi ya watumishi ni wengi zaidi ya watumishi 60; watumishi 60 siyo jambo dogo na halitaki maamuzi ya nanihi. Naishukuru sana Kamati imetuelekeza vizuri na hata hivyo tuliunda timu maalum ambayo ilienda kule *site* na Jumapili, ina maana keshokutwa hapa itatolewa ripoti ya watumishi wale 60 jinsi gani kwa kadri iwezekanavyo hatua kwa wale kuhusu labda suala zima la kinidhamu, mtu apelekwe wapi, kama mtu ana mambo ya kijinai. Mambo hayo yote yako katika utekelezaji, hata hivyo Kamati ilielekeza wale watumishi mbalimbali wengine waweze kurudishwa na hivi sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeanza kulitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie wewe na Wajumbe wa Kamati, jukumu letu sisi kubwa ni kuhakikisha kwamba ripoti ya *CAG* lakini maelekezo ya Kamati tutaendelea kuyatekeleza kwa kadri tutakavyoona inafaa. Lengo kubwa ni kuonyesha jinsi gani nchi yetu tunakwenda kujibu matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali yao hivi sasa, Serikali hii ambayo kwa sasa ukiangalia *trend* ya utendaji wake wa kazi tumebadilisha utaratibu wetu wa kazi, tunakwenda kujibu matatizo ya wanachi kwa kubaini changamoto na kuzitafutia majawabu. Hili ndiyo jambo la kushukuru. Hali hii zamani haikuwepo hivi lakini sasa hivi tunaona jinsi gani uwajibikaji umekuwa mkubwa sana, nidhamu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa sasa imebadilika tofauti na mwanzo watu walikuwa wanafanya kazi kwa mazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru Kamati imetushauri jinsi gani tuongeze kada ya watumishi mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha tunapata watumishi wa kuweza kutenda vyema katika maeneo yetu. Ndiyo maana hapa karibuni tumeajiri zaidi ya watumishi 21,000 katika sekta mbili tu ya afya ambayo tumeajiri zaidi ya watumishi 8,800 hali kadhalika sekta ya elimu zaidi ya watumishi 13,000. Najua

kwamba bado matatizo yapo na ndiyo maana Serikali inajieleza kuhakikisha katika kila eneo tunatatua matatizo haya kwa kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeona changamoto ya idadi ya Wakaguzi wa Ndani na kuweka mifumo. Hili jambo tumelipokea lakini naomba niseme, Ofisi ya TAMISEMI sasa hivi imejiimarisha katika mifumo ya TEHAMA na sasa hivi kuna mifumo ya *GoT-HoMIS* na mifumo mingine ya ukusanyaji wa mapato. Katika vituo vyetu vya afya vyote fedha zinakwenda moja kwa moja na eneo hili tumeajiri zaidi ya watumishi 530, hawa ni wahasibu. Lengo kubwa ni kuhakikisha fedha zote zinazofika katika kituo cha afya ziweze kusimamiwa vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wajumbe wameshauri, inawezekana *technicalities* za watumishi wetu uwezo bado mdogo. Ndiyo maana jambo hili tumeendelea kutoa maelekezo na hivi sasa wataalam wangu wengine wako Morogoro pale kwa ajili ya kutoa mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, nikushukuru sana lakini niseme kwamba Ofisi yangu itaendelea kufanya kila iwezekanavyo kwa mustakabali mzuri wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetufikisha hapa tulipo leo na Serikali ya Dkta John Pombe Magufuli mbele ya Watanzania inaendelea kuthibitisha kwamba ni safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia na napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi anazoendelea kuzifanya, nampongeza sana. Aendelee kukaza kamba, Watanzania wamemuelewa na sisi tutaendelea kutenda kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza kuyasema haya ili tuweze kuwa na uelewa wa pamoja kwa sababu yamesemwa hapa kulikuwa na *Special Audit,* hivi hata kusoma kawaida tu hatujui? *Special Audit,* nini kilichoandikwa ndani ya taarifa ya Mkaguzi Mkuu na nini kilichoandikwa ndani ya hotuba ya Mwenyekiti na Kamati yake? Mheshimiwa Mwenyekiti nikupongeze sana na Kamati yako kwa kuendelea kusimama imara, hukutikisika hata pale ulipotikiswa na ukahakikisha Watanzania wanakuwa na taarifa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru sana wachangiaji wote waliochangia, nimshukuru sana Waziri wa Kilimo ile sehemu ya kwanza niliyotaka kuisema ameisema, sasa naomba niende kwenye sehemu ya pili. Tukichukua taarifa hii tukaisoma vizuri, hii ya Mwenyekiti wa Kamati na Kamati ya *PAC,* tunakwenda kwenye hadidu za rejea kwa nini *CAG* alitakiwa kufanya uhakiki *(verification).* Alitakiwa kufanya uhakiki huu na Bunge lako Tukufu kwa sababu, kwanza, siyo kwamba yeye alikuwa na hoja ya upotevu wa shilingi trilioni 1.5. Taarifa zake za mwanzo alizowasilisha mbele ya Mheshimiwa Rais, alizozikabidhi Bungeni hazikuwa na hiyo hoja lakini watu wasiolitakia mema Taifa hili, wasioitakia mema Serikali ya CCM ya Awamu ya Tano wakaja na hoja hii ya upotevu wa shilingi trilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Serikali tulipotoa kauli hapa tarehe 20 Aprili, bado waliendelea kusema na kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, tulisikia na tukaruhusu na tukatoa vielelezo vyote hata vya ziada vilivyotakiwa ili waambiwe kuna wizi au hakuna wizi. Nashangaa leo wanaposimama wale wale wanasema kwamba anayetakiwa kuthibitisha siyo *CAG,* mnakula matapishi yenu leo? Kwa hiyo, lazima tu tuseme ukweli, tuseme wazi ndicho walichokihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye taarifa ya Kamati ukurasa wa 18, aliyejibu hakuwa *PST,* hakuwa *Paymaster General* alikuwa ni Msaidizi wa *CAG*. Alisema: "*... The difference of Tanzania Shillings 1.515.18 resulted from factors*

*such as differences in information reviewed and adjustments passed by management...".* Mimi tarehe 20 mbele ya Bunge lako Tukufu nilisema wazi kwamba haya yamesababishwa na Ofisi ya *CAG* kutumia *budget execution report* ambayo haina *adjustments. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndicho nilicholiambia Bunge lako Tukufu kwa kuwa nilikuwa naamini wataalam wangu ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango wako makini, hawana tatizo lolote kuhakikisha rasilimali za Taifa hili zinasimamiwa ipasavyo. Naomba niwaambie Watanzania waendelee kumuamini Dkt. John Pombe Magufuli, waendelee kumuamini Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango, waendelee kuwaamini watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Dotto James. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina wasiwasi wa kuaminika mbele ya Watanzania, wananchi wa Jimbo la Kondoa waliniamini. Kwa hiyo, naamini naaminika sina tatizo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuondoka hapo tunakwenda kwenye hadidu za rejea. Mheshimiwa Catherine, shika hadidu za rejea kwenye taarifa uliyoitumia kutudanyanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye taarifa ya Kamati, twende kwenye aya 2.2.2.2, ukurasa wa 26, nini Kamati imesema, naomba kununukuu: "*CAG* alifanya hitimisho kuwa utekelezaji wa awali na wa sasa unafanana" Watanzania mnajua nini kilikuwa kinatafutwa kwenye hili? Walikuwa wanatafuta kuthibitisha *rumors* zao mitaani kwamba kuna pesa zinazotumika bila kufuata kanuni na taratibu na Katiba ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anawathibitihia hapa *CAG* na ili tuweze kumuelewa vizuri, *CAG page* ya 20 kwa wale wenye taarifa yake someni kaandika nini. Tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani, Katiba ya nchi

haijavunjwa kwenye matumizi ya fedha za Serikali. Hicho ndicho kinachotafutwa na sasa wamedhihirishiwa wanakuja na hoja zisizo na mantiki yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye 2.2.2.3, *page* hiyo hiyo ya 26, nini kilisemwa na *conclusion* ni nini? Kwa nini tuondoke kwenye hoja? Nilisema asubuhi *reallocation between vote* siyo kazi ya *CAG,* ni kazi ya Waziri wa Fedha na Mipango kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini *CAG* ameandika, ukurasa wa 16, Mheshimiwa Zitto fungua, *recommendation*, alichokisema: *We also recommend that, the Treasury ensure that the Minister's approval, it is the approval of the Minister not of the CAG, not of the* Bunge. Kwa hiyo, haya yote yamekwenda ku-*cancel* uongo wote mtaani leo tunarudi na 2.4 ambayo haipo popote kwenye taarifa ya *CAG,* haipo popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limeongelewa jambo moja hapa la *warrant and exchequer issue notification.* Hili kwa kuwa Mheshimiwa Hassunga hakulisema naomba nitoe darasa. Liko hivi, *exchequer issue warrant* ni nini? *Exchequer issue warrant* ni nyaraka inayoandaliwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali kwenda kwa *Governor* wa Benki Kuu ya Tanzania baada ya idhini ya Mlipaji Mkuu ili ahamishe fedha kutoka akaunti ya mapato kwenda kwenye akaunti ya matumizi. Inapoingia kwenye akaunti ya matumizi kama yule ambaye aliiandika hii pesa kwenye bajeti yake hajatuletea taarifa inayothibitisha kutumia pesa hii hawezi kupelekewa *exchequer issue notification.* Mhasibu Mkuu wa Serikali anapoandaa *exchequer issue reports* hii haiwezi kuingia kwenye ripoti yake kwa sababu haijatumiwa na mtu anayetakiwa kutumia. Kwa hiyo, hili lieleweke wazi, tuwaachie wenye *CPA* zao waongee kuhusu *CPA* zao lakini wakiwa na uhakika wa nini kinachotakiwa kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi/Vigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka ili ahitimishe hoja yake.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika na Bunge lako Tukufu, nishukuru kupata tena nafasi hii kuweza kuhitimisha hoja hii ambayo imeleta sijui niite malumbano au utata mkubwa sana au mjadala mkubwa ndiyo Kiswahili hicho, mimi Mpare kwa hiyo Kiswahili wakati mwingine inakuwa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhtasari wa kuhitimisha hoja ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC).* Naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Kamati, jumla yao walikuwa Wabunge kama 11 waliochangia kwa kuzungumza hapa ndani ya Bunge. Sijapata michango yoyote kwa maandishi na nadhani labda haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na wajumbe ambazo kwa ujumla wake zote zimelenga kuboresha usimamizi wa fedha za umma katika Serikali Kuu na Mashirika ya Umma. Nikianza na wenzangu tuliokuwa nao kwenye Kamati na kutengeneza ripoti hii Mheshimiwa Kiswaga amezungumzia kuhusu miradi ya *NSSF* na viashiria vya ubadhirifu katika miradi hiyo. Nakubaliana naye ni muhimu kwa Serikali kufanya uchunguzi wa kina kwa watu wote waliohusika na manunuzi haya ya ardhi na kuchukua hatua stahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kiula ameongelea suala la tofauti ya shilingi trilioni 1.5 na kubainisha kuwa ni kweli kulikuwa na changamoto za takwimu katika suala hilo wakati ukaguzi unakamilika. Kama mapendekezo ya Kamati yalivyofafanua, tumependekeza kuongeza nguvu zaidi katika utunzaji wa kumbukumbu na wafanyakazi wenye weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ameongelea suala la mikopo ya matrekta ya SUMA JKT. Kamati inasisitiza kuwa madeni haya yalipwe na viongozi wa Serikali waliokopa matrekta hayo waonyeshe mfano kwa kulipa madeni hayo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ali Salim ameongelea kuhusu kuboreshwa kwa mfumo wa Hazina wa utunzaji wa taarifa za hesabu. Amesisitiza kuwa uhamisho wa fedha ufanyike kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Stanslaus Mabula ameongelea kuhusu suala la uwezo wa kibajeti wa *CAG.* Ni kweli kwa mwaka huu *CAG* amefanikiwa kukamilisha kazi ya ukaguzi wa wakati. Aidha, amesisitiza kuwa watuhumiwa wa suala la malipo ya *ration* kwa watu wasiokuwa askari ni lazima wahusika wafikishwe kwenye vyombo vya sheria haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zitto Kabwe aliongelea kuhusu suala la *over released funds from the Consolidated Fund to some votes.* Naomba kufafanua tu suala hilo kwa ufupi, kufuatia mabadiliko ya mzunguko wa bajeti hapo awali, uhamisho wa bajeti uliandaliwa baada ya kufungwa mwaka wa fedha na kuletwa Bungeni wakati Bunge likiendelea hadi mwezi Agosti. Baada ya mzunguko wa bajeti kubadilika, taarifa za uhamisho wa bajeti zimekuwa zikiandaliwa mapema ili kuwasilishwa kabla ya mkutano wa bajeti kukamilika tarehe 30 Juni kila mwaka. Hivyo Hazina imekuwa ikisitisha maombi ya uhamisho wa fedha kila ifikapo tarehe 15 Juni ya kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, panapokuwa na mahitaji maalum baada ya tarehe hiyo, maombi hayo hupokelewa na taarifa yake hutolewa katika taarifa ya mwisho wa mwaka. Kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na mzunguko mpana wa bajeti, taarifa za uhamisho wa fedha hutolewa kila baada ya utekelezaji wa bajeti wa kipindi cha nusu mwaka. Kutokana na majibu hayo, baada

ya uhakiki wa *CAG* kukamilika, hapakuwa na fedha zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa kwenye mafungu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Felister Bura amesisitiza kuhusu tofauti iliyokuwa imejitokeza hapo awali kwenye tofauti ya makusanyo na fedha zilizotolewa. Nakubaliana naye kuwa ni muhimu Serikali ikaendelea kuchukua hatua kwa watu ambao wanahusika na miradi isiyokuwa na tija. Ametolea mfano hatua zilizochukuliwa *NSSF* kwa Wakurugenzi waliokuwepo hapo awali. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ni muhimu hatua zaidi zikachukuliwa *NSSF* hasa kwenye suala la miradi ya ununuzi ya ardhi ambayo imeonyesha kutokuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khadija Nassir amezungumza kuhusu ushauri ambao umekuwa ukitolewa na Kamati. Katika hili nipenda kuishauri Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati na Maazimio ya Bunge kwa wakati. Haipendezi Maazimio ya Bunge kutolewa kwa zaidi ya mwaka mmoja bila ya kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Anatropia ameongelea suala la uweledi wa watumishi katika Wizara ya Fedha na Mipango. Jambo hili tumelilisitiza kuwa ni muhimu likaangaliwa kwa makini, ni sahihi kuwa maboresho ya mifumo iliyopo Hazina ni lazima iendane na kuongeza weledi wa watumishi ili kumbukumbu za Mfuko Mkuu ziwe sahihi na Mheshimiwa Omari Kigua amejaribu tu kufafanua kwamba kumekuwa na mikanganyo ya kutumia *MS Excel* pamoja mifumo mingine. Hata hivyo ni kweli *CAG* aligusia kwamba kuna taarifa ambazo zilitengenezwa kwa kutumia *excel* na kwa ajili hiyo ndiyo maana hata kwenye Kamati kulikuwa na hoja kwamba je hizi taarifa nyingine ambazo zilitumika kwa kutumia *excel* ni za kuaminika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena namshukuru Mheshimiwa Spika kwa uongozi wake dhabiti nakushukuru pia wewe binafsi kwa uongozi wa Bunge letu, nawashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati kwa ushirikiano wao mkubwa hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu kuwa Serikali itazingatia kwa ukamilifu uchambuzi wa Kamati na kutekeleza mapendekezo ya Kamati. Nipende kuchukua nafasi hii kusema kwamba Bunge lako limeshuhudia mapendekezo yalitolewa mara ya mwisho mwaka jana kipindi kama hiki manne yote ambayo ni muhimu sana hayajafanyiwa kazi. Sasa hapo ni wazi kwamba wale wahusika wote ni kama wamedharau Bunge, maana wasingekuwa wamelidharau Bunge wangeweza kuleta angalau taaarifa ya kuonyesha kwamba wamefikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipende kusema kwamba hapa kumetokea majadiliano mazito kutokana na fedha hii ya trilioni 1.5, kwa mtu aliyeko nje ni rahisi aone kwamba kuna kitu kinafichwa katika hela hii. Pamoja na kwamba tumesikia pande zote zinazosema kuna tatizo na zile zinazosema hazina tatizo, nipende kusema kwa kipindi kinachokuja wakati *CAG* atakapofanya ukaguzi ni vyema akapitia kwa undani suala hili pamoja na matatizo mengine ambayo yametokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili kwa nini? Ni kwa sababu kwanza hii halikuja kama hoja haikuwa imekuja kama hoja kwa hiyo hata sisi kwenye Kamati tulipata shida sana kwamba tunalibebaje wakati halikujaa kama hoja. Lakini sasa tunaona muda mwingi Bunge limechukua katika kuzungumzia hili trilioni 1.5 kwa maana hiyo ni kwamba hata Mheshimiwa Rais unakumbuka mwaka jana alimuuliza *CAG* kwamba je, hii hela imeibiwa? Na akaendelea kusema kama ingekuwa imeibiwa ningechukua hatua kali sana kwa wahusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naamini Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli huko aliko akisikia hii mijadala lazima aingie na mashaka kwamba kulikoni nitaangalia vile vifungu vyote vya taarifa yetu ambavyo vimeonesha kwamba Hazina walikubali kwamba kuna sehemu ambayo wamekosea wakakiri. Kwa maana hiyo ni kwamba kuna maeneo ambayo hayajatendewa haki. *(Makofi)*

Kama ukiongelea masuala yaliyoleta utata limetokana na mfumo swali ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi ambao wanaweza kujiuliza wa pande zote mbili kama mfumo una matatizo je, taarifa zilizokuja inawezekana zisiwe na matatizo? *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unapoongelea mfumo unaongelea kwamba huo mfumo na *CAG* amesisitiza hata sisi kwenye Kamati tumezungumzia mifumo unaweza ukatupa taarifa zisizo sahihi, ndiyo maana nasema *CAG* atakapofanya ukaguzi kipindi kinachokuja na kwa vile Hazina wamesema wanaweka mfumo bora basi atuletee taarifa maalum ya kuonesha kwamba mifumo imekaaje na je, mfumo wa awali umetuleta taarifa sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu weledi wa *CAG* amezungumza kwa urefu sana jinsi ambavyo alipata taarifa kwa shida ukiangalia taarifa inaonyesha akitaka taarifa hii inachukua muda sansa kupata majibu, wale wafanyakazi watakwenda huko watakaa muda mrefu bila kuleta taarifa kwa wakati, kwa maana hiyo hii ina maana gani ni kwamba Hazina haijawa-*well organized*, ama wafanyakazi lingine wanaloweza kufanya pia *by profession* ni *administrator* ni kwamba kunawezekana kuna wafanyakazi wengi wapya ambao hawakufanyiwa mafunzo ya kuweza kuweka taarifa vizuri kiasi kwamba ukitafuta taarifa huipati. *(Makofi)*

Kwa hiyo ndiyo maana pamoja na kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kweli kuna wabobezi kwenye mahesabu, lakini pia ikubalike kwamba kama hakuna utaratibu mzuri wa kuweka taarifa haiwezi kuleta tija katika sehemu kubwa au katika jicho la nchi ya Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo ndiyo tulisema hata wakati itakapofanyiwa ukaguzi tutahitaji *CAG* atueleze kuhusu utata huu wa kutopata taarifa kwa wakati aliohuitaji kwamba alichukua muda mrefu katika hii *verification* kupata *documents* imetokana na nini? Je, ni uzembe ule ule wa kimfumo? Je, ni uzembe wa wafanyakazi?

Je, ni kwamba hapakuwa na mafunzo ya kuelimisha wale wapya walioingia jinsi ya kuweka taarifa hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo twende kusema kwamba hapa wote tukubali maana siye tunaongea kama Bunge na wananchi wanatusikiliza sana na hatupo katika ushabiki wa vyama, na mimi kama Mwenyekiti wa *PAC* nipende kusema tunapenda popote walipo wananchi wetu waelewe kwamba Bunge liko *serious* kutokana na haya ambayo yanateandeka au ambayo yameonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo tusichukulie kisiasa tukazungumzia juu juu kwamba suala hili limefungwa lazima tunapoona suala limeleta utata mkubwa tuangalie kwanza aulize kwa nini hapakuwa na hoja ya *CAG* ili *verification* hii ambayo imefanywa na mfumo au mifumo ambayo ina utata je imeleta taarifa sahihi? Kwa hiyo nipende kusema kwamba naomba Bunge lako likubali kwamba wakati *CAG* atakapofanya ukaguzi unaokuja atuangalizie haya masuala ambayo yamefikisha Bunge lako kuwa na *discussion* kubwa kwenye trilioni 1.5 ambayo kwanza haikuwa hoja, lakini mfumo na weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona matatizo mengi ya fedha ambayo yamechukuliwa kwenye mashirika ambayo tungechukua muda mwingi pia kuangalia hao wote waliochukua fedha nyingi hivyo na bado wapo wengine kwenye kazi, hao waliochukua mikopo ambao bado wapo Serikalini na ambao wamestaafu. Imekuwaje kuwe na kigugumizi cha kuchukua hatua stahiki, kwa nini Benki ambazo zinatumia fedha za umma waoe kigugumizi kuchukulia watu hatua ambao ni wadaiwa sugu wakati benki zetu nyingine za biashara hawatoi mwanya kama huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nategemea Bunge lako lizamie katika sehemu hii ambapo kuna pesa nyingi inapotea na ujue kwamba hii ripoti iliyokuja ni ndogo tu ya sehemu kubwa ya tatizo kubwa ambalo tungekwenda maradi hadi mradi kuanzia *NSSF* na mashirika yote mngeona

matrilion ambayo yamepotea. Kwa hiyo, tusingezungumzia tena trilioni 1.5 kwa uzito huo ukilinganilisha na hizi zinazopotea katika miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe kwamba Bunge lako lijalo kama ni semina tupatiwe semina ya kwamba hizi taarifa tunazichambuaje kwa uweledi tutakapokwenda kivyama tutapoteza mwelekeo na utashi wa Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwamba baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge likubali mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *PAC* ili yawe Maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono tutaendelea, Mwenyekiti ahsante sana kwa taarifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa hapa Jedwali la Marekebisho...

Mheshimiwa Bungara sasa naona....*(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge nimeletewa hapa Jedwali la Marekebisho na kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 57 mwenye jedwali hili Mheshimiwa Richard Mbogo atueleze marekebisho yake halafu nitawahoji, Mheshimiwa Richard Mbogo. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi, kwanza nipongeze kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na Kamati ambayo ni kwa mujibu wa Kanuni na Katiba yetu ya nchi. Lakini katika maazimio ambayo yamewasilishwa ndani ya hii taarifa ya Kamati nina

Jedwali hili la Marekebisho katika Azimio Namba 3.31 inayohusu matokeo ya uchambuzi ya taarifa ya *CAG* kuhusu uhakiki wa Mfuko Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Azimio (a) nitakuwa sina haja ya kulisoma lote ninachopenda kurekebisha ili liweze kusomeka vyema na kazi tuvyojua inavyofanyika ya ukaguzi kwamba; Menejimenti ya Mfuko Mkuu iendelee kuboresha mifumo ya utunzaji kumbukumbu ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati."

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Azimio ambalo limeelezwa na Kamati kidogo lilikuwa linaleta mkanganyiko kwa sababu tunajua timu ya *auditing* inavyotengenezwa huwa wanagawana majukumu. Ukichukua ile *scope* kwa ujumla wanagawana majukumu kama mtu ataenda kwenye *balance sheet item* au ataenda kwenye *income statement item* au *cash flow* wanagawana kiujumla. Kwa hiyo, sasa kwa sababu majukumu yanagawanywa hatuna haja ya kwamba taarifa zikae kwa mtu mmoja na pia tukizingatia kwamba kila idara huwa inakuwa na mtnza kumbukumbu yaani *custodian* wa taarifa zake. Kwa hiyo, kimsingi kwa minajili hiyo naomba Kamati ikubali marekebisho haya kutokana na utendaji ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio (c) ambalo lineelezea sina haja ya kulisoma wote vitabu tunavyo kimsingi kwa kuwepo lile azimio kwamba taarifa Hazina ipeleke kila mwezi maana yake ni nini tunakuwa tunaenda tofauti na sheria ambazo tumezipitisha katika hili Bunge lako tukufu. Tuna Sheria ya Bajeti na mwaka jana tulifanya mabadiliko badala ya ku-*report* kila *quarter* tukaenda kwa nusu mwaka yaani mara mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna sheria ya fedha za umma ambapo mwaka wa fedha ukishaisha tarehe 30 Juni kufikia tarehe 30 Septemba taasisi inatakiwa zikabidhi hizi *draft report* zao kwa *CAG*. Kwa hiyo, kimsingi sasa kwa kupitisha azimio hili tutakuwa tunapingana na sheria ambazo tumezipitisha katika hili Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, azimio linalofuata ni (e) ambapo sina haja ya kulisoma lote linahitaji kwamba Ofisi ya *CAG* washirikiane na Hazina katika kuusimamia huu Mfuko Mkuu. Sasa kimsingi Mkaguzi unapomuhusisha katika kazi za kiutendaji maana yake unavuruga ule uhuru wake wa kazi na kwa lugha nyingine tunasema una-*in pair independence* na siku zote huwa tunahitaji mkaguzi awe huru ili atoe *opinion* yake ambayo inakuwa haijaingiliwa katika mazingira yake ya kazi. Sasa pendekezo ambalo nalitoa kwamba tuondoe yale maneno ya juu na tubakize hili ya kuongeza uwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa toa hoja!

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja kama Kamati haitaridhia basi nitaomba Waheshimiwa Wabunge waniuunge mkono ili tuweze kuichambua.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono Mwenyekiti wa Kamati kwa mapendekezo hayo.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli alivyoiweka haina matatizo maana ukiangalia ni kweli kulikuwa na hii ya ile miezi sita, sita ambayo ilibadilishwa na hii anayoizungumzia kwamba katika kaguzi zijazo mawanda ya ukaguzi yaongezwe ili kuhakikisha madhumuni ya uwepo ya akaunti moja ya Hazina inafikiwa. Ukisema kuendelea kushirikiana haina maana kwamba wanakaa wakitengeneza wote kushirikiana ina maana msiwe na migongano lakini nalo halina tatizo alivyotaka kuliweka hivi naona halina tatizo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa minajili hiyo sasa nitawahoji, Mwenyekiti wa Kamati amekubaliana na haya makubaliano. Kwa hiyo nitawahoji. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa pamoja na Mapendekezo na Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2018 Ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nianze kwanza kwa kuipongeza sana Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kupitia taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali na kutuletea hapa taarifa ambayo imesheheni mambo mengi na mapendekezo mengi ambayo sasa Bunge limeshaamua haya ndiyo maamuzi yake na ndiyo maamuzi yake. Kwa upande wa Serikali sasa kinachofuata ni utekelezaji wa yale ambayo Bunge limeamua. Kwa hiyo, niwapongeze sana Kamati lakini pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna amlivyoshiriki kwenye michango miliyoitoa na Serikali iko hapa imesikia kwa yale yalitolewa kama mapendekezo nje ya haya ambayo tumeyahoji sasa.

Kwa kuwa tunamaliza hii *report* ya Kamati ya Hesabu za Serikali nizungumze mambo mawili aliyoyazungumza Mwenyekiti. Jambo la kwanza ni kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kwa upande wa Serikali. Serikali kwa sababu ipo humu Bungeni na haya mapendekezo huwa ni sehemu ya Bunge na wao, nitoe wito kwa Serikali tunapokubaliana kutekeleza haya ambayo yako kwenye taarifa hii maana yake taarifa mnazo tayari na kama kungekuwa na shida kwenye utekelezaji basi tungeweza pengine kurekebisha hapa na pale ili muweze kwenda kutekeleza maamuzi ya Bunge.

Kwa hiyo Kamati, Mwenyekiti ameeleza kwamba kuna tatizo la utekelezaji ikiwa ni pamoja na maamuzi ya Bunge ya mwaka jana. Nitoe kwa wito kuyachukua haya ambayo yameamuliwa leo lakini pia yale ambayo yamepita

ili yafanyiwe kazi na tuweze kuboresha utendaji kazi wa Bunge kwa ujumla, lakini pia kuweza kulifanya Bunge liweze kufanya kazi yake vizuri ya kuisimamia Serikali. Inapokamilisha utaratibu huu wa kuisimamia Serikali, Serikali ifanye kwa upande wake. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo Mwenyekiti amelizungumza, nalazimika kulieleza kidogo; Mwenyekiti, ameeleza, kwa sababu iko kwenye Taarifa Rasmi za Bunge anaeleza kwamba matatizo ni makubwa kuliko taarifa iliyoletwa hapa na kamati. Sasa huko nyuma yameshawahi kutolewa maelezo na mimi kwa sababu wajumbe mko hapa na Mwenyekiti yuko hapa, Kamati hii na Mwenyekiti ndio tunaowategemea kutuletea hayo hapa Bungeni. Sasa ikiwa mlikaa huko kama Kamati mkija hapa tena mnatueleza yako matatizo makubwa zaidi kuliko mliyoyaleta hapa mnatupa wasiwasi kidogo. *(Makofi)*

Mnatupa wasiwasi kwa sababu sisi wote hapa tunawategemea ninyi muwe mmefanya huko kazi ndipo mtuletee hapa. Sasa ukisema hivyo Mwenyekiti kwamba mataizo ni makubwa kuliko haya uliyoyaleta hapa, sisi Wabunge humu ndani yanatupa wasiwasi. Kwa hiyo, niiombe kamati kama ambavyo imekasimiwa hayo madaraka ifanye kazi yake, isije hapa ndani tunaanza tena kuambiwa yako na mengine ambayo ninyi ndio tumewapa hiyo kazi ya kwenda kufanya, Kwa hiyo ni kazi yenu kufanya, hakuna mtu mwingine wa kufanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo tutaendelea na utaratibu wetu. Nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, ili ahitimishe hoja yake.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha majadiliano ya Taarifa ya Kamati yako tukufu ya Hesabu za

Serikali za Mitaa mbele ya Bunge lako tukufu, naomba kuhitimisha kwa kulieleza Bunge lako tukufu kwamba Kamati ya *LAAC* ilihoji Halmashauri 58. Kamati iliainisha maeneo yenye matatizo makubwa kwenye Halmashauri zote nchini, kutokana na muda kuwa mfupi wa ufuatiliaji, utendaji na kuhoji kuwa mfupi Taarifa ya Kamati ilibaini mapungufu katika maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ilikuwa ni ubadhirifu wa fedha za miradi ya maendeleo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kilichofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 hadi 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili ilikuwa ni kutotekelezwa kikamilifu kwa mapendekezo ya Kamati na tatu, kucheleweshwa kwa mchakato wa kukamilisha Kanuni za Uendeshaji wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Kamati hii imechangiwa na jumla ya Wabunge watano, hakukuwa na michango ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa ufafanuzi wa michango ya Waheshimiwa Wabunge naomba nilieleze na kulisisitiza Bunge lako tukufu kuhusiana na mapendekezo ya Kamati ya *LAAC* katika Ukaguzi Maalum katika Halmashauri ya Kaliua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa imebainika kuwa kuna ubadhirifu wa fedha za miradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kilichofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 hadi 2016/2017;

Na kwa kuwa hadi sasa Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepokea taarifa hizo lakini haijachukua hatua stahiki dhidi ya watu wote walioshiriki katika ubadhirifu huo;

Kwa Hiyo Basi Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liazimie:-

(a) Ofisi ya Rais, TAMISEMI ichukue hatua stahiki dhidi ya wahusika wote walioshiriki katika ubadhirifu huo mara moja kwani suala hili lina sura ya kijinai.

(b) Watumishi wanaohusika moja kwa moja na ubadhirifu huu warejeshwe kwenye kituo hicho ili waweze kujibu tuhuma hizo za jinai.

(c) Taarifa hii ya ukaguzi maalum ikabidhiwe kwenye vyombo vya dola kwa ajili ya kuendelea na taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati ya *LAAC* inafanya kazi kwa kupitia Taarifa Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, ikiwemo pamoja na Ukaguzi Maalum wa Halmashauri ya Kaliua;

Na kwa kuwa Ukaguzi Maalum ni *conclusive;*

Kwa hiyo basi, watumishi wote waliotajwa na ripoti ya ukaguzi huo kama ilivyoelezwa na kusisitizwa na Mheshimiwa Juma Hamad, Mheshimiwa Tunza Malapo pamoja na Mheshimiwa Felister Bura ikiwemo aliyekuwa Mkurugenzi Dkt. Athumani Kihamia na Wakurugenzi wengine wote waliohudumu katika Halmashauri hiyo kuanzia mwaka 2012 hadi 2017 pamoja na Mkuu wa Mkoa, Ndugu Fatma Mwassa, watawajibika kulingana na mapendekezo ya taarifa ya Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa Abdallah Chikota walieleza pia kuhusiana na matumizi mabaya ya shilingi bilioni 12.6 kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 4.6 tu katika miradi ya ujenzi wa barabara pale Morogoro ambayo ingeweza kutumika kujenga zaidi ya kilometa kumi. Kamati inasubiri Taarifa ya Ukaguzi Maalum *(Comprehensive Specific Audit)* katika miradi yote ambayo inatekelezwa chini ya mradi huu wa *Urban Local Government*

*Strengthening Program (ULGSP)* ili kuweza kuishauri Serikali vizuri juu ya hatua zaidi zinazopaswa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Selemani Zedi alieleza kuhusiana na suala zima la kufutwa kwa malimbikizo ya madeni ya Mfuko wa Wanawake na Vijana na Watu Wenye Ulemavu yanayofikia kiasi cha shilingi bilioni 13.9; Kamati inakubaliana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia alieleza kuhusu suala zima la kutopelekwa kwa fedha za maendeleo zilizopidhinishwa katika bajeti; pia Kamati inakubaliana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini alieleza suala zima la udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani; Kamati inakubaliana naye pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa kutuwezesha Kamati kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota - Makamu Mwenyekiti wangu ambaye tunashirikiana bega kwa bega katika kuiongoza Kamati hii. Vilevile nichukue nafasi hii kumshukuru Ndugu Dismas Muyanja Katibu wa Kamati, Ndugu Victor Mhagama - Katibu Msaidizi wa Kamati, Ndugu Waziri Kizingiti - Msaidizi wa Kamati, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ambao tumekuwa tukishirikiana bega kwa bega kuhakikisha Taarifa ya Kamati hii inakuwa imekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itazingatia mapendekezo ya Kamati hii ambayo yatakuwa ni Maazimio ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge likubali Mapendekezo ya Kamati hii ya *LAAC* ili yawe Maazimio ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaritibu, ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji, ili tuelewane tunahojiana kwenye jambo lipi, Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa wote tunayo, lakini wakati akizungumza hapo amezungumza kana kwamba anataka kubadilisha kidogo maudhui ya yale mapendekezo ama maazimio yaliyoko kwenye kitabu.

Kwa hiyo, ninapowahoji kwa sabahu, sikuletewa hapa Jedwali la Marekebisho, ninapowahoji nawahoji yaliyoko kwenye kitabu na si yale aliyoyasoma Mwenyekiti hapo, ili tuelewane vizuri. Kwa sababu hapo ametaja na majina yale ambayo humu hayapo, kwa hiyo, ninapowahoji nawahoji kwa mujibu wa kitabu hiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa pamoja na Mapendekezo na Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2018 Ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumeshaazimia sasa kama Bunge kwamba mapendekezo yote yaliyotolewa katika Taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa sasa ni Maamuzi ya Bunge. Kwa namna ya kipekee kabisa niipongeze Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo imetuwezesha sisi kama Bunge kufikia

maamuzi ya kuweza kuiambia Serikali nini cha kufanya inapokuja kwenye Hesabu za Serikali za Mitaa.

Lakini pia nitambue kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alisimama hapa akiahidi utekelezaji wa yale yote ambayo Bunge litaazimia leo. Na kwa kuwa tumeshaazimia na yeye yuko hapa, ameshayapata haya maazimio na ninamtakia kila la heri kwenye utekelezaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia, ninawashukuru sana kwa ushiriki wenu katika kuzungumzia taarifa hii, lakini kutupa uelewa wa pamoja sisi ambao ni Wajumbe wa Kamati nyingine na hata tumeweza kufikia maamuzi ya pamoja kama Bunge kwenye maamuzi haya. Kwa hiyo, ninaitakia Serikali kwa ujumla utekelezaji mwema wa maamuzi ya Bunge kwa upande wa Hesabu za Serikali za Mitaa, lakini pia Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Tunaamini haya ambayo yameelezwa na Wabunge yatasaidia kuboresha utendaji wa Serikali, ili wakati mwingine haya ambayo nyameonekana ni mapungufu basi hayatajitokeza kwani Bunge limeshaeleza shida iko wapi na wapi panaweza kurekebishwa. Nawatakia utekelezaji mwema upande wa Serikali kwenye maamuzi haya ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho asubuhi saa tatu kamili.

*(Saa 1.10 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 2 Februari, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*